

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 8 Mei, 2019**

*(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wetu wa 15 na Kikao cha leo ni cha 23.

Katibu!

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Ahsante sana *Engineer*, tunakushukuru sana.

Katibu!

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Swali la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, litaulizwa na Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Munira.

Na. 186

### **Kupunguza Makato ya Watumishi kwa Vyama vya Wafanyakazi**

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB** aliuliza:-

Vyama vya Wafanyakazi nchini licha kuwa na uwezo wa kujitegemea bado vinaendelea kutoza ada kubwa ya Uachama mathalan, Chama cha Walimu (CWT) kinatoza asilimia mbili.

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kulinda maslahi ya Watumishi kwa kuleta Sheria ya kupunguza makato hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Munira Mustapha Khatibu, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napeda kueleza kwamba, Serikali imeweka utaratibu chini ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Namba sita (6) ya mwaka 2004 unatoa uhuru na haki kwa Chama cha Wafanyakazi na Chama cha Waajiri, kuamua na kufanya mambo yao wanayotaka kwa maslahi yao ikiwa ni pamoja na masuala yanayohusu Katiba zao. Kifungu cha 11 cha sheria hiyo, kimeeleza bayana kuhusiana na haki hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha na kuboresha maslahi ya Wanachama, Wanachama wa Chama cha

Wafanyakazi wanao uhuru na haki ya kufanya mabadiliko katika Katiba zao ambazo zinasimamia uendeshaji wa shughuli za chama chao. Hivyo, suala la kupunguza makato ya Watumishi kwa Vyama vya Wafanyakazi lipo chini ya mamlaka ya Chama cha Wafanyakazi husika na Wanchama wenyewe kupitia vikao vya kikatiba kwa kufanya mabadiliko katika Katiba ya chama chao.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kusimamia viwango vya michango ya wanachama ni kukiuka Mikataba ya Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) Na. 87 na 189 juu ya uhuru wa kujumuika na majadiliano ya pamoja ambayo Serikali yetu imeridhia na kuzingatia katika Katiba ya nchi na Sheria mbalimbali za Kazi nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa elimu juu ya haki na wajibu, uhuru wa kujumuika na mambo muhimu yahasuyo Wanachama na Katiba zao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Munira nilikuona.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwa kuwa watumishi wengi hasa wanaoanza kazi wamekuwa wakiunganishwa kwenye mikataba ya wafanyakazi bila ya ridhaa yao.

Je, Serikali haioni haja sasa ya kutoa mwongozo kwa maafisa utumishi juu ya kulinda haki za watumishi hao? (*Makofi*)

Swali la pili, Serikali ina mkakati gani wa kujiondoa kuwa mawakala wa makato ya wafanyakazi?

**SPIKA:** Swali la pili liweke vizuri.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, Je, Serikali ina mkakati gani wa kujiondoa kuwa mawakala wa vyama vya wafanyakazi?

**SPIKA:** Kivipi yaani, ili ujibiwe swali lako.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, kwenye majibu yake ya msingi, amesema vyama vya wafanyakazi, naomba ninukuu” watumishi wa vyama vya wafanyakazi licha ya kuwa na mamlaka nchini, wafanyakazi husika, vyama vya wafanyakazi hupitia vikao vyao , katiba kwa kufanya mabadiliko katika...

**SPIKA:** Ahsante sana Munira, Mheshimiwa Waziri jibu hilo swali la kwanza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa wafanyakazi kujiunga katika vyama vya wafanyakazi ni utaratibu ambao umewekwa kwa mujibu wa sheria na kuna uhuru wa wafanyakazi kujiunga ambapo chama husika kwa kuzungumza na mwajiri, hufanya mikutano na kutoa elimu mbalimbali na baadaye ndiko wafanyakazi wanajiunga.

Mheshimiwa Spika, hivyo, niseme tu kwamba wafanyakazi wengi wanajiunga kwa mujibu wa taratibu za kisheria ambazo zimewekwa na Katiba na katika mazingira ambayo wafanyakazi wanalazimishwa kujiunga pasipo wao kufahamu na ridhaa yao, hiyo ni kinyume na utaratibu na nitoe tu maelekezo kwamba vyama vyote vya wafanyakazi vihakikishe kwamba vinazingatia sheria za kazi ili wanachama wote wanaojiunga wawe wanajiunga katika uhuru na ridhaa yao.

**SPIKA:** Ahsante tunaendelea na swali la Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Mheshimiwa Kiteto!

Na. 187

### **Kuwawezesha Vijana Kupata Ajira Nchini**

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuelekeza taasisi zote nchini kuwa sifa mojawapo ya kuajiriwa iwe ni umri wa miaka

21- 35 ili kuwezesha Vijana wengi wanaotoka vyuoni kupata ajira.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tuko Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, litajibiwa na Naibu Waziri Anthony Mavunde, Mbunge wa Dodoma Mjini.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mijibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya Mwaka 2004, Kifungu cha 5 kimekataza mtoto chini ya umri wa miaka 18 kuajiriwa isipokuwa katika mazingira maalum yaliyotajwa katika kifungu hiki. Kwa msingi huo, umri wa kuajiriwa ni miaka 18 na kuendelea pamoja na masharti yaliyotajwa katika kifungu cha 5 cha Sheria Na. 6 ya mwaka 2004. Hivyo nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuendelea kuwahimiza waajiri wote kutii Sheria za kazi na kuhakikiahisa vijana wote wenye sifa wanapomaliza mafunzo yao na kutimiza umri wa kuajiriwa wanaajiriwa kwa kuzingatia fursa zilizopo kwa waajiri na masharti ya kazi husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiteto!

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na sheria kuelekeza umri wa kuajiriwa kazini, bado ajira nyingi zinapotangazwa hapa nchini hutoa sharti la kuwa na uzoefu wa kazi, kuanzia umri wa miaka mitano na kuendelea, na hivyo hii huwaondolea fursa vijana wengi wanaotoka vyuoni kutokupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, naomba Serikali itoe majibu hapa kwamba ni lini itatoa tamko kwa waajiriwa kuondoa sharti la vigezo ili kuwapa fursa vijana wanaotoka vyuoni, isipokuwa tu kwa zile ajira ambazo zinahusu nafasi za juu?

**SPIKA:** Hivi wewe Kiteto ukiwa una ajira zako mwenyewe utampa mtu asiyekuwa na uzoefu! Mambo mengine Waheshimiwa Wabunge, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kwamba kumekuwepo na changamoto kubwa sana kwa vijana wahitimu wa vyuo vikuu na vyuo vya elimu ya juu kupata kazi kwa kikwazo cha uzoefu. Ofisi ya Waziri Mkuu katika utekelezaji wa programu ya ukuzaji ujuzi nchini, imeanzisha *program* maalum kabisa ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu alizindua miongozo yake ya mafunzo ya Uanagenzi na mafunzo ya Vitendo Kazini (*Internship*). Ambayo hivi sasa kwa mujibu wa utaratibu tuliouweka, tunawachukua vijana kutoka vyuo vikuu, kutokana na fani walizonazo na makubaliano ambao.

Mheshimiwa Spika, sisi Serikali tumeingia na chama cha waajiri na sekta binafsi, tunawapeleka katika kampuni husika kwenda kufanya kazi kivitendo, ambako wanakaa miezi sita mpaka miezi 12 na baadaye mwajiri katika eneo husika, anampatia cheti cha kumtambua kama ni mwanachuo ambaye amekaa kwake katika fani husika kwa miezi 12 ili baadaye ikitangazwa nafasi ya ajira ya kazi ambayo ameifanyia kwa vitendo, iwe pia ni sehemu ya yeye kumsaidia kupata ajira, kwa maana ya kutumia ule utambulisho wa kwamba tayari ameshafanya kazi katika mwajiri husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama Serikali na sisi tumeliona jambo hilo, na ndiyo maana tumeweka nguvu kubwa sasa hivi katika kuhakikishi kuwa tunawajengea ujuzi vijana wetu ili waweze kuwa na sifa za kuajirika na baadaye kuwasaidia kupata ajira pasipo kikwazo cha uzoefu.

**SPIKA:** Safi kabisa Mheshimiwa Naibu Waziri, hiyo ndiyo njia ya kufanya, wafanye *internship*, wajue nini cha kufanya, waajiriwe, lakini hii ya kusema tu, twende twende. Mwakajoka nimekuona.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri mwaka jana niliuliza swali kuhusiana na vijana wanaosindikiza kopa zinazovuka mpaka wa Tunduma kuelekea Dar es Salaam zinazotoka Zambia na Congo, wamefanya kazi zaidi ya miaka mitatu na miaka minne pale, lakini mpaka leo hawajapata mikataba ya ajira na uliagiza ukasema kwamba Kazi Mkoa atahakikisha kwamba anashughulikia jambo hili, mpaka leo halijashughulikiwa. Nini kauli ya Serikali Mheshimiwa Naibu Waziri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka swali hilo halina uhusiano kabisa na swali la msingi, swali la msingi linahusiana na vijanan wanaomaliza vyo vikiu kupata ajira moja kwa moja bila kulazimika kuwa na uzoefu kazini. Kwa hiyo, hilo nalikataa, tunaendelea na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Profesa Jumanne Maghembe.

Na. 188

### **Uhaba Mkubwa wa Walimu wa Shule za Msingi Wilayani Mwanga**

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE** aliuliza:-

Kuna uhaba mkubwa wa Walimu wa Shule za Msingi Wilayani Mwanga:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Walimu 384 wanaohitajika?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mwita Mkwabe Waitara, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe, Mbunge wa Mwangi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna changamoto ya upungufu wa walimu wa shule za msingi nchini, na Halmashauri ya Wilaya ya Mwangi ina jumla ya shule za msingi 110, za Serikali zenye jumla ya walimu 590, hadi kufikia Novemba, 2018 kulikuwa na upungufu wa walimu 384.

Mheshimiwa Spika, Mwezi Aprili, mwaka 2019, Serikali imeajiri walimu 4,549 wa shule za msingi na sekondari ili kuziba nafasi zilizoachwa wazi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Halmashauri ya Mwangi, na kati ya walimu hao 3,089 ni kwa shule za msingi na walimu 1,460 ni shule za sekondari. Walimu hawa wameshapangwa katika halmashauri mbalimbali nchini na walipaswa kulipoti kuanzia jana mpaka tarehe 21 na wale ambao hawataripoti, nafasi zao zitapewa watu wengine ambao wana uhitaji kama huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri ya Mwangi imepelekewa walimu 21 wa shule za msingi nawalimu watano wa shule za sekondari. Serikali itaendelea kuajiri walimu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Haya Profesa umeletewa walimu, swali la nyongeza Mheshimiwa Maghembe tafadhali.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kuwapa pole sana wananchi wa Machame na hasa familia ya Marehemu Dkt. Reginald Mengi kwa msiba uliowapata. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho haye mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, sasa niulize maswali mawili ya nyongeza, kwanza, uhaba wa walimu 384 tumepewa walimu



21! Katika shule zetu, shule 50 zina walimu wawili wawili na shule zingine 40 zina walimu watatu watatu, sasa ujue hizo zingine ndiyo... na shule za msingi zina madarasa nane, darasa la awali na madarasa saba, kwa hiyo, hali iliyoko pale ni ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, na kwa sababu uhaba huu umetokana na walimu kustaafu, kuhama na kufariki. Suala la fedha halipo hapa, kwa sababu nafasi zipo, na mishahara ipo, ni kwa nini sasa Serikali haichukui hatua ikaajiri bila kutumia visingizio ambavyo havina msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ni lini Serikali itabadilisha urasimu huu, kama mwalimu yupo na yuko kwenye ikama, na amestaafu. Kwa nini Serikali hairuhusu halmashauri ikaajiri kutoka kwenye soko mara moja ili kutoathiri upatikanaji wa elimu katika shule. Inaacha mpaka shule zinakuwa na mwalimu mmoja?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mwikwabe Mwita Waitara, maswali hayo muhimu sana, Mwanga upungufu wa walimu 300, Kongwa upungufu walimu 1000. Majibu tafadhali. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli, tuna upungufu wa walimu wa shule za msingi 66,000 nchi nzima, na upungufu wa walimu wa sekondari 14,000, kwa hiyo, ni kweli kwamba kuna upungufu, ni jambo ambalo liko wazi.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, hizi ajira mpya ni ajira za kuziba nafasi. Sasa hivi inayofuata ni ajira zile za kawaida za kila mwaka za kuongeza na kupunguza upungufu uliopo. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie kwamba Serikali imeshaliona hili, tulifanya uhakiki, pamoja na watumishi hewa, waliofariki, waliofukuzwa kazi na wengine wamestafu na wengine wameacha kwa

sababu mbalimbali. Kwa hiyo, hili ilikuwa ni kuziba nafasi hizi, sasa inakuja ya ajira za kila mwaka za kuweza kuziba kwa utaratibu wa kawaida na hili linafanyiwa kazi na Serikali inajua kwa kweli kuwa kuna upungufu mkubwa nchini wa walimu.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ni kwamba, ni kuziba nafasi kwa maana ya kutoa kibali kwa halmashauri. Hizi ni ajira, cha muhimu hapa siyo kuruhusu utaratibu usioelekeweka utumike kuajiri walimu, kumekuwa na mambo mengi sana katika halmashauri zetu ambayo yanafanyika katika ajira hizi, kwa hiyo, tunajiridhisha kwanza. Lakini cha muhimu ni kwamba tumekubaliana kama Serikali kuchukua hatua mahususi kupunguza upungufu wa walimu shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Maswali ya nyongeza wanatakiwa wasimame walimu tu. Mwalimu Susan Kiwanga!

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kama ilivyo kwa Mheshimiwa Maghembe Mwanga, Wilaya ya Kilombero yenye majimbo mawili ilikuwa na upungufu wa walimu 1,118 na hivi juzi tu tumeletewa walimu 34, wanne wa sayansi sekondari na 30 wa msingi na kufanya nakisi upungufu huo ubaki 1,084.

Je, Serikali ni lini sasa itapeleka walimu ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, ili watoto wale wapate chakula cha akili, ukizingatia na miundombinu yetu si rafiki?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo ambalo ndiyo la Wabunge walio wengi, najua ulijibu lakini hebu rudia tena Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli, kama nilivyosema, tumeajiri walimu 4,549, tuna shule za msingi 16,000 za Serikali na tuna shule zaidi ya 4000 za sekondari. Katika hali ya kawaida upungufu huo naupokea

kama Serikali ni kweli, kuna upungufu mkubwa na tusingeweza kupeleka kila mahali. Lakini tuliangalia kwa mfano kuna shule ambazo pale kulikuwa na wakumu ambao wanapelekwa shule za msingi, wameenda mahitaji maalumu, wameenda na masomo ya sayansi na hisabati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, angalau tukaangalia shule ambazo zina upungufu mkubwa zaidi tukapeleka pale, kwingine tumepeleka walimu mpaka watano, wengine wanne.

Mheshimiwa Spika, lakini, Mheshimiwa Susan Kiwanga wiki iliyopita aliuliza swali hap ana walimu hao. Tumeshatoa maelekezo, kwanza kuna walimu wapo kwenye halmashauri, makao makuu ya wilaya au ya mji, lakini unakuita pembezoni kule unakuta walimu ni wachache, lakini walimu wapo. Tumeshapeleka fedha katika halmashauri zote nchini za kuweza ku-*balance* ikama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunatarajia kwamba kazi hii itafanyika kwa kusimamiwa na Makatibu Tawala Mikoa na Wakurugenzi, ndani ya wiki mbili mpaka tatu, tupate taarifa rasmi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ilikuwa kuhamisha walimu kupeleka pembezoni ilikuwa ni ngumu kwa sababu fedha hazipo, sasa fedha wameshapelekewa Halmashauri zote, zinatakiwa kazi ifanyike, halafu ajira inayofuata tutazingatia maeneo yote ambayo yana upungufu mkubwa. Shule za msingi, hisabati na masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Spika, ahsante, likiwemo na eneo la Kongwa.

**SPIKA:** Ahsante sana nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge tunaedelea, bado tuko TAMISEMI, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Mbogwe, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele.

Na. 189

## Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya-Mbogwe

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbogwe.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Mtemi wa Wasukuma, Mheshimiwa Masele, Mbunge wa Mbogwe tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali ilitoa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali 67 za Halmashauri. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali imetenga shilingi bilioni 23.9 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya 52 na Hospitali 27 za Wilaya. Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ni miongoni mwa Hospitali hizo 27 na imetengewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masele swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali madogo ya nyongeza. Swali la kwanza ni kwamba Wilaya ya Mbogwe ni Wilaya mpya na katika Mkoa wa Geita, ni Wilaya pekee ambayo kwa kweli ina watumishi wachache sana wa Idara ya Afya: Je, Serikali ina mpango gani wa kutuongezea watumishi hao?

Swali la pili ni kwamba Serikali imejitahidi kutupatia vituo viwili vya afya na huduma mojawapo ni ya *mortuary*:

lakini kuna shida ya *mortuary cabinets*, yale mafriji ya kuhifadhia maiti hayajaletwa na watu MSD. Sasa Serikali ina mpango gani kupitia MSD kutuletea hiyo huduma mara moja? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Naibu Waziri TAMISEMI tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza Mheshimiwa Masele anaongelea upungufu wa watumishi wa Kada ya Afya katika Wilaya yake ambayo ni miongoni mwa Wilaya mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika na wewe umekuwa shuhuda kwamba wakati mwingi zinapoanzishwa Halmashauri mpya kumekuwa na nakutopata watumishi wa kutosha. Kwa hiyo, naomba kwanza niagize Ofisi ya RAS wahakikishe kwanza ndani ya Mkoa watazame ikama ilivyo ili katika maeneo ambayo yana upungufu mkubwa kama eneo la Mheshimiwa Mbunge waweze ku-*balance*.

Mheshimiwa Spika, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati nafasi nyingine zikitoka kwa ajili ya kuajiri, tutahakikisha kwamba tunazingatia maeneo yenye upungufu ikiwa ni pamoja na eneo lake kuwapeleka watumishi wale.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni juu ya kupatikana kwa friji kwa ajili ya kutunza maiti. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni azima ya Serikali kuhakikisha maeneo yote ambayo *mortuary* zimejengwa, friji zinapelekwa. Naomba tuwasilaine na Mheshimiwa Mbunge baada ya kipindi cha maswali na majibu ili tujue MSD lini watapeleka hayo masanduku.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Gashaza, swali la nyongeza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niliulize swali dogo la nyongeza. Hospitali ya Nyamiaga ni Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ambayo ilipatiwa hadhi kutoka kituo cha afya mwaka 2013, lakini mpaka sasa hivi hakuna maboresho ya miundombinu katika hospitali hiyo. Kwa hiyo kuna upungufu wa jengo la utawala, jengo la upasuaji, jengo la *X-Ray*, *mortuary* na *labor Ward*:-

Ni lini Serikali itaweza kutenga fedha kwa ajili kuboresha hospitali hiyo ukizingatia kwamba hatuna hospitali ya Wilaya?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gashaza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba maeneo mengi ambayo vilikuwa aidha vituo vya afya au ilikuwa zahanati ikapandihswa hadhi; kwanza tumekuwa na changamoto ya eneo, hata pale ambapo tumepandisha hadhi kituo cha afya kuwa hospitali ya Wilaya inakuwa haina hadhi ya kulingana na hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba Serikali katika utaratibu mziwa wa kuboresha na kujenga Hospitali za Wilaya zile za mwanzo zinaanza kuonekana kwamba zimeanza kuwa *outdated*. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kadri ambavyo tumeanza na hospitali 67, zikaongezeka 27 kwa kadri bajeti itakavyoruhusu hakika na wao hatutawasahau ili wale na Hospitali ya Wilaya yenye hadhi ya kulingana na Hospitali za Wilaya za Halmashauri nyingine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lubeleje, swali fupi.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa ujenzi wa Kituo cha Afya Mbori ambacho hata wewe unakifahamu, Waziri wa TAMISEMI anakifahamu, sasa ni zaidi ya miaka kumi kinajengwa kwa nguvu za wananchi na Halmashauri ambayo haina fedha; na kwa kuwa nimeomba shilingi milioni 500 TAMISEMI wasaidie kukamilisha jengo lile:-

Je, TAMISEMI au Serikali inasemaje kuhusu kukamilisha Kituo cha Afya Mbori?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, kama kuna Waheshimiwa Wabunge ambao wamekuwa wakiongelea kituo cha afya kwa kurudia mara nyingi ni pamoja na Mheshimiwa Lubeleje; na hivi karibuni alipata fursa ya kuonana na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na akamhakikishia.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumepata fedha kiasi, tumepeleka kwenye hospitali na vituo vya afya ikiwa ni pamoja na Kongwa shilingi milioni 400. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Lubeleje, ahadi ya Mheshimiwa Waziri hakika atatekeleza kama alivyomwahidi. Naomba avute subira fedha yoyote ikipatikana hatumsahau Mheshimiwa Lubeleje.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wiazara ya Kilimo, swali la Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani, kwa niaba yake.

Na. 190

### **Kilimo Kisichotumia Mbolea za Viwandani**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM (K.n.y. MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN)** aliuliza:-

Tanzania ina ardhi kubwa yenye rutuba ya kutosha na inawezekana kabisa kulima mazao yasiyotumia mbolea za viwanda ambayo bei zake ni kubwa sana katika Soko la Dunia:-

(a) Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kutoa elimu hiyo kwa wakulima?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kuona kuwa Tanzania ni nchi inayoongoza kwa kuzalisha mazao yasiyokuzwa kwa kutumia mbolea za viwandani?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Mgumba, Naibu Waziri Kilimo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani, lenye sehemu (a)na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi za Sekta Binafsi imeendelea kutoa elimu ya kilimo bora inayojumuisha matumizi sahihi ya mbolea za asili, viuatilifu vya asili, mbegu bora na hifadhi ya mazingira ili kuzalisha mazao kwa tija na kuwa na kilimo endelevu.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa muda mrefu wa matumizi sahihi ya virutubisho vya udongo, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania yaani (*TARI*) inafanya utafiti wa afya ya udongo katika Kanda zote saba za kiikolojia za kilimo nchini. Utafiti huo unalenga kubaini aina za virutubisho na tabia za udongo katika maeneo mbalimbali nchini ili kuweza kutoa elimu kwa wakulima kuhusu kiasi, aina na matumizi sahihi ya mbolea za viwandani na asili. Utafiti huo umeanza kwa kuchukua sampuli za udongo katika Kanda za Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kati, Kanda ya



Kaskazini na sehemu ya Kanda ya Mashariki na utaendelea katika maeneo mengine nchini na utakamilika Juni 2020.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua ongezeko la mahitaji ya mazao na bidhaa za kilimo zinazozalishwa kwa kutumia mbolea za asili na viuatilifu vya asili, Serikali imeboresha mtaala wa mafunzo katika Vyuo vya Kilimo ambapo mada za kilimo hai na hifadhi ya mazingira zimejumuishwa ili kuwawezesha Maafisa Ugani na wakulima kupata elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na *Tanzania Organic Agriculture Movement, Sustainable Agriculture Tanzania, Ecology Agriculture chini ya SWISSAID, Zanzibar Organic Producers, Tanzania Alliance for Biodiversity* na *TANCERT* inatoa elimu ya kilimo hai kwa wakulima na kutoa vyeti vya ubora wa mazao kwa ajili ya masoko maalum. Baadhi ya mazao ambayo yanazalishwa katika mfumo wa kilimo hai hapa nchini ni pamoja na kakao, kahawa, pamba na viungo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masoud, uliuliza swali.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kasi ya uzalishaji wa kilimo cha viungo kama vile hiliki, mdalasini, pilipili manga, binzari nyembamba kwa nyumbani Zanzibar tunaita uzile, imekuwa bado ni ndogo sana na kuna maeneo mengi ambayo yanaweza yakastawi mazao haya.

Mheshimiwa Spika, Serikali ituambie katika kuhakikisha kwamba kwa hali ya hewa na udongo, mahitaji ya mazao haya bila mbolea, ina mkakati gani wa ziada kuona kwamba mazao haya yanalimwa na wakulima wakapata faida na Serikali inapata tija kubwa?

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna malalamiko makubwa kwa baadhi ya wakulima kwamba Maafisa Ugani hawatoi

elimu inayostahili katika maeneo ambayo wakulima wangeweza kulima kilimo cha aina yoyote bila kutumia mbolea: Serikali ituambie ina mkakati gani katika kuwawezesha Maafisa Ugani ili waweze kuwafikia wakulima walio wengi zaidi?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Swali la kwanza la Mheshimiwa Masoud anataka kujua mkakati wa Serikali ambao tunaweza kuwawesha wakulima ili waweze kuongeza uzalishaji na tija.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, yaani kilimo tulichokuwa tunalima, kilikuwa cha kubahatisha; mkakati mkubwa wa Serikali uliopo sasa kwanza ni kufanya utafiti wa afya ya udongo ili kubaini asili na kuangalia aina ya udongo iliyoko pale ili kuwashauri wakulima ni zao gani ambalo linakubali kwa udogo wa ikolojia eneo walipo? Kwa hiyo, huo mkakati ambao utakamalizika muda mfupi ili kwamba tutoe elimu sahihi na kuwashauri wakulima aina gani ya zao walime? Mbolea gani watumie? Namna gani ambayo wanaweza kufaidika kwa kuongeza uzalishaji na tija?

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili, anazungumzia kuhusu Maafisa Ugani kwamba wapo lakini hawawafikii wakulima kutoa elimu sahihi. Kwanza, nichukue nafasi hii kueleza kwamba Maafisa Ugani ni kweli anachosema Mheshimiwa Mbunge kwamba wako wachache. Mahitaji Maafisa Ugani ni zaidi ya 20,000 nchini hii, tuliokuwa nao ni 8,600. Kwa hiyo, tuna upungufu zaidi ya 11,400.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali, kwa kujua hilo kwa sasa hivi ni kwamba Serikali imeshaanza kutoa vibali kwa ajili ya kuajiri watumishi na mkazo mmoja utaelekezwa huko ili tupate Maafisa Ugani kwa ajili ya kwenda kutoa elimu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kama Serikali tuna mkakati ambao ulikuwepo tangu katika *ASDP I* wa kujenga vituo vya elimu kwa wakulima kila Kata, mkakati huo utaendelea, lengo ni kuwakusanya wakulima kutoka katika vijiji mbalimbali kukutana pale kunapokuwepo na mashamba darasa ya mazao yanayokubali katika maeneo yao ili wapate elimu ya pamoja kwa ajili ya kuwasaidia katika kuongeza tija na uzalishaji. (*Makofi*)

**SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, bado tuko Wizara ya Kilimo. Kwa niaba yake, nimekuona Mheshimiwa Shally Rymond.

Na. 191

### **Ushiriki wa Wanawake Kwenye Fursa ya Kilimo**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND (K.n.y. MHE. ESTER M. MMASI)**  
aliuliza:-

Changamoto kubwa inayowafanya wanawake wa Tanzania washiriki kwenye Sekta ya Kilimo na ufinyu wa Bajeti na mitaji kutoka kwenye Taasisi za Kifedha:-

Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya ushiriki wa wanawake kwenye Sekta ya Kilimo ukizingatia changamoto hizo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo inajumuisha sekta ndogo za kilimo mazao, mifugo, uvuvi na misitu. Bajeti ya Wizara za Sekta ya Kilimo zinajumuisha bajeti ya Wizara za sekta husika, Bodi za mazao na Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara hizo za Kisekta. Utekelezaji wa bajeti hizo huwawezesha wanaume na wanawake katika shughuli za

kilimo. Wanawake wanachangia asilimia 90.4 ya nguvukazi ya wanawake inayotumika katika shughuli za kilimo na huchangia wastani wa asilimia 70 ya mahitaji ya chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto hizo, Serikali inaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 kupitia mifuko ya uwezeshaji ikiwemo Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ambao huchangia 4% ya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kila mwaka. Kwa mfano, katika mwaka 2017/2018, jumla ya shilingi 15,633,312,764.91 zimetolewa kwa vikundi 2,919 vya wanawake na vijana vyenye jumla ya wanawake wajasiriamali 29,190 katika Halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa wanawake katika kilimo Serikali, imeilekeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo (*TADB*) katika mikopo inayotoa yote isipungue asilimia 20, mikopo hiyo itolewe kwa vikundi vya wanawake na miradi inayoongozwa na akina mama. Hadi Januari, 2019, asilimia 33 ya mikopo iliyotolewa katika vikundi vya wanawake na Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilienda kwa wanawake.

Mheshimiwa Spika, vilevile, benki za *NMB* na Azania zimeanzisha madirisha maalum ya kutoa mikopo kwa vikundi vinavyojishughulisha na kilimo na miradi mbalimbali. Pia Serikali imehamisisha wanawake kujiunga kwenye vikundi vya ushirika wa akiba na mikopo kama *SACCOS*, *VICOBA* ili kupata huduma za kifedha na mikopo kwa urahisi ili kuongeza mitaji yao katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeuelekeza Mfuko wa Pembejeo za kilimo kutoa kipaumbele kwa vikundi vya wanawake vinavyoomba mikopo ya kuendeleza kilimo. Vilevile, Serikali imeendelea kutoa hatimiliki za ardhi za kimila na hatimiliki za ardhi za muda mrefu kwa ajili ya kuwawezesha wanawake kumiliki ardhi na kuzitumia hati hizo kama dhamana, kukopa katika Taasisi mbalimbali za kifedha ili

waweze kupata mitaji ya kununua pembejeo na zana bora za kilimo ili kuongeza uzalishaji, tija na kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya usindikaji wa mazao kwa kuongeza tija na vipato vyao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Rymond, nimekuona.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Awali ya yote, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na nimeyapokea.

Swali la kwanza; kwa kuwa Benki ya Kilimo mpaka sasa haijaweza kuwa katika Mikoa yote na hizo benki nyingine alizozitungumzia kama *MMB* na alitaja benki mbili zote hizo ni *Commercial* na zinahitaji wewe unayekwenda kukopa lazima uwe na dhamana na wanawake wengi hawana nyumba wala hawana dhamana ambazo zinatambulika kibenki: Je, Serikali iko tayari ku-*guarantee* mikopo hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Tatizo katika kilimo ni pamoja na mbegu bora na mara nyingi unakuta kwamba mbegu hizo ni ghari na pia siyo rahisi kumfikia mkulima. Ni lini sasa mbegu hizo zitagaiwa kwa wanawake hao kupitia katika Kata zao? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Swali la kwanza la Mheshimiwa Shally Rymond anataka kujua kwamba kwa sababu benki ya Maendeleo ya Kilimo haipo kila Mkoa na kwamba hizi benki nyingine ni za kibiashara, anataka kujua mikakati ya Serikali kama iko tayari kudhamini mikopo hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali tupo tayari na tulishaanza na ndiyo maana kama alivyosema Benki ya Maendeleo ya Kilimo haipo kila Mkoa, ni kwa sababu hii ni

Benki ya Maendeleo, ni benki ya kimkakati na lengo lake ni kuwasaidia wakulima kupitia madirisha mbalimbali ya Taasisi za Fedha.

Moja, tulichokifanya, Serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo tumedhamini mikopo yote ambayo inayotolewa na Benki ya *NMB* ili kwenda kwenye Sekta ya Kilimo hususan pamoja na akina mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba ni lini Serikali itatengeneza mazingira ya mbegu hizi zikapatikana katika ngazi za Kata ili wanawake wazipate kiurahisi?

Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba Serikali siku zote kwamba tuko tayari. Mbegu hizi kupitia Shirika letu la Mbegu (*ASA*) na Taasisi nyingine binafsi na mawakala mbalimbali, tumeweka mazingira mazuri kwamba mbegu hizi zinapatikana Tanzania kote, siyo kwa kwenye Kata tu, mpaka ngazi za vijiji kwa kuzingatia mahitaji. Kama kuna mahitaji maalum katika eneo unalotoka, baada ya Bunge hili tuone ili tuwaelekeze wenzetu wa *ASA* ili waweze kupeleka mbegu haraka iwezekanavyo ziwafikie wakulima.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ukiacha Taasisi nyingi kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake lakini Benki ya Kilimo ndiyo yenye dhamana ya kutoa mikopo. Benki ya Kilimo imekuwa na tabia ya ubaguzi, inatoa mikopo kwa wale wanawake ambao wana uwezo au wake za vigogo, lakini wale wanawake ambao wana uwezo mdogo na wamejiunga kwenye vikundi wamekuwa wakipewa masharti magumu.

Je, Serikali inatoa kauli gani hususan kwa wanawake wa Ulanga, Kilimanjaro na juzi nilikuwa Mbeya kule, hamna hata mmoja aliyepata mkopo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya tuhuma hiyo nzito, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):**

Mheshimiwa Spika, nashukuru. Napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mlinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza siyo kweli kama Serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo tunatoa mikopo kwa kibaguzi. Hii kama nilivyosema ni benki ya maendeleo, ni benki ya kimakakati na tumeianzisha maalum kwa ajili ya kuendeleza sekta ya kilimo hapa nchini. Kwa hiyo hizi ni pesa za umma, kama pesa za umma lazima zina taratibu zake na zina masharti. Labda hao wanaoona wanapata maana yake ni wanawake waliotimiza vigezo vinavyohitajika na benki ili waweze kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niendeleo kumshauri kama nilivyosema kwenye jibu letu la msingi, tumewaelekeza wanawake hao hususani wale wa vijijini wajunge kwenye vikundi, vile vikundi vyao ndiyo vitatumika kama dhamana na benki hii itaendelea kutoa mikopo. Hivi ninavyozungumza, pamoja na maelekezo ya Serikali tuliwaambia kwamba mikopo wanayotoa asilimia 20 watoe kwa akinamama, lakini benki hii imeweza kutoa mpaka leo tunavyozungumzia zaidi ya asilimia 33 ya mikopo yote waliyotoa imekwenda kwa akinamama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe nilikuona tafadhali.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwenye Wizara ya Kilimo. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo mwaka juzi walianzisha utaratibu wa kwamba zao la korosho lilimwe katika kila mkoa hapa Tanzania kwenye mikoa 17. Wakati wa uhamasishaji huo, wakawahamasisha pia akinamama wengi sana kwenye Wilaya ya Masasi, Wilaya ya Tandahimba ikiwemo pamoja na Newala, Lulindi pamoja na Ruangwa wakope pesa kwenye mabanki lakini pia walikopeshwa pesa pamoja na Halmashauri. Sasa bahati mbya sana mpaka sasa hivi Serikali haijalipa pesa hizo za hao akinamama na wameanza kutaifishwa, kufilisiwa na wanashindwa kufanya shughuli zao na hapa tunasema tunataka tuwawezeshe

akinamama. Sasa nataka tusikie kauli ya Serikali, je, ni lini watawalipa akinamama hao waliozalisha miche iliyopeleka mikoa mingine 17 pesa zao?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mwambe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli Serikali miaka yote tuna mradi wa kuongeza uzalishaji wa korosho hapa nchini kutoka tani 300,000 za sasa kwenda tani milioni moja ndani ya miaka mitano ijayo.

Kwa hiyo miongoni mwa miradi hiyo lazima tulikuwa tuongeze eneo la uzalishaji na moja ya mikakati ilikuwa kwamba kuzalisha miche zaidi ya milioni 10 kwa kila mwaka kwa muda wa miaka hiyo mitatu. Pia ni kweli kwamba miche hii ilizalishwa kwa vikundi mbalimbali vya akinamama na vijana, lakini baada ya kupitia yale madeni, tumegundua kwamba kuna kasoro nyingi katika yale madeni.

Mheshimiwa Spika, kama ninavyosema siku zote kwamba hizi ni pesa za umma, kama Serikali tuliona ni busara kwamba tufanye uhakiki wa kina ili tujue, tubainishe na kutambua yapi madai halali na yapi madai yaliyopikwa ili wale halali waweze kulipwa. Niendeleo kumsihi tu Mheshimiwa Mwambe na wengine wote waendeleo kuvuta subira, jambo hili karibu linafika mwisho, timu ya uchunguzi iko katika hatua za mwisho kumaliza, tukimaliza hela zipo na tutawalipa wote waliozalisha miche hii.

**SPIKA:** Sijui utaratibu huo utaendelea au hautaendelea. Mheshimiwa Mama Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-



Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto wanayoipata wakulima wakiwemo Wanawake hasa wanaolima tumbaku ni upatikanaji wa pembejeo kwa wakati hususan mbolea aina ya *NPK*.

Je, Serikali inawahakikishiaje wakulima wa tumbaku kwamba watapata mbolea ya *NPK* kabla ya mwezi wa Nane mwaka huu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu sana la mbolea ya *NPK*.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Sitta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli yaani mwaka jana mbolea zilichelewa kufika kwa wakulima na sababu ndiyo mwaka wa kwanza ambao tulikuwa tunatekeleza ule mfumo wa *bulk procurement* (uagizaji wa mbolea kwa pamoja) na kitu chochote kikiwa cha kwanza lazima kina changamoto zake. Tumeona hizo changamoto, lakini mwaka huu ambao mchakato wa kufahamu kiwango cha uzalishaji na mahitaji ya mbolea tumeshakifanya mapema na tayari sasa hivi watu tuko kwenye mchakato wa kupata Mawakala wa kuagiza hizo mbolea na vyama vyenyewe tumevipa ruhusa ya kuagiza. Kwa hiyo, hilo tatizo mwaka huu halitakuwepo na mbolea zitafika kwa wakati kwa wakulima wa tumbaku na hasa akinamama wa Tabora.

**SPIKA:** Nashukuru. Sasa tuendelee na Wizara ya Nishati. Swali la Mheshimiwa Daimu Idd Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini. Mheshimiwa Mpakate uliza swali lako.

Na. 192

**Umeme wa REA Katika Vijiji 61- Tunduru Kusini**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Jimbo la Tunduru Kusini lina jumla ya vijiji 65, kati ya hivyo ni vijiji vinne tu ndiyo vimefikiwa na umeme wa REA Awamu ya I na ya II:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa REA katika vijiji 61 vilivyobaki?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Subira Mgalu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Idd Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inatekeleza miradi ya kusambaza umeme katika vijiji vyote nchini. Jimbo la Tunduru Kusini lina vijiji 65, kati ya vijiji hivyo Vijiji vinne vya Azimio, Chiwana, Mkandu na Mbesa ndivyo vimekwishapata umeme kupitia mradi wa REA II na Vijiji vingine vinne vya Mchuluka, Umoja, Masalau na Msinjini vinatarajiwa kupatiwa umeme kupitia mradi wa REA III mzunguko wa kwanza unaoendelea na unaotegemea kukamilika mwezi Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupeleka umeme katika Jimbo la Tunduru Kusini inahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa *kilovolt* 33 yenye urefu wa kilometa 9.4, ujenzi wa njia ya msongo wa umeme wa *kilovolts* 0.4 yenye urefu wa kilometa nane, ufungaji wa transfoma nne za KVA 50 pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 275. Gharama za kupeleka umeme katika vijiji hivyo ni shilingi milioni 644.

Mheshimiwa Spika, vijiji 57 vya Kata za Chiwana, Mchuluka, Mtina, Nalasi, Mchoteka, Ligoma, Tuwemacho na Lukumbulu vitapatiwa umeme kupitia Mradi wa REA Awamu ya III, mzunguko wa pili unaotarajiwa kuanza mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2021. ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpakate tafadhali, nimekuona swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Katika Vijiji alivyovitaja kuwa vilipata umeme awamu ya kwanza na ya pili vya Azimio, Chiwana, Mkandu na Mbesa umeme ulipita barabarani ndani ya mita 100 kutoka barabara kuu ilikopita nguzo kubwa. Je, ni lini mradi wa kujazilizia mitaa iliyobaki katika Vijiji hivyo vya Azimio, Chwana, Mkandu na Kijiji cha Airport itanza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mwaka 2017 nilipeleka maombi maalum kungeza vijiji katika Mradi wa *REA* katika Vijiji vya Tuwemacho, Chemchem, Ligoma, Makoteni, Nasia, Semeni, Mtina, Angalia, Nalasi, Mchoteka, Kitani, Mkolola pamoja na Masakata. Nini kauli ya Serikali kuhusu uwekaji wa awamu ya tatu ya umeme katika Vijiji hivyo?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu. Namwona Mheshimiwa Waziri amesimama, Mheshimiwa Waziri, tafadhali.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali la msingi la Mheshimiwa Mpakate, lakini vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mpakate jinsi anavyofuatilia umeme katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, ni kweli vijiji vingi tuliviweka kwenye *round II* ya awamu ya tatu inayoendelea, lakini baada ya kuona changamoto kubwa sana katika Jimbo la Tunduru Kusini tulifanya mapitio mapya na vijiji 13 tuliviingiza kwenye *round* inayoendelea. Kwa hiyo katika utaratibu tunaajenga *line* kwa sasa kutoka Tunduru Mjini mpaka Msingi umbali wa kilometa 20 tumechukua vijiji vingine 13 vikiwemo vijiji ambavyo anavisema vya Angalia, Semeni ambako Mheshimiwa Mbunge anatoka lakini mpaka Tuwemacho, Chemchem mpaka Chilundundu kwa vijiji vyote hivyo viko

kwenye mpango. Pia Wakandarasi kupitia *TANESCO* sasa wanavifanyia kazi, kwa hiyo nimpe tu taarifa Mheshimiwa Mbunge pamoja na kumpongeza, vijiji 13 vya nyongeza tayari vimeshaanza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu nyongeza ya vijiji vya ujazilizi; mradi umeshaanza na utekelezaji wa maeneo ya kujaziliza, maeneo ya vitongoji unanza mwezi huu utachukua miezi 12, lakini maeneo ya Azimio pamoja na Mbesa ambako tayari umeme upo kwenye Vitongoji 17, tayari pia *TANESCO* wameanza kuvifanyia kazi.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Huu mradi wa kujaziliza ni muhimu mno maana yako maeneo yenye makosa mengi mno yanahitaji kusahihishwa.

Nilikuona Mheshimiwa Monko, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Jimbo la Singida Kaskazini lina miradi ya *REA II, REA III, phase I* pamoja na umeme wa *backbone* kwenye vijiji 54. Hadi sasa ni vijiji 13 tu ndiyo ambavyo vimekwishakufikiwa na umeme na vingine mpaka sasa bado. Je, Mheshimiwa Waziri wa Nishati yuko tayari kuambatana nami kutembelea Jimbo la Singida Kaskazini kujionea changamoto zilizopo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Subira Mgalu uko tayari kwenda Singida Kaskazini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Monko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Monko amerejea Mradi wa *REA* awamu ya pili ambapo kwa kweli kama Serikali tuliwaomba radhi wakazi wa Mkoa wa Singida na Kilimanjaro baada ya makosa ambayo yalitendeka katika Mradi wa *REA* awamu ya pili na tukafanya kazi na kumweka Mkandarasi mpya ambaye anaendelea na kazi kwa kushirikiana na *REA*.

Mheshimiwa Spika, swali lake ameulizia utayari wetu wa kuambatana naye; nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge nipo tayari mimi pamoja na Waziri kwa wakati tofuati kutembelea Jimbo lake kama ambavyo tulishafanya mwezi wa Nane tulitemebelea Jimbo lake ikiwemo Kijiji cha Iddi Simba na tuliwasha umeme pia aliwakilishwa na Mheshimiwa Mbunge Aisharose Matembe. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge niko tayari muda wowote kutembelea eneo lake na kuendelea kuwasha umeme na kukagua kazi inavyoendelea. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nawaona Waheshimiwa masuala ya umeme mnayo mengi, lakini niwaombe tu tuvumiliane kidogo kwa sababu muda uliobakia ni mdogo sana.

Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini, kwa niaba yake Mheshimiwa Esther Matiko, tafadhali muulizie.

Na. 193

**Malipo ya Fidia Kwa Wananchi wa Kijiji cha Nyabeu,  
Wilaya ya Bunda**

**MHE. ESTHER N. MATIKO (K.n.y. MHE. ESTER A. BULAYA)**  
aliuliza:-

*TANESCO* Mkoa wa Mara katika zoezi la kupeleka umeme vijijini walipitisha nguzo za umeme kwenye maeneo ya watu katika Kijiji cha Nyabeu, Kata ya Guta na uthamini ulifanyika na iliahidi malipo kufanyika lakini hadi leo hawajalipwa na badala yake wanaambiwa maeneo hayo ni ya *TANESCO*:-

(a) Je, ni lini Serikali itawalipa wananchi hao fidia stahiki?

(b) Je, ni kwa nini *TANESCO* inamiliki maeneo kabla ya kulipa fidia?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi ya kupeleka umeme katika Wilaya za Serengeti, Bunda na Ukerewe ilitekelezwa kati ya mwaka 2003 na 2006 chini ya ufadhili za Serikali za Sweden na Hispania kupitia Mashirika yake ya Kimataifa ya Maendeleo *SIDA* na *Spanish Funding Agency* pamoja na Serikali ya Tanzania. Kazi ya tathmini ya mali za wananchi waliopisha mradi ilifanywa na Mtathmini Mkuu wa Serikali na malipo yalifanyika mwaka 2009. Ulipaji wa fidia hiyo ulifanyika kwa kuwashirikisha Watendaji wa Vijiji, Kata, Tarafa, Wilaya na Mkoa kuridhia orodha ya wananchi waliostahili kulipwa fidia hiyo. Jumla ya Sh.135,820,993 zililipwa kwa wananchi waliopisha mradi huo ikiwa ni pamoja na wananchi wa Kijiji cha Nyabeu.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* huchukua maeneo baada ya kufanya tathmini kupitia Mthamini Mkuu wa Serikali na kuwalipa wananchi wanaopisha ujenzi wa mradi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa sasa tunajua kwamba tuna mradi wa *REA* ambao ndiyo umejielekeza kupeleka umeme vijijini. Katika Kijiji cha Sazira katika Jimbo la Bunda Mjini ambalo lina Vitongoji vitatu cha Nyamungu, Wisegere na Kinamo havijawahi kupitiwa na mradi huu wa *REA phase I, phase II* na hata *phase III*. Sasa ningependa kujua hawa wananchi wa Kijiji cha Sazira ni lini watapatiwa umeme ili na wenyewe waweze kupata umeme katika shughuli zao za kimaendeleo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; katika Mji wa Tarime pia tumepitiwa na umeme wa *REA* ambao unapita kwenye aidha Kijiji sehemu ndogo tu au kata. Ningependa kujua maeneo ambayo yana Taasisi kama sekondari, zahanati au vituo vya afya na shule ya msingi kama vile Kitale tuna Kijiji cha Nkongole ambacho kina hizo Taasisi zote, Kenyamanyori Senta tuna Kibaga ambayo ina mgodi pale haijapitiwa na umeme wa *REA*. Ni lini sasa Serikali itahakikisha kwamba inapeleka huu umeme wa *REA* kwenye yale maeneo ambayo hayajaguswa kabisa na Mheshimiwa Naibu Waziri aliniahidi kwamba ungeweza kwenda Tarime kujihakikishia hayo maeneo ambayo kila siku nayauliza hapa? Ahsante.

**SPIKA:** Kwenda Tarime inabidi apate ruhusa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu maana kule Tarime ni Kanda maalum. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ameulizia Kijiji cha Sazira ambacho kipo Bunda Mjini ambacho kina vitongoji vitatu na hakina umeme. Kama ambavyo tumepata kujibu maswali hapa ya msingi kwamba mpango wa Serikali ni kupeleka umeme vijiji vyote. Kwa sasa tuna mradi huu unaoendelea wa *REA* awamu ya tatu ambao unahusisha vijiji 3,559 lakini ukichanganya na miradi mingine yote ya Ujazilizi, *BTIP* tunatarajia kufikisha umeme ifikapo Julai, 2020 kwa vijiji 9,299.

Kwa hiyo kijiji ambacho amekitaja kwenye Wilaya ya Bunda Mjini hapo vipo katika mpango wa *REA* awamu ya tatu, mzunguko wa pili ambao utaanza Julai, 2019 na kukamilika 2021. Kwa hiyo niwatoe hofu tu wananchi wote nchi nzima, mpango wa Serikali ya Awamu ya Tano ni kupeleka umeme katika vijiji vyote nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ameulizia suala la Jimbo lake la Tarime; ni kweli niliahidi kutembelea Jimbo hilo

kama utaratibu wetu ndani ya Wizara, lakini nitazingatia angalizo lako kwamba kwa ruhusa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini nimtoe hofu tu Mheshimiwa Esther kwamba katika maeneo ambayo ameyataja na hasa Taasisi za Umma, Wizara imetoa maelekezo mahususi na naendelea kurejea hayo maelekezo kwamba Taasisi za umma ni moja ya kipaumbele katika kuzipelekea umeme iwe shule ya msingi, sekondari, kituo cha afya au miradi ya maji.

Kwa hiyo naomba niwaelekeze Wakandarasi kuzingatia maelekezo hayo na Mameneja wote wa *TANESCO* na wasimamizi wa miradi hii ya *REA* kwamba umeme ufikishwe kwenye Taasisi za Umma ili kuboresha utoaji wa huduma ambazo zinatokana na hizo Taasisi za umma.

Mheshimiwa Spika, katika haya maeneo aliyoyasema Mheshimiwa kwanza mojawapo lipo katika *REA* awamu ya tatu, mradi unaoendelea na Mkandraso Derm yupo, anaendelea vizuri na ni moja wa Wakandarasi ambao kwa kweli wanafanya kazi vizuri na nimhakikishie tu mpaka Juni, 2019 hii miradi itakuwa imekamilika. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Maji, swali la Mheshimiwa Peter Ambrose Lijualikali, tafadhali uliza swali lako.

Na.194

### **Kufuta Kodi za Vifaa vya Kusambaza Maji**

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali isifute kodi kwenye vifaa vya kusambazia maji kutokana na matatizo ya maji tuliyonayo katika Taifa letu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Jumaa Hamidu Awesu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-



Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Peter Ambrose Lijualikali, Mbunge wa Jimbo la Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 12 Septemba, 2017, Bunge lako Tukufu lilipitisha marekebisho ya Sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148. Marekebisho ya Sheria hiyo ya VAT yalihusisha vifungu vya 6 na 7 pamoja na aya ya 9 ya sehemu ya pili ya Jedwali la Sheria ya VAT ambayo vina lengo la kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kuongeza tija ya matumizi ya fedha za umma na kuhakikisha miradi inayotekelezwa kwa fedha za Serikali na za washirika wa maendeleo inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji tayari imeshasambaza Waraka wa Hazina namba sita uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu utaratibu wa kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa miradi ya maji itakayotekelezwa kote nchini. Ni wajibu kwa Maafisa Masuuli wote kuzingatia utaratibu ulioainishwa na Serikali katika misamaha ya kodi kwa vifaa vya kusambazia maji ili miradi yetu ya maji ikamilike kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lijualikali.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Spika, nafahamu Serikali imetoa msamaha wa kodi kwenye miradi yake lakini natamani nifahamu ni kwa nini sasa miradi ya watu binafsi wanaofanya kazi hii wenyewe hawapati misamaha? Maana yangu ni kwa nini kwenye vifaa vingine watu wanaofanya kazi hizi hawapati misamaha ya kodi ili kusaidia Serikali kupeleka huduma hii? Msamaha huu ungekuwa *inclusive* yaani usiwe tu kwa watu wanaofanya kazi Serikali peke yake. Kwa hiyo, napenda kufahamu ni kwa nini watu wengine pia hawapati misamaha huo?

Mheshimiwa Spika, pia naomba nifahamu kama Mheshimiwa Waziri atakubali kwenda nami sambamba kwenye Jimbo langu hasa kwenye Kata za Kipangalala na

Kibaoni ambako kuna miradi mikubwa ya maji ya takribani shilingi milioni 600 lakini ni kama vile imesimama na fedha hizi ni kama zimelala. Kwa hiyo, naomba nifahamu *commitment* ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu anafahamu haya mambo nilishakaa naye ofisini kwake na kuzungumza kwa kirefu.

Kwa hiyo, naomba nijue kama yuko tayari twende Jimboni kwangu ili tukaone nini shida na tupate majibu kwenye mambo haya. Nashukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri lakini kubwa sisi kama Wizara ya Maji lengo letu na nia ya Mheshimiwa Rais ni kumtua mwana mama ndoo kichwani na kuhakikisha Watanzania waishio mijini na vijijini wanapata maji safi salama na yenye kuwatosheleza. Kwa mazingatio na ushauri wako niseme tu kwamba tumepokea ushauri na tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *commitment* ya mimi kuongozana naye katika Jimbo lake, Mheshimiwa Lijualikali mimi sina kikwazo chochote, nipo tayari kuhakikisha tunakagua miradi ya maji. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Mshimba Jechauliza swali lako la mifugo na uvuvi.

Na. 195

### **Kufaidika na Ukanda wa Bahari na Maziwa**

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA** aliuliza:-

Tanzania imebarikiwa kuwa na Ukanda wa Bahari na Maziwa.

Je, wananchi wa maeneo hayo wameandaliwaje kufaidika na rasilimali zinazopatikana katika Ukanda wa Bahari na Maziwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ulega, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sekta ya uvuvi nchini inasimiwa na sera, sheria pamoja na miongozo mbalimbali iliyoandaliwa kwa lengo la kuhakikishwa wananchi na Taifa linanufaika na rasilimali za uvuvi. Pia Sera ya Uvuvi inaelekeza ushirikishwaji wa wananchi katika kusimamia rasilimali za uvuvi ambapo vimeanzishwa vikundi vya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi kwa maana ya BMU. Vikundi hivi vinalenga kuwawezesha wananchi katika maeneo vilipoanzishwa kuwa wanufaikaji wa kwanza wa rasilimali hizi kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya uvuvi endelevu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha Wakala wa Mafunzo ya Uvuvi ili kuwapatia elimu vijana wa Kitanzania kuhusu masuala ya uvuvi ili nchi inufaike na rasilimali za uvuvi tulizojaliwa. Pia, Serikali imeanzisha Taasisi ya Utafiti yaani TAFIRI ili kufanya tafiti na kuvumbua teknolojia zitakazosaidia kuleta tija kwenye tasnia ya uvuvi. Taasisi hizi husaidia kuwapatia elimu na maarifa wadau wa uvuvi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara ina mikakati mbalimbali inayolenga kuleta maendeleo katika sekta ya uvuvi na kuwasaidia wavuvi ambayo ni pamoja na:-

(i) Kuendelea kutoa elimu kwa wavuvi na wadau wote kuhusu uvuvi endelevu, sera, sheria na kanuni za uvuvi ili kulinda, kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za uvuvi nchini kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo;

(ii) Kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu kwa kufufua Shirika la Uvuvi (TAFICO), kujenga bandari ya uvuvi, kununua meli mbili kubwa za uvuvi ili kuchochea ukuaji wa viwanda vya kuchakata samaki, kuongeza thamani ya mazao, ajira na kuongeza mapato ya Serikali; na

(iii) Serikali itaendelea kutoa elimu kwa wavuvi kuhusu ukuzaji wa viumbe katika maji yaani *aquaculture* na ufugaji samaki kwenye vizimba kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa samaki kwenye maziwa na baharini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeanzisha Dawati la Sekta Binafsi ili kuwasaidia wavuvi kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili ikiwemo kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha nimekuona, uliza swali lako.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina suala moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mipango mizuri ya Serikali lakini bado wavuvi wana hali ngumu, uduni wa vifaa, utaalum na kadhalika. Je, ni lini Serikali itaanzisha vyuo vya uvuvi vingine kwa sababu navyofahamu chuo kilichopo ni kimoja tu lakini hata wahitimu wake hawapati nafasi ya kuajiriwa pamoja na kwamba tumezungukwa na ukanda mkubwa wa bahari na maziwa. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwatumia wataalam wanaomaliza katika chuo hicho lakini pia kuanzisha vyuo vingine kwa lengo la kuwanyanyua wavuvi ili waweze kuwa na tija na bahari na maziwa? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mazuri kabisa, Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili mazuri sana ya

nyongeza ya Mama yangu Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali tunao mpango wa kuhakikisha tunafungua vyo vingine. Hapa karibuni tumefungua chuo cha uvuvi katika Mikoa ya Kusini kwa maana ya Mtwara Mikindani, Chuo cha FETA ambacho kinafanya kazi ya kutoa elimu. Mipango mingine ya Serikali ni pamoja na kuboresha chuo chetu kilichopo pale Pangani maarufu kama KIM kwa kushirikiana na Taasisi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Halmashauri ya Pangani kwa lengo la kuhakikisha wananchi hasa vijana walio wengi wa maeneo haya ya ukanda wa bahari wanapata elimu. Kwa upande wa Ziwa Victoria chuo chetu kilichopo katika Wilaya ya Rorya pale Gabimori na chenye tunakwenda kukiongezea nguvu ili kusudi kitoa elimu zaidi kwa wananchi wengi wa maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ameuliza mipango yetu tuliyonayo ya kuhakikisha wale wataalam wanaotoka katika vyo hivi wanakwenda kupata kazi na kuisaidia jamii yetu. Katika majibu yangu ya msingi nimeeleza kuwa Serikali inao mpango wa kufufua Shirika letu la Uvuvi la *TAFICO* na tayari tumeshalifufua, hivi sasa tunakwenda katika hatua ya kununua meli. Tayari tumepata msaada kwa maana ya *grants* kutoka Serikali ya Japan wa takribani bilioni nne ambazo tunakwenda kununua meli na kutengeneza miundombinu ya kuhifadhia samaki katika eneo la ukanda wa pwani. Hii ni chachu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wale wengi wenye utaalam wataajiriwa na mashirika haya.

Vilevile tunao mpango wa kuhakikisha wanajajiri wao wenyewe kwa kufanya kazi za uvuvi endelevu wa kisasa na vilevile ufugaji wa samaki.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Dau, uliza swali lako.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini Serikali sasa itahakikisha kwamba bandari ya uvuvi

inajengwa ili fursa ya uvuvi wa bahari kuu iweze kutumika vizuri sana? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu kutoka kwa Mbunge wa Mafia, Mheshimiwa Dau, bandari ya uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la ndugu yangu Mbunge wa Mafia, jirani yangu, Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni lini bandari itajengwa. Hivi sasa tuko katika kumaliza mchakato wa upembuzi yakinifu wa eneo itakapokwenda kujengwa bandari ya uvuvi. Tayari mkandarasi huyu kupitia pesa zetu wenyewe, pesa za ndani tumeshamlipa na anamalizia kazi ya kutuelekeza mahali gani katika ukanda wetu wa pwani tutakwenda kujenga bandari ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, habari njema zaidi, nadhani wote tumemsikia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alipokuwa katika Mei Mosi pale Mbeya ameeleza juu ya nia njema ya nchi rafiki ya Korea ambapo wameonesha nia ya kutaka kushirikiana nasi katika kwenda kujenga bandari hii ya uvuvi.

Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania kwa ujumla kwamba nia yetu hii itakwenda kutimia na hatimaye kuweza kupata faida ya uvuvi katika eneo la bahari kuu.

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, tuendeleo na matangazo.

Naomba niwatambulisha wageni 20 wa Mheshimiwa Spika ambao ni wanachana wa Chama cha Wanasayansi wa Maabara za Afya hapa nchini wakiongozwa na Rais wa Chama hicho Ndugu Yahya Mnung' a. Wanamaabara karibuni sana wageni wetu hapa Bungeni. *(Makofi)*

Wamekuwa na maonesho yao pale Nyerere *Square*, Waheshimiwa Wabunge tunakaribishwa kushiriki pale tujifunze mambo mbalimbali na *advancement* ya masuala ya maabara za afya hapa Tanzania. Tukipita mjini katikati pale tupitie pale Nyerere *Square* tuone shughuli zao zinazoendelea pale. Ahsante sana ndugu zangu wa maabara. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni pamoja na mgeni wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Waziri wa Kilimo ambaye ni mpiga kura wake kutoka Vwawa Mkoani Songwe, Ndugu Agripa Mwashambwa. Karibu sana Agripa. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Mwita Waitara, Naibu Waziri wa TAMISEMI ambaye ni Mbunge Mstaafu kutoka Rorya Mkoani Mara, Ndugu Gregori Mogendi. Karibu sana Mbunge Mstaafu Mogendi. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Waheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambao ni ndugu zake kutoka Dar es Salaam na Tanga wakiongozwa na msanii Ndugu Thadei Onesmo. Sina hakiki kama na Ndugu Nurdin Ally naye yupo, kama yupo karibuni sana, msanii maarufu huyo. Ahsante sana. (*Makofi*)

Wageni 61 wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambao ni wanafunzi 57 na walimu wanne wa *Real Hope Secondary School* kutoka Mafinga Mkoani Iringa wakiongozwa na Mkurugenzi wa shule hiyo Ndugu Dickson Mwipopo. Aisee, hii shule ya *Hope* Mafinga inaelekea ni moja ya shule nzuri sana. Naona vijana mko *smart* kabisa. Hongereni sana na karibuni sana hapa Bungeni. (*Makofi*)

Kwa kweli haishangazi kuona Iringa kule kuna shule nzuri namna hii, kabisa. Maana nilikuwa namuona Mheshimiwa Lukuvi leo, Mheshimiwa Cosato Chumi na Wabunge wengine wa Mkoa wa Iringa tumekutana nao asubuhi wananisalimia wanasema Kamwene, Kamwene, nikasema nini tena? Nikaelewa tu ni yale mambo yale, Iringa bwana hakuna mchezo. Kama hamuamini Iringa wako moto

waulizeni Yanga. Yanga bwana, sijui baridi ya Iringa inawafanyaje? *(Makofi/Kicheko)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Rose Tweve ambao ni wanakwaya wa Tanzania *Assemblies of God* kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kwaya hiyo Ndugu Happy Mwajunga. Karibuni sana kutoka TAG Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa John Kadutu ambaye ni mtoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Peter Kadutu. Karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambaye ni mpwa wake kutoka Mang'ula Mkoani Morogoro, Ndugu Mikidadi Kilwanda. Karibu Mikidadi. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka ambao ni Maafisa wa Umoja wa Mataifa kutoka Geneva Uswisi, Eng. Wilhelmina Malima, Dkt. Simon Msukwa na Eng. Upendo Kimaro. Wale pale karibuni sana kutoka huko Geneva. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Esther Matiko ambao ni wapiga kura wake kutoka Tarime, Ndugu John Maganga na Ndugu Saimon Chacha. Karibuni sana wageni kutoka Isiebania huko. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Kassim Jamal ambao ni wadau wa afya ya uzazi wa mpango na afya kwa ujumla kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Salvatory Hokororo. Karibu sana Hokororo. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 22 na walimu wanne kutoka Shule ya Awali na Msingi ya *Aglam* iliyopo Wilayani Mpwapwa, Mkoa wa Dodoma ambao wamelitembelea Bunge kujifunza jinsi linavyofanya kazi zake. Wale wa kutoka Mpwapwa, karibuni sana na Mbunge wenu Mheshimiwa Lubeleje yuko hapa. *(Makofi)*



Wale msiofahamu Mpwapwa ni Kiswahili lakini jina lenyewe kabisa panaitwa Mhanvwa. Kwa hiyo, karibuni sana wageni wetu kutoka Mhanvwa. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wanne kutoka Benki ya *CRDB*, tawi la Dodoma ambao ni Mameneja Mahusiano kuhusiana na wateja maalum wakiongozwa na Meneja wetu maarufu Agusta Mfuru. *CRDB* pale mlipo karibuni sana, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

*CRDB* makofi hayo ni kwa ajili ya Grace kwa huduma zako nzuri. Tunaomba timu iliyotoka Makao Makuu mpeleke salamu za Wabunge kwa uongozi wa *CRDB* kwa kazi nzuri anayofanya Grace. Anastahili kupandishwa cheo, ni mfanyakazi bora kwa makofi haya. *(Makofi/Vigelegele)*

Pia Grace anawataarifu kwamba *credit cards* mpya za *CRDB* mpitie kule muweze kuzipata. Za hivi sasa ni matata kabisa. Kwa hiyo, mpitie huko muweze kuchukua kadi zenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mawili, tangazo la kwanza, baadhi yetu hatuko makini kidogo na matumizi ya bendera za Wabunge, zile zinazopepea kwenye magari. Yamepatikana baadhi ya magari yakipuyanga huko mikoani yana bendera ya Mbunge lakini hata Mbunge mwenyewe hayupmo ndani ya gari. Sasa vitu hivyo vinaweza kukuletea matatizo tu bure, matumizi ya bendera yanaenda kisheria na yana taratibu zake. Hilo gari lako linaweza kupatikana na magendo huko na lina bendera yako likakuharibia kabisa mfumo na mpangilio wako wa maisha. Kwa hiyo, naomba tuwe makini sana na matumizi ya bendera hizo.

Waheshimiwa Wabunge, lakini bendera zingine zinatundikwa kwenye magari ambayo hayana hata hadhi, kule Afrika Kusini wanaita Skorokoro. Wewe gari mkweche ina bendera ya Mbunge, kweli, si uache tu kwani kuna hside gani? Wewe mwenyewe umekaa pale kigari kinakwenda hakieleweki na hasa rafiki zangu fulani sitaki kuwataja. Kwa

hiyo, tujitahidi bendera iende na hadhi yako mwenyewe na chombo chenyewe pia, tuangalie jambo hili ni muhimu sana. *(Makofi/kicheko)*

Pia nina tangazo la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Moore hapa Bungeni, anasema leo Jumatano tarehe 8 Mei kutakuwa na Ibada ya Misa ya Wakristo Wakatoliki mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana pale Pius Msekwa, ghorofa ya pili ambapo huwa mnakutana. Mnaopenda kwenda kwenye Ibada hiyo basi mfanye hivyo. Leo Jumatano Wakatoliki Msekwa, ghorofa ya pili muweze kukutana.

Baada ya matangazo haya, naomba sasa nimpishe Mheshimiwa Naibu Spika ili aweze kuendelea na ratiba zilizoko hapa mezani.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutaendelea.

Katibu!

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya,  
Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka  
wa Fedha 2019/2020**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Anna Tibajjuka, Mheshimiwa Anna Gidarya ajiandae.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ili niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Afya. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya katika nchi hii ya kutoa huduma za afya kwa Wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili naiunga mkono hoja hii asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni ujenzi wa zahanati pamoja na Vituo vya Afya. wananchi wamehamasika wanajenga Vituo vya Afya, wanajenga zahanati kila kijiji. Lakini changamoto kubwa ambayo tunayo pamoja na ujenzi wa zahanati na Vituo vya Afya changamoto ambayo inatukabili ni upungufu wa watumishi wa Idara ya Afya kada mbalimbali. Kwa hiyo, nilikuwa naishauri Serikali iongeze watumishi katika vituo vya afya, zahanati pamoja na hospitali za wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya ilikuwa na mpango wa kujenga vyuo kwa ajili ya ku-*train* wahudumu wa afya, kwa mfano matabibu, hawa *clinical officers* pamoja na tabibu wasaidizi (*clinical assistants*), sasa mpango huu uliishia wapi? Kwa sababu, ilikuwa ndio mikakati ya Wizara hii ili kuongeza watumishi katika vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusu Bohari ya Dawa – *MSD*. Bohari ya Dawa – *MSD* inafanya kazi nzuri sana; Bohari ya Dawa ndiyo inayosambaza dawa nchi nzima, vituo vya afya, zahanati, hospitali za wilaya, hospitali za mikoa, hospitali za rufaa. Lakini pamoja na kuongeza fedha za dawa katika bohari ya dawa bado changamoto hiyo inaikabili bohari ya dawa. Sasa Mheshimiwa Waziri je, mwaka huu mmeongeza fedha kiasi gani kwa ajili ya bohari ya dawa kwa sababu, zahanati zinaongezeka, vituo vya afya vinaongezeka, lakini dawa ni zilezile? Sanduku moja la dawa halitoshi kwenye zahanati kwa sababu, sasa kuna ongezeko kubwa sana la wananchi. kwa hiyo, je, mwaka huu mmeongeza fedha kiasi gani kwa ajili ya bohari ya dawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, ni kuhusu vyuo vya maafisa afya. Mpwapwa kuna chuo cha maafisa afya, lakini chuo hiki hakijakarabatiwa, hakina vifaa vya kutosha, walimu ni wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naishauri Serikali kwamba, hivi vyuo vya afya vyote nchini naomba Mheshimiwa Waziri hawa maafisa wa afya vilevile ni watumishi katika idara yako, lakini vyuo hivi sijui Wizara ya afya kama mnaviangalia kwa kweli, kwa sababu hii kada ya maafisa afya ni muhimu sana na hawa ndio wanashughulikia hasa zaidi afya, kinga na ndio wanaopambana na magonjwa ya kuambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa vyuo hivi naomba sana Mheshimiwa, kwanza bajeti mnayovitengea ni kidogo sana, halafu vifaa havitoshi, walimu hawatoshi, majengo hayafanyiwi ukarabati, kwa hiyo, nilikuwa nashauri Mheshimiwa Waziri uviangalie kwa huruma vituo hivi vya maafisa afya, na bahati nzuri mimi ni afisa afya mstaafu kwa hiyo, kada hii naifahamu vizuri sana. Hawa ndio wanaopambana na magonjwa ya kuambukiza, kutoa elimu ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwenye hotuba yako umeelezea mambo ya elimu ya afya kwa umma (*Health Education*), elimu ya afya ni muhimu kweli. Katika Wizara ya Afya tuna kinga na tiba, sasa tunasema kinga ni bora kuliko tiba kwa sababu, kinga ni gharama ndogo, lakini tiba ni gharama kubwa. Kwa hiyo, nadhani kada hii ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri ungeiangalia kwa huruma zaidi, ili waweze kupata maslahi ya kutosha, vyuo hivi mdahili wanafunzi wa kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ni upungufu wa watumishi katika Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa. Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Mpwapwa ni kubwa, ina wananchi zaidi ya 400,000 na tuna vituo vingi kama nilivyosema, lakini tuna upungufu wa watumishi kama 450 wa kada mbalimbali za afya. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana

Idara ya Utumishi, Wizara ya Utumishi, tukiomba tukipeleka maombi yetu pale kutaka watumishi tunapata watumishi 6, tunapata watumishi 10, lakini tuna upungufu wa watumishi zaidi ya 450 kwa hiyo, tulikuwa tunaomba watumishi waongezewe katika Hospitali hii ya Wilaya ya Mpwapwa.

**NAIBU SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga. Waheshimiwa Wabunge, ili muweze kujipanga vizuri wachangiaji wote wa CCM wanachangia kwa dakika 7 kila mmoja anayelitwa. Na wachangiaji wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo wanachangia kwa dakika kumi, kumi wachangiaji wa Chama cha Wananchi – CUF wanachangia kwa dakika tano kila anayelitwa.

Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Gidarya, Mheshimiwa Selemani Zedi ajiandae.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nfasi. Naomba nianze kabisa kuungana na Taifa kwa ujumla katika simanzi kubwa iliyotukuta kuondokewa na mojawapo ya Mtanzania maarufu aliyefanya mambo mengi, Dkt. Reginald Abrahamu Mengi. Nachukua nafasi hii kutoa pole sana kwa wanafamilia na pia kumshukuru sana kwa msaada wake aliutoa kwa watu mbalimbali, hususan kwa sisi ambao tunashughulikia elimu bora kwa wasichana ambao hawana uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mengi alikuwa ni mtu mkarimu na waswahili wanasema kutoa ni moyo sio utajiri. Kwa hiyo, tunaomba sana familia yake iyachukue kama yalivyokuja na Mwenyezi Mungu ampe pumziko la milele.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kusema kwamba, pigo kubwa kwa sababu, siku kadhaa zilizopita wakati Marehemu Ruge Mutahaba amefariki, pia na Ephraim Kibonde wote tulikuwa katika chumba kimoja pale Karimjee, lakini hizo ndizo njia za Mwenyezi Mungu ni pigo kubwa kwa Taifa. Na ninasimama hapa kwa majonzi makubwa leo, jana

tumempoteza Prof. Robert Mabele wa Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam na yeye nichukue nafasi hii kumshukuru kwa mchango wake katika kufundisha wachumi wengi ndani ya chumba hiki, nadhani na Waziri wetu wa Fedha ni wanafunzi wake kwa hiyo, ni pigo kubwa kwa Taifa, Mwenyezi Mungu amrehemu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana sasa niende kwenye ajenda, nianze kuungana pia na wengine kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Ummy na Makamu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mheshimiwa Dkt. Ndugulile alipata nafasi kunitembelea kule na kwa sababu yeye ni daktari mambo ya Muleba aliyaona kwa karibu na alifuata hata na Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu ulifika pale *Rubya Hospital* ukatembelea hospitali teule ya wilaya, kwa hiyo, naomba nianzie hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa nchi hii katika kutoa huduma ya afya ambayo sina budi kupongeza juhudi kubwa ambazo zimefanyika katika Awamu ya Tano. Juhudi ambazo tumesikia wakati Waziri Jafo anaorodhesha hospitali ambazo tumejenga za wilaya ni jambo la kujivunia. Mwemyewe kwa upande wa Muleba Kusini tunashukuru kwamba, vituo vya afya viwili Kimea na Kaigara vimeimarishwa, upasuaji sasa hivi unaendelea. Jambo hili kwa kweli, tunashukuru sana juhudi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa Hospitali Teule ya Wilaya ya Rubya naomba niseme kwamba, nikiiangalia Rubya kwa karibu, lakini na hospitali nyingine kwa ujumla hizi zinaitwa *designated hospitals*. Utaratibu wa *public private partnership* naomba nichukue nafasi hii kusema kwamba, ni utaratibu muhimu sana. Na tunapoboresha hospitali za Serikali tuisahau pia umuhimu wa kuhakikisha kwamba, zole ambazo tulikuwanazo nazo tunalinda uwezo wake kwa sababu, isije ikawa ni wazungu wanesema, *you rob Peter to pay Paul*; tusimuibie Paulo kumlipa Petro, hapa inatikiwa *balance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba sana Mheshimiwa Waziri anapojumuisha tusikie mkakati alionao

kuhakikisha kwamba, hizo hospitali tulizokuwanazo zinaendelea pia, kufaidika na hii *partnership* iliyokuwepo la sivyo tunaweza tukajikuta kwamba, hospitali zinadidimia. Sina budi kusema kwamba, hospitali sio majengo, hospitali ni huduma na katika hili niunganishe hapohapo kusema kwamba, Mheshimiwa Waziri pia, aangalie hali halisi ya *referral hospital* zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana juhudi za Serikali ya Awamu ya Nne iliyokamilisha Hospitali ya Mloganzila, lakini Mloganzila hospitali majengo, hakuna *Hospital town* pale kwa ajili ya madaktari kukaa karibu na hospitali. Na hata huyo Profesa Mabele ambaye namsema kafia Mloganzila nilikwenda kumuangalia tu juzi nikakuta kwamba, kama kuna dharura daktari anafikaje Mloganzila? Kwa hiyo, nadhani kuna haja ya kufanya uwekezaji kuhakikisha kwamba, kituo kinafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye Hospitali ya Rubya ninaomba sana Mheshimiwa Waziri Umy unapafahamu, ulikuwa unataka kuleta mashine ya *viral load* kwa ajili ya upimaji. Sasa hivi mashine hiyo tunasikia kwamba, imehamishwa imepelekwa Bukoba na vifaa vingine. Hata na watumishi wa maabara tunapozungumza hospitali haina *any degree holder* kwenye *pharmacy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hospitali inayohudumia wilaya, wakazi laki saba. Kama una wananchi 700,000, huna maabara ambayo ina *a qualified technician* unaona kwamba, hapo huwezi kwa kweli, kutoa huduma inayostahiki. Kitengo cha meno pale kiko katika hali mbaya kwa hiyo, nafikiria kwamba, Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri mnayoifanya na utaalumu mlionao ni muhimu sana kwamba, pia, kuweko na uboreshaji tuhakikishe kwamba, hospitali zetu za zamani hazitasambaratika.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mwisho kabisa...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa, ahsante sana. Mheshimiwa Anna Gidarya, atafuatiwa na Mheshimiwa selemani Zedi, Mheshimiwa Azza Hilal Hamad ajiandae.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kwanza kabisa niungane na hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie maeneo machache katika Wizara hii ya Afya, nianze na eneo la maboma wazi katika maeneo yetu ya vituo vya afya. Tuna maboma wazi katika maeneo mengi nchini na maboma wazi haya yamejengwa na wananchi, lakini Serikali haipeleki hela kwa kile kiwango ambacho kimeridhiwa kwamba, wananchi wanajenga maboma na Serikali inamalizia. Mpaka sasa kuna maboma zaidi ya 3000 nchi nzima ambayo hayajaezekwa na ni nguvu za wananchi zinapotea bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendeleo na miradi isiyokidhi hadhi. Miradi hii ipo mingi, lakini unaenda kwenye zahanati unaenda kukagua zahanati unakuta kuna mapungufu mengi na zahanati nyingi zimejengwa chini ya viwango, huu ni ubadhirifu wa pesa za umma. Tunaomba Wizara iangalie ni jinsi gani wanaweza kwenda mbele zaidi kwa kutafuta wakandarasi wenye elimu na wenye utaalam mzuri katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye eneo la ukusanyaji wa damu salama. Katika maeneo mengi ya mkoa kulianzishwa vituo vya ukusanyaji damu salama, lakini tangu mwaka 2015 mfadhili aliyekuwa wa mradi huu alikabidhi magari ya *Red Cross* Serikalini, lakini magari hayo mpaka sasa hayajawahi kufanya kazi, jambo ambalo linasababisha vifo vingi kwa sababu vituo hivi vimeshindwa kukusanya damu salama katika maeneo mengi. Mfano mzuri ni Mkoa wa Kagera na Mkoa wangu wa Manyara damu salama haiko kabisa. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye eneo la ustawi wa jamii. Kumekuwa na tabia ya ukatili wa watoto katika maeneo mengi, lakini tuna mabaraza yanayohusika katika maeneo mengi, kwenye kata kwenye mikoa kwa ajili ya kusikiliza hizi kesi za watoto, lakini mabaraza hayo hayafanyi kazi vizuri. Tuna kesi nyingi ambazo hazitatuliwi kwa wakati, lakini nyingi zinazimwa na watoto tayari wameshapata madhara makubwa. Sasa Wizara ituambie wana mpango gani wa kuwawezesha maafisa maendeleo ya jamii katika maeneo mengi nchini, ili waende sasa wakafanye hii kazi kwa weledi?

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wengi wameathirika na wamefanyiwa vitendo vya kikatili. Mfano mzuri ni Hanang ambapo ni Basutu, Balangalalu na Babati pia wapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye eneo la utatuzi wa migororo ya ndoa na matunzo ya watoto. Kila siku hapa Bungeni tunalia na hali ya kusema watoto wa mitaani. Watoto wa mitaani tunawatengeneza sisi wenyewe, kwa nini tunawatengeneza sisi wenyewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inayotakiwa isimamie unakuta kesi nyingi zinaendeshwa, lakini kwa sababu unakuta mama au mzazi mmojawapo hana uwezo mzuri kesi tayari imepelekwa Mahakamani, kesi inaamuliwa mtoto aende kwa upande mmoja wa mzazi mmoja. Matokeo yake ule mgogoro kama haukutatuliwa vizuri ndio maana unaona unasikia kesho mkoa fulani watoto wamechunjwa, mkoa fulani baba ameuwa mtoto, haya ni mambo yanayoumiza Taifa, lazima yaangaliwe kwa wakati na lazima yasimamiwe na wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechoka kusikia vifo vya watoto kila siku watoto wanachinjwa, Tanzania nzima hakuna siku mtoto hachinjwi ni kwa sababu ya ubadhirifu wa kutokutumia sheria. Hongo zinatembea huko, mzazi anasema ana uwezo wa kumchukua mtoto wake, anamchukua anampeleka kwa mama wa kambo, yule mtoto anaendelea kunyanyasika, mwisho wa siku kisaikolojia anaathirika halafu

tunasema tuna watoto wa mtaani, hiyo haiwezekani. Nendeni mkakae mliangalie hili namna ya ku-so/ve watoto wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo la vyumba vya wagonjwa mahututi. Hospitali nyingi za wilaya hazina vyumba ambavyo vinakidhi mahitaji ya mgonjwa mahututi; mfano mzuri ni Hospitali ya Mrara chumba cha wagonjwa mahututi ni sawa na gereji ya magari. Nendeni mkaangalie pale Babati, mkashuhudie hili ninalozungumza, boresheni hizi huduma mtusaidie, tuwasaidie Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie eneo moja ambalo nafikiri litakuwa ni la mwisho. Maeneo mengi ukienda kwenye hospitali za wilaya, kila unapomfikisha mgonjwa, hasa wale wagonjwa wanaopata ajali wanasema damu haipo. Sasa kwenye hotuba ya Waziri ameandika amesema damu sijui lita elfu ngapi hizi, hizi damu kwa nchi nzima hazitoshi na tunasema tunachangia damu salama kwa hiyari, ile kampeni endezeeni, ili tusaidie Watanzania walio wengi. Hii idadi ya damu uliyoandika hapa Mheshimiwa Waziri haitoshi kwa nchi nzima Tanzania kila siku watu wanahitaji damu salama na wanahitaji kuongezewa damu kupitia magonjwa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru wewe kwa haya machache niliyochangia. Kuna eneo hili la maendeleo na uwezeshaji wa wanawake. Eneo hili sidhani kama Wizara inafuatilia vizuri katika maeneo yake. Hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii kwenye maeneo yao wamekuwa miungu watu. Hii mikopo mnayosema namna ya kuwezesha wanawake *VICOBA*, hawa watu hawafanyi hii kazi kwa weledi. Afisa Maendeleo anataka rushwa ili mradi tu wanawake wapate mkopo. Hii siyo sahihi! Hii ni haki yao ya msingi akina mama kupata huu mkopo na upo kwenye sera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, angalieni hivi vitu ambavyo vinagusa jamii. Kila siku tunaimba hapa *issue* ya

dawa lakini kuna mambo ambayo tukiyasimamia mambo mengine yanaweza yakaenda sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Azza Hamad na Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata ajjandae.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Wizara ya Afya ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza kwa dhati Waziri wa Afya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa kazi kubwa anayofanya na hakuna mtu yeyote ambaye ana mashaka na uchapakazi wao. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka miwili iliyopita, nilisimama hapa Bungeni nikalalamika sana kuhusu ubovu wa *X-Ray* katika Hospitali ya Wilaya ya Nzega ambapo kuna wakati fulani ilikuwa inachukua mpaka miezi sita *X-Ray* haifanyi kazi. Leo hii nasimama hapa kutoa pongezi za dhati kwa niaba ya wananchi wote wa Wilaya ya Nzega kwamba Serikali sasa imesikia kilio hicho na imetupatia *X-Ray* mpya kabisa ya kidigitali ambayo inafanya kazi kwa ufanisi na inatoa picha za ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya aananchi wa Nzega lazima niishukuru Serikali kwa kutupatia *X-Ray* hiyo mpya kabisa. Kwa hiyo, sasa hivi uchunguzi wa magonjwa unafanyika kwa usahihi na maana yake ni kwamba tiba itapatikana kwa usahihi. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleo kuipongeza Serikali. Nimeangalia ukurasa wa 54, kwa kweli kuna mambo makubwa ambayo sisi kama wawakilishi wa wananchi ni lazima tuipongeze. Kabla ya mwaka 2017, kuna matibabu makubwa ya kibingwa yalikuwa hayawezi kufanyika hapa

nchini, lakini sasa yanafanyika. Kwa mfano, kupandikiza figo, jambo hili limeokoa zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa kipindi hiki tu ambapo wagonjwa 38 wameweza kupandikizwa figo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna mambo makubwa yamefanyika. Kwa mfano, kabla ya mwaka 2017, hatukuwa na uwezo wa kupandikiza vifaa vya usikivu kwa watoto wadogo. Hili ni jambo kubwa ambalo sisi wawakilishi wa wananchi tunatakiwa kutoa pongezi za dhati. Fikiria mtoto anazaliwa hawezi kusikia, lakini anafanyiwa operesheni, anawekewa vifaa vya usikivu, anaweza kusikia. Kwa hiyo, anaweza kufanya mambo yote ya kupata elimu na haki nyingine zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili ni jambo ambalo siyo dogo, ni kubwa na ninachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kufanikisha jambo kama hili. Pia jambo kama hili linaokoa fedha nyingi ambazo zinatumika katika mambo mengine muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaungana na mapendekezo ya Kamati ya Huduma za Jamii. Ukiangalia ukurasa wa 20 mpaka 21, Kamati imeitaka Wizara ya Afya kuwaangalia kwa makini wahudumu wa afya katika ngazi ya jamii kwa sababu hawa wanasaidia sana katika kuhakikisha kwamba tunapata kinga na kila mmoja anajua kwamba kinga ni bora kuliko tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mapendekezo yote ya Kamati ya Huduma za Jamii yaliyo katika ukurasa wa 20 mpaka 21 ninakubaliana nayo kwamba Wizara ya Afya iangalie namna ambavyo itaweza kuwa-*accommodate* hawa wahudumu wa afya ngazi ya jamii ili tuweze kuhamasisha akina mama wakajifungulie kwenye zahanati, tuweze kuhamasisha matumizi bora ya vyoo, tuhamasishe unywaji wa majisafi na salama ili kuepuka magonjwa ambayo yanaweza yakasumbua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kuongelea ni uhaba wa watumishi hasa Waganga katika zahanati zetu. Ningependa Wizara ingetoa mwongozo wa kuhakikisha kwamba angalau katika kila zahanati kunakuwa na Mganga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyo sasa hivi, kwa mfano katika Halmashauri yangu ya Nzega Vijijini, katika zahanati 39 tulizonazo, zahanati 12 hazina kabisa Waganga, zinaendeshwa na *Ma-nurse*. Jambo hili siyo jema kwa sababu tunapaswa tuwe na Waganga ambao mgonjwa akifika anahudumiwa, anakuwa *prescribed* na Mganga halafu ndiyo wanahudumiwa na *Nurse*.

Mheshimiwa Naibu Spika. Zahanati 12; Zahanati ya Mboga, Zahanati ya Semembela, Zahanati ya Nkindu, Ikindwa, Lakui, Mwangoye, Mwasala, Malilita, Uhemeli, Mirambo Itobo, Magengati na Shila; hizi zahanati hazina kabisa Waganga. Kwa hiyo, ombi na ushauri wangu kwa Wizara ni kwamba tuhakikishe kwamba zahanati hizi ambazo tayari zipo angalau zinakuwa na Waganga ili wagonjwa wakifika pale waweze kupata huduma za tiba za uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili litakwenda sambamba na Ilani yetu ya uchaguzi ambayo tunahimiza kwamba kila Kijiji kiwe na zahanati. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba tunakwenda kujenga zahanati za kutosha nyingi. Sasa zahanati ili ziweze kufanya kazi, ni lazima ziwe na Waganga na *Ma-nurse*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawapongeza Wizara kwa kazi kubwa wanayofanya kuimarisha afya katika Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Azza Hillary Hamad, atafuatiwa na Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata na Mheshimiwa Taska Mbogo ajiandae.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya na uzima na hatimaye nimeweza kusimama na kuweza kuchangia bajeti ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa pongezi nyingi kwa Wizara ya Afya, kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wao wote katika Wizara ya Afya. Kazi mnayoifanya ni kubwa na hakika mmeleta mabadiliko makubwa katika Sekta ya Afya. Hongereni sana. Mwenye macho haambiwi tazama, yanaonekana yale yote ambayo mmeyafanya katika Sekta ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia kwa uboreshwaji wa huduma katika hospitali zetu maalum; Hospitali ya *Ocean Road*, Hospitali ya Jakaya Mrisho Kikwete ya kitengo cha Moyo na hospitali zote za mikoa, Wilaya na uboreshwaji wa vituo vya afya. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda ni mfupi, niende moja kwa moja katika Mkoa wangu wa Shinyanga ili niwasemee wananchi walionileta ndani ya ukumbi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuisemea Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga. Mwaka 2018 nilisimama humu ndani nikasema kuhusu ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga. Ujenzi huu umeanza bajeti ya mwaka 2013/2014; kuna jengo moja kubwa ambalo limekamilika, jengo la utawala. Jengo hili wanaishi popo, halina kazi yoyote. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, tarehe 24/01/2019 alitembelea ujenzi wa hospitali hii katika Mkoa wa Shinyanga na baada ya kutembelea alitoa ahadi kwamba atatoa fedha, shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya *maternity block* ili hospitali ile ianze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namkumbusha Mheshimiwa Waziri wa Afya, ahadi yake Wana-Shinyanga tunaisubiri kwa sababu ulisema jengo lile litakamilika na mwishoni mwa

mwaka huu hospitali ile itaanza kufanya kazi, sijui umekwamishwa na kitu gani? Nakuomba sana, nakusihi sana, ahadi ni deni. Vitabu vya dini vinasema, ukiahidi halafu bahati mbaya Mwenyezi Mungu ikatokea lolote, umekufa deni. Naomba ahadi hii uitekeleze Wana-Shinyanga tunaisubiri kwa hamu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa bajeti mwaka 2018 nilisimama nikasema ubovu wa *X-Ray machine* katika Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga. Namshukuru Mheshimiwa Waziri pia alipokuja Shinyanga alituahidi wana Shinyanga kwamba atatuletea *X-Ray machine* ya kisasa, lakini mpaka sasa hivi hatujapata *X-Ray machine* ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado namkumbusha Mheshimiwa Waziri, aliahidi mwenyewe na Wana-Shinyanga tunasubiri na watendaji wake wanamsikia. Ahadi ni deni, tunasubiri *X-Ray machine* ya kisasa kwa sababu tuliyonayo ni mbovu na haifanyi kazi vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niendeleo kukumbusha ahadi za Serikali. Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Mkoa wa Shinyanga, nilisimama katika Jimbo la Ushetu nikaomba *ambulance* kwa ajili ya Jimbo la Ushetu. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokea ombi hilo na akatuahidi kwa Mkoa wa Shinyanga kutuletea *ambulance* nne na Mheshimiwa Waziri mwenyewe akiwepo. Tunahitaji *Ambulance* kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Tinde, kwa ajili ya Jimbo la Ushetu, Jimbo la Msalala na Jimbo la Kishapu. Ahadi hizo hazijakamilika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleo kusemea kuhusu watumishi katika Mkoa wa Shinyanga. Watumishi wa Idara ya Afya katika Mkoa wa Shinyanga mahitaji ni 3,606, waliopo ni 1,446 na upungufu ni 2,160. Naomba Wizara, tutazameni, mmeboresha vituo vya afya lakini vituo hivi kama havina watumishi bado vitakuwa haviwezi kufanya kazi vizuri. Upungufu tulionao ni mkubwa, watumishi waliopo wanalazimika kufanya kazi kwa shida kwa sababu wanafanya kazi ambazo zinawazidi uwezo. Watumishi ni

wachache katika vituo, kwa hiyo, tunawaomba sana fanyeni utaratibu muweze kutuongeza watumishi katika idara ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali katika ujenzi wa vituo vya afya 11 ndani ya Mkoa wa Shinyanga. Vituo hivi vimekamilika, lakini kinachonisikitisha mpaka sasa hivi hatujapata vifaa tiba. Kwa hiyo, niwakumbushe Wizara ya Afya, vituo hivi vinahitaji kufanya kazi ili viende vikatimize lengo ambalo mmelikusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo hili ni zuri na linapendeza hata ukiangalia hali ambayo inaonekana katika vituo vyetu vya afya, lakini haviwezi kufanya kazi kwa sababu lengo lililokusudiwa halijaanza kufanya kazi. Hakuna vifaa ambavyo vimeletwa katika vituo vyetu vyote 11 vilivyopo ndani ya Mkoa wa Shinyanga na hivyo lengo lile la kwenda kufanya upasuaji bado halijaanza kufanya kazi. Kwa hiyo, niwaumbushe mtuletee vifaa tiba katika vituo 11 ambavyo mmetujengea katika Mkoa wetu wa Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie kusema kwamba naipongeza sana Serikali, nilikuwa nikisema sana kuhusu Hospitali ya Wilaya ya Shinyaga, hospitali sasa hivi inaendelea. Nawashukuru sana kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona unanitazama, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Mbogo na Mheshimiwa Sonia Magogo ajiandae.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na tunaweza kusimama katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Ummu Mwalimu na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile kwa kazi kubwa wanazozifanya. Hakika wanaitendea haki Wizara hii. Mheshimiwa Ummu, kwa kweli umetupa heshima wanawake wenzio, Mwenyezi Mungu aendelee kukupigania na kukuinua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia Katibu Wakuu, Naibu Katibu Mkuu na Madaktari wote Tanzania nzima kuanzia Taifa na wale wa wilayani na mikoani. Kwa kweli madaktari wanafanya kazi nzuri na kubwa. Mwenyezi Mungu aendelee kuwatia nguvu na kuwabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa na nzuri anazozifanya. Ndani ya kipindi kifupi ameweza kufanya mambo makubwa; nikianza la kwanza, ameweza kuboresha upatikanaji wa madawa hospitalini; pia ameweza kukarabati vituo vya afya takribani 325; na amefanikiwa kutoa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali za mkoa mipya. Kazi nyingi sana amezifanya Mheshimiwa Rais, nikianza kuziorodhesha hapa nina dakika saba zitaisha. Kwa kweli anastahili pongezi. Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi nikaitendea haki roho yangu bila kumwomba Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli. Naanza kwa kusema Baba katika Jina la Yesu, mbariki sana Mheshimiwa Dkt. Magufuli, mbariki Mheshimiwa Waziri Mkuu, mbariki Mheshimiwa Ummu Mwalimu, wabariki Mawaziri wote akiwemo Mheshimiwa Jenista Mhagama, wabariki Mawaziri wote na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Tanzania. Mwenyezi Mungu kibariki Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nasema wote tuseme Amen. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Amen! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niingie sasa kwenye hoja za msingi. Nianze kwa kuomba. Jimbo la Nkasi Kusini lipo umbali mrefu sana kutoka Makao Makuu ya Wilaya. Wanawake wanaotoka Kata za Kara, Ninde na Nkandase wanapata shida sana wanapopata ujauzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi juzi mwanamke mmoja amefia njiani wakati anakwenda hospitali kujifungua. Namwomba mdogo wangu Mheshimiwa Umyy Mwalimu atufikirie sana Jimbo la Nkasi Kusini kutuletea *ambulance*. Wanawake wale wakipata *ambulance* tutakuwa tumeoko maisha ya akina mama wengi katika Tanzania hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niipongeze Serikali kwa kutujengea Hospitali za Wilaya. Katika Mkoa wa Rukwa wilaya zote zimepata Hospitali za Wilaya, lakini bado Wilaya moja ya Sumbawanga Mjini haijapatiwa Hospitali ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia bajeti iliyopita ilipanga kujenga Hospitali ya Rufaa katika Mkoa wa Rukwa ambapo ilipanga kujenga katika Kijiji cha Milanzi, lakini mpaka sasa hivi hatujaona ujenzi ukianza Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Rukwa. Pia hospitali iliyopo ya mkoa majengo yake yamechakaa, jengo la *mortuary* limechakaa, halina hadhi ya mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili, ile hospitali ya rufaa ianze kujengwa, itasaidia sana kuepusha msongamano katika hospitali iliyopo ya mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee sasa Wilaya ya Nkasi, kuna vituo vya afya vimeanza kujengwa, wananchi wanajenga kwa nguvu zao.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata muda wako umeisha, lakini kwa maombi uliyopiga, nakuongeza dakika mbili. *(Makofi)*

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nakushukuru sana, Mungu akubariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Akasu, Kate, Ninde na King'ombe wameanza kujenga maboma ya vituo vya afya. Naomba Mheshimiwa Waziri atuongeze nguvu, awape moyo wale wananchi wanaojenga wapate *support* ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpongeze Mkurugenzi wa Manispaa ya Sumbawanga Mjini, kaka yangu Jacob Ntalitinginya ameweza kuwakopesha wanawake vikundi karibia 99 ambapo walikuwa wanasubiri kwamba labda Benki ya Wanawake ingejengwa Mkoa wa Rukwa lakini haijajengwa. Yeye ameweza kuwakopesha wanawake, pia ameweza kukusanya mapato karibia asilimia 110. Kwa hiyo, nampongeza sana Jacob Ntalitinginya, Mkurugenzi wa Manispaa ya Sumbawanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika mbili zimeisha na nilikuwa na hoja nyingi lakini naomba kwa haya tu, niongelee sana suala la *ambulance* kwa wanawake katika Jimbo la Nkasi Kusini kwa Mheshimiwa Mipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, naona Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa alikuwa anapokea hayo maombi kwa namna ya tofauti kidogo, kwa hiyo naamini Mheshimiwa Ummu atasema neno.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wachangiaji wetu; Mheshimiwa Taska Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Sonia Magogo, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa muda huu ili kuchangia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu kwa kutupa uhai leo hii na uzima. Napenda niungane na Watanzania wote kutoa pole kwa kifo cha Mheshimiwa Dkt. Mengi ambaye amesaidia sana makundi mbalimbali ya jamii, natoa pole kwa wananchi wote wa Tanzania, familia yake na wote waliloguswa na msiba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda nitoe pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri Umy na Makamu wake, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, kwa kazi nzuri wanazozifanya za kuboresha afya za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba nitoe pongezi kwa Madaktari wote wa nchi hii ya Tanzania kwa huduma wanazotupatia za kuboresha afya za Watanzania wote, ndiyo maana tunaweza kuja humu Bungeni na tunaweza kufanya kazi zetu kwa sababu ya Madaktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa sababu muda ni mdogo, niende moja kwa moja kwenye changamoto. Mkoa wetu wa Katavi baada ya ile changamoto ya kuwatoa Madaktari na Manesi feki, tumekumbwa na tatizo la uhaba wa watumishi. Nimwombe Mheshimiwa Umy aweze kutupatia Madaktari kule Mkoani kwetu Katavi, atupatie Madaktari Bingwa; hatuna *Gynecologist*, hatuna Madaktari wa Macho, hatuna Madaktari wa Mifupa, kiasi kwamba mtu akivunjika mguu kule Katavi inabidi asafiri kutoka Katavi mpaka Muhimbili kwenda kufanyiwa matibabu ya mguu. Kwa hiyo niombe sana watakapokuwa wanaajiri Madaktari auangalie Mkoa wetu wa Katavi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho napenda kukiomba Mkoani kwetu Katavi, naomba kukiombea Kituo cha Afya cha Mamba, naomba akipatie *ambulance*, kituo hiki kipo umbali wa kilometa 150 kutoka

pale Mpanda Mjini na hakina *ambulance*. Pia nimwombe Mheshimiwa Waziri, kuna kituo cha afya kilikuwa kinajengwa cha Mwamapuli katika Jimbo la Kavuu, naomba akipatie pesa ili kiweze kwisha kwa sababu anafahamu jiografia ya Mkoa wetu wa Katavi, Jimbo la Kavuu liko kiasi cha kilometa 150 kutoka Mpanda kwenda Makao Makuu ya Wilaya, kwa hiyo naomba akiangalie kituo hiki cha afya. Niombe pia vitendeakazi kama *x-ray* na *ultra sound* kwa vituo vya afya vyote vya Mkoani kwetu Katavi kwa sababu viko mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya, umbali wa kilometa 150. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho napenda kuzungumzia, nimwombe Mheshimiwa Ummu, iko Sera ya Wazee ambayo Serikali ilipitisha toka mwaka 2003, niombe sasa alete Sheria ya Wazee kwa sababu Sera ya Wazee imekaa umri wa miaka 15, lakini hakuna Sheria ya Wazee, sasa sera ikikaa hivihivi kama sera inaweza siku nyingine Serikali ikaamua tu kwamba inafuta ile Sera ya Wazee lakini ikiwa ndani ya sheria wazee watakuwa *protected* zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho ninakiomba ni kuhusu kuajiri hii Sekta ya Afya upande wa *Community Health Service*. Hawa watu ni muhimu sana kwa sababu wao wanakwenda *deep* kwenye kaya, ina maana wana uwezo wa kwenda nyumba kwa nyumba kwenda kufundisha mambo ya afya. Ukiangalia kwamba mara nyingi nchi yetu huwa tunapata matatizo ya kipindipindu, ni kwa sababu tuna uhaba wa hawa Maafisa Afya Jamii. Hawa ni muhimu sana kwa sababu wao wanakwenda kwenye kijiji, wanaweza kufundisha umuhimu wa kutumia vyoo, umuhimu wa kunawa mikono kabla ya kula, hii yote itasaidia wananchi wa Tanzania wasiweze kupata magojwa ambukizi. Kwa hiyo, niombe waweze kuajiri hawa Maafisa Afya Jamii kwa manufaa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia, Mheshimiwa Ummu katika Sekta ya Afya amefanya vizuri sana upande wa madawa, upande wa kujenga hospitali, upande wa kujenga vituo vya afya,

lakini upande wa wanawake nimwombe kabla hajaondoka aweke *legacy* kwa wanawake, aangalie sheria ambazo zinamkandamiza mwanamke, zije humu Bungeni zibadilishwe. Nafikiri hiki ndicho kitakachomfanya aweke historia kwa wanawake, Sheria kama ya Ndoa ya Mwaka 1971, kipengele cha 13 ambacho kimekuwa kigugumizi katika nchi hii kubadilisha umri wa mtoto wa kike kuolewa na mtoto wa kiume kuoa, aweke *legacy* kwa kubadilisha sheria hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo sheria nyingine pia ambazo ni kandamizi kwa wanawake. Kwa mfano, ipo *GN* ya mwaka 1963 ambayo ina vipengele vingi sana vinamkandamiza mwanamke. *GN* hii bado inatumika na nashangaa sana hata kuna kesi ambayo ilishatolewa kwamba *GN* hii ifutwe, lakini bado nimeona kwamba ni kigugumizi sana kufuta *GN* hii. Haiwezekani utumie *GN* ya mwaka 1963 kwa wanawake wa Tanzania ambayo inawabagua sana katika mambo ya mirathi, inawabagua sana katika kutumia ardhi mume wako akifa na pia ina kipengele ambacho kinasema kwamba mwanamke akifiwa na mume wake arithiwe na mdogo wake na akikataa atoke katika ukoo huo.

Nimuombe sana afuatilie hizi sheria zote azilete hapa na atakuwa ameweka *legacy*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *GN* hiyohiyo pia inamtambua mtoto wa kiume kwamba ndio mrithi halali, wanamwita *principal heir*, lakini haimtambui mtoto wa kike kwamba ni mrithi wa mali za baba yake. Nimwombe Mheshimiwa Waziri basi aweke *legacy* kwa kubadilisha sheria hizi ambazo ni mbovu, zinamnyanyasa mtoto wa kike ili tutakapoondoka katika Bunge hili, basi akinamama waseme tulikuwa na Waziri mwanamke ambaye pia alishughulikia masuala ya wanawake. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taska Mbogo kengele ya pili imegonga muda mrefu sana, lakini kwa umuhimu wa hoja ulizokuwa unasema ilibidi nikuache umalize. Ahsante sana kwa mchango mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Sonia Magogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala ajiandae.

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii. Kwanza kabisa nianze kwa kuwapongeza watendaji wote wa Wizara hii kutokana na ugumu wa kazi yao, lakini pamoja na vile wanavyojitahidi kuendana na hizo changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikuja na mpango mzuri sana wa huduma ya afya kwa wannachi na hii imekuwa ikiwasaidia sana wananchi wengi, hasa pale wanapopata matatizo mbalimbali ya afya. Hata hivyo, tumekuwa tukishuhudia mrundikano wa watu wengi kwenye madirisha zinapotolewa huduma hizi kwenye hospitali zetu, hivyo kusababisha wagonjwa kuchukua muda mrefu sana mpaka kuja kuhudumiwa. Naiomba Serikali iangalie utatuzi wa changamoto hii kwa kuongeza waajiriwa, hasa katika madirisha haya yanayotoa huduma hizi za afya kwenye hospitali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea kuhusu watoto; tumekuwa tukizungumza sana kuhusu tatizo la lishe kwa watoto wetu na tumeona changamoto zinazojitokeza, hasa maeneo ya vijijini. Kwa upande wangu sioni kama changamoto hapa ni ukosefu wa chakula, kwa mfano, kama tunavyoongelea huko vijijini ambako ndiyo kuna vyakula vingi vinapatikana na vingi ni *natural* kabisa, lakini bado watoto wengi wa maeneo hayo wanapata utapiamlo na udumavu. Hivyo hapa naona tatizo ni elimu kwa hii jamii na hivyo Serikali iangalie uwezekano wa kuwapa elimu hawa wananchi hasa wa vijijini ni jinsi gani wanaweza kuwasaidia watoto wao wakapata lishe bora na kuondokana na haya matatizo ya udumavu na utapiamlo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile jamii ingefundishwa kuhusu sheria mbalimbali ambazo zinasaidia kumlinda na

kumtetea mtoto anapokutana na changamoto mbalimbali huko katika jamii. Changamoto nyingi zimekuwa zikijitokeza, lakini unakuta mzazi hajui aanzie wapi, inasababisha mtoto anakosa haki yake na kuishia kuishi kwenye janga la umaskini ama kuishia kwenye matatizo ambayo baadaye yanakuwa ni changamoto kubwa sana kwake. Hivyo niombe Serikali iendelee kutoa elimu kwa jamii kuwasaidia hawa watoto na kuwalinda ili tuweze kujenga kizazi bora cha kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine nililoliona ni katika tafiti na elimu mbalimbali. Kwenye jamii yetu sasa hivi kuna matatizo mbalimbali ya kiafya, mathalani, tunaona watu wengi hata kushika mimba limekuwa ni tatizo; pia kuna tatizo lingine la kutoka mimba kabla ya wakati; kuna tatizo la mimba kutunga nje ya kizazi; kuna vifo vya watoto wachanga; na kuna tatizo la nguvu za kiume. Haya matatizo yamekuwa ni mengi sana katika jamii na hivyo napenda kuishauri Serikali ifanye tafiti mbalimbali na kuja na majibu ambayo yataisaidia jamii yetu kuondokana na haya matatizo ambayo yamekuwa ni changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe pia Wizara iangalie hospitali zetu. Hospitali nyingi zinakuwa hazina vifaa vya kutosha, mathalani ni Kituo cha Afya cha Mombo. Kile kituo cha afya kipo katika njipanda na kinahudumia watu wengi sana, lakini kituo kile hakina *x ray*, hakina *ultra sound*, hakina hata jenereta. Hivyo niwaombe watusaidie kwa sababu ni sehemu kubwa sana ya wananchi wanaohudumiwa na kituo kile, lakini kutokana na changamoto hizi wanashindwa kutekeleza kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamida Mohammed Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Diodorus Kamala na Mheshimiwa Deo Sanga ajiandae.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami niendelee kuungana na Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi katika



kuhakikisha kwamba tunaendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri Umy na Naibu wake na timu nzima ya Wizara hii ya Afya katika kuhakikisha kwamba wanaendelea kuchapa kazi na kazi zao zinaonekana. Mheshimiwa mmoja amesema aliye na macho haambiwi tazama, kwa sababu kazi hizi zinaonekana, tunaendelea kuboresha afya za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niendeleo kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Umy Mwalimu kwa kufanya ziara katika Mkoa wetu wa Lindi. Imeleta tija sana na faida kubwa kwetu, lakini ameweza kujionea changamoto mbalimbali ambazo zipo katika Mkoa wetu wa Lindi katika eneo hili la vituo vya afya ambavyo vinaendelea kujengwa. Vipo ambavyo vimekamilika na vipo ambavyo havijakamilika lakini vinaendelea viko katika hatua nzuri sana, tunaendelea kuvisimamia kuhakikisha kwamba vituo hivi vinakamilika na vianze mara moja kutoa huduma. Vile vile vipo vituo vya afya ambavyo vimekamilika; Kituo cha Mnazi Mmoja pale Lindi Manispaa, lakini kituo kimoja pale Lindi Vijijini, kule Nyangamala, tunasubiri tu ufunguzi ufanyike vituo hivi vianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Umy Mwalimu, alifanya uzinduzi wa upimaji wa Saratani ya Shingo ya Kizazi pale Sokoine, Lindi Manispaa, huduma hii imeweza kusaidia kuwafikia wanawake wengi wameweza kujitokeza katika kuhakikisha kwamba wamekwenda kupima tatizo hili la Saratani ya Shingo ya Kizazi. Niendeleo kuipongeza Serikali na niishauri Serikali kuendelea kutoa huduma hii ya *mobile* katika maeneo mbalimbali nchini Tanzania kuhakikisha kwamba wanawake wengi wanajitokeza kuendelea kupima tatizo hili ambalo linaonekana sasa linakua kwa kasi kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kufanya kampeni ya utoaji wa chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi kwa watoto wetu wa kike kuanzia umri wa miaka 14 japokuwa tunapata changamoto ya kwamba wazazi wa watoto hawa hawawaruhusu kupata hii chanjo. Naomba tuendeleo kutoa elimu kwa wazazi hawa na watoto wetu ili waweze kupata

kinga hii ambayo inatolewa na Serikali kwa sababu tatizo hili mbele ya safari linasababisha wanawake kunyanyapaliwa na waume zao kutokana na tatizo hili la kansa ya shingo ya kizazi na wanawake wengi wanapoteza maisha kutokana na tatizo hili kubwa ambalo linaendelea kukua katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishirikiana na Mheshimiwa Umyy Mwalimu katika kuhakikisha kwamba tunahamasisha wananchi kujiunga na *NHIF* katika Mkoa wetu wa Lindi. Tatizo lililopo ni kwamba wananchi wengi hawana elimu ya kutosha ya upatikanaji wa kadi hizi za bima ya afya. Nashuhudia pale Ruangwa alitoa elimu na wananchi palepale hospitali walidiriki kukata na kujiunga na *NHIF*. Kwa hiyo, suala kubwa ni tuendelee na kampeni kuwahamasisha wananchi wetu kujiunga na *NHIF* ili waweze kupata huduma ya matibabu pale wanapopatawa na matatizo na inasaidia pale wanapokuwa hawana fedha, basi kupata matibabu bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, la msingi ni kuendelea kuimarisha vituo vyetu vya afya vyote viwe na dawa za kutosha ili wananchi wale wenye bima za afya wasikate tamaa na itakuwa ni njia nzuri ya kuwafanya hao wenye bima ya afya kuendelea kuhamasisha watu wengine ili waweze kujiunga na wao katika mpango huu wa bima ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio makubwa tuliyoyapata katika ujenzi wa vituo hivi vya afya, bado tunazo changamoto mbalimbali. Ukiangalia katika Mkoa wetu wa Lindi eneo hili la watumishi tuna changamoto kubwa sana na Mheshimiwa Waziri Umyy alipokuja alipata taarifa ya mahitaji ya watumishi katika Mkoa wa Lindi. Mahitaji yalikuwa ni watumishi 4,898 lakini watumishi waliopo ni 1,784, sawa na asilimia 36 na pungufu ilikuwa ni 3,114 sawa na asilimia 64. Kwa hiyo upungufu huu wa watumishi katika eneo hili la afya katika Mkoa wa Lindi ni kubwa sana na ni changamoto kwa sababu wananchi wengi wanakosa kupata huduma hii kwa kukosa Madaktari na watumishi mbalimbali katika maeneo haya ya vituo vyetu vya afya,

zahanati na hospitali ambazo zipo. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Ummu Mwalimu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imegonga.

Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa Edwin Sannda ajiandae.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Naomba nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nina mambo machache ambayo napenda nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, natoa shukrani zangu za dhati kwa fedha iliyotolewa na Serikali kwa ajili ya kukarabati Kituo cha Afya cha Bonazi, nashukuru sana. Mara nyingi huwa nasema mafanikio ni baba wa matatizo kwa sababu unapokarabati kituo cha afya kikawa bora maana yake kitavutia wagonjwa wengi zaidi kukitumia na maana yake ni kwamba kituo kikishakuwa bora zaidi kukitumia na ni kwamba kituo kikishakuwa bora zaidi kikavutia wagonjwa wengi zaidi maana yake unahitaji kuongeza bajeti ya madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nasema mafanikio ni baba wa matatizo na huwezi ukaliepuka hilo kwa sababu ukiliepuka hatutaendelea. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Afya na TAMISEMI wafanye kila kinachowezekana kuongeza bajeti ya Kituo cha Afya cha Bunazi na hasa upande wa madawa ili tuweze kukabiliana na ongezeko la wagonjwa ambao sasa watatumia kituo hicho na wameanza kukitumia kwa sababu sasa operesheni pale zinaweza kufanyika na mambo mengine ambayo hapo kabla yalikuwa hayafikiriwi kufanyika pale sasa yanafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya kwa kujenga Kituo cha Afya cha kisasa Kabyire. Mheshimiwa Waziri niliwasilisha maombi maalum kwa ajili ya kituo hicho cha kisasa ambacho ni bora kuliko vituo vyote katika Mkoa wa Kagera, naweza nikasema, lakini changamoto kubwa ni bajeti, inabidi tutoe bajeti maalumu kwa ajili kuhakikisha kituo hicho kinafanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu Wilaya yetu ni mpya, hatuna Hospitali ya Wilaya, tunatumia Hospitali Teule. Tulishatenga eneo la kujenga Hospitali ya Wilaya, tunaomba sana Serikali ituweke katika awamu itakayofuata ili na sisi tuweze kujenga hospitali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha hotuba Mheshimiwa Waziri ameonyesha fursa mbalimbali za Tanzania katika ununuaji wa madawa na sasa tunawakilisha nchi 15. Pia nampongeza amefuta tozo mbalimbali na ameeleza kwamba wameandaa mwongozo wa uwekezaji katika viwanda vya dawa. Nimejaribu kutafuta mwongozo huo sijauona lakini uzoefu wangu unanituma kwamba mwongozo kama unaeleza tu fursa zilizopo bila kueleza *incentive* za kisheria zitakazotolewa kwa wale watakaowekeza, bila kutoa ardhi, mimi niseme Halmashauri ya Misenyi tuko tayari kutoa heka 400 kwa ajili ya kujenga viwanda vya madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mbunge wa eneo hilo nikizungumza na Halmashauri ya Misenyi imezungumza, mje niwakabidhi eneo hilo ili muweke hiyo *center* ya madawa. Ukijenga *center* ya madawa Misenyi maana yake umejenga Afrika Mashariki kwa sababu utaenda Uganda, South Sudan, Rwanda, utaenda kokote kule. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuwakaribisha ili tufanye ujenzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri katika bajeti yake atenge fedha za kutosha za madawa, tunaita *noncommunicable disease* kwa sababu katika ngazi ya zahanati na vituo vya afya mara nyingi bajeti zao ni ndogo, madawa ya presha na kadhalika

wanakuwa hawana. Mara nyingi nimekutana na watu wengi wako Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wakifuatilia dawa hizo nikawa najjuliza kama ikishajulikana fulani anaumwa na yuko sehemu fulani na dawa anazotumia ni aina fulani na katika Hospitali ya Rufaa zipo, utaratibu ufanywe kuhakikisha dawa hizi zinapelekwa mpaka ngazi ya vijiji na vitongoji ili kuwasaidia wagonjwa hawa kupata dawa ambazo vituo vyetu au zahanati haviwezi kuwa nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilima mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Deo Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Sannda na Mheshimiwa Vedasto Ngombale.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuishukuru Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Magufuli pamoja na wanaomsaidia kazi, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu yuko hapa ambaye kila wakati tunamweleza matatizo ya maeneo yetu na Mawaziri wote wanaotusaidia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimshukuru Waziri, Mheshimiwa Umyy pamoja na Naibu Waziri wake na Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara ya Afya pamoja na TAMISEMI kwa maboresho waliyofanya ndani ya sekta ya afya. Wanafanya kazi nzuri nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na Jimbo langu la Makambako, nilipewa shilingi milioni 400 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya cha Lyamkena, shughuli ya ujenzi imeshakamilika tangu Desemba, 2018. Tunaomba sasa tupatiwe vifaa tiba na waganga ili kituo kile kiweze kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili, tunaomba kituo mama ambacho kilikuwa kama ni hospitali

ya mji wa Makambako ambacho ni Kituo cha Afya cha Makambako ambacho kinafanya kazi nzuri lakini tatizo kubwa ni ukosefu wa *X-ray* na *Utra Sound*. Mheshimiwa Rais alivyokuja tulimueleza matatizo yetu na nashukuru aliwaagiza watendaji ikiwemo Wizara ya Afya na TAMISEMI na bahati nzuri nilipokutana na Waziri wa Afya ambaye ni Mheshimiwa Umyy Mwalimu nilikueleza juu ya jambo hili na uliniahidi kwamba utanipa *X-ray*. Nakushukuru kwa dhati kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makambako. Vilevile niombe sasa atakapotupa *X-ray* usisahau muwasiliane na wenzako wa TAMISEMI angalau tupate *Utra Sound* ili vifaa tiba hivi viweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaiomba Serikali angalau tupate fedha za kujenga wodi ya akina baba. Mlitupa fedha za kujengea wodi ya akina mama na watoto imeshakamilika na inafanya kazi katika Kituo hiki cha Afya Makambako bado wodi ya akina baba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tupate wodi ya akina baba kwa sababu jengo lililopo ambalo lilijengwa kwa ajili ya kuweka vifaa tiba vya *X-ray* na *Utra Sound* ndiyo vyumba kadhaa vimegawiwa vinafanya kazi kama wodi. Kwa hiyo, tunaomba tupate fedha kwa ajili ya kujenga wodi ya akina baba.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Serikali kwa kutupa fedha za kujenga hospitali ya halmashauri yetu shilingi bilioni moja na milioni mia tano. Kwa dhati nakushukuru sana kwamba sasa tunakwenda kupata ukombozi wa tiba kwa wananchi wetu wa Makambako.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna zahanati nyingi ambazo tumezijinga katika halmashauri yetu. Halmashauri yetu kwa kushirikiana na wananchi, mimi Mbunge, Waheshimiwa Madiwani na wadau wengine zimejengwa zahanati zaidi ya 13. Tulitegemea katika bajeti hii ambayo tunaendelea nayo angalau tungepata fedha kiasi ili zahanati kadha kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020 ziweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefikia mahali pazuri, zimeshapigwa lipu na kadhalika. Zimeshakamilika vimebaki vitu vidogo tu. Tumeshaanza kujenga nyumba za waganga katika zahanati hizo. Naomba Serikali ione umuhimu wa kutupatia fedha mwaka huu wa 2019/2020 ili baadhi ya zahanati hizi ziweze kukamilika. Hata hivyo, naishukuru Serikali kwa kuongeza fedha kwa ajili ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nimwombe Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Umyy Mwalimu, Kituo cha Afya mama cha Makambako kipo katika *center* kubwa ya Makambako, kwenda Njombe, Mbeya, Iringa na sehemu nyingine, mtuongeze dawa kwa sababu tunapata kwa kiwango kidogo sana wakati kituo hiki kilikuwa kama hospitali kabla ya kutupa fedha za kujenga hospitali. Nikuombe sana uone namna ya kutuongezea dawa ili kukidhi kuwahudumia wananchi wa Makambako.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Edwin Sannda atafuatiwa na Mheshimiwa Vedasto Ngombale, Mheshimiwa Aisharose Matembe ajiandae.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii. Nianze kwa kupongeza sana Wizara hii kwa wasilisho wao, nikupongeze Waziri (shemeji yangu), nikupongeze Naibu Waziri (kaka yangu) lakini pia na Makatibu wote Wakuu na watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri ambayo tunathibitisha kwamba mnaendelea kuifanya. Pia naunga mkono hoja hii iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali ya Mji wa Kondoa imeendelea kukua na kuongeza uhitaji wa huduma kwa maeneo mbalimbali. Hospitali ya Kondoa Mjini inahudumia zaidi ya halmashauri tano, tunazungumzia Vijijini, Chemba, Kiteto mpaka Babati na Katesh wengine wengi wanategemea huduma ya Kondoa Mjini. Mara baada ya

barabara yetu kumalizika, uhitaji umekuwa mkubwa kwelikweli. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wale watu ambao tulikadiria wataudumiwa na hospitali ile takribani 60,000 sasa imekwenda zaidi ya wagonjwa, siku hizi wanawaita wateja, zaidi ya 400,000 au 500,000, sasa tumekuwa na upungufu mkubwa sana kwanza ni suala la *ambulance*. Nimekuwa nikipigia kelele sana kuhusiana na kupata *ambulance*. Tumejitahidi tukakarabati iliyokuwa mbovu lakini tunaomba sana tupate *ambulance*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya barabara ile ya kutoka Dodoma kwenda Kondoa kumalizika ajali zimeongezeka, uhitaji wa wagonjwa kupatiwa rufaa kwenda Dodoma umekuwa mkubwa lakini hatuna *ambulance*. Mwaka jana hata Mbunge mwenzetu mmoja alipata ajali pale tulilazimika kuungaunga, unaomba Chemba, Kondoa Vijijini na ile mbovu ya kwetu kuwaleta majeruhi hapa Dodoma. Tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri na timu yako angalia Hospitali ya Mji wa Kondoa ipate *ambulance*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa uongezekaji wa mahitaji ya huduma hivyo hivyo hatuna *X-ray*. *X-ray* yetu imekuwa ni ya muda mrefu ni ya toka 2000, inaharibika mara kwa mara, ni ya zamani kweli kweli, inakaa hata miezi mitatu mpaka sita, sasa inatokea ajali watu inabidi kupata *X-ray* tu waje mpaka Dodoma. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri tuangalie kwenye hili suala la *X-ray* kwenye Hospitali ya Mji Kondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kuipongeza Serikali yetu kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya barabara. Sasa barabara imekuwa nzuri lakini pia na ajali na watu wanaopoteza maisha wanaongezeka, mochwari yetu ni ndogo na ya zamani sana, kichumba kile ni kidogo hata maeneo ya kuoshea, *fridge* ni mbovu na imezeeka. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri tuangalie kwenye Hospitali yetu ya Mji Kondoa tuweze kupatiwa mochwari



itakayokidhi mahitaji na haja ya huduma za afya pale Kondoaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtanzamo huo huo tena bajeti yetu kwenye *basket fund* inatuangalia sisi watu wa Kondoaa peke yake ilhali tunahudumia watu zaidi ya 400,000 au 500,000. Sasa hivi bajeti yetu kwa mwaka tupo kwenye milioni 32 wakati tukiangalia mahitaji inakwenda kwenye milioni 100 mpaka milioni 120. Hebu na hapo pia mtufikirie tuweze kuwahudumia wagonjwa ambao wanaitegemea Hospitali hii ya Mji Kondoaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri yetu wa Mji wa Kondoaa imegawanyika katika kanda kama tatu. Kanda ya kwanza ya Kusini, Kanda ya Kati ndiyo Hospitali ya Mji ipo pale na Kanda ya Kaskazini. Tunazo zahanati na tunashukuru Serikali tumepata kituo cha afya kimoja kwenye hii Kanda ya Kusini kwenye Kata moja Kingale. Watu sasa kutoka Ukanda wa Kusini wanakwenda kupunguza uhitaji wa kwenda mjini kwa ajili ya kufuata huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoomba tupatiwe walau kituo kingine cha afya kwenye hii Kanda ya Kaskazini katika Kata ya Kolo na jambo ambalo nimelongea sana kwenye Bunge letu hili Tukufu ili kuwaondolea adha ya kusafiri umbali mrefu wananchi hawa wa kutoka Ukanda huu wa Kaskazini kutafuta huduma za afya kwenye Hospitali ya Kondoaa Mji. Tukipata Kituo cha Afya, Kata ya Kolo, matokeo yake tutakuwa tumewasaidia watu wote wa Ukanda huu wa Kaskazini pamoja na Kata za Bolisa na majirani wa Sowera na kadhalika. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri tuweze kupatiwa kituo hiki cha afya ili tusogeze huduma karibu kadiri ya mpango na sera zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Vedasto Ngombale atafuatiwa na Mheshimiwa

Aisharose Matembe, Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu ajiandae.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuungana na Watanzania kwa msiba mzito uliotupata wa Dkt. Mengi. Sisi watu wa Kilwa tunamkumbuka sana Dkt. Mengi. Mwaka 1993 Mzee Kingunge Ngombale Mwiru alitisha harambee ya kuchangisha ujenzi wa sekondari ambapo Mheshimiwa Dkt. Mengi alitoa milioni 20, tutakukumbuka daima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala zima la kuhitaji mtaalam wa mionzi katika Hospitali ya St. Marks Kipatimu. Hospitali hii tayari tumepata *X-ray* mpya lakini hatuna huyo mtaalamu. Naomba Serikali itupatie huyo mtaalamu ili wananchi waweze kupata uduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili naomba nizungumzie gharama za utoaji maiti katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, kuna changamoto kubwa. Kama ambavyo tunafahamu Hospitali ya Muhimbili ndiyo hospitali kuu ya rufaa, kwa hivyo, wagonjwa wengi wakishindikana wanakwenda pale na upo uwezekano wakatibiwa kwa muda mrefu sana. Sasa kitokea mgonjwa amepata umauti kuna mtihani mkubwa wa gharama na kinachofanyika pale ni kuzuia maiti isitoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo kubwa sana hili na wauguzaji walio wengi wanashindwa kugharimia gharama hizo na matokeo yake ile maiti inazuiwa na hatimaye huenda kuzikwa na *city*. Naomba tuangalie upya utaratibu katika suala hili kwa sababu binadamu anastahili heshima na azikwe kwa mujibu wa mila na desturi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiti chako kilishawahi kutoa *ruling* kikasema kwamba marehemu hadaiwi, sasa hii sijui inakuwaje? Kusudio siyo kukopa ni kupata tiba na ni haki yake, sasa hana uwezo na yeye ameshafariki kwa nini wauguzaji

wasiruhusiwe kuchukua maiti wakamzike ndugu yao kwa heshima kubwa? Naomba Serikali iangalie suala hili ni tatizo kubwa, Wabunge tumekuwa tukipigiwa simu mara kwa mara kusaidia katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningeaona niliseme leo ni kuhusiana na suala nzima matibabu ya wazee na hii Sera ya Matibabu Bure kwa Wazee. Ni sera ambayo imeanza kutekelezwa lakini kwa kusuasua. Niishauri Serikali basi ilete Muswada wa sheria ili sasa iwe kwa mujibu wa sheria na siyo sera ili basi wazee wetu wa kuanzia miaka 60 waweze kupata matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizingumzie suala la Kituo cha Afya Njinjo pale kwangu, tungeomba Serikali itupatie fedha kama ambavyo vituo vingine vimepata. Kituo kile kimekuwa chakavu sana, tunaomba nacho kipatiwe fedha hizo ili kiweze kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia wananchi wameanza kujenga Kituo cha Afya Chumo na Somanga. Tunaiomba Serikali nayo itusaidie ili vituo hivi vikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala zima la UKIMWI. Wafadhili wameendelea kujiondoa katika kufadhili ugonjwa huu. Kwa mfano, hawa wenzetu *PEPFAR* wao wenyewe wamepunguza msaada wao katika suala nzima la UKIMWI kwa kiasi cha dola milioni 119. Hii ni kwa sababu kasi ya kupima bure kufikia asilimia 90 ni kama inaenda kwa kusuasua. Kwa hiyo, ni nini mkakati wa Serikali wa kuwaruhusu wananchi wajipime binafsi kwa kutumia kile kipimo cha mate. Naomba Serikali iharakishe ili wafadhili hawa waendeleo kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala zima la homa ya ini. Sisi Wabunge tumepata chanjo ya homa ya ini ni vizuri lakini Watanzania walio wengi bado hawajapata chanjo hii. Niiombe Serikali iangalie uwezekano wa kutoa chanjo hii kwa Watanzania wote kwa sababu ugonjwa huu ni hatari na unatishia amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la bima ya afya kwa wote. Mimi ni miongoni mwa Wabunge tuliotembelea nchi ya Rwanda kuona namna gani wenzetu wanatoa hii bima ya afya kwa wote. Wenzetu wamefanikiwa sana na wanachokifanya ni kuhusisha wahudumu wale wa ngazi za chini, wanawapa majukumu na wao ndio wanafanya ushawishi kwa wananchi lakini wanawa-*train* kiasi kwamba wawe wanaweza kutoa huduma ya kuzalisha, kuchoma sindano na vitu vya namna hiyo. Niombe Serikali ije na huu Muswada wa Sheria ili basi huduma ya bima ya afya itolewe kwa watu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Aisharose Matembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo ajiandae.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii muhimu ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kutuwezesha kufikia mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. Niwatakie Waislam wote kheri ya Mfungo wa Ramadhani hususani wananchi wa Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya chama changu chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwatumikia wananchi wa Tanzania. Uzalendo uchapakazi wake maono amejipambanua ni kiongozi makini na ni mfano wa kuigwa Mheshimiwa Rais endelea kuchapa kazi sisi Watanzania tuko nyuma yako na tunakuombea sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Afya dada yangu Ummy Mwalimu,

Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndungulile, Katibu Mkuu bi. Zainab Chaula pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Afya hakika wanafanyakazi nzuri sana. Nimekisoma kitabu hiki cha hotuba ya afya kwa namna kilivyopangwa na kilivyochapishwa, inaonyesha viongozi wa Wizara hii wako makini sana nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika afya ndiyo utajiri na afya ndiyo mtaji wa kila mwanadamu. Niipongeze sana Serikali kwa juhudi kubwa inazochukua za kuboresha huduma za afya nchini kote. Kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Singida ninaomba kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutupa zaidi ya shilingi bilioni 5 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya 11, katika wilaya zangu zote za Mkoa wa Singida tumepata Kituo cha Afya Mkalama, Iramba, Singida Manispaa, Singida Vijijini pamoja na Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Namshukuru sana Mheshimiwa Rais hakika uwepo wa vituo hivi vya afya umeokoa sana vifo vya akinamama na watoto. Lakini Sera ya afya inasema kwamba kila kata iwe na Kituo cha Afya, basi niombe pamoja na uwepo wa vituo hivi vya afya jiografia ya Mkoa wangu wa Singida ni ngumu sana niombe vituo vya afya viongezwe ili wananchi waweze kupata huduma bora za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishukuru sana Serikali kwa kutupa bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa hospitali za wilaya, hospitali ya Mkalama na hospitali ya Singida DC. Sasa hivi ziko katika hatua ya ujenzi na mwaka huu pia katika bajeti hii tumepata hospitali kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya ya Ikungi naishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na pongezi hizi na shukrani hizi mkoa wangu wa Singida una changamoto lukuki katika sekta ya afya. Nikianza na hospitali ya Wilaya ya Manyoni, hospitali hii ilijengwa kama kituo cha afya mwaka 1971 na ni ya muda mrefu. Kwa hiyo, majengo ya *OPD* limeshakuwa ni finyu na dogo, wodi ya akinababa, wodi

ya watoto, wodi ya majeruhi haiendani kabisa na idadi ya watu katika wilaya hii ya Manyoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na ifahamike kwamba wilaya ya Manyoni ipo katika barabara kuu ya Mkoa wa Singida na Dodoma na ajali nyingi zimekuwa zikitokea kwa hiyo inakuwa ni changamoto sana kuwahudumia wagonjwa au majeruhi inapokuwa majeruhi hawa ni wengi ninalomba sana Serikali itupatie fedha ili tuweze kujenga hospitali mpya ya Manyoni itakayoendana sambamba na idadi ya watu kwa wilaya yangu ya Manyoni lakini pia vilevile iweze kutoa huduma bora zaidi za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu hospitali yangu ya Rufaa ya Mkoa wa Singida, hospitali hii ina changamoto nyingi na hospitali hii ilianza kujengwa mwaka 2009 ni takriban sasa miaka tisa imepita hospitali hii haijakamilika lakini jambo kubwa la kusikitisha hospitali hii ya rufaa kwa mwaka wa fedha uliopita haijatengewa fedha zozote na inatoa huduma katika maeneo mawili ipo hospitali ya rufaa ambayo ni ya zamani, ipo katika Kata ya Ipembe, lakini pia hospitali ya rufaa ambayo ni mpya iliyoko katika Kata ya Mandewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jambo hili linapelekea kwa kweli ugumu katika uendeshaji wa hospitali hizi mbili kwa wakati mmoja. Nimuombe Mheshimiwa Waziri najua ni msikivu na ananisikia ifike wakati sasa zitengwe fedha za kutosha ili kumaliza ujenzi wa hospitali hii.

Mheshimiwa dada yangu Umyy ninakuomba sana kwa kuwa sasa imepelekea bajeti ndogo ambayo tunaipata kulipia bili za maji, umeme, ulinzi na usafi... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pili ilishagonga. Asante sana.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nauunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mheshimiwa Mussa Mbarouk ajiandae.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kupata nafasi hii. Nianze kwanza kwa kumshukuru mwenyezi mungu kwa kutujaalia leo kuweza kujadili bajeti hii ya Wizara ya Afya. Lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano Dkt. John Pombe Magufuli, halikadhalika nimpongeze Waziri wa Afya Mheshimiwa Umy Mwalimu na Naibu wake Mheshimiwa Faustine Ndungulile, Katibu wa Wizara wajina wangu Zainab Chaula pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri wanayoifanya na wala haina kificho kwa sababu tunaona na tunashuhudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ambalo tunaliona katika awamu hii ambayo limefanywa kwa juhudi kubwa ni Taasisi ya Moyo ambayo wameweza kupeleka vifaa vingi vya kisasa wameleta wataalam kutoka nje pamoja na wataalam wa ndani wakisimamiwa na Prof. Jannabi tunawapa pongezi nyingi sana kinachobakia hapo ni kuhakikisha wale wagonjwa ambao wako nje ya mji wa Dar es Salaam, wako nje ya mikoa wako vijijini wengi wapo wanaopata matatizo ya moyo elimu ipelekwe na utaratibu uelekezwe jinsi gani tunaweza tukawatoa kule wakaja kupata huduma hapo kwenye Taasisi ya Moyo Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo limeshirishwa kwamba Wizara yetu pamoja na Serikali imesimama kidete kuweka madaktari wengi, kuweka vifaa tiba vingi matokeo yake idadi ya wagonjwa ambao ilikuwa wanakwenda kutibiwa nje imepungua kutoka 683 2014/2015 hadi wagonjwa 62 kwa mwaka huu tunaongea leo hii inabidi tuwapongeze na ningekuwa kwenye mkutano wa nje ningesema watu wote wawapigie makofi Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, twende kwenye suala la matibabu lakini kupitia bima ya afya, bima ya afya ni suala ambalo ni muhimu kwa Taifa letu bado Serikali ina jukumu la kuhakikisha Watanzania wote wanapata elimu na kujua faida na umuhimu wa bima ya afya. Baadhi ya Wabunge humu ndani wamezungumza jinsi mgonjwa anavyoenda kutibiwa anakutwa na deni kubwa anashindwa kulipa maiti zinashindwa kutolewa kwa sababu ya deni lakini elimu ya bima ya afya ikitolewa vya kutosha yule mtu hatodaiwa na niseme tu kwa maiti za kiislamu lazima itangazwe anadaiwa au hadaiwi?

Sasa kama anadaiwa tunamtwisha mzigo ambao haustahili nishauri tu suala la bima ya afya liendeleo kutolewa elimu na ikiwezekana uwekwe utaratibu wa kuwa na bima ya afya ambayo kila mtu ataimudu, kila mtanzania atamudu na kila mtanzania ataitumia hiyo bima ya afya kokote kule isiwe tu kama mimi natoka Mkoa wa Pwani basi bima ile iishie Pwani hapana siku nikipelekwa Muhimbili nitatibiwa na tiba gani kwa hiyo naomba hilo nalo litizamwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Sera ya tiba ya wazee hili lifanyiwe bidii wakati ndiyo huu unakuta wazee wengi ukienda huko kwa watani zangu Shinyanga wengi wanapigwa wanauwawa hawana mahala pa kukimbilia mpaka wapate hifadhi kwa hiyo kuna haja ya kutengeneza sera si tu matibabu waangaliwe na mambo mengine muhimu wazee wote watarajiwa ndiyo sisi na wengine wanakuja weze kupata utaratibu mzuri wa sera ya wazee kwa ajili ya maisha yao na tiba halikadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kuhakikisha elimu ya afya ya mama mzazi mtarajiwa ilivyoboreshwa lakini bado kuna haja na kuna kila sababu hawa akinamama huko chini zahanati zetu tumeziboresha, vituo vya afya tumeboresha tuhakikishe basi wanakwenda hospitali. Nimeona takwimu kwenye jedwali humu kwamba wanatakiwa waende mara nne katika kipindi cha ujauzito lakini wengi wamekwenda mara moja wengine mara mbili bado kuna haja ya kuboresha zahanati zetu na vituo vya



afya ili mama mjamzito ashawishike kwenda kwa sababu kwingine huduma hazipo zipo mbali kwa hiyo inamuwia vigumu kuna haja ya kuongeza miundombinu ya vifaa tiba na hata watumishi katika zahanati zetu katika vituo vya afya ili waweze kwenda sambamba na mahitaji ya jamii wanayowazunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nagusa kidogo kidogo kwa sababu muda hautoshi.

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa. Ahsante sana.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Mbarouk, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia na kipekee nipongeze sana hotuba ya kamati pamoja na hotuba ya Kambi ya Upinzani ambapo ni mwanakamati. Ninaomba sana Wizara itekeleze yale yote hasa maoni hayo ambayo kwa kweli ni ya msingi na ninaamini mkiyachukua tutaboresha sana sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa suala zima la bajeti. Wizara hii kama ambavyo wote tunajua ni Wizara muhimu sana kwa afya ya Taifa letu na hata hivyo tunavyosema kwamba Tanzania ya viwanda haitawezekana kama rasilimali watu wetu watakuwa wagonjwa na hawapati huduma bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba Wizara hii pamoja na kutengewa bajeti kubwa tulipitisha takriban shilingi trilioni moja lakini kwenye fedha za maendeleo tulipeleka bilioni 561 mpaka leo tunapozungumza imeenda shilingi bilioni 91 tu sawa na

asilimia 16, hivi kweli asilimia 84 ya fedha tulizozipitisha ndani ya Bunge hili bado hazijapatikana na tunafikia mwisho wa mwaka tunaomba kujua ni kwa kiasi gani tunategemea ubora wa huduma za afya kama fedha ambazo tumekaa hapa ndani kwa kipindi cha miezi mitatu haziendi tunaiuliza Serikali tuna sababu gani ya kukaa hapa Bungeni tunapitisha fedha nyingi kiasi hicho ambacho tunaamini zinaenda kufanyakazi lakini fedha hazitoki huku tukiambiwa kwamba Serikali inakusanya fedha fedha nyingi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atapokuja ku-*windup* atuambie hivi hiyo asilimia 84 inategemewa kwenda lini na hizo huduma zote ambazo zimekwama kwa huu muda ni kwa kiasi gani wananchi wame-*suffer* ni kwa kiasi gani watu wamefariki kwa sababu ya kukosa hizi fedha? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo kutokana na uchache huu wa fedha naamini ndiyo sababu tunakuwa na matatizo mengi kwenye Wizara hii. Kwa mfano kuna watu wengi sana wanaenda kwenye hospitali wanafanyiwa vipimo lakini vipimo vinakuwa tofauti na ugonjwa alionao. nitatoa mifano hata Waziri akiita baadhi ya Wabunge ambao wamepata matatizo hayo ni wengi sana. Kwa mfano majuzi hapa niliangalia kwenye TV kuna binti mmoja amepimwa Muhimbili, amekutwa na matatizo ameambiwa ana matatizo ya ini, ini limeungua amekaa karibu anakufa amepelekwa India *only to find* ana matatizo ya moyo sasa watu wa namna hii wako wengi kiasi gani. Nilikuwa naomba Waziri atuambie tatizo ni uelewa wa madaktari wetu au *technician* au tatizo ni vifaa tulivyonyavyo haifanyi kazi nilikuwa naomba hilo sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la magonjwa yasiyoambukiza limekuwa kubwa sana na tatizo kubwa sasa hivi pamoja na *diabetes* ni pamoja na tatizo kubwa la kansa. Leo tunavyozungumza ni hospitali mbili tu za Serikali zina mashine ya mionzi yaani *radiograph* sasa na hii iko hospitali ya *Ocean Road* na hospitali ya Bugando lakini tuna hospitali zaidi ya mbili za rufaa tuna hospitali ya Kanda ya Mbeya,

tuna hospitali ya Kanda ya Kilimanjaro kwa maana ya KCMC Kanda ya Kaskazini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nipo kwenye kamati ya maendeleo ya jamii kwa muda mrefu madaktari au wakuu wa hospitali hizi mbili kilio chao kikubwa kimekuwa ni fedha kwaajili ya kununua *bunkers* kwa ajili ya kuweka hizo *bunkers* ili waweze kuweka hizo mashine hospitali ya KCMC na hospitali ya Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna sababu ya kupandisha hadhi au kuwa na hospitali za Kanda kama hatuna vifaa. Kwa hiyo, tatizo la *Ocean Road* kuwa na mrundikano litakuwa palepale kwa sababu wagonjwa katika Kanda kwa mfano Nyanda za juu kusini, wagonjwa katika Kanda ya Kusini, wagonjwa katika Kanda ya Kaskazini, wanapopata matatizo ya kansa wameshakuwa wameshatambulika wana kansa wanatakiwa wapate mionzi hawapati mionzi wanatakiwa tena waende *Ocean Road* kwa hiyo tunarudisha tatizo palepale. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ukiangalia hata kitabu cha maendeleo cha mwaka huu hakuna fedha yeyote ya maendeleo iliyotolewa katika hospitali ya KCMC wala hospitali ya Mbeya. Kwa hiyo, wagonjwa wetu katika maeneo husika wataendelea kufariki kwa kukosa huduma za msingi kwa sababu tunaambiwa huduma kansa inaweza ikatibika kama imeweza kujulikana mapema lakini watu wamegundua lakini bado hawana *access* kwenye hizo hospitali, kwa hiyo. nilikuwa naomba hilo pia Waziri atusaidie. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala zima la watumishi ni wazi kwamba watumishi wa Wizara ya Afya, sekta ya afya kwa ujumla wake ni wachache sana na Waziri wanakiri ni karibu asilimia 50 lakini vijijini asilimia mpaka 74 hakuna wauguzi, hakuna wataalam wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa na tunaendelea pia kujenga vituo vya afya tunaendelea kujenga zahanati lakini suala la watumishi halijaonyeshwa. Inasikitishwa kuambiwa

kwamba ni kwasababu ya kuondolewa kwa wale waliokuwa na vyeti feki, sijui waliokufa. Wewe unatambua kwamba kama ikama ipo tayari na fedha zao za mishahara zipo sasa kama hawa wameondolewa *replacement* ipo madaktari wapo kibao wana-*graduate* lakini vilevile wauguzi wanajaa sasa hoja ni nini hapa watuambie labda Serikali haina fedha lakini kutuambia wanaendelea na uhakiki na uhakiki wakati hawa watu walikuwa kwenye ikama na fedha zao zipo maana yake ukimuondoa, lazima umrudishe ambaye yupo na wapo mitaani ukipiga filimbi hapa madaktari ambao wako mitaani wapo kibao manesi wako kibao kwa sababu kila siku kila mwaka wana-*graduate*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa kweli tunaendelea kuweka afya za watu wetu rehani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nielezee kwamba ni makamu mwenyekiti wa Baraza la Wazee wa chama changu na kwa maana hiyo sina budi kuongelea suala la wazee, toka nimeingia kwenye Bunge hili tumekuwa tukiambiwa tuna Sera ya wazee toka 2001 lakini mpaka ninavyozungumza sheria haijaja na ndiyo sababu wazee wanaendelea kudhalilika katika nchi hii. Wazee wanaendeshwa kwa sera kwa miongozo kwa taratibu lakini hakuna sheria nilikuwa naomba kila siku tunapigwa danadana tuwambia kwanini wanasema wanaendelea kuboresha, wanaendelea kufanya hivi lakini kwa nini msilete sheria? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli hatuoni aibu kwamba wazee hawa ndiyo wametulea wazee hawa ndio wameleta uhuru katika nchi hii lakini wazee hawa leo mmesema mara mtawapa vitambulisho, mara sijui mtawapa nini lakini wazee hawa wananyanyasika kwelikweli na ninajua kwamba siyo wazee wote hawana uwezo lakini hata wale wasio na uwezo ikija sheria itawatambua kwa sababu hata leo nikimuuliza Waziri mwenye dhamana tuna wazee kiasi gani katika nchi hii sidhani kama wana-*database*. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana suala la wazee ni la muhimu lakini vilevile suala la pensheni ya wazee ni la muhimu siyo wazee tu waliokuwa wanafanyakazi, hata wasiokuwa na kazi

walitakiwa walau wawe na posho ambayo itawasaidia kujikimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nije kwenye suala la ndoa za utotoni limeelezwa kwa kina lakini niseme ni jambo la aibu sana kuona kwamba sheria yetu ya mwaka 71 bado ndiyo tuliyonayo lakini kipekee niseme kwamba jambo hili lilipelekwa mahakamani na tayari limeshakuwa *ruled out* kwamba sheria hiyo ibadilike vile vifungu vilitakiwa vibadilishwe lakini kinachosikitisha Serikali kupitia AG wamekata rufaa.

Sasa nashindwa kuelewa hivi ni kweli tunataka watoto wetu waolewe katika umri huo? Sheria ya mwaka 71 wakati tulikuwa hatuna shule leo tunasema kila mtoto aende shule yeye eti sheria bado ni ileile kwahiyu kuna *confusion* na ni lazima huo utata uweze kutatuliwa kwa sisi Wabunge kukaa pamoja na kuona umuhimu wa kubadili sheria hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo nilitaka kuzungumiza ni suala zima la huduma ya unasihi. Tuna matatizo makubwa sana Tanzania. Sasa hivi kuna suala *stress* na sonona (*depression*) na hii inatokana na changamoto za maisha ikiwa ni pamoja na kutopandishwa mishahara ikiwa ni pamoja na vyuma kukazwa na mambo mengi. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hili linahitaji ushauri nasaha. Tuna vyo vyetu vya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii, hasa cha Ustawi wa Jamii...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan kengele ya pili ilishagonga. Ahsante sana. Nilikuwa nasubiri umalize hoja yako muhimu.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwanza.

**NAIBU SPIKA:** Zimeshagonga mbili Mheshimiwa. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mussa Mbarouk, dakika tano atafautiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na Mheshimiwa Margaret Sitta ajandae.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Labda nami niungane na wenzangu katika kutoa pole kwa Watanzania wote baada ya kuondokewa na mzee wetu, Reginald Mengi. Namkumbuka tu Tanga, baada kuanzishwa kwa *ITV* alituletea *television* kubwa sana pale katika uwanja wa Tangamano ikawa wananchi wa Tanga wanapitia taarifa na burudani mbalimbali kupitia katika television hiyo. Mwenyenzi Mungu amweke mahali panapostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba katika taarifa ya Kamati iliyotolewa, kuna upungufu ulielezwa kwamba Kamati ilivyotembelea miradi, miradi mingi ilikuwa haijapelekewa fedha za kutosha. Vile vile hata ukingalia katika bajeti, nayo inakuwa imetekelezwa kwa 16% badala ya 100% na 84% bado haikuweza kutimizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwape pongezi Mheshimwia Waziri na Naibu wake wa kufanya kazi katika mazingira magumu. Pamoja na hivyo, naitaka Serikali nayo sasa iangalie kwamba Wizara ya Afya ndiyo kitengo au Wizara muhimu katika maisha binadamu, kwa sababu binadamu bila kuwa na afya bora hapawezi kukawa na uzalishaji mali, hapawezi pakawa na Jeshi ambalo lina ngumu kamili, lakini pia sekta mbalimbali zinaweza kufeli kama watumishi watakuwa hawana afya bora. Kwa hiyo, pamoja na mazingira magumu, lakini endeleeni kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba wakati mwingine lazima Serikali yetu nayo inapopanga bajeti, basi ihakikishe kwamba bajeti inapelekwa. Kuna jambo lingine gumu ambalo naliona katika bajeti zetu, mafungu makubwa ya fedha tunategemea katika fedha za wahisani.

Wakati mwingine wahisani nao ama hawatuletei fedha kwa wakati ama wanatoa visingizo na matokeo yake fedha hizo zinakuwa haziji na matokeo yake mambo hayakamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niende katika hotuba hii ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kuna eneo limesema kwamba kwa mwaka wanakufa akina mama wajawazito 11,000,000, sawa na akina mama 30 kila siku kutokana na vifo vya uzazi. Kwa nchi kama Tanzania ambapo kuna Madaktari wasomi wakubwa, ina rasilimali nyingi; kushindwa kulishughulikia suala hili kwa kweli naona ni tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika akili za kawaida, kila siku kuna akina mama 30 wanapoteza maisha kutokana na vifo vinavyotokana na uzazi. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atueleze, wana mkakati gani wa kupunguza vifo hivi? Kwa sababu Watanzania 30 kupoteza maisha kutokana na vifo vya uzazi, hii idadi ya ni kubwa sana. Kwa mwaka watu 11,000,000. Hili siyo jambo dogo. Yakipangwa majeneza hapa 30 kwa siku au kwa mwaka kwamba ni watu 11,000,000 ni idadi kubwa sana. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atueleze wana mpango gani kuhakikisha jambo hili linakwisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine limezungumzwa hapa kwamba katika Mkoa wa Tabora kuna Wakunga wanaozalisha kwa kutumia mifuko ya rambo au mifuko ya plastiki. Serikali imeshapiga marufuku mifuko ya Rambo, sijui Wakunga huko Tabora watatumia vitu gani katika kuzalisha akina mama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo halitoshi, kwenye ziara ya Mheshimiwa Rais alipokwenda Malawi, amepata taarifa moja ilinifariji, kwamba Malawi wameweza kuanza kutoa chanjo ya Malaria. Malawi ndiyo nchi ya kwanza Barani Afrika kuanza kutoa chanjo ya Malaria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind-up* naomba atueleze, nasi Tanzania

tuna mpango gani wa kutoa chanjo ya Malaria ili nasi tuwe nchi ya pili Barani Afrika kwa kutoa chanjo ya Malaria? Tukumbuke kwamba kila dakika tano, Tanzania Malaria inaua Mtanzania mmoja. Sasa hili nalo naomba tuje tuelezwe, tuna mpango gani na sisi kuwa nchi ya pili kutoa chanjo ya Malaria?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nirudi kwenye...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na Mheshimiwa Selemani Kakoso, ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Naomba niipongeze sana Wizara ya Afya. Kipekee kabisa nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Katibu Mkuu wake. Wao wanajua ni kwa nini nawapongeza. Bila jitihada zako Mheshimiwa Ummy ukishirikiana na mama wakati akiwa TAMISEMI, sisi watu wa vijijini huko Nzera tusingekuwe na Hospitali. Nataka nikuhakikishie kazi mliyoifanya ni kubwa sana na tutawakumbuka milele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa nazungumza mara nyingi, hii Wizara wakati tunaanza Ubunge ilikuwa ni Wizara ambayo kila mtu anailalamikia, lakini leo Wizara hii ukisikiliza michango ya Wabunge, nadhani mwaka ujao tutakuwa tunaijadili siku moja tu mambo yanaisha tunapitisha bajeti. Hata kama kungekuwa na tuzo ya kutunzwa Mheshimiwa Waziri anayefanya vizuri, kiukweli bila upendeleo Mheshimiwa



Ummu unastahili kuwa Waziri bora kabisa katika Bunge la 2018.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, alipopita kule kwetu aliahidi hospitali, umetupa. Jimbo zima watu laki 500,000 hatuna kituo cha afya. Kwa huruma yake alipandisha vituo viwili. Tusaidiwe pesa ili tuweze kupata kituo cha afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunajenga Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita. Hii hospitali imesimama toka mwezi wa Kwanza, *certificate* hawataki kulipa. Lipeni *certificate* tuweze kujenga hospitali yetu. Kuna tatizo gani? Tunategemea hiyo hospitali ndiyo iwe hospitali ya kutukomboa sisi watu wa Geita. Tuko zaidi milioni tano na kitu. Tusaidieni kulipa hiyo *certificate* ili waweze kuendelea kujenga hospitali yetu ya mkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri sana kiukweli, alipofanya ziara kwenye Hospitali ya Rufaa ya Bugando alitualika Wabunge wa Kanda ya Ziwa, nami nilikuwepo. Bahati nzuri Gwajima alikuwa bado Wizarani, naye alikuwepo. Niwapongeze sana. Katika miaka yote inaoneka kweli Serikali mmekuwa *serious* kutukomboa sisi watu wa Kanda ya Ziwa. Ninaona kabisa jitihada za Serikali kujiona ni sehemu ya ile Hospitali ya Kanda ya Ziwa ya Rufaa ya Bungando. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale tukiwa na Mheshimiwa Waziri tulizungukia majengo, aliyaona majengo mazuri, lakini kule ndani hakuna *MRI* na wagonjwa wengi wanatoka Kanda ya Ziwa. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri aweke mpango mkakati tununuliwe *MRI*, watu wetu wanakufa kwa kukosa gharama za kufuata *MRI* Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunaishukuru Serikali. Tunatibu wagonjwa wa saratani. Wagonjwa wa saratani Tanzania wanaongoza toka Kanda ya Ziwa. Tunaomba mlete wataalam wakae Mwanza. Mtu wa kuanzia Singida hana nauli ya kuja Dar es Salaam, atakuja Mwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia watujengee wodi, pamoja na kwamba vifaa vipo, lakini mtu anapotaka kufanyiwa *operation*, hakuna wodi ya kuwalaza wale watu. Kwa hiyo, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri kwa ukaribu alionao, namkushukuru sana Mheshimiwa Waziri na ninamwomba sasa awe karibu na hiyo hospitali aweze kutasadia watu wa Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunashukuru, juzi nilitembelea nikaona; mlituhidi kutujengea jengo la *TB*kama la Kibong'oto na lenyewe limejengwa kwa shilingi milioni 120. Ni suala ambalo kweli tunaona Serikali mpo karibu na watu wa Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia waliahidi kutoa matibabu ya bure kwa wagonjwa wenye saratani. Tunaona, tunatuma watu wetu wanasaidiwa masikini bure. Tunaiomba Serikali ingalie kwa jicho la huruma, ikamilishe vitendea kazi kwenye hospitali yetu ya Bugando. Hiyo ndiyo hospitali kombozi kwenye kanda ya ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Umyy anakumbuka, wakati tulikuwa tunaenda, hospitali ilikuwa inakusanya shilingi bilioni mbili. Leo inakusanya shilingi bilioni tisa. Na mimi napenda huyu mtu mngempongeza Wabunge wa Kanda ya Ziwa. Kutoka shilingi bilioni mbili hadi shilingi bilioni tisa na siyo matibabu ya kugombana, ni matibabu rafiki; leo watu hawaendi hospitali za mtaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani ilikuwa ukiambiwa unaenda Bugando unajihesabu unaenda kufa, lakini leo ukifika pale unatibiwa vizuri, unakaribishwa vizuri na watu wanatoa pesa zao bila wasiwasi. Watu kama hawa, Wakurugenzi akina Makubi wangukuwa wanaalikwa kwenye Mabunge kama haya tunawapa pongezi na wao wanajisikia ili waweze kwenda kuongeza morali.

**MBUNGE FULANI:** Yuko hapo.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Yuko hapa, nashukuru sana Mheshimiwa Waziri. Leo ukienda Bugando, ni kweli kabisa, hata *operation* za mitaani zimepungua. Watu wanapewa motisha kule ndani, Bugando imekuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni hayo. Nakupongeza sana Mheshimiwa Umyy; ya Jimboni kwangu unikumbuke lakini na hospitali yetu ya Bugando hatuhitaji sana kuwafuata Madaktari Dar es Salaam, tunataka tutibiwe Mwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuruku sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge, wakati mwingine mnaweza mkakosa majibu kwa ku-*address* watu mahsusi. Humu Bungeni kinakuwa *addressed* kiti. Kwa hiyo, inabidi uzungumze na anayezungumza hapa mbele na sio moja kwa moja na Waziri.

Mheshimiwa Umyy pongezi zote hizo zimekuja lakini zilitaka kuja moja kwa moja hivi. Kwa hiyo, tuzungumze na kiti kwa sababu wakati wa majibizano huwa tunapata changamoto kidogo, lakini Bunge likiwa limetulia namna hii tunayaacha yanaenda. Tukumbuke tu kuzungumza na kiti badala ya kuzungumza na mwenye hoja moja kwa moja.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Kakoso na Mheshimiwa Oscar Mukasa ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi name nichangie hoja iliyoko mezani. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, lakini bado naendelea kuwashukuru wananchi wa Urambo kwa kunipa ushirikiano. Nami niungane na wenzangu kuipa pole familia iliyoondokewa na Mzee wetu, Marehemu Reginald Mengi, naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawajibika kuishukuru sana Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na kadhalika kwa jinsi ambavyo wanachapa kazi katika Awamu hii ya Tano. Namwomba Mwenyezi Mungu awabariki sana Mheshimiwa Umy mwenyewe ambaye anathibisha wanawake wanaweza. Pia nampongeza Mheshimiwa Dkt. Ndungulile kwa namna anavyochapa kazi na Mwenzie. Nampongeza pia Katibu Mkuu, Dkt. Chaula, kwa kweli hawa watu wanafanya kazi wakisaidiwa na wafanyakazi. Mwenyezi Mungu awapeni nguvu, endeleeni kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni shukrani kwa niaba ya wananchi wa Urambo kwa kumaliziwa Kituo cha Afya cha Usoke. Naishukuru sana Serikali kwa kutupa shilingi milioni 400 kwa kumalizia Kituo cha Afya cha Usoke na sasa hivi wametuongezea kimoja ambacho kinaendelea kujengwa katika Kata ya Yumbu Usoke Mlimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukurani hiyo, naomba nielezee Serikali kwamba sisi kama Urambo tuna kata 18. Maana yake ni kwamba kituo hiki cha pili kikimalizika tutakuwa na vituo viwili vya afya. Ni ombi kwa niaba ya wananchi wa Urambo kwamba tuongezewe kituo cha afya angalau katika Kata ya Songambe; na ikiwezekana hata viwili katika kata pia ya Vumilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la uwazi kwamba sisi kama Urambo bado tunahudumia Wilaya ya Kaliua ambao bado; ukienda kwenye wodi ukitembelea wagonjwa waliolazwa utashangaa, wengi wanatoka Kaliua, wengine wanatoka kwa jirani zangu Uyui hasa maeneo ya Ndonu na mpaka Uvinza sisi tunapata. Kwa hiyo, tunapomba huduma ya afya kuongezewa ni kwa sababu pia tunahudumia wananchi wanaotoka katika maeneo ya jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Waziri Umy. Alikuwa kufanya ziara na ziara yake ilizaa matunda. Tulipoenda Usoke alifurahishwa sana na kazi iliyofanywa pale Usoke ya kumalizia kituo cha afya ambapo ulikuwa ni mradi uliokuwa wa ADB tangu 2010. Mheshimiwa

Ummy alifurahi kwa jinsi ambavyo kituo kilimalizwa vizuri na akaahidi kwamba majengo mengine ambayo yapo yanaharibu sura ya kituo kile kwamba atatoa shilingi milioni 50. Mheshimiwa Waziri tunashukuru sana kwa ahadi yako, naamini itatimizwa tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kituo cha Afya cha Usoke kilikuwa ni mabaki ya mradi wa *ADB*, *ADB* iliacha mradi mwingine ambao bado haujakamika. Inasikitisha kwamba tangu mwaka 2010 *theater* ambayo ipo karibu na wodi ya akina mama ilianza kujengwa pale, sasa hivi iko kwenye ngazi ya lenta, kwa kujua kwamba wakitoka pale *theater* wanaingizwa kwenye wodi ya akina mama. Mpaka leo haijaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali imalize ilie *theater* nasi tunaamini kwamba tukipewa shilingi milioni 200 itamaliza hiyo *theater* ili akina mama ambao wapo karibu, ambao walikuwa walengwa, wakitoka *theater* pale wanaingia wodini na *vice versa*, wakitoka wodini wanapelekwa *theater*. Tunaomba *theater* ikamilishwe ambayo iko kwenye ngazi ya lenta. Inasikitisha, jengo zuri lakini tangu 2010 halijaisha ambayo itausaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi *theater* kwa kuwa tunahudumia na watu kutoka maeneo mengine, wengine inabidi wasubiri lakini *theater* ikiisha wagonjwa, wakiwepo akina mama na watoto watanufaika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika tuna mradi mwingine ambao uliachwa, ni mradi wa *LGDB* ambapo ni *ICU*. Huwezi kuamini Urambo hatuna *ICU* na ni Hospitali ya Wilaya. Tunaomba kwa heshima na taadhima kabisa Awamu ya Tano itusaidie tuwe na *ICU* na sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika na *X-Ray*, nimeshukuru Wabunge wengine wamesimama hapa wanafurahi kwamba tuna *X-Ray* ya kisasa ya kidijitali, sisi bado tupo kwenye *analogy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisaidie nawe kuiomba Serikali itusaidie *X-Ray* ya kisasa. Kwa sababu hata haya majibu tunayopata sasa hivi tuna wasiwasi nayo, kwa sababu bado tupo kwenye enzi ya Ujima, tunatumia *X-Ray* ya *analogy*. Tunaomba tusaidiwe hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, suala la wafanyakazi ni la muhimu sana. Bado tuna uhaba wa wafanyakazi kwa asilimia 48. Tunaomba nasi mtakapokuwa mkipanga wafanyakazi mtukumbuke nasi Urambo tuongezewe wafanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifurahi sana ziara ya Mheshimiwa Waziri Umyy. Namwomba Mwenyenzi Mungu ampe afya ili arudi tena aone mabadiliko gani tumeyafanya tangu alipotoka. Kuna maneno mazuri uliyaacha Urambo bado watu wanakukumbuka nayo na hasa pale ulipokumbuka kile Kituo cha Afya cha Uyogo kinachojengwa kwa kushirikiana na Waingereza. Nawe ulitaka kuonyesha kuunga mkono nguvu ya wananchi na marafiki zao kutoka Uingereza ukaahidi shilingi milioni 20. Tushukuru sana kama utawapa shilingi milioni 20 Uyogo ili wamalizie kituo chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya yote, bado wanamkumbuka Mheshimiwa Waziri alipotamka neno la maana sana kwamba atawapa *ambulance*. Kwa sababu wao wapo mbali na Hospitali ya Wilaya, akiwapa *ambulance* itawasaidia sana kuwawahisha akina mama hasa wanaokwenda kujifungua usiku, maana yake saa za kujifungua huwa hazijulikani; usiku na kadhalika, *ambulance* itasaidia sana. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika Mheshimiwa Waziri alipokwenda zahanati ya Itebulanda, aliahidi nako shilingi milioni 20. Mheshimiwa Waziri tuna imani kabisa utatimiza kwa sababu uliipenda sana ile zahanati, inafanya kazi vizuri na imeanzisha wodi ya akina

mama na kwamba utawaunga mkono kwa shilingi milioni 20.

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umeisha Mheshimiwa. Ahsante sana.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, nashukuru Wizara nzima na ninaunga mkono hoja. Endeleeeni kuchapa kazi. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Selemeni Moshi Kakoso atafutiwa na Mheshimiwa Oscar Mukasa, Mheshimiwa Khatib Haji ajjandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii kuweza kuchangia hotuba ya Wizara ya Afya. Awali ya yote, niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo anayoifanya akisaidiana na wasidizi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu imefanya kazi karibu maeneo yote ya nchi yetu. Mkoa wa Katavi hatuna Hospitali ya Mkoa. Mheshimiwa Waziri anafahamu na fedha ambazo zimetengwa na Wizara ni kidogo sana. Tulikuwa tunaomba Mheshimiwa Waziri aangalie mazingira ya Mkoa wa Katavi aongeze fedha ili tuweze kujenga Hospitali ya Mkoa ambayo itasaidia kutoa huduma ya afya kwenye maeneo ya mkoa na kutoa huduma za afya kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutoa fedha za ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika, imepata shilingi bilioni moja na nusu kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali Tanganyika. Hilo tunawapongeza sana Wizara kwa kazi kubwa na Mheshimiwa Waziri na timu ya wataalam ambao wametoa hizo fedha kwa ajili ya kutoa huduma. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aendelee kutusaidia kwenye Vituo vya Afya ambavyo viko kwenye maeneo husika. Nilishamwomba

Kituo cha Afya cha Nyagala, naamini anakikumbuka, naomba sana hiki Kituo akiwekee kipaumbele kwa ajili ya kuwapa wananchi wa eneo hilo. Walishaanza hatua za awali, wamejitolea, wamejenga baadhi ya majengo, kwa hiyo tunategemea Mheshimiwa Waziri kwenye fedha atakazozipata, atusaidie kituo hicho ili tuweze kuwasaidia wananchi wa eneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambasamba na hilo, tunaipongeza Serikali kwa kujenga Vituo vya Afya vya Mwese na Mishamo. Kwenye hivyo vituo viwili ambavyo vilitolewa fedha na Serikali upo upungufu ambao tunahitaji Wizara isaidie. Tunaomba vifaa tiba, kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Mwese, tunaomba vifaa tiba kwa ajili ya Kituo cha Mishamo. Naamini tukipata hivyo vifaa tiba vitawasaidia kutoa huduma iliyo nzuri na wananchi wakanufaika na kile kilichoelekezwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwenye maeneo ambayo alifika Mheshimiwa Waziri, alifika eneo la Kituo cha Afya cha Karema, eneo lile tunahitaji watusaidie watupatie *ambulance*, yeye aliahidi na alifika akaona mazingira yalivyo, kwa hiyo tunaomba kumkumbusha Mheshimiwa Waziri ahadi ambayo aliwapa Wanatanganyika, eneo lile la Karema aweze kukamilisha ili aweze kuwasaidia wananchi kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, tunaomba Madaktari na vituo vya afya, zahanati na hospitali inayojengwa sasa inahitaji wahudumu wa afya, Wilaya ya Tanganyika ina Daktari mmoja tu. Naomba kwenye bajeti hii, aangalie uwezekano wa kupeleka wataalam watakaotoa huduma kwenye vituo vya afya. Vituo vya afya hivyo vilivyojengwa ni vizuri, lakini vina tatizo la wahudumu ambao wanaweza wakatoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naendelea kumpongeza kwa kazi nzuri ambazo anazifanya. Ahsante. *(Makofi)*



**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Oscar Mukasa, atafuatiwa na Mheshimiwa Khatib Haji na Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua ajiandae.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa kipaumbele cha juu kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa hii nafasi ya kufanya shughuli ya leo. Pia nawashukuru wananchi wa Biharamulo kwa kuendelea kuniunga mkono, lakini kwa namna ya pekee napenda kuipongeza Serikali, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwenye Sekta hii ya Afya mambo yanaonekana, lakini Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile na wasaidizi wenu Katibu Mkuu na wengine wote tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi uko wazi, mimi nitatoa ushahidi mmoja kwamba mkononi kwangu nina ripoti, utafiti uliofanywa na Taasisi ya *Institute for Health Metrics and Evaluation*, moja ya mambo ambayo wamepima ni habari ya *maternal mortality* kwa watoto wa chini ya miaka mitano na *infants* wale chini ya mwaka mmoja, inaonesha kabisa takwimu ziko wazi hapo kwamba hatujafika tunapotakiwa kufika, lakini tunakwenda vizuri kulingana na matarajio namna wanavyopima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawapongeza sana, lakini tumesikia hapa, Mheshimiwa Mbunge mmoja amesema namna ambavyo Wizara hii inapata pesa kidogo ukilinganisha na mahitaji ambalo sio jambo zuri, lakini hata Mheshimiwa Ummy na Mheshimiwa Ndugulile na timu yao, kwa kweli wamejitahidi sana kuratibu wadau wengine wa nje ya Serikali. Ndiyo maana mambo mengine yanakwenda, ukipata fursa ya kuwa nao karibu utaona hilo na kweli huwa linanitia moyo sana, naona mwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme mawili ya Biharamulo; moja tunashukuru tumejengewa Kituo cha Afya Nemba, lakini kinaleta mahitaji kwa sasa tutafanya upasuaji pale wa akinamama wajawazito, wale wanaohitaji upasuaji, tunahitaji *ambulance*, jiografia ya Biharamulo ni ngumu sana

kwa sasa tuna Kituo Nyakahura na Nyakanazi ambavyo ni mbali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambasamba na hilo, tunahitaji wataalam wengine wa dawa za usingizi, yako matukio kadhaa ya upungufu yanayosababisha vifo vya akinamama kutokana na upungufu wa wale wataalam wa dawa za usingizi. Tuna Madaktari, ama MD mmoja ama wawili, wako kwenye hivyo vituo, lakini kwa sababu watu wa usingizi hawatoshi, mara nyingine ucheleweshwaji inakuwa haiwezekani kufanya upasuaji kwenye Kituo cha Afya na safari ya kwenda Biharamulo Mjini kwa ajili ya upasuaji inakuwa ndefu inasababisha vifo. Hayo ndiyo mahitaji yetu mawili makubwa kwa Biharamulo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije suala la Kitaifa, pamoja na pongezi na kazi nzuri inayofanyika yako maeneo ya kuboresha. Ukitazama ripoti hii hii ya *Institute of Health Metrics and Evaluation*, inasema kwa mwaka 2017 wamelinganisha 2007 na 2017, hii ni taasisi maarufu sana duniani na inaheshimika, wame-*rank* wameweka uwiano, wamepanga ule uzito wa sababu za vifo kwenye nchi yetu hii. Katika sababu hizo, ziko ambazo zinatokana na UKIMWI, TB, Malaria lakini hata na magonjwa ya kuhara ni miongoni mwa sababu kumi za vifo ambavyo zinachukua uzito wa juu. *Metrics*

Mheshimiwa Naibu Spika, na sababu za vifo, kabla ya wakati, yaani zile *pre-mature death* wame-*rank* mambo hapo, kuna *tuberculosis*, lakini kuna *protein energy malnutrition*, mambo ya utapiamlo, mambo yanayozuilika kabisa na sababu za ulemavu, inayoongoza kabisa ni *dietary iron deficiency* na ukiangalia zaidi kwenye ripoti yao wanasema, vifo pamoja na ulemavu kwa pamoja sababu inayoongoza ni *malnutrition*, utapiamlo, yaani nchi hii tuna tatizo kubwa la utapiamlo, pamoja na kufanya kazi vizuri sana huko kwenye tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningependa, nijikite zaidi kwenye utapiamlo huo, Sera ya lishe nchi hii, imepitwa

na wakati, toka mwaka 1992. Kwa bahati mbaya, ilikuwa inatazama zaidi mchango wa lishe kutoka kwenye Sekta ya Afya, haitazami mchango wa lishe kutoka kwenye sekta nyingine, hili ni tatizo. Tunaomba tufanye mapitio ya Sera, kama asilimia, tatizo linaloongoza kwa habari ya vifo na ulemavu kwa pamoja, namba moja ni utapiamlo wala sio kipindupindu, sio jambo lingine wala sio *malaria*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima twende kwenye Sera yetu, tuone namna gani sekta zote zitaingia. Nakumbuka mwaka jana, waliwaita Wakuu wa Mikoa hapa, nikaona wanaweka sahihi, lilikuwa ni jambo zuri, lakini nikawa najjuliza hivi hizi sahihi zitasaidia, kama hatuna *framework*? Pia sijasikia ushahidi wowote kwamba hizo sahihi zimesaidia, wameleta *improvement*, ni kwa sababu lazima likae kimfumo, tuzialike Sera zote kisera na tunaomba katika hili, ikae Sera ya Lishe sio kuchukua habari ya lishe kuiweka kwenye Sera ya Afya, kwa sababu hili jambo ni mtambuka na kubwa. Naomba kusema kwamba hili tutalipigia kelele sana. Tunaomba Sera ya Lishe ije haraka iwezekanavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, usafi; moja ya sababu zinazosababisha vifo, ukichanganya vifo na ulemavu kwa pamoja, ni habari ya *wash*, mtu anatoka kujisaidia hanawi mikono, anakuja kumsalimia mwenzake na hapa ukiangalia kama mtu angekuwa anapima watu tunavyosalimiana, hapa kwa mikono lakini asilimia zaidi ya sabini ngapi hawanawi mikono baada ya kujisaidia. Hili linahitaji elimu tu na wamesema Wabunge wengi hapa, twende kule kwenye zahanati na vituo vya afya tuweke wahudumu wa afya wa kwenda kuelimisha vijijini wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwenye Ikama ya Watumishi wa Afya wanayo ya zahanati inasema *Clinical Officer* kwa siku aone wagonjwa 40. Mtu wa madawa kwa siku ahudumie *prescription* 40, lakini ikifika kwa yule *Community Health Worker* inasema aunganishe tu kituo na kijijini, haimpi kwamba leo katazame vyoo saba ukatazame wangapi wameweka sehemu za kunawa, twende huko, tuondoke kwenye tiba sasa tumeshafanya vizuri, twende

kwenye afya. Watanzania wanahitaji Afya, nimesikia watu wanawapongeza Madaktari na mimi nawapongeza, lakini ifikie hatua, tuanze kupongeza, tunawapongeza Mabwana Afya, wamehamasisha sasa huku hatuharishi, kwa sababu ukiangalia hapa inasema asilimia 2.7 ya wananchi nchi hii hawana vyoo kabisa...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mukasa kwa mchango huo. Nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Khatib Haji dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua, halafu Mheshimiwa Fatma Toufiq ajandae.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Namshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kuweza kusimama hapa, na niwatakie heri na baraka katika mfungo wa mwezi wa Ramadhani wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kutoa shukrani na pongezi za dhati kabisa kwa namna Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji wake wanavyoisimamia Wizara hii, Wizara ambayo ni uhai wa Taifa la Tanzania, ni uhai wetu sote. Mimi binafsi hata kama sitasema hadhara, lakini kwa kusema kweli naikubali sana Wizara hii na Watendaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nianze kuhusu suala la wagonjwa wa figo, Mheshimiwa Waziri, binafsi anafahamu, mimi nimewahi kuugua ugonjwa huo, nimepitia mazito ambayo kwa kweli kati ya magonjwa mazito na magumu sana ni ugonjwa wa figo. Kwa hivyo ninapozungumza hapa nazungumza kitu ambacho nimekipitia, nakijua na naendelea nacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka Mheshimiwa Waziri, kuna jambo moja linatatiza sana wagonjwa wa figo, jambo hili ni upatikanaji wa dawa za

wagonjwa wa figo, wagonjwa wa figo ambao wako kwenye bima, Watanzania wengi hali zao za kiuchumi ni za chini sana, wale walioko kwenye bima, hizo bima hata ukikata lakini kuna masharti ya kufikia kupata dawa za figo, yako masharti, mtu kawaida ukikata ile bima unaambiwa lazima ikae muda fulani iwe ndiyo inakuwa *matured* ya kuweza kupatiwa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna binadamu yeyote anayejiombea ugonjwa kumfika, kama imewezekana kwa wagonjwa wa UKIMWI kupewa dawa hizi pasipo na masharti na wagonjwa wa figo waangaliwe urahisi wa kuzipata dawa hizi. Kwa kweli, hili jambo ni la kuliangalia sana, pamoja na hilo Mheshimiwa Waziri anajua mgonjwa wa figo anapopata tu ugonjwa huu, akithibitika kuna hatua za kupitia wakati anasubiri upasuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya uchujaji wa damu, huduma za uchuchaji wa damu, kwa mtu asiye na bima ya afya sasa hivi ni 180,000. Watanzania wa hali ya chini kwenda kupatiwa huduma hii kwa 180,000 kila siku anayokwenda kwenye huduma hii ni jambo zito na ambalo Watanzania wengi hawawezi kulimudu. Hili linapelekea vifo vyao kabla hata hawajafikia kwenye kufanyiwa *transplant*. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri, aliangalie hili sana, kwa sababu Watanzania wengi wasio na uwezo wanafikia, hawafikii hatua ya kutafuta ndugu kuwasaidia upandikizaji tayari wamekuwa wamekufa katika hatua ya kufanyiwa uchujaji wa damu *dialysis*, kwa hivyo naomba suala hili liangaliwe nalo kwa umakini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo mimi ni mmoja wa wanachama wa Chama cha Wagonjwa wa Figo na wanachama wenzangu wamenituma hapa nilisemee hilo, kwa hivyo Mheshimiwa Waziri, naomba alichukue kwa uzito stahiki. Naongea kama Khatib na naongea kama mwakilishi wa wagonjwa wenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kulizungumzia, Mheshimiwa Ummy katika Hospitali ya Rufaa ya Bombo lipo tatizo, lipo tatizo ambalo sasa ni karibu miaka

mitano, tatizo la *lift* katika wodi ya Galanosi ambayo wazazi wanakaa kwenye ghorofa ya tatu, *theatre room* iko chini. Kinachotokea sasa hivi anapofanyiwa *operation*, akipelekwa kule juu lazima abebwe mzega mzega. Tanzania ya leo mgonjwa kubebwa kwenye machela akapandishwa kwenye ngazi hilo ni jambo ambalo halikubaliki. Akinamama hao, ambao wanajifungua kwa *operation* wako chini, akinamama hao Mheshimiwa Waziri ajue ndiyo wengine wanajifungua Marais, wengine watajifungua Mawaziri Wakuu, wengine watajifungua Waziri wa Afya kama yeye, wengine watajifungua wachungaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni vizuri sana Mheshimiwa Waziri jambo hili aliangalie na nataka nimpe rai, kwa sababu mimi ni mdau wa Tanga, mimi ni mpiga kura ambaye natokea Zanzibar lakini mimi ni mkazi wa Tanga na familia yangu yote. Namwomba sasa, kama hili jambo limekuwa zito na mwaka wa tano limeshindikana, tuna bahati sana Mkoa wa Tanga na Jimbo la Tanga Mheshimiwa Waziri wa Afya ni mtu wa Tanga; Katibu Mkuu wa Wizara hii ni mtu wa Tanga, Dkt. Chaula; yupo Mbunge wa Jimbo la Tanga Mheshimiwa Mussa Mbarouk na nipo Mbunge mimi kutoka Zanzibar, lakini ni mdau mkubwa wa Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri ahitishie harambee mimi na wenzangu niliowataja tuwashirikishe matajiri wa Tanga wapo pale wa kina *RATCO*, yupo pale Raha Leo, yupo Simba Mtoto, tuitishe na harambee kubwa ambayo itasaidia kuitengeneza *lift* ile ili wagonjwa wetu, akinamama wetu wa Tanga waepukane na adhabu ile. Namwomba sana Mheshimiwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Khatib.

Sina hakika kama anapiga kura mara mbili ama vipi, naona kama amepata kigugumizi hivi, anaweza kuwa ni mpiga kura wako Mheshimiwa Ummy. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tumalizie na Wabunge waliosalia, Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mheshimiwa Josephine Genzabuke atamalizia.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa mimi kupata fursa ya kuzungumza kidogo kwa ajili ya kuchangia hotuba ya bajeti hii ya Wizara ya Afya. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuisimamia Wizara hii, lakini kusimamia na kupigania afya za Watanzania. Tunao ushahidi, tunaona kwa macho, Hospitali zinajengwa, hospitali za rufaa na vinajegwa vituo vya afya kila kona. Kwa kweli, kazi kubwa inafanyika, lakini nimpongeze sana mama yetu mama Umyy, Watanzania wanamwona namna anavyofanya kazi na hakika Mwenyezi Mungu atamlipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikumbushe mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, Mheshimiwa Umyy alikuja Mtwara wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais katika Mkoa wa Mtwara, Mheshimiwa Umyy alisikia kilio cha Wabunge wa Mtwara na Wabunge wa Kusini kwa ujumla pamoja na wananchi kuhusiana na suala zima la Hospitali ya Kanda ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Umyy kwa kweli moyo wake mwema, uendelee hivyo hivyo kwa kuhakikisha kwamba hospitali hii inajengwa na inakamilika kwa sababu kwa muda mrefu ujenzi ule umesimama na sisi tunaisubiri kwa hamu sana hospitali hiyo ili tuweze kupata huduma za afya kubwa kubwa kama wanavyopata katika maeneo mengine waliopata Hospitali za Kanda za Rufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitumie fursa hii kumkumbusha Mheshimiwa Umyy alipokuja Masasi katika ziara yake ya kikazi, alipata fursa ya kufanya mkutano wa

hadhara. Katika mkutano ule tulimwomba *ambulance* moja na aliahidi kutupatia, tunaomba moyo wake mwema, uendelee hivyo hivyo atusaidie tuweze kupata *ambulance* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbusha tena Mheshimiwa Ummu kwamba alipata fursa ya kutembelea Hospitali ya Mkomaindo, aliona changamoto kubwa tuliyonayo kwenye upande wa *x-ray*, *x-ray* ni chakavu na haifanyi kazi. Tunamwomba moyo wake uendelee kuwaangalia kwa jicho la kipekee watu wa Masasi atulettee *x-ray* mpya ya ki-*digital* kama katika maeneo mengine ili wananchi waweze kupata huduma inayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimkumbushe tena dada yetu Mheshimiwa Ummu, kwamba ameona hali halisi ya Hospitali yetu ya Mkomaindo na namna ambavyo chumba cha upasuaji hakiwezi hata kuchukua zaidi ya mgonjwa mmoja katika kutoa huduma. Tunaomba mabadiliko makubwa ya chumba hiki ili wananchi wetu waweze kupata huduma inayostahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimkumbushe tena Mheshimiwa Ummu, kwamba kama ilivyo katika maeneo mengine, tuna uhaba mkubwa wa Madaktari na wahudumu wa afya katika Jimbo la Masasi, tunaomba pia atuangalie kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Fatma Toufiq, tutamalizia na Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa na mimi fursa ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Nami niungane na wenzangu wote kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu Bi. Ummu Mwalimu, lakini pia nimpungeze Naibu Waziri, Dkt. Faustine Ndugulile. Watendaji wote, Katibu Mkuu wa Afya, mdogo



wangu Dkt. Zainabu Chaula, pongezi sana pamoja na Katibu Mkuu wa Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niungane na maoni ya Kamati kwamba fedha zote ambazo hazijakamilishwa kutolewa katika Wizara hii zitolewe kwa wakati ili kusudi waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 121 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu mpango mkakati wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto 2017/2018 hadi 2021/2022. Naipongeza sana Serikali kwa kuratibu na kuanzisha hizi Kamati za Ulinzi wa Watoto na Wanawake na inasemekana mpaka sasa hivi Kamati hizi zimefikia 7,383. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, napenda tu kufahamu kwamba Wizara imejiandaaje katika kuhakikisha kwamba mpango huu unafahamika zaidi katika jamii yetu hasa kule pembezoni. Kwa sababu mpango huu dhima yake najua ni nzuri sana kuhakikisha kwamba wanawake na watoto wanakuwa hawafanyiwi ukatili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kufahamu Serikali ina mkakati gani wa kutunga sheria ya jinsia ili kusudi sasa iweze kuangalia masuala yote kwa jicho la kijinsia. Kama tukiwa na sheria hii naamini kabisa masuala mengi ya kijinsia yanaweza yakafanyiwa utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti zimebainisha kwamba ukatili unaanzia majumbani na wengi wanaofanyia watu ukatili ni ndugu wa karibu. Wizara imejipangaje kuelimisha jamii kuhusiana na suala hili ili kusudi watu wasione tabu kulizungumzia na hatimaye wahusika wanaofanya ukatili waweze kuchukuliwa hatua zinazostahiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie kuhusu ustawi wa wazee, wenzangu wengi wamezungumzia.

Suala la ile sheria na mimi pia naomba nisisitize kwamba sheria inabidi itungwe kwa sababu nchi yetu imeridhia matamko mbalimbali lakini pia mwaka 2016 Umoja wa Afrika ulikuwa umekubaliana kupitisha mwongozo kuhusu haki za wazee lakini inaelekea kwamba nchi yetu bado haijaridhia makubaliano hayo. Naomba basi ifanyike ili kusudi wazee wetu waweze kupata tija, kwa kweli wazee nao wanahitaji fursa nyingi na mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie kuhusu makao ya wazee. Kwa kweli kuna changamoto kubwa sana, haya makao ya wazee 17 ambayo ni ya Serikali bado yako katika hali mbaya sana. Naomba Serikali ifanye matengenezo yanayohitajika ili kusudi hadhi ya wazee iweze kupatikana kwa sababu inaonekana kwamba wazee wameachwa nyuma sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu masuala ya makuzi ya watoto, hii imezungumziwa katika ukurasa wa 123 hadi 132 katika hotuba hii. Sasa hivi watoto wengi sana ambao tulikuwa tukiwategemea wawe mayaya au walezi wanakwenda kusoma shule. Kwa sababu ya elimu bure watoto wengi wa kike siku hizi tena hawaendi kufanya kazi za majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokuwa naomba nishauri ni kwamba Serikali ione utaratibu wa kufanya ili kusudi viwepo vituo vingi vya malezi ya watoto wakati wa mchana ili kusudi sasa wazazi na walezi waweze kuwapeleka watoto wao katika vituo hivi. Watoto kwa kukaa katika vituo hivi ni ili ustawi wa wale wao uwepo lakini pia waweze kuwa katika mazingira salama. Vituo hivi vitumike kama sehemu bora ya ulinzi na usalama wa watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nizungumzie kuhusu suala la afya ya kinywa na meno. Tatizo ni kwamba sasa hivi watu wengi sana wamekuwa na tatizo hili la afya ya kinywa na meno Serikali ituambie ina mkakati gani wa kwanza kuzuia ili kusudi watu wengi wasipate madhara na pia wataalam wengi wa masuala ya kinywa nao pia

wapatikane. Kwa sababu inaonekana kwamba maeneo mengi wataalam hao hawapo, kwa hiyo, wananchi wanapata shida sana kwa ajili ya afya ya kinywa na meno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama ndani ya Bunge lako na kuchangia hoja hii ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Kwanza napenda nimpongeze Waziri wa Afya, Mheshimiwa Umyy Mwalimu, Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, Katibu Mkuu - Dkt. Chaula kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipongeze kwa moyo wa dhati kabisa jinsi Serikali ya Awamu ya Tano inavyofanya kazi ya kujenga hospitali pamoja na vituo vya afya. Naomba nishukuru kwa moyo wa dhati kabisa kwa Serikali kuweza kusaidia Hospitali ya Maweni kwa kupeleka shilingi milioni 500 ili kuendelea kuimarisha hospitali ile ambayo inatumiwa na wananchi wote wa Mkoa wa Kigoma. Ahsante sana, tunaamini pesa hizo zikifika zitaendelea kukarabati hospitali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru Serikali kwa kuweza kukubali kujenga Hospitali ya Wilaya ya Kakonko. Waziri Mkuu alipokuja alikubali kupeleka shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Kakonko na tayari shilingi milioni 500 zimepangwa kwa ajili ya kuanza ujenzi huo. Nashukuru kwa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya Hospitali ya Kasulu DC, tayari

fedha zimeshafika na tayari wameshaanza ujenzi. Nashukuru na ujenzi wa hospitali inayoendelea katika Wilaya ya Buhigwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia wakati huu vituo vya afya vinakarabatiwa na vingine vinajengwa, tunaishukuru sana Serikali. Naomba vituo hivyo vinavyojengwa ambavyo vipo tayari na vingine ambavyo bado viweze kupelekewa madaktari, wauguzi pamoja na vifaa tiba, sambamba na wataalamu wa dawa za usingizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi kwa Waziri wa Afya pamoja na Katibu Mkuu, kwa sababu wao ni akina mama, vipo vituo vingine karibu na hospitali ya wilaya lakini kuna maeneo mengine yapo mbali kabisa. Kwa mfano, kutoka Kasulu Mjini kwenda eneo moja la Kitanga ni kilometa 123 lakini hawana kituo cha afya. Lipo eneo lingine tena linaitwa Kagera Nkanda, kutoka Kasulu Mjini ni kilometa 78. Naomba kwa vile wao ni akina mama washirikiane na Waziri wa TAMISEMI kuona ni namna gani wanaweza kuwasaidia akina mama ambao wanaishi umbali mrefu sana na hawana vituo vya afya ili tuweze kupata vituo vya afya katika maeneo hayo ambayo yako mbali kutoka Wilaya ya Kasulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile katika Wilaya ya Kakonko, Gwanuku wameshapata kituo cha afya lakini Mgunzu pamoja na eneo moja linaitwa Muhangi na wao wako mpakani hawana vituo vya afya. Naomba na wao waangaliwe kwa sababu wako mpakani waweze kupewa vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nilichotaka kuzungumzia, mara nyingi sana wananchi wanapoenda kutibiwa katika maeneo mbalimbali wakipangiwa kwenda maabara kupima hawezi kurudi bila kuambiwa kwamba hajapatikana na tatizo la UTI. Kila vipimo vinapotoka mgonjwa akipimwa ni lazima ataambiwa kwamba ana tatizo la UTI. Namwomba Mheshimiwa Dkt. Ndugulile atueleze ni kwa nini wagonjwa walio wengi hasa vijijini na hata mijini hawawezi

kutibiwa bila kuambiwa kwamba wana UTI? Ni kwa nini maeneo mengi wanapatikana na matatizo hayo? Nilitaka nijue ni vipimo gani vinavyotoa majibu mengi yanayofanana? Kwa sababu mimi napata wasiwasi isijekuwa kuna maeneo mengine watu wanaambiwa kwamba wana UTI kumbe watu wanafanyabiashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee maeneo mengi wanalalamika kwa kutokupata huduma ya kutibiwa bure. Hiki kimekuwa ni kilio kikubwa cha wazee, maeneo mengi ukienda hata tunapoenda kwenye ziara wazee wengi wanatulalamikia kwamba Serikali ilisema itatoa huduma ya matibabu bure lakini bado huduma hiyo maeneo mengine hawajaweza kutibiwa bure. Yapo maeneo ambayo wanatibiwa bure lakini maeneo mengine bado wazee hawajapa huduma hiyo ya kutibiwa bure. Nafahamu Serikali yangu ni sikivu, itafanya utaratibu ili wazee hawa waweze kupata huduma bure na hasa waletе sheria Bungeni ili iweze kufanyiwa utaratibu kusudi itambulike kihalali kabisa kwamba wazee wote sasa wanatakiwa kutibiwa bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba niunge mkono hoja lakini nisisitize hospitali na vituo vya afya vile ambavyo havina waganga na wauguzi wapatiwe wataalam hao ili wananchi wetu waweze kupata huduma bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha uchangiaji. Nina mambo mawili, moja ni tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge. Mnatangaziwa kuwa kwaya ya *SPA Church* ya Yombo Dovya Jijini Dar es Salaam ambayo ilitembelea Bunge siku ya Jumatatu tarehe 6 Mei, 2019, kwa kushirikiana na Mbunge wa Temeke Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea imetoa zawadi ya vitabu kwa Wabunge wote kwa lengo la kusaidia kuongeza furaha ya kiroho na amani ya moyo. Vitabu hivyo vitagawiwa bure kwa Wabunge wote na vitatolewa kupitia

masanduku yetu ya nyaraka kwa maana ya *pigeon holes*. Kwa hiyo, mvichukue hivi vitabu ambavyo vitasaidia kwenye furaha ya kiroho na amani ya moyo, naamini watu wote tunapenda kuwa na amani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ni la kukumbushana Kanuni yetu ya 154 kwa sababu tunapokaa Bungeni hatuko peke yetu, wako wenzetu ambao huwa hawaji siku zote lakini pia wapo wageni wanaokuja kujifunza namna tunavyoendesha Bunge. Kanuni ya 154 inatuongoza kwenye kutoa pongezi lakini pia kutoa pole zile ambazo Bunge linapaswa kutoa. Bunge lilikwisha kutoa pole kwa msiba mkubwa uliolipata Taifa letu na kwa mujibu wa Kanuni zetu watu wanapaswa kuendelea kwenye michango moja kwa moja.

Hata hivyo, wale ambao waliendelea kutoa pole hizo hawakukumbushwa matumizi ya Kanuni hizi kwa sababu muda wao uliendelea kuhesabiwa. Niwakumbushe tu matumizi ya kanuni ambazo tumejitungia wenyewe ili wageni wetu wasione Wabunge ambao hawajatoa pole kwa namna fulani kwamba pengine wao hawatambui uzito. Kanuni zetu zinatungoza, kwa hiyo, Bunge kama Bunge linatambua uzito wa jambo lililotupata kama Taifa. Wote mtakuwa ni mashahidi kwa uzito huo huo Mheshimiwa Spika ameelekea huko kwa ajili ya maziko. Kwa hiyo, Bunge kama Bunge linatambua jambo zito ambalo Taifa limetupata. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi alasiri leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae. Katibu!

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Ilikuwa tuanze na Mheshimiwa Mwita Waitara, Mheshimiwa Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata fursa ya kuweza kuchangia hoja iliyowasilishwa na Wizara ya Afya, Jinsia, Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja na kipekee naomba uniruhusu nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Umyy Mwalimu na Naibu wake na Katibu Mkuu na Watumishi wote kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakitoa kwetu sisi Wizara ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na kimsingi Watanzania wote ni mashuhuda. Kazi kubwa ambayo inafanywa katika kuboresha afya za Watanzania haitiliwi mashaka hata Mtanzania mmoja. Kwa hiyo, naamini kwa moto huu ambao umeanza hakika Watanzania watarajie mambo makubwa mazuri chini ya uongozi wa viongozi wetu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wako Wabunge wengi ambao wamechangia na karibu wote walikuwa wakipongeza. Kama kuna mtu ambaye hakupongeza basi labda amepongeza kimoyo moyo lakini hata upande wa pili nao ni mashuhuda kwamba kazi nzuri inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna hoja ambazo zimeibuliwa na ambazo sisi kama TAMISEMI ni vizuri tukajibu kiasi. Katika hoja mojawapo ni pamoja na upungufu wa

watumishi wa afya katika hospitali za Wilaya, vituo vya afya na zahanati. Tunakiri kabisa kwamba kuna upungufu, mpaka sasa hivi tunao watumishi wapatao 56,881 sawa sawa na asilimia 48, kwa hiyo tuna upungufu wa asilimia 52, lakini maelezo yapo ambayo yanajisheheni kwamba kwanini tunao upungufu kiasi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi sote Watanzania ni mashuhuda kwamba kama kuna sehemu ambayo uwekezaji umefanyika ni katika Sekta ya afya, vituo vya afya vimeongezeka, zahanati zimeongezeka, kwa vyovyote vile lazima ionekane kwamba kuna *gap*, lakini pia kuna sababu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mfano, katika wataalam ambao wanazalishwa tumekuwa na wataalam wachache sana hasa madaktari kuhusiana na masuala mazima ya meno, lakini hata kuhusiana na suala zima la mionzi lakini ziko jitihada ambazo zimechukuliwa na Serikali za makusudi kuhakikisha kwamba upungufu huu ambao unaonekana kwa sababu azma ya Serikali inayoongozwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, afya ya Mtanzania ndiyo kipaumbele. Kuna jitihada za makusudi ambazo zinafanywa ili kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anapata huduma ya afya tena kwa umbali usiokuwa mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeomba na naamini kibali kitapatikana, tumeomba kuweza kuajiri watumishi 15,000. Lakini pia naomba nichukue fursa hii kupongeza Mfuko wa Benjamini Mkapa na wametusaidia wameajiri watumishi kama 300 kwa muda wa miaka miwili na sasa hivi wanafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi ambalo naomba nitoe maelekezo katika Mikoa yote, tuhakikishe maeneo yale na hasa ya pembezoni na vijijini ambako ndiyo kuna upungufu mkubwa, tuhakikishe kwamba wataalam hawa wanapelekwa kwa sababu kumekuwa na namna unakuta mijini wako watumishi wa afya wengi lakini ukienda vijijini unakuta wako wachache. Kwa hiyo, pale ambapo inatajwa



upungufu, ukienda maeneo ya mjini hukuti upungufu kama ambavyo iko mijini. Nitoe maelekezo mahsusi tuhakikishe kwamba inafanyika *redistribution* ili maeneo yenye upungufu mkubwa yaweze kupelekwa hao wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe mwenyewe ni shuhuda, tukiwa hapa wakati Mheshimiwa Waziri wa Utumishi aliwasihi Wabunge kama kuna kituo chochote au zahanati yoyote ambayo inalazimika kufungwa kwa sababu eti hakuna mtumishi, aliwaomba Waheshimiwa Wabunge waandike barua ili tuweze kujaza pengo hilo na amini Waheshimiwa Wabunge walitenda haki katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja pia zimeibuliwa kuhusiana na *Community Health Workers*, hoja ya msingi tunaiunga mkono lakini ni vizuri tuka-*balance* hizi *equation*. Si rahisi pamoja na nia njema ya kuhakikisha kwamba tunawaajiri hawa, lakini itakuwa si busara pale ambapo tuna kituo cha afya au tuna zahanati ambayo tunashindwa kuifungua kwa sababu hakuna mhudumu wa afya tukaenda kuwaajiri hawa. Kwa hiyo, pamoja na nia njema ni vizuri tukatumia *structure* iliyopo, tunao Maafisa Ustawi wa Jamii ni rahisi kuweza kuwa-*train* na wakaweza kuwasaidia watu wetu lakini azma kwa siku za usoni tutahakikisha kwamba nao watu wanaweza kuajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wamelisema vizuri kuhusiana na suala zima la lishe. Hakuna namna pekee ambayo unaweza ukawekeza kuhakikisha kwamba unawapata Watanzania wenye *brain* nzuri kama hatuwekezi katika siku 1,000 za mwanzo. Wataalam wanatuambia kwamba tunaanza kuhesabu tangu pale ambapo mimba inatungwa mpaka mtoto anapokuja kuzaliwa na miezi ile miwili ndiyo muhimu sana katika kuweza kuhakikisha tunawekeza katika hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumepokea, tunajua umuhimu wa jambo hili na ndiyo maana nina kila sababu ya kumshukuru Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumewekeana mikataba na

Wakuu wa Mikoa wote Tanzania, Mikoa 26 kuhakikisha kwamba suala la udumavu linabaki historia na tumekuwa na utaratibu wa kupimana kila baada ya miezi sita na muelekeo ni mzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na sisi kwa nafasi zetu za uongozi ni mabalozi, tunapofanya mikutano yetu ni vizuri tukahakikisha kwamba elimu hii tunaifikisha kwa Watanzania wenzetu. Maana hakuna namna pekee ambayo unaweza uhakikisha kwamba watoto wetu wanakuja kushindana na mataifa mengine kama hatujawekeza katika umri wao wakiwa bado watoto wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwasihi Waheshimiwa Wabunge limesemwa juu ya kujihakikishia afya kwa kila Mtanzania. Namna pekee na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana atakuja aliseme kwa kirefu ni kuhakikisha kwamba Watanzania mwelekeo ni kujiunga na Bima ya Afya. Bima ya afya ndiyo mkombozi wa kuhakikisha kila Mtanzania anaenda kupata tiba pale ambapo anapatwa ugonjwa tena tiba ambayo ya kisasa kabisa. Haipendezi pale ambapo inatokea Mtanzania anaenda wakati anaumwa, anashindwa kupata matibabu eti kwa sababu hana fedha au hajajunga na bima ya afya. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge sisi ni viongozi ni vizuri tukatoa hamasa kwa Watanzania, mataifa yote duniani utaratibu ndiyo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Waheshimiwa Wabunge walichangia na alianza kusema Mheshimiwa Nachuma, akataja Mkoa wake wa Mtwara na hasa na maeneo yote ambayo ni mwambao mwa bahari. Kuna mazalia mengi sana ya mbu, akaomba ifanyike jitihada za makusudi. Sisi sote ni kwamba Tanzania tuna kiwanda chetu cha viuadudu ambacho kipo pale Mkoa wa Pwani na kipekee Mheshimiwa Rais naomba tumshukuru aliweza kuwekeza shilingi bilioni 1.3 na fedha hizo zikatumika katika kununua viuatilifu hivyo kwa ajili ya kusambaza halmashauri zote Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni wajibu wetu Wakurugenzi wote Tanzania tuhakikishe kwamba hicho ambacho kilianzishwa na Mheshimiwa Rais kiwe endelevu kwa kuhakikisha kwamba tunatenga kwenye bajeti zetu fedha kwa ajili ya kuanza kununua viuatilifu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapambana na mazalia ya mbu. Lakini pia ni vizuri hamasa ikatolewa kuhakikisha kwamba mazalia ya mbu tunatokomeza. Wenzetu Zanzibar wameweza Tanzania Bara pia tunaweza, ni suala la kuamua na tukishirikishana sisi sote inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, itoshe katika hayo ambayo sisi yamejitokeza tukaona tuyatolee ufafanuzi, naomba niendeleo kuunga mkono hoja, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

### MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu wahudumu wa afya katika ngazi ya jamii. Serikali imetoa mafunzo kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii 10,000. Wahudumu hawa wamekuwa msaada mkubwa sana kwenye ngazi ya jamii kwa kuzuia vifo vya watoto na akina mama lakini Serikali haiajiri tena wahudumu hawa. Naomba Serikali ione namna ya kuwapatia motisha na siyo mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, bima ya afya. Naomba Serikali iharakishe Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kuwa matibabu ni gharama na watu wengi wanapoteza maisha kwa kukosa pesa za matibabu. Pia watu wanaotumia bima wanakosa baadhi ya dawa za magonjwa makubwa kama moyo na mengine. Hivyo, naomba bima hizo ziingize matibabu yote na siyo baadhi ya magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Maafisa Ustawi wa Jamii. Maafisa hawa ni muhimu sana lakini hawana bajeti ya kutosha. Mara nyingi wanatumia fedha zao za mfukoni kwa

ajili ya kazi za kutembelea na kufuatilia watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Hivyo, naomba Maafisa Ustawi wa Jamii wapewe bajeti ya kutosha kwa ajili ya kutembelea na kufuatilia familia mbalimbali zenye matatizo pamoja na watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ada ya usajili wa *dental clinics*. Gharama za usajili wa *clinic* hizi ya Sh.1,000,000 ni kubwa. Naomba gharama hizo zipunguzwe kwani ni huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. OMARI A. KIGODA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kuwapongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Handeni Mji ni ya zamani na kwa sasa inaelemewa sana na idadi ya wagonjwa. Inahudumia majimbo *almost* manne na mpaka sasa hakuna utaratibu wa kupata hospitali katika majimbo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, tuna zahanati eneo la Kwamagome ambalo Mheshimiwa Waziri Ummy alifika kwenye ufunguzi, tumefikia pazuri na ikiwezekana tunaweza kupafanya pale na kuwa kituo cha afya. Naomba Waziri aliangalie eneo hili ili kuondoa msongamano wa wagonjwa kwenye hospitali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kule kwetu hatujapata mgao wowote kwenye kuongeza au kujenga kituo cha afya. Tunaomba Wizara itufikirie na sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Hospitali ya Wilaya katika Manispaa ya Moshi. Manispaa ya Moshi ina mahitaji makubwa sana ya Hospitali ya Wilaya kwa vile Hospitali ya Mkoa ya Mawenzi imezidiwa

na wagonjwa na Hospitali ya *KCMC* pia imezidiwa na wagonjwa. Hospitali zote hizi mbili zinahudumia wagonjwa kutoka maeneo mbalimbali nje ya Manispaa ya Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Manispaa ya Moshi ina eneo ambalo imelitenga kwa ajili ya ujenzi huo wa Hospitali ya Wilaya. Hivyo, ni matumaini yangu kwamba Serikali itaifanyia kazi ombi langu kwa niaba ya wananchi wa Moshi Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupandishwa hadhi vituo vitatu vya zahanati kuwa vituo vya afya. Manispaa ya Moshi imeleta maombi ya muda mrefu Serikalini ya kupandisha hadhi zahanati tatu za Shirimatunda, Msaranga na Longuo B. Maombi hayo ni muhimu sana kwa vile idadi ya watu inaongezeka kila siku katika Manispaa ya Moshi. Kutokana na ongezeko hilo, mahitaji ya huduma ya matibabu yanaongezeka kwa kasi. Naomba Serikali ipandishe hadhi zahanati tajwa hapo juu kuwa vituo vya afya ili kuwasaidia wananchi kupata huduma kirahisi zaidi na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa niaba ya wananchi wa Manispaa ya Moshi, Serikali itenge fedha kwa ajili ya kuboresha kituo cha afya kimoja katika Manispaa ya Moshi ili kutoa huduma bora kwa wakazi wa Manispaa ya Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitangulie kwa kuunga mkono hoja hii ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, bila kumsahau Katibu Mkuu wa Wizara hii, Mheshimiwa Dkt. Zainab Chaula kwa kazi nzuri wanayoifanya katika nchi hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi, naomba kukukumbushia ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa

Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto alipokuja Itigi katika Hospitali ya Rufaa ya St.Gaspar katika Siku ya Wauguzi 2017 na kuahidi kutoa gari kwa Kituo cha Afya Mitundu ambacho kipo zaidi ya kilometa 100 toka Hospitali yetu ya Wilaya ya Manyoni. Nia yangu ni kukukumbusha tu ahadi hii aliyotoa kwa wananchi wa Halmashauri ya Itigi, Jimbo la Manyoni Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Serikali kwa kazi nzuri inayofanya ya kuboresha huduma za afya nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuelezea changamoto za Hospitali yangu ya Rufaa ya Mkoa wa Singida. Hospitali hii inatoa huduma katika maeneo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo hospitali ya rufaa ya zamani katika Kata ya Ipembe na hospitali mpya ya rufaa iliyopo katika Kata ya Mandewa. Uendeshaji wa hospitali hizi mbili kwa wakati mmoja imepelekea gharama za uendeshaji kuwa kubwa kwa kuwa inatumika bajeti moja kulipia bili ya maji, umeme, ulinzi na usafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini sasa Serikali isimalizie Hospitali ya Rufaa ya Mandewa yale majengo muhimu kama maabara, *pharmacy*, wodi ya upasuaji kwa magonjwa ya kwaida na mifupa, wodi ya watoto, jengo la macho na jengo la meno? Iwapo majengo haya yatakamilika yatasaidia sana hospitali ya rufaa ya zamani iliyopo Kata ya Ipembe kuhamia hospitali ya rufaa mpya ya Mandewa. Naiomba Serikali itenge fedha za kutosha ili kumaliza Hospitali hii ya Rufaa ya Mandewa kwa kuwa majengo ambayo yalishakamilika yameanza kuchakaa hata kabla ya kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali yangu ya rufaa ina changamoto lukuki; haina madaktari bingwa wa kutosha,

waliopo ni sita tu na kati ya hao sita hakuna daktari bingwa wa magonjwa ya wanawake na watoto lakini pia ina wauguzi wachache. Wauguzi waliopo katika hospitali hii ni 144 kati ya 305 wanaotakiwa. Naomba Serikali itupatie watumishi wa kutosha wakiwemo wauguzi kwani hospitali hii ndiyo tegemeo la wananchi wa Mkoa wa Singida katika kupata huduma za afya za kibingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali hii pia haina gari la kubebea wagonjwa (*ambulance*), gari lililopo lilipata *accident* takribani miaka mitano iliyopita. Jambo hili nimekuwa nikilileta kwenu mara kwa mara, naomba sana sana kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Sindida ifike wakati sasa Hospitali hii ya Rufaa ya Mkoa wa Singida ipatiwe gari la kubebea wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hospitali zangu zote za Wilaya ikiwemo ya Wilaya ya Iramba na Manyoni hazina magari ya kubebea wagonjwa. Naomba sana hospitali hizi za Wilaya zipatiwe magari ya kubebea wagonjwa ili kuokoa vifo vya akina mama na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, naomba kuwasilisha.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya vifaa vya upasuaji. Naishukuru Wizara kwa kuelewa hali halisi ya Hospitali ya Mafinga ambayo inahudumia Halmashauri ya Mafinga Mji, Mufindi DC na Wilaya za jirani ikiwemo Mbarali (Madibira), Mlimba, Iringa Vijijini na Makambako na hivyo Serikali kutupatia fedha za kujenga na kuboresha Kituo cha Afya cha Ihongole angalau imeleta nafuu kwa Hospitali ya Mafinga ambayo pia ipo kandokando ya barabara kuu ya Tanzania-Zambia (TANZAM I).

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na huduma kuendelea kuboreshwa, tumejikuta idadi ya watu wanaohudumiwa ikiongezeka hasa akina mama wajawazito ambao theluthi moja hufanyiwa upasuaji. Kutokana na hali

hiyo, tulipata msaada kutoka Ubalizi wa Japan ambapo tumejenga jengo la upasuaji. Hata hivyo, msaada huo ulihusu jengo tu na siyo vifaa. Halmashauri tumejipanga na tumenunua baadhi ya vifaa. Naomba Wizara ione uwezekano wa kutusaidia baadhi ya vifaa ili tufungue na tuanze kutoa huduma kwa baadhi ya vyumba kwa kuwa jengo lina vyumba vitatu vya upasuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango huu wa maandishi, naambatanisha barua ambayo niliwasilisha kwako na maelezo ya ziada kuhusu mradi huu. Naamini chochote kitu, *anything can make a difference*. Nafahamu mna jukumu kubwa kupitia *MSD*, tunaomba sehemu ya vifaa tusaidiwe kwa kiwango chochote.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa ya kuchangia bajeti hii. Nampongeza Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa maono yake makubwa ya kuwasogezea wananchi wa Tanzania huduma muhimu za jamii, hususan katika sekta hii ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Umy Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile na Makatibu Wakuu wote kwa kazi kubwa na ya kutukuka wanayoifanya kwa uadilifu, upendo, bidii na weledi mkubwa. Tunapongeza huduma kubwa za kisasa na utaalim mkubwa katika hospitali zetu za rufaa. Nipongeze utolewaji wa miundombinu ya vifaatiba na madawa. Tunapongeza sana juhudi za kukuza uwezo wa watumishi wa sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba nitoe rai kwa Wizara hii kuzingatia umuhimu na haja ya kuajiri watumishi wengi katika zahanati na vituo vya afya, hasa katika kada ya *Medical Officers* ambao wanahitajika kwa wingi sana. Naomba kutoa rai pia kwa Wizara kuhakikisha kuwa zahanati zilizojengwa katika vijiji vyetu kwa nguvu za wananchi zinamalizika na zilizomaliziwa zipatiwe vifaa na watumishi ili zifanye kazi.



Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Jimbo langu la Wilaya ya Ileje, Kituo cha Afya Mbebe bado hakijamaliziwa na kwa sasa kwa miundombinu ya Wilaya ya Ileje wananchi wanalazimika kupeleka wagonjwa Malawi ambako ni karibu zaidi kuliko kwenda Itumba kwenye Hospitali ya Wilaya. Zahanati ya Mapogoro hukohuko Mbebe haijamaliziwa na hivyo kuifanya Mbebe ikose huduma za afya kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi walijitoa kujenga Kituo cha Afya Itale, tunaomba Serikali itusaidie fedha za kumalizia kituo hiki cha afya. Tunashukuru Serikali kwa kutoa *ambulance* ndogo, tunaomba basi Kituo cha Afya cha Itale kikamilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali itusaidie kuwezesha Vituo viwili vya Ibaba na Lubanda vilivyomaliziwa kwa fedha ya Serikali basi vizinduliwe ili vianze kazi. Mheshimiwa Ummy aliahidi *ambulance* Kata ya Lubanda, tunaomba sasa ipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Ikinga, Zahanati ya Kikota imemaliziwa ujenzi bado kufunguliwa. Tunaomba ifunguliwe ili wananchi wa Ikinga wapate huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Isongole ni kubwa na ipo kwenye Mji Mdogo wa Wilaya ya Ileje. Kata hii ina watu wengi sana lakini inakosa kituo cha afya na kuifanya Zahanati ya Isongole kuzidiwa na wagonjwa na kushindwa kumudu mahitaji ya huduma za afya kwa wananchi. Sasa hivi barabara kuu inajengwa na imepita Isongole kwa hiyo kutakuwa na ongezeko kubwa zaidi la wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ileje ina miundombinu migumu sana na Mheshimiwa Waziri alishatembelea, anafahamu. Kata ya Ndola inahitaji kituo cha afya kupunguza adha kwa wananchi wa Ndola. Kata ina hosteli ya wasichana na changamoto zikitokea wanakosa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Itumba ndiyo Makao Makuu ya Wilaya na ndipo ilipo hospitali ya wilaya.

Tunaendelea kuishukuru Serikali kwa kutupatia fedha za kujenga hospitali ya wilaya shilingi bilioni 1.5 pamoja na zilizotolewa siku za nyuma. Hospitali itakuwa na majengo muhimu saba na itajitoshesheza lakini kwa sasa tunahitaji X-ray mashine ya kisasa ya *radiologist* na friji ya kuhifadhia damu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Isoko ni hospitali ya *mission* lakini imekuwa ikitoa huduma kubwa sana kwa Wanaileje na kuunga mkono juhudi za Serikali. Tunaomba Wizara iwafanyie *secondment Medical Officers* kwenda Isoko kuziba pengo. Hospitali ya Isoko haina uwezo wa kuajiri *Medical Officers* kuziba pengo lakini kwa kuwa wanahudumia wananchi wa Ileje na Watanzania na kwa kuwa wanashirikiana na Serikali, tunaomba sana Serikali iridhie kutoa *secondment* kwa watumishi wawili au watatu kwenye ngazi ya *Medical Officer* ili kukidhi ufanisi wa huduma zinazotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo. Nimpongeze Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kwa kazi nzuri na kubwa anayofanya katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na wataalam mbalimbali waliopo Wizarani na katika taasisi zetu chini ya Wizara hii. Mheshimiwa Waziri ni msikivu sana na anapokea ushauri kutoka kwa kila mdau. Naibu Waziri pia amekuwa mstari wa mbele kutoa ushauri wa kitaalam na kuweka mfumo bora katika utekelezaji wa shughuli za Wizara. Wataalam wote hutupa ushirikiano wa karibu na pia elimu tunapohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri katika maeneo machache ili kuboresha huduma. Kwanza, nishauri kuendelea kupunguza gharama zisizo za lazima ili

kuongeza ufanisi kama mliyopokea ushauri wangu wa ujenzi wa vituo vya afya na hospitali kutoka shilingi bilioni 4.5 kituo cha afya hadi milioni 500 au milioni 400 na Hospitali za Wilaya kutoka shilingi bilioni 705 hadi shilingi bilioni 1.5, hali ambayo ilifanya tujenge vituo vingi zaidi na pia hospitali nyingi za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Kitengo cha Manunuzi (*procurement*) cha *MSD* kiboreshwe na tuwe na *team* ndogo nyingine ambayo itafanya kazi ya kuhakiki manunuzi. Naamini bado tunaweza kupunguza gharama za manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze kwa kuendelea kutumia *force account*. Muhimu pia ni kutumia mfumo wa PPP katika kuboresha huduma za afya. Mfano eneo la huduma za maabara, nchi nyingi huwa na wataalam na vifaa vya maabara ambazo wanashirikiana na hospitali, vituo vya afya na zahanati kutoa huduma. Siyo lazima tuwekeze sisi katika kila hospitali au kituo cha afya. Pia huduma za *Radiology* za *X-Ray*, *Ultrasound*, *CT-Scan*, *MRI*, tushirikiane na watoa huduma *private*. Naamini kwa kufanya hivyo bei za huduma hizo zitateremka.

Mheshimiwa Naibu, nishauri pia suala la *telemedicine* lipewe kipaumbele. Hii itasaidia kusogeza huduma ya mabingwa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kitengo cha kutengeneza viungo bandia kiboreshwe. Watanzania wengi wenye uhitaji wa viungo bandia hushindwa kuvinunua kutokana na kuwa na gharama kubwa. Tuangalie namna ya kuboresha na kutoa huduma hii katika maeneo mbalimbali nchini badala ya maeneo machache kwa bei kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri Serikali iangalie namna ya kuwa na mpango wa Bima ya Afya kwa Wote itakayokuwa ni lazima (*universal health care insurance*). Leteni sheria mapema Bungeni ili Watanzania wengi wapate bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nishauri tuendeleze sera yetu ya kinga bora kuliko tiba. Katika magonjwa mengi tunaweza kutoa elimu ya kinga badala ya kuingia gharama ya tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la usalama wa chakula na lishe, nashauri Serikali tujikite katika kinga kupunguza tatizo la lishe bora ili kuepuka tatizo la kudumaa na utapiamlo. Nashauri Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto ishirikiane na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Maliasili na Utalii na Viwanda na Biashara ili kwa pamoja tuweke mpango na mkakati wa kutokomeza utapiamlo na suala la kudumaa (*malnutrition stunting*). Pia elimu zaidi juu ya namna ya kupata lishe na mazoezi kwa ajili ya magonjwa yasiyoambukiza (*non-communicable diseases*) itolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri *TFDA* iweke vifaa vya kupima mazao hasa ya mboga mboga na matunda katika masoko yetu yote makubwa. Leo hii tunakula vyakula hasa mbogamboga na matunda vilivyopigwa dawa (sumu) kabla ya kumaliza muda maalum wa tahadhari kumalizika (*chemical residuals from insecticides*). Pia katika mifugo tunalishwa nyama na maziwa ya mifugo kutoka kwa mifugo iliyopigwa chanjo na dawa za matibabu kabla ya muda maalum kuisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri pia Serikali iangalie uwezekano wa kuondoa kodi katika vifaa tiba na vifaa wanaotumia wenye matatizo mbalimbali ya afya. Mfano baiskeli za walemavu na viti maalaum vya wagonjwa (*wheel chairs*) pamoja na magongo na vifaa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe pia Serikali isaidie kuboresha huduma katika Kituo cha Wazee Sarame-Magugu. Pia kutupatia *X-Ray* katika Kituo cha Afya Magugu. Niwashukuru kwa kupata vituo viwili Jimbo la Babati Vijijini, Magugu na Haiti. Naomba sana kupata vifaa vyote katika vituo hivyo ili kuboresha huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iangalie namna ya kuboresha na kuweka utaratibu wa kuboresha sekta ya dawa za asili. Katika nchi mbalimbali hasa Bara la Asia na Mashariki ya Mbali (*South East Asia*), wameweza kuratibu, kuweka rekodi na kufanya utafiti wa mimea na dawa za asili kwa manufaa ya raia wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Tanzania katika kila eneo kuna dawa za asili na zote hazina rekodi wala kufanyiwa utafiti katika maabara ili kuwa na uhakika wa hizo dawa na nini kipo ndani yake (*herbal medicine*). Nashauri tungeanzisha mafunzo ya dawa za asili katika vyuo vyetu. Tuna rasilimali nyingi sana ambazo zinaweza kutumika kuleta tiba mbadala (*homeopathy* na *allopathy*).

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nashauri wataalam wa jadi au wa asili wapatiwe mafunzo ya kitaalam. Mfano tunao wataalam wa asili wenye uwezo wa kufunga mifupa, kurudisha mifupa iliyosogea katika sehemu zake (*dislocation*), wakipatiwa mafunzo zaidi wanaweza kutoa huduma vizuri zaidi. Hospitali ya Daseda Haydom wanawashirikisha na kuwasaidia kusoma *X-ray* ili wafunge mifupa vizuri. Nashauri Serikali iweke maabara maalum kwa ajili ya kupima mimea mbalimbali na dawa hapa nchini pamoja na kuweka rekodi za dawa hizo ili kupata dawa za uhakika na bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiboresha sekta hii na pia katika vipodozi (*cosmetics*) tunaweza kukuza ajira na kuongeza mapato na ikawa ni kivutio cha utalii. Mfano Morocco, Jordan, India, Indonesia, Thailand na nchi zingine zinapata mapato makubwa kutokana na dawa za asili na vipodozi (*cosmetics*). Ni sekta kubwa sana, nashauri vyuo vyetu vya tiba na maendeleo ya jamii viboreshwe sana. Mitaala yake iboreshwe na vifaa vya kufundishia na kujifunza ili wanaohitimu wawe na viwango vya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nirudie, tuboreshe vyuo vyetu vya uuguzi pamoja na vya afya (*nursing and medicine*) nchini ili Watanzania wengi wasome na hata kama hakuna ajira nchini waweze kwenda nchi za nje. Tukiwa na

wataalam wetu nje ya nchi, watatangaza nchi yetu na kuleta mapato ya fedha za nje. Nchi nyingi za Asia hufanya hivyo. Huduma pia ya mazoezi ya viungo ni muhimu na wataalam ni wachache (*physiotherapists*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama katika Bunge hili Tukufu na kuchangia machache kwa maandishi, hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Pia, nachukua nafasi hii kumpa pongezi Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wa Wizara nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya mambo mengi mazuri, hasa kuhusu mambo ya afya ikiwepo ujenzi wa vituo vya afya na upatikanaji wa dawa. Natoa shukrani kwa Hospitali yetu ya Mkoa/Rufaa Morogoro kwa kutupatia *X-ray* ya kidigitali, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa Hospitali ya Rufaa Morogoro, tunaleta ombi letu kuhusu kupewa mashine ya *CT-Scan* ambayo ni muhimu sana. Hii ni kukumbushia ahadi ambayo ilitolewa hapo awali na viongozi wetu wa taifa wakati wa ziara Morogoro. Nashukuru kwa yote mazuri yaliyotendeka kwa kutupatia gari la wagonjwa na *X-ray*, kwa imani hii naamini hata *CT-Scan* tutapewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri na naomba Hospitali za Wilaya za Mkoa wetu za Gairo, Ifakara, Morogoro Vijijini na Mjini ziendeele kupewa fedha na kujengwa na kukamilika. Mheshimiwa Waziri nasema haya kwa sababu Hospitali ya Mkoa inazidiwa na wagonjwa (mrundikano wa wagonjwa) kwani Wilaya za Mkoa hazina hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kwa ujenzi wa Kituo cha Afya Mikumi, majengo ni mazuri na hivi karibuni kitaanza kutumika. Mpaka sasa ameletwa daktari mmoja,

naomba na kushauri waletwe wataalam wengine zaidi kusudi wananchi wapate matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo nililoliona katika kituo hiki ni ukosefu wa jengo la *mortuary*. Ujenzi mzima unaendelea kukamilika ila hakuna mpango wa *mortuary*. Naiomba Serikali yangu ifikirie jambo hili kwani Mikumi, hususan Wilaya ya Kilosa, kuna watu wengi na hivyo hata jengo hili ni muhimu ingawaje watu hatutaki kusikia kifo.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa vituo vya afya vinavyoendelea kujengwa. Nashauri mpango huu uendeleo kuvifikia vituo vya afya ambavyo wananchi wamejenga na kuachia ngazi ya maboma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa Vituo vya Afya Dutumi na kumaliza majengo yaliyokaa muda mrefu, hilo ni ombi letu wananchi wa Morogoro Vijijini. Katika ziara zangu Zahanati ya Hembeti ambayo inatumika pia kama Kituo cha Afya kwenye Kata ya Hembeti, Wilaya ya Mvomero, majengo yake yamechakaa sana tena sana. Naiomba Serikali zahanati/kituo cha afya hiki kikarabatiwe. Pia, hakuna wataalam wa kutosha kuanzia madaktari hadi manesi. Kituo hiki nashauri kiangaliwe vizuri ili kizidi kutoa huduma nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina tatizo la utapiamlo na hasa udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano. Tatizo kubwa ninaloliona ni elimu kwa wananchi. Nashauri elimu ya lishe ya mkakati na ya vitendo itolewe zaidi. Wananchi wakipata elimu ya kutosha kuhusu mambo ya lishe hasa kwa akina mama wajawazito na akina mama wanaonyonyesha utapiamlo utapungua au utakwisha kabisa hapa nchini Tanzania kwani kwa ujumla vyakula vya kutosha tunavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vya maendeleo ya jamii. Naomba na kushauri ukarabati wa vituo hivi. Ni kweli wataalam wa maendeleo ya jamii wanatakiwa sana na muhimu kwa kusukuma maendeleo ya jamii yetu hapa nchini. Watumishi hawa ni muhimu sana kwa kusukuma maendeleo.

Nashauri kila kijiji kiweze kupata Afisa Maendeleo ya Jamii ili kuharakisha maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ndoa. Na mimi naungana na Wabunge wenzangu kusema kuwa kutokana na hali na maendeleo tuliyonayo sheria hii ni ya muda mrefu na imepitwa na wakati. Nashauri iletwe humu Bungeni ili ibadilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ugonjwa wa malaria udhibiti wake uangaliwe kwa undani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto wa kike, hasa majumbani na wapatapo shida hawana pa kuwatunzia wakati usuluhisho unaendelea hivyo kupelekea kurudi katika majumba yao ambayo sio salama kwa wakati huo. Nashauri Serikali ijenge majengo salama kwa usalama wa waathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na upungufu wa wodi za wanawake, hasa katika Hospitali ya Makandana, Tukuyu. Tunaomba Wizara kwa kusaidiana na Halmashauri ya Rungwe kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimba za utotoni. Tunaomba Wizara itoe tamko kwa mabinti wapatao mimba katika umri mdogo kurudi shule hasa walio chini ya miaka 15 kwani kutorudi shuleni kunapoteza haki yao ya kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa/chanjo ya mbwa. Kwa wagonjwa waliong'atwa na mbwa matibabu ni ghali sana. Tunaomba Wizara ipunguze kama sio kutoa bure chanjo hizo kwa waathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipodozi hatarishi. Wizara na wadau wa afya kwa pamoja wafuatilie madawa/vipodozi



hatarishi vinavyoathiri afya za wanawake na watoto. Kumekuwa na madawa yasiyo rasmi katika maduka mengi na dawa kama za kuongeza makalio, matiti, uume na hata wanaojichubua, Wizara ya Afya, *TFDA* na *TBS* kwa umoja wasaidie jamii yetu kutopata matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa watumishi. Wizara ipeleke wataalam hasa wa magonjwa ya wanawake na watoto katika Mkoa wa Mbeya, Wilaya za Chunya na Mbarali, ndiyo zenye changamoto kubwa.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja sambamba na kupompongeza Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho lake zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuzuia miili ya marehemu (maiti) kama sababu ya deni la matibabu hususani katika Hospitali za Muhimbili na Mloganzila ni kero kubwa sana na ni jambo ambalo limekuwa likiigombanisha Serikali yetu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ilianganalie suala hili na ilifanyie uamuzi wa kulifuta haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni mapambano dhidi ya malaria. Tuna kiwanda chetu pale Kibaha cha kutengeneza dawa ya kuulia vimelea vya vidudu vya malaria. Kiwanda kile kinakabiliwa na changamoto ya soko. Lile agizo la Mheshimiwa Rais kuwa kila Halmashauri ikanunue dawa pale halijatekelezwa sawasawa. Niiombe Serikali yangu sikivu kukiokoa kiwanda kile kwa kukipatia soko la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na timu nzima kwa kazi nzuri ya bajeti waliyotuletea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeahidiwa gari la wagonjwa Kituo cha Afya Engusero. Tunaomba yatakopatikana basi tupatiwe gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa watumishi. Tuna watumishi 296 na upungufu ni watumishi 210, tunaomba tupatiwe watumishi hao kwa ajili ya zahanati, vituo vya afya na hospitali ya wilaya. Vilevile, tunaomba Waziri kutembelea Wilaya ya Kiteto kuzungumza na watumishi na kuangalia uchakavu wa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja, Mungu awabariki.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya. Hakika mnaitendea haki Wizara hii, nawatakia kila la kheri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana kutembelewa na Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu kwa nyakati tofauti. Ziara zote zimezaa matunda ya msaada wa kifedha na vifaa, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Wilaya ya Urambo ina vijiji 59, zahanati 22, tunaomba tusaidiwe kumalizia maboma 8 ambayo yamejengwa ili tuongeze huduma kwa wananchi. Tuna kata 18, vituo vya afya vipo viwili, kimoja kimekamilika tunashukuru na kimoja kinaendelea kujengwa. Tunaomba tuongezewe vituo viwili katika Kata za Songambe na Vumilia ambapo wananchi wameanza msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kituo cha Afya Uyogo ambacho wananchi wanajenga kwa kushirikiana na marafiki kutoka Uingereza. Tunaomba ahadi za Waziri zitimizwe za *ambulance* kwa kuwa ni mbali na Hospitali ya Wilaya na tupewe shilingi milioni 20 alizoahidi ili kukamilisha kituo kinachojengwa. Vilevile, tunaomba tupewe shilingi milioni 50

alizoahidi Waziri alipotembelea Kituo cha Afya cha Usoke kwa lengo la kukamilisha miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kupitia mradi wa *ADB* ulianza kujenga jengo la *theater* ambalo liko tangu mwaka 2010. Tunaomba Serikali itusaidie kumaliza jengo hilo ambalo linahitaji fedha zipatazo shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, Urambo haina chumba cha wagonjwa mahututi (*ICU*). Kuna jengo lililoanza kujengwa kwa mpango wa *LGDG* linaloweza kukamilika kwa gharama ya shilingi milioni 20. Tunaomba Waziri akumbuke ahadi hii na aitekeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Waziri aliahidi kutoa shilingi milioni 20 kwa ajili ya kukamilisha wodi ya akina mama. Tunaomba tusaidiwe fedha hizo kwa ajili ya Zahanati ya Itebulanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Urambo ina *X-ray* ya kizamani ya *analogue*. Tunaomba *X-ray* ya kisasa ya *digital*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tunaomba tuongezewe wafanyakazi kwa kuwa tuna upungufu wa asilimia 48.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza Viongozi wa Wizara hii, Waziri Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile kwa kazi nzuri wanayofanya ya kusimamia Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita katika maeneo matatu. Kwanza, Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini inayojengwa Mtwara. Ujenzi wa Hospitali hii umeanza muda mrefu na sasa umesimama. Mheshimiwa Waziri alipotembelea ujenzi huu mwaka juzi aliahidi kuwa ni bora jengo lililopo likakamilika na baadhi ya Idara zikaanza kufanya kazi. Nashauri ujenzi uendelezwe kwenye eneo hili

na hospitali ifunguliwe kwa kuanza na idara ambazo zinaweza kutumia jengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mtwara (Ligula). Hospitali hii inahitaji ukarabati mkubwa wa majengo yake na ina idadi chache ya watumishi kwa maana ya madaktari na wauguzi. Hatua zichukuliwe ili kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, dawa za magonjwa yasiyoambukiza (kisukari na shinikizo la juu la damu). Kuna ongezeko kubwa la wagonjwa wa magonjwa hayo na kwa kuwa wagonjwa hao hutumia dawa muda mrefu na bei zake ni za juu, nashauri Serikali iangalie kwa karibu tatizo hili kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuwa na programu za kutoa elimu kwa jamii ili kupunguza watu wanaoambukizwa;

(ii) Kuhakikisha kuwa dawa zinapatikana kwa bei nafuu hadi ngazi za chini; na

(iii) Kliniki za binafsi zidhibitiwe kwa kuwa zinatoa huduma kwa bei ya juu.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100 kwa sababu Mheshimiwa Waziri Umyy Ally Mwalimu na Naibu Waziri, Dkt. Faustine Ndugulile wametufanyia mambo makubwa ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Wamehamasisha upatikanaji wa shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Namtumbo na ujenzi umekamilika.

(ii) Wamehamasisha upatikanaji wa shilingi milioni 1,500 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo na ujenzi unaendelea.

(iii) Wamenihamasisha mimi Mbunge wa Namtumbo kutumia Mfuko wa Jimbo pamoja na mchango wangu binafsi kukamilisha ujenzi wa zahanati saba za Njoomlote, Mwangaza, Namanguli, Mageuzi, Ruvuma, Kitanda na Songambebe, pamoja na zahanati zinazoendelea kujengwa kwa nguvu za wananchi na mchango kidogo wa mimi Mbunge za Nahimbo, Ulamboni, Mwinuko, Ukiwayuyu, Msufini, Mhangazi na Luhangano. Hatua hii ikikamilika tutakuwa tumeongeza vijiji 15 vitakavyokuwa na zahanati.

(iv) Wamehamasisha nguvu za wananchi zitumike kuunga mkono Mbunge wao katika kujenga Kituo cha Afya cha Mchomoro na kukamilisha ujenzi wa baadhi ya majengo ya Kituo cha Afya cha Lusewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna alivyotuchekecha sisi Wabunge na kugundua kipaji kikubwa cha uongozi na unyenyekevu alionao Waziri na kumteua kuwa Waziri mwenye dhamana ya afya ya Watanzania. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais na Waziri hongera kwa kazi iliyotukuka unayoifanya. Naamini chini ya ushawishi wa Waziri akiungwa mkono na Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, wana Namtumbo wanatarajia yafuatayo:-

(i) Vituo vya afya kwa umuhimu na au mpangilio huu wa Lusewa, Mchomoro, Mkongo Gulioni na Mtakanini vitaimarishwa kwa kujenga majengo mapya.

(ii) Vituo vya afya nane vilivyopo na vitakavyojengwa katika Wilaya ya Namtumbo viimarishwe kwa kupatiwa wahudumu wa afya, vifaa tiba, vitendanishi na madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Namtumbo ina changamoto kubwa za upatikanaji wa huduma za upasuaji. Kutokana na umbali uliopo kwenda Kituo cha Afya cha Lusewa na Hospitali ya Mkoa kunakopatikana huduma hiyo ya upasuaji, naomba tusaidie kwa uharaka utakaowezekana

tupatiwe fedha za kujenga Kituo hicho cha Lusewa pamoja na vituo vingine vitatu vya Mchomoro (ambako Mheshimiwa Rais ameahidi kuchangia shilingi milioni 100), Mkongo Gulioni (kinahudumia Kata sita za Mkongo Gulioni, Mkongo, Luchili, Limamu, Ligeri na Lisimonji na mwisho Kituo cha Mtakanini kilichoahidiwa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli huduma za afya bure kwa watoto wa chini ya miaka mitano, wajawazito na wazee wenye umri zaidi ya miaka 60 ni changamoto kubwa lakini kabla ya miundombinu ya afya kukamilika kujengwa ni kazi bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie kukupongeza na kukushukuru kwa namna unavyoakisi dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuwagusa na kuwainua wanyonge katika sekta zako hususan sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa kwa ajili ya *ICU*. Pamoja na mazingira magumu kijiografia kwenye visiwa vya Ukerewe bado Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe haikuwa na *ICU*. Hivi sasa tumepata mfadhili anayetujengea jengo la upasuaji (*theatre*). Hivyo basi, lililokuwa jengo la upasuaji linabadilishwa kuwa chumba cha wagonjwa mahututi (*ICU*) lakini patakuwa hakuna vifaa kwa ajili ya chumba hicho. Naomba Wizara isaidie kutoa vifaa kwa ajili ya chumba cha wagonjwa mahututi (*ICU*) kwenye Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe (Nansio).

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la umeme. Shughuli za utoaji huduma za afya zinaathiriwa sana na tatizo la umeme. Mpango wa wilaya ilikuwa kutumia shilingi milioni 70 kutoka mfumo wa RBF lakini pesa hizo zimezuiliwa mpaka sasa kutokana na mgongano kati ya Wizara mbili, pesa hizi ilikuwa zitumike kununua *generator/solar system* kama *standby power system*. Naomba Wizara itusaidie kupata

ruhusa ya kutumia pesa hizi kutatua tatizo la umeme kwenye Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, gari la wagonjwa. Baada ya ajali ya MV Nyerere tarehe 20/09/2018 katika Kisiwa cha Ukara, Mheshimiwa Rais alielekeza ujenzi/ukarabati wa Kituo cha Afya Bwisa ambacho kiko hatua za mwisho kukamilika. Tarehe 15/11/2018 Mheshimiwa Waziri wa Afya wakati akijibu swali langu Bungeni aliahidi kutupatia gari la wagonjwa kwa ajili ya Kituo cha Afya Bwisa. Gari hili ni muhimu sana kuokoa maisha ya watu wetu katika visiwa hivi. Naomba gari hili litolewe na kupelekwa kwenye Kituo cha Afya Bwisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vya afya. Ili kufika katika Kisiwa cha Irugwa inakubidi utumie zaidi ya saa nne kwa usafiri wa majini. Hali hii ya kijiografia inaweka hatarini maisha ya wananchi walio katika Visiwa hivi vya Irugwa vyenye wakazi zaidi ya 20,000. Hivyo, Kituo cha Afya kinahitajika kwenye kisiwa hiki ili kuokoa maisha ya watu wetu. Kwa kuwa wananchi wameanza ujenzi wa Kituo cha Afya Irugwa basi Wizara ituunge mkono ili tukamilishe kituo hiki kwa kukiingiza kwenye mpango wa uboreshaji wa vituo vya afya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi na vifaa. Kwa kuwa Kituo cha Afya Bwisa kinakamilika kama ilivyo Kituo cha Afya cha Muriti, Wizara ifanye maandalizi ya kupeleka vifaa na watumishi kwenye vituo hivi bila kusahau Hospitali ya wilaya ili wananchi wetu wapate huduma ili kukidhi malengo tarajiwa.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Tabora Kaskazini lina kituo kimoja tu cha afya. Namwomba sana Waziri tuipandishe hadhi Zahanati ya Ilangulu iwe kituo cha afya ili kwa jumla tuwe na vituo viwili vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya, hongereni sana. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwajali

wanyonge, Wilaya ya Uyui tumepewa Hospitali ya Wilaya inayojengwa kwa shilingi bilioni 1.5 pia Kituo cha Afya cha Upuge kwa shilingi milioni 500. Namkaribisha Mheshimiwa Waziri atembelee Jimbo langu na Kituo cha Afya cha Upuge lakini pia Zahanati ya Ilolangu ili ajionee mwenyewe ujenzi uliofanyika hasa katika zahanati na akiridhia kiwe kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba gari la wagonjwa (*ambulance*) kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Upuge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Umy Mwalimu kwa hotuba nzuri ya Wizara ya Afya. Nampongeza Waziri kwa utendaji mzuri na kuiongoza Wizara vizuri. Nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile kwa uchapakazi wake na watendaji wakuu wa Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Jimbo la Nkasi Kusini kupatiwa gari la wagonjwa liende Kata ya Kala ambayo iko kilomita 150 kufika Makao Makuu ya Wilaya. Umbali huu umesababisha vifo vingi vya akina mama na watoto hasa wanapopata uzazi pingamizi kwa vile huduma zilizopo Kata ya Kala ni za kiwango cha zahanati ambapo wataalam hawapo lakini pia hakuna gari la wagonjwa ili kunusuru wazazi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi Desderius John Mipata tuko Wilaya moja na Mheshimiwa Keissy ambaye alipewa *ambulance* mbili. Nina wakati ngumu sana wakati kiuhalisia Jimbo langu kijiografia ni gumu zaidi. Kwa heshima na taadhima namwomba Mheshimiwa Waziri anipe gari moja tu la wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la pili, watumishi wa afya Wilayani Nkasi ni wachache sana. Pale Wilayani namuona Dkt. Mwakapimba pekee ndiyo yuko *active* zaidi



na mwenye uwezo mzuri wa kielimu na anafanya kazi sana sana. Yeye ni *Medical Officer*, wapo *AMO's* wengine lakini kiutendaji utagundua kuwa *MD's* ni muhimu waongezeke asiwe yeye pekee maana Mkuu wa Idara mara nyingi yuko kwenye mambo ya utawala zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, manesi yaani wauguzi ni wachache sana. Pia *clinical officer* ni wachache sana, zahanati nyingi zinaendeshwa na manesi na wahudumu. Watumishi wa usingizi ni wachache sana Nkasi au niseme hatuna. Naomba suala hili la kupatiwa watumishi lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitambulisho vya wazee kutibiwa bado Halmashauri hawajatoa kipaumbele licha ya kuagizwa na Madiwani mara kwa mara. Naomba uwaagize na kufuatilia hasa *Nkasi District Council*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nawaombea Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara Mungu awajalie afya na nguvu ili muendeele kusaidia Watanzania. Kwa ujumla Watanzania wanaridhishwa na utendaji kazi wa Wizara hasa upatikanaji wa dawa, mmefanya vizuri sana.

**MHE. ZAINAB M. AMIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, niwapongeze Mheshimiwa Waziri Umyy Mwalimu pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile kwa kazi nzuri wanazozifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali fedha zinazopitishwa katika bajeti zifikishwe kwa wakati ili majukumu yaliyopangwa yaweze kutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipimo cha Dengue ni ghali sana kwa wananchi wenye kipato cha chini. Mfano katika Hospitali ya Temeke ni Sh.40,000 na Regency Hospitali ni Sh.77,000 na hata kama una Bima ya *NHIF* ya Bunge unalipia *cash* hususan Regency Hospitali. Nashauri kutokana na ugonjwa huu kuwa katika Mikoa ya Pwani, Tanga, Dar es Salaam na kadhalika na kipindi hiki cha mvua watu wengi

huugua na kushindwa kupata fedha za kulipia kipimo cha Dengue, Serikali ipunguze gharama za upimaji wa ugonjwa huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Rufaa Temeke Dar es Salaam, eneo lake ni dogo na wodi nyingi ni chakavu na hazikidhi mahitaji ya wagonjwa. Nashauri zile wodi za zamani zibomolewe yajengwe maghorofa. Mfano mzuri Regency Hospitali Dar es Salaam eneo lilikuwa dogo likabomolewa wakajenga maghorofa ili kukidhi mahitaji wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Rufaa Muhimbili na Mloganzila Dar es Salaam. Naishauri Serikali ijenge jengo la kusubiria wagonjwa kwa wale ndugu na jamaa wanaowasindikiza wagonjwa wao watokao Mikoani ili waweze kutoa msaada wa kijamii kwa wagonjwa wao maana siyo wagonjwa wote wana ndugu katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wale wananchi wanaonunua miwani hovyoy bila kupimwa iwe kwa ajili ya urembo au la, wasivae bila kupewa ushauri kutoka kwa madaktari wa macho. Maana kuna baadhi ya wananchi wamepata matatizo ya macho kwa kununua miwani bila kufuata ushauri wa daktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilitoa ushauri Serikali iondoe tozo katika maiti hususani katika hospitali zetu zote. Maana ni kero kwa wafiwa na wakati mwingine walimuuguza ndugu yao kwa kipindi kirefu na walitumia gharama nyingi sana na marehemu wakati wa uhai wake alikuwa na mlipa kodi mzuri kwa kununua bidhaa mbalimbali kwa mahitaji ya kila siku. Hivyo, naishauri Serikali iondoe tozo/ malipo kwa maiti katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na matangazo mengi haswa Dar es Salaam ya Waganga wa Jadi na vipeperushi vingi hugaiwa katika makutano ya barabara. Naishauri Serikali hawa Waganga wa Jadi watoe matangazo

yao katika vyombo husika kama redio, televisheni na magazeti na siyo kubandika katika nguzo za umeme, miti na kutoa vipeperushi barabarani.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Umy Mwalimu, Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa hotuba nzuri yenye uelewa, pia kwa kazi nzuri wanayofanya kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kwa ongezeko la madawa na vifaa tiba. Ushauri; kwa kuwa Hospitali ya Rufaa Kitete ina majengo ambayo hayajakamilika, niombe Serikali ikamilishe ili yaweze kutumika hasa Chuo cha Uuguzi. Nishauri pia katika majengo yanayojengwa sasa ni vema yakazingatia ujenzi na jengo la mama Ngojea, ili wanawake wengi waweze kupumzika wanaposubiri kujifungua, ishirikiane na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara kutenga sehemu maalum katika kila Kituo cha Afya kwa ajili ya kutunzia watoto Njiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, magonjwa; niombe elimu iendelee kutolewa kwa ajili ya ugonjwa wa *dengue*, Ini, ili wananchi wengi waweze kujua tiba yake, tahadhari pia. Kwa nini ugonjwa huu wa *dengue* haupo kwenye Bima za Afya? Kwani wananchi wengi wanasumbuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba Serikali ipeleke mashine za kupimia sukari katika Vituo vya Afya na Zahanati ili kuokoa maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wanawake; kwa kuwa benki hii tangu ianze haijatoa gawio lolote mpaka sasa na mimi nikiwa ni mhanga wa kutoa hisa (hisa Milioni mbili) nini hatima yangu? Kwa kuwa fedha yangu imekaa muda mrefu, je, naruhusiwa kuuza hisa zangu, ili niipate fedha yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Benki ya Wanawake lini itafika Mkoa wa Tabora ili wanawake waweze kukopa. Niombe Serikali iweke Dirisha la ukopaji kwenye Benki ya *TPB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafi wa mazingira, kwa kuwa maeneo mengi hususan Hospitali ya Rufaa Kitete kuna vifaa chakavu kama vile vitanda, meza na magari, je, hakuna utaratibu wa kuuza au kuviondoa kwenye eneo la hospitali na kupeleka eneo lingine? Kwa kuwa vinawekwa eneo la nje na kusababisha mazalia ya mbu. Niombe Wizara itembelee hospitali yangu na kuona hali halisi (Kitete Tabora).

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971; niishauri Serikali kuleta haraka Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Ndoa ili wanawake na watoto wapewe haki zao. Ukatili wa kijinsia unaongezeka hapa nchini, kunyimwa haki wajane na kudhumiwa mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Serikali kwa ujumla na kwa Wizara kwa namna ya pekee kwa kazi nzuri. Changamoto za Wizara hii (Sekta ya Afya) ni nyingi na za muda mrefu na za aina mbalimbali, hivyo, hata utatuzi wake unahitaji muda, rasilimali fedha na kadhalika, lakini taratibu zitapungua sana kutokana na kasi hii. Nawatakikakila la kheri.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto Kitaifa, ziko nyingi bado, lakini hotuba ya Waziri Ukarasa 155 wa kitabu cha hotuba umeainisha vipaumbele vya Wizara na Bajeti kwa mwaka huu. Wakipata fedha kila mwaka, kama wanavyoomba watafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vipaumbele 11, nimechagua kipaumbele cha (iii) na cha (v) ambavyo vinagusa pia moja kwa moja Jimbo la Tunduru Kaskazini na Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wataalam; uhaba wa Wataalam Kitaifa ni 50% na Tunduru ni 35%. Serikali iendelee kuzalisha Wataalam kupitia Vyuu vyetu vilivyopo, Mabaraza ya Wanataaluma na Bodi za Ushauri yafanye kazi zao vema, ikiwa ni pamoja na kusimamia *Professional Ethics*, Kanuni za Kusimamia Taaluma ikiwemo mafunzo ya utarajali zikamilike na zitumike, pia (*CPD - Continuing Professional Development*) iwekewe msisitizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za kushughulikia nidhamu ya Wataalam zitokane na Vyombo vya Taaluma, isipokuwa kwa makosa yasiyokuwa na kitaalam, watumishi waboreshewe maslahi yao, Vyuu viongoze udahili, uwiano (*Ratio*) kati ya Madaktari na Wataalamu wa Kada nyingine za juu na Wataalam wa Kada za Kati kwa mujibu wa *ILO* uzingatiwe. Hatua hii itatoa nafasi ya utoaji wa huduma bora, *concentration* na kupumzika vikiwa ni vichocheo vinavyotegemeana.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru na Jimbo la Tunduru Kaskazini; Hospitali ya Wilaya ni ya siku nyingi, imechakaa (miundombinu), tunaomba ifanyiwe ukarabati. Chumba cha upasuaji mkubwa (*major theatre*), chumba cha upasuaji mdogo, (*minor theatre*) *OPD, X-Ray, RCH, Maabara, Wards* miundombinu yote hii ni chakavu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vifaa tiba; Vituo vya Afya na Zahanati; Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Jimbo la Tunduru Kaskazini lina Kata 24, lakini kuna Vituo vya Afya viwili na kimoja ambacho kinajengwa. Tunaomba *Ambulance* ziweze kusaidia kutoa huduma kwa Vituo vya Afya viwili ambavyo viko kilomita 64 pande tofauti (180<sup>o</sup>).

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Kituo cha Afya cha Nakapanya kipatiwe fedha kwa ajili ya ukarabati kama tulivyobahatika kwa Kituo cha Matemanga. Hii inachagizwa na ukweli huu wa idadi ndogo ya Vituo vya Afya, vitatu tu katika Kata 24. Zahanati pia ni chache, lakini kwa sasa tukiboreshewa Vituo vya Afya tulivyonavyo kwa Wataalam,

miundombinu na Vifaa tiba na kupatiwa *Ambulances* itatusaidia sana.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kazi nzuri ambayo anafanya na wasaidizi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kushukuru kwa kutuletea *ambulance* mpya kwa ajili ya Kituo cha Mwamashimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Kwimba ambayo iko Ngudu ina changamoto nyingi; hatuna mashine ya kufua nguo, *x-ray* ni ya zamani sana inaharibika mara kwa mara, ni *analogue*, tunaomba *digital*, duka la dawa la *MSD*, tunaomba watufungulie pale kwenye hospitali yetu ili wananchi wapate dawa kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Daktari wa Macho walituletea lakini sehemu ya kufanyia kazi hakuna, hatuna chumba cha huduma ya macho, tuna jengo, lakini halijakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri watoto wetu wanaokwenda shule za msingi na sekondari wengi wana magonjwa yafuatayo; pumu, sikosell, kisukari. Watoto wengi wanapata shida shuleni lakini Mwalimu hana uwezo wa kuwasaidia kwa sababu hatujawawezesha. Nashauri Mheshimiwa Waziri awapatie *emergency kit* kwenye shule zote za msingi na sekondari na Walimu wafundishwe jinsi ya kutoa *first aid* kwa mtoto ili wakati anapelekwa hospitali awe amepata huduma ya kwanza ili maisha yake yapone.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Hungumarwa unakua kwa kasi kubwa sana, tunaomba watujengee kituo cha afya kwani zahanati zinaelemewa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri sana na nimtakie mfungo mtukufu wa Ramadhani (*Ramadhan Kareem*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishukuru sana Serikali kwa kutuboreshea Kituo cha Afya cha Malya, kwa niaba ya wananchi wanaozunguka kituo hicho pamoja na wa Jimbo la Maswa, tunaomba kutupatia watalaam hasa daktari, aliyepo ni *clinical officer*, Wauguzi na wahudumu pamoja na watalaam wa maabara, Wafamasia na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumkumbusha Mheshimiwa Waziri ombi la gari kwa ajili ya hospitali ya Sumve kama barua yetu kwako tuliyowasilisha kutokana na jiografia ya eneo. Gari hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa sana kuokoa maisha ya wazazi na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitangulize ombi la kukiboresha Kituo cha Afya cha Nyambiti. Nyambiti ni Mji unaokuwa kwa kasi na kwa haraka sana kutokana na kuwa na viwanda viwili vya kuchambua pamba. Kuna kituo cha treni (*railway station*), sekondari mbili, shule za msingi nne na jamii inayoendelea kukua. Naomba katika mpango wa uboreshaji wa vituo vya afya, Kituo cha Afya cha Nyambiti kiwe kimojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtakie Mheshimiwa Waziri Ummu kila la kheri katika njozi zake na Mungu atamsimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia machache katika Wizara hii muhimu kwa afya ya Watanzania. Nianze kwa kuunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani ambayo imesheheni ushauri na mambo mazuri kwa sekta yetu ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete chini ya uongozi mzuri wa Profesa Janabi na pongezi hizi ziende kwa madaktari wote, wauguzi na watumishi wote wa taasisi hiyo. Taasisi hii imekuwa ikifanya kazi nzuri na imesaidia sana kupunguza gharama za matibabu nje ya nchi, lakini bado kuna mtatizo ya vitendea kazi ambavyo vitarahisha matibabu kwa wagonjwa na hata kwa watoa huduma. Mfano, kuwa na mashine zote kwa ajili ya vipimo hapo hapo hospitali kuzuia kwenda kufanya vipimo nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi hii imekuwa inakusanya fedha nyingi, lakini pale inapoomba tena fedha ambazo walikusanya wao hawapati. Mfano, mwaka jana waliomba bilioni nne, hawakupata wakati waliweza ku-save zaidi ya shilingi bilioni 12 za kwenda kutibu wagonjwa nje ya nchi. Nashauri Serikali itenge 30% ya mapato hayo ili kuwawezesha kuboresha huduma kwa wagonjwa na kurahisisha kazi kwa madaktari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhaifu wa vipimo vya tiba katika hospitali zetu, kumekuwa na tatizo hili kwa wagonjwa kupewa majibu tofauti na maradhi waliyonayo na hii husababisha wagonjwa kutopona maradhi waliyonayo pamoja na kupewa dawa ambazo si sahihi kwa wagonjwa hayo na kufanya dawa hizo kuwa sumu mwilini, badala ya kuwa tiba na hata kusababisha vifo kwa wagonjwa wetu. Wanaopona ni wale wenye uwezo wa kwenda hospitali nyingi kwa ajili ya kupima upya au kwenda nje ya nchi. Je, ni wangapi ambao hawana uwezo huo wanapoteza maisha. Nashauri Serikali kuchukua hatua kwenye suala hili ili kunusuru maisha ya Watanzania na kuhakikisha umakini unakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwajibikaji wa watumishi wa Sekta ya Afya; zipo taratibu na sheria zilizowekwa kwa ajili ya uwajibishaji wa watumishi wa afya, yapo Mabaraza ya Madaktari na Baraza la Wauguzi; haya ndiyo yenye jukumu la kuwawajibisha na si vinginevyo. Toka Awamu hii ya Tano imeanza tumeona viongozi wa kisiasa na wasiokuwa na mamlaka wala taaluma hiyo kuingilia kuwawajibisha



Madaktari na Wauguzi pasipo kufuata taratibu. Tunajua upo upungufu unaofanwa na watumishi hao, lakini ni muhimu kufuata taratibu zilizopo. Tusipofanya hivyo tunapunguza morali wa kufanya kazi kwa watumishi hao muhimu wa sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu huo mdogo wa sekta hii ya afya.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Tano chini ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa jitihada zake za kuboresha huduma ya afya kote nchini hususan ujenzi wa miundombinu ya majengo nchini kote; kupunguza upungufu mkubwa wa dawa na vifaatiba kote nchini; kupunguza upungufu mkubwa wa watumishi wa kada za afya kote nchini; kupambana na maambukizi ya VVU nchini na mpango mkakati wake wa kuboresha sekta hii kila mwaka, hali inayowafanya wananchi kuwa na imani kubwa kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itazame upya mtawanyiko wa Madaktari katika Hospitali za Wilaya na Mikoa ili kuhakikisha angalau kila hospitali inapata mtaalam mmoja kwa kila kitengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali iangalie sera ya familia kutunza wazee na watoto kupitia familia zao badala ya kutelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya Hospitali ya Mji wa Mbulu kupatiwa gari la kusafirisha wagonjwa (*ambulance*) kwani gari lililoko limechakaa sana na wagonjwa wengi wanapata rufaa ya kupelekwa Hospitali ya Rufaa ya Haydom na *KCMC* Moshi nako ni mbali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la Tarafa ya Nambis katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu haina hata kituo kimoja katika kata zote tano na ni mbali kutoka Hospitali ya Wilaya

hali inayosababisha akinamama wajawazito kukosa huduma na kutembea zaidi ya kilomita 30 mpaka 40 kufika Mbulu Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba Mheshimiwa Waziri wa Afya afanye ziara katika Jimbo la Mbulu Mjini hususan Tarafa hiyo ya Nambis kwa kuwa alishaahidi kufanya ziara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanazofanya. Nashukuru kwa kuimarisha huduma ya afya ya Mama na Mtoto hali ambayo imesababisha katika Hospitali ya Temeke mwezi Machi hakuna kifo cha uzazi. Yote hayo yametokana na kuimarika kwa huduma zote za afya ya Mama na Mtoto katika Hospitali ya Temeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yafuatayo yazingatiwe (changamoto):-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba mashine za *CT Scan* kwa Hospitali za Mkoa wa Dar es Salaam, Temeke, Mwananyamala na Amana. Hospitali hizo hazina mashine za kufulia nguo, mashuka mpaka yapelekwe Muhimbili jambo ambalo linafanya kipindi fulani mashuka yanapungua hospitalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama kubwa za matibabu kwa hospitali zinazopitia Wakala wa *CRDB*, unatakiwa ununue kadi kwa Sh.10,000 au utumie ya Wakala kwa Sh.2,000 kila unapokwenda hospitali. Mifumo ya Serikali itumike, kwani inaweza kusaidia zaidi wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya fedha kwa maiti ni changamoto kubwa. Mtu anapofariki na deni la dawa anatakiwa kulipiwa na ndugu, unafikia wakati ndugu wanashindwa kulipia hapo viongozi tunashirikishwa na maiti

kukaa muda mrefu. Naomba Serikali watoe ufafanuzi kuhusiana na jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapoenda na mgonjwa mara nyingine *Emergency* Muhimbili unamlipia mgonjwa, tena unapewa *bill* ya dawa usiku Sh.500,000 na zaidi, lakini baada ya sekunde unakuta mgonjwa amefariki. Kutokana na *panic* unaacha kila kitu, kwa nini tusiwe na kianzio cha dawa kwa wagonjwa wanaokuja kuanza matibabu kabla ya kupewa *bill*?

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali/zahanati ya Mbagala Zakhem imezidiwa sana, eneo ni dogo na wananchi wanaohitaji huduma ni wengi sana kutokana na kukua kwa Mji wa Mbagala na ongezeko kubwa la watu. Pamoja na jitihada za halmashauri kujenga zahanati ya Maji Matitu na Charambe, lakini jiografia inakataa kwa kuwa mgonjwa akitoka Zakhem anaenda Temeke na Zakhem ni katikati ya Mji wa Mbagala. Naomba Serikali isadie hata kujenga ghorofa la *OPD* kwa wagonjwa wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga hoja mkono na kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi nzuri inayoonekana. Hata hivyo, bado ningependa kushauri na kujua hatima ya uanzishaji wa Chuo cha Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (*NIMR*) maeneo ya Amani -Muheza. Majengo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyaona yanazidi kuharibika bila kutumiwa, ningeshukuru kama suala hili litapewa umuhimu wa kipekee. Aidha, bado tunakumbushia suala la gari la wagonjwa, (*Ambulance*) ambapo katika Jimbo la Muheza hatuna kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la dawa ya nyoka kupewa bure kwa wananchi naomba lizingatiwe kwani bei ya dawa hizo ni ghali sana.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Wizara ya Afya kwa juhudi kubwa zinazoonekana za kuongeza na kuboresha huduma za afya na usafi wa mazingira nchini. Hivyo kwa dhati kabisa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kuwatakia utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kwa fedha za ujenzi wa hospitali shilingi bilioni 1.05 na ukarabati wa kituo cha afya cha Mgori shilingi milioni 400 na Msange shilingi milioni 700. Sambamba na mafanikio haya, tulipata pia usajili wa Hospitali ya St. Carolos Mtinko kuwa Hospitali Teule ya Wilaya. Sambamba na upatikanaji wa dawa kwa kiwango cha kuridhisha, hongera sana kwa Mheshimiwa Umy na timu yake kwa mafanikio haya katika Jimbo la Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mafanikio hakukosi kuwa na changamoto, Jimbo la Singida Kaskazini lina wananchi zaidi ya 250,000 ambapo kwa wastani wa watu 5,000 kwa kituo cha afya tuna uhitaji wa zaidi ya vituo vitatu vya afya ili kuboresha utoaji wa huduma za afya. Hivyo niombe Wizara kwa moyo wa dhati kutusaidia fedha za ukarabati kwa kituo cha afya cha Ilongerero na angalau ukamilishaji wa majengo yaliyoanzishwa na wananchi kwa Kata za Ngimu na Makuro ambayo yana zaidi ya miaka nane kusubiri kupauliwa. Ningeshauri kwa hatua ya sasa tuombe shilingi milioni 300 kukamilisha hatua ya awali tukisubiri upanuzi katika awamu zinazokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua pia juhudi za Serikali katika kuongeza Watumishi wa Sekta ya Afya, hivyo niombe sana Serikali kutusaidia watumishi katika Hospitali Teule ya Wilaya (St. Carolos Mtinko) na zahanati na kituo cha

afya. Vilevile uboreshaji na usimamizi wa Maendeleo ya Jamii unahitajika maana kuna huduma zisizoridhisha kabisa kwa wananchi hasa vijijini. Hii inatokana na usimamizi usioridhisha na ukosefu wa vitendea kazi ambavyo vimekuwa ndiyo visingizio vya kutokutekeleza wajibu wao. Mheshimiwa Waziri tumefanya kazi kubwa ila tusipoangalia watendaji hawa watatuangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa wananchi tutaendelea kushiriki katika miradi ya maendeleo inayopata fedha kutoka Serikalini na kuendelea na ujenzi wa zahanati katika vijiji vyetu ili kuunga mkono juhudi za Serikali kuboresha hali ya huduma nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Afya kwa juhudi inazofanya za kuboresha Sekta ya Afya nchini. Katika Jimbo la Korogwe lenye tarafa tatu na kila tarafa ikiwa na kituo cha afya, tuna gari moja tu la kubebea wagonjwa. Gari ambalo na lenyewe limechakaa sana maana ni la muda mrefu, naiomba sana Wizara kwa unyenyekevu mkubwa watusaidie tupate gari la wagonjwa maana vituo vya afya viko mbali na hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokea fedha za ujenzi wa Kituo cha Afya kipyaa katika Kata za Mkumbara, kituo kimekamilika. Tunaiomba Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI kutupatia vifaa ili kituo hiki kianze kufanya kazi ya kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa watumishi katika Wilaya ya Korogwe kwa zaidi ya 46%; tunaiomba Wizara kusaidia upatikanaji wa watumishi hawa ili kuboresha huduma za afya wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha na kuratibu vizuri huduma za wazee, ni vyema Serikali ikaandaa Sheria ya Wazee kama ilivyo kwa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, viko vituo vya afya vya muda mrefu kama Kituo cha Afya cha Magoma na Bungu ambavyo vinahitaji ukarabati na upanuzi. Pamoja na uhitaji wa ukarabati na upanuzi, pia vifaa kama vitanda vimechakaa sana vinahitaji kubadilishwa kama siyo kuongezwa. Naiomba Wizara ianzishe utaratibu wa kuongeza vifaa kwenye vituo vya afya kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ustawi wa Jamii; viko vituo vya kulelea watoto/makao ya watoto ambavyo havina hadhi ya kuwa makao ya watoto na vingine vinatuhumiwa kwa kashfa mbalimbali kama unyanyasaji na ukatili wa kijinsia na Maafisa Ustawi walioko wilayani baadhi yao siyo waaminifu, ni vyema Wizara iimarishe utaratibu wa ukaguzi wa makao ya watoto.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Serikali kwa kutujengea Kituo cha Afya Malangali, Kata ya Malangali ambacho kitatoa huduma katika Kata tatu za Ihwanza, Idunda na Malangali yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi pia kwa kutujengea Hospitali ya Halmashauri ya Mufindi ambayo itahudumia kata 27 katika Wilaya ya Mufindi pia itatoa huduma kwa watu wote ndani na nje ya Watanzania sababu ni Halmashauri yenye wafanyakazi wengi sana na wawekezaji wengi wakubwa na wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali kumalizia Kituo cha Afya cha Kata ya Mtwango na Kituo cha Afya cha Kata ya Mninga. Serikali imalizie ujenzi wa Zahanati katika Kijiji cha Nzivi, Kinegembasi, Iramba, Nyigo, Udumka na Ikaning'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali ituletee Watumishi katika vituo vyetu tuna tatizo kubwa la watumishi katika Jimbo la Mufindi Kusini. Nitashukuru sana kama Serikali itatekeleza kwa muda maombi hayo.

Ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja, lakini pia naomba kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya. Pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na Wizara, naomba kuchangia hoja kwa kuangazia maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, uhamasishaji wa akinamama kujifungulia zahanati, vituo vya afya na hospitali. Kuna changamoto kubwa ya wodi za kujifungulia, wataalam na vifaa katika *facilities* tulizonazo katika Wilaya ya Longido. Vijiji vingi havina zahanati na kwa vichache vilivyonavyo nafasi na huduma hazitoshelezi kulingana na uhitaji.

Naomba Serikali iongeze kasi katika kujenga zahanati na vituo vya afya katika vijiji na Kata za Ketumbeine, Kimokouwa/Namanga na Tarafa ya Enduiment.

Mheshimiwa Naibu Spika, Suala la Afya kwa Umma (*Public Health*); Wilaya ya Longido tuna changamoto kubwa ya kutokuwa na gari la kuzoa taka kwenye miji yetu midogo na pia gari la kunyonya maji machafu vyoo vinapojaa. Naomba kumuuliza Waziri kuwa Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa watu kila wilaya (Halmashauri) imepata gari la taka na la kunyonya maji machafu kwenye vyoo hasa vya Taasisi za Umma kama hospitali, shule na kwingineko?

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji dawa kwenye zahanati na vituo vya afya; katika Wilaya ya Longido, tuna kata ambazo zinategemea zahanati moja tu kama Namanga ni kuwa Idadi ya Wakazi ni kubwa sana (zaidi ya wakazi 12,000) mgao wa dawa wanayopata kila baada ya miezi mitatu toka *MSD* hazimalizi hata mwezi mmoja kabla ya kwisha na wananchi hulazimika kwenda kununua madawa kwenye maduka ya binafsi. Hali hii imepelekea wananchi kutoona manufaa ya kujiunga na Mfuko wa Bima ya Jamii (*CHF*) kwa sababu hawapati dawa nyakati zote. Naomba kuishauri Serikali kugawa dawa kulingana na idadi ya watu na wanaohudumiwa katika kituo husika badala ya kuangalia kiwango kuwa ni zahanati au kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Mandatory Health Cover*, ulazima wa kila mtu/Mtanzania kuwa na Bima ya Afya); naunga mkono hoja ya kutaka kila Mtanzania kuwa na Bima ya Afya, lakini nashauri kuwa kabla ya kupitisha Sheria ya kusimamia zoezi hili, Serikali ihakikishe kuwa kila kituo cha huduma ya Afya (Zahanati, Kituo cha Afya, Hospitali) kinakuwa na dawa zate za msingi wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uhaba wa nyumba za Wahudumu wa Afya hasa vijijini; katika Wilaya ya Longido tuna changamoto kubwa ya nyumba za Wauguzi hasa katika Zahanati zetu za vijijini. Kwa mfano katika Kijiji cha Losirwa, Kata ya Iloinenito, Tarafa ya Longido, Madaktari na Nesi wanaishi ndani ya zahanati kutokana na ukosefu wa nyumba za kuishi na kijiji kilichoko katika eneo lenye mazingira magumu kwa barabara, mawasiliano na hata maji. Naomba Serikali itenge bajeti ya kusaidia maeneo kama hayo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumalizia ujenzi wa vituo vitatu vya afya, naomba kushukuru Serikali kwa kuwa ilitutengea fedha mwaka uliopita kwa ajili ya ujenzi wa vituo viwili vya Afya – Kata ya Engiromibor shilingi milioni 400 na Kata ya Kimokouwa shilingi milioni 700. Kwa Vituo hivi viko katika hatua za umaliziaji na fedha tulizopewa zimemalizika, naomba Serikali itenge tena fedha katika bajeti hii ili tuweze kumalizia Kituo cha Engareneibor kinahitaji shilingi milioni 269 kumalizika ni Kimokouwa tunahitaji shilingi milioni 310 kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tuna Kituo cha Afya kipya tulichoanza kujenga kwa nguvu za wananchi katika Tarafa ya Ketumbeine, Kata ya Ketumbaine. Tumeweza kujenga hadi kupaua na sasa naomba Serikali ituunge mkono ili kumalizia kituo hicho mwaka huu wa fedha ili kianze kutoa huduma kwa wananchi wa vijiji 20 vya Tarafa ya Ketumbeine ambao kwa miaka yote wamekuwa wakifuatilia huduma za afya Longido ambavyo kwa vijiji vingine ni zaidi ya kilomita 110 kwenye barabara mbovu za vumbi.



Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba tena kusema naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri, lakini pia naipongeze Wizara yote kwa ujumla kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi pamoja na changamoto ya ufinyu wa Bajeti (fedha) zinazowakabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za kinga hususan chanjo ni muhimu sana katika suala la afya za watoto miaka walio na umri wa chini ya miaka mitano na wanawake wajawazito. Ili Wizara iweze kutekeleza kwa ukamilifu huduma hii inahitaji uwepo wa dawa, chanjo na vifaa vya kutolea chanjo pamoja na usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Malinyi inatekeleza huduma za chanjo kwa ugumu sana kwa kutokuwepo na gari la chanjo. Kubwa zaidi wilaya inakabiliwa na uhaba mkubwa na magari, hivyo kusababisha Idara yote ya Afya katika Wilaya ya Malinyi haina kabisa gari la kuhudumia shughuli za afya ikiwemo huduma za utoaji chanjo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kutokuwepo na gari la chanjo au gari maalum kwa huduma za afya katika Wilaya ya Malinyi; nimemtaarifu Waziri wa Afya Mheshimiwa Umyy Mwalimu naye aliahidi kutupatia gari moja zitakapowasili gari maalum za chanjo mwishoni kwa 2018. Gari hizo za chanjo zimefika, lakini Wilaya ya Malinyi haijatangewa gari hata moja, tunaomba gari moja toka Wizara ya Afya kwa huduma za afya katika Wilaya ya Malinyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Njombe ni miongoni mwa mikoa inayojengewa Hospitali za Rufaa. Hospitali ya Mkoa wa Njombe imewekwa jiwe la msingi na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Waziri katika maelezo yake kabla kuwekewa jiwe la msingi mbele ya Mheshimiwa Rais na mbele ya umati wa wananchi wa Njombe Mjini, aliahidi hospitali yetu itaanza kazi mwezi Julai na maelezo hayo yalirudiwa tena wakati wa kumkaribisha Mheshimiwa Rais kuweka jiwe la msingi. Wananchi wa Njombe tungefurahi sana kuona Hospitali yetu mpya inaanza kutoa huduma kama alivyoahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jambo ambalo linanitia shaka wakati Mheshimiwa Waziri akiwasilisha bajeti yake hajaonesha bayana kama hospitali hii itafunguliwa kama alivyoahidi. Nimepitia Kitabu cha Hotuba sijaona kabisa fungu mahususi kwa vifaa vya hospitali vipya. Naomba wakati wa kuhitimisha hotuba, Mheshimiwa Waziri atoe kauli ya Serikali ndani ya Bunge kututhibitishia wananchi wa Mkoa wa Njombe kuwa hospitali yetu itaanza kutoa huduma kama alivyotuahidi. Vinginevyo namfahamisha mapema Mheshimiwa Waziri kwamba nitazuia shilingi ya mshahara wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ni vyema nikamshukuru Mwenyezi Mungu wa rehema kwa kunipatia afya njema na busara ya kuweza kuchangia mada iliyopo hapa mezani. Pia, nikushukuru kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa homa ya matumbo ya kuendesha, imekuwa ni tabia ya kawaida kila baada ya miongo ya mvua hutokea maradhi ya milipuko ya matumbo. Ni vyema Serikali ingefikiria zaidi namna ya kuwalinda wananchi wetu ili kuzuia maafa haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya maambukizi ya UKIMWI, ni hali yenye kutisha, mazingira ya kupambana na UKIMWI hayajaridhisha kabisa, bado vijana wetu hawajakuwa na hadhari ya kutosha na maambukizi bado yanaendelea kutisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kuhusiana na maradhi yasiyo ya kuambukizwa. Kumekuwa na hadhari kubwa kuwaeleza wananchi kufanya mazoezi na timu mbalimbali zimeanzishwa ili kukidhi haya mahitaji lakini je, Serikali ina mkakati gani mahususi wa kulisimamia hili na kulipigia debe kwa wananchi wote hasa vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye *medical instruments* kama *ct-scan, ultra sounds, x-rays tube*. Hivi vyombo ni muhimu na ni bado havijaenea nchini, bado vijijini hizi zana hazijafika. Niombe sana Serikali kwa namna ya pekee ieneze hizi zana kwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kuchangia hoja hii. Pia napenda kuwapongeza kwa dhati Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa anazofanya kwa kweli, wanajituma kwa nguvu zao zote kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya matibabu ya afya kwa kutupatia dawa na kupatikana vifaatiba katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NHIF*; huduma ya matumizi ya kadi ya bima ya afya *NHIF* tunahitaji watu wote wapate huduma hii ili wapate matibabu kwa kutumia huduma hii kwa urahisi, lakini bado tuko nyuma, mpaka sasa wanaotumia huduma hii ni asilimia 34 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Watanzania wanataka elimu ya kutosha itolewe hasa vijijini, ili wapate uelewa juu ya matumizi ya bima ya afya na vievile waweze kutibiwa kwa daraja lake ili yule mwenye maisha duni aweze kutibiwa kwa uwezo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viongozi wanaotumia huduma hii mfano Wabunge, wanatibiwa yeye pamoja na mwenza wake na watoto wanne, lakini mzazi

wake hapati huduma hii. Swali langu ni hili je, hatuoni Serikali haijawatendea haki wazee kuwakosesha huduma hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kuipongeza Serikali kwa Taasisi ya Moyo kuweza kutupatia tiba na wataalam mbalimbali kuhusu tatizo hilo. Tunaomba tiba hii ipatikane katika hospitali nyingine za rufaa mbalimbali katika nchi yetu, ili kuipunguzia mzigo Hospitali ya Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madaktari na Wauguzi pamoja na wafanyakazi mbalimbali wa sekta ya afya. Hawa wote wanafanya kazi katika mazingira magumu kutokana na kazi zao. Kwanza tunaomba waangaliwe, maslahi yao yaboreshwe ili waweze kupata ari na upendo wa kazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madaktari, Wauguzi na Nesi wana changamoto mbalimbali zikiwemo posho ya nyumba, motisha ya saa za ziada. Hili tatizo kubwa linaweza kuathiri utendaji kazi wao, kwa hiyo, naiomba Serikali iliingalie tatizo hili kwani hawa ndio wanaotuokoa katika maisha yetu ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vifo vya wajawazito bado ni changamoto katika nchi yetu, baada ya kupungua bado vinaongezeka katika Taifa letu. Kwanza naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Afya, juzi nilishuhudia kwenye vyombo vya habari kuwa inatoa michango mbali ya fedha kutaka kuwasajili Wakunga wa Jadi ili kuweza kusaidia kupunguza vifo vya akinamama wajawazito na watoto. Ahsante sana Waziri Umyy, wanawake tunaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu, naunga mkono hoja.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wa afya kwa kazi nzuri zilizotukuka na kumuunga mkono wa dhati Rais Dkt. J.P. Magufuli na kuwezesha kuwa na matumaini ya kutimiza azma yake kwa akinamama na watoto hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana Mkoa wa Rukwa wamepatiwa pesa kwa ujenzi wa vituo vya afya na hospitali za wilaya zote nne na kuanza maandalizi ya awali ya ujenzi wa hospitali ya rufaa ya mkoa. Ombi letu ni Wizara ya Afya kutoa msukumo kwa TAMISEMI kuhakikisha wanaunga mkono jitihada na nguvu za wananchi katika kuyakamilisha maboma ya majengo ya zahanati yapatayo 50. Pia tunaomba vifaa tiba kwa wakati, ili zahanati takribani 15 zilizokamilika zipatiwe watumishi na zianze kazi kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kujengewa vituo vya afya vya kihistoria na bajeti ya 2019/2020 tumeongezewa vituo viwili ndani ya mkoa, ingawa bado mahitaji ni makubwa kwa Mkoa wa Rukwa kwani tupo pembezoni mwa nchi yetu (Congo DRC na Zambia). Tunaomba vifaa tiba na watumishi wa kukidhi mahitaji kwani majengo mazuri bila kuwa na hayo mahitaji hatutakuwa tumewafikishia wananchi huduma njema kwao.

Naomba Wizara kuona umuhimu wa Vituo vya Afya – Sopa, Kitete, Kala, Kabwe na kadhalika. Tuzingatie jiografia ya Rukwa ni mtihani kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi kwa hali halisi ya Waziri, bado Mkoa wa Rukwa tunaomba kuangaliwa kwa jicho la aina yake kwani, akinamama na vijana wameibuka katika kuinua uchumi wao kwa kujiunga kwenye vikundi vya ujasiriamali, tatizo lililopo ni elimu kwao, lakini Maafisa wa Maendeleo ya Jamii hawakidhi mahitaji. Si rahisi mmoja kushika vijiji viwili au mitaa sita au kata tatu, utendaji wao unakuwa hauna ufanisi na hata tija haipo. Tunaomba ajira itendeke kwa sasa, watumishi hawa ni muhimu sana vijijini, mitaani kwa afya, uchumi, maendeleo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maafisa hawa hawana usafiri. Tunaomba usafiri kwao na pikipiki kwa vijiji, mitaa na kata, magari kwa ngazi ya wilaya na mkoa kwani sasa inategemea huruma ya Mkurugenzi au RAS. Tunawarudisha nyuma kiufanisi kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba upande wa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii kuwa na ukaimu kwenye nafasi zao. Tunaomba eneo husika kuona kama vigezo vinakubalika waweze kupata nafasi hizo kikamilifu, ili wafanye kazi kwa tija na ufanisi uliotukuka kwa maslahi ya nchi yetu, hususan Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wakati wa sherehe za Siku ya Wanawake Duniani, Mkoa wa Rukwa, alitoa ahadi ya kutoa *ambulance* ya Manispaa na Hospitali ya Mkoa, hivyo tunasubiri bado hizo *ambulance* mbili. Tunaomba Waziri aone namna ya kutimiza ahadi hii, kwani akinamama wanayumba sana kwa huduma hii ya usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwa hatua iliyofikiwa hadi sasa. Tunaomba kasi kuongezwa ili tufanane na mikoa iliyokamilishiwa kwa asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, tunaomba utaratibu wa Bima ya *NHIF* ukamilishwe haraka kwa kutolewa kwa wananchi wote kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hii muhimu kwa mustakabali wa afya za wananchi wa Tarime. Kwanza niombe Wizara izingatie maoni yaliyotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, hasa maeneo ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kufanyiwa marekebisho ili kuweza kumlinda mtoto wa kike, maana ilivyo sasa inakinzana na sheria nyingine zinazomlinda mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu hospitali yangu ya Mji wa Tarime ambayo ina hadhi ya kuwa Hospitali ya Mkoa wa Tarime/Rorya au kuifanya angalau hospitali ya wilaya. Tunakuwa *treated* kama vile hospitali inahudumia wananchi wa Tarime Mjini tu ilhali tunahudumia na wananchi wote toka Tarime Vijijini, Serengeti, baadhi ya maeneo ya Rorya na wengine wanatoka nchi jirani ya Kenya, lakini fedha tunazopokea za *basket fund* ni ndogo sana pamoja na stahiki

nyingi za kuwezesha utolewaji wa huduma bora ya afya kama vile idadi ya Wauguzi/Wauguzi Wasaidizi inatolewa kwa idadi ya *population* ya Mji wa Tarime. Hii sio haki na inasababisha utolewaji wa huduma duni za afya na hatimaye kusababisha umauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna upungufu mkubwa wa Madaktari uliopelekea mosi na uchukuliwaji na ugawaji wa *basket fund* kwa kuzingatia idadi ndogo kuliko uhalisia; zoezi la vyeti feki; kustaafu na vifo. Tuna upungufu mkubwa sana. Wahudumu hawa, Madaktari wanafanya kazi kwa muda mrefu sana bila mapumziko na stahiki zao haziridhishi. Niiombe Serikali na juzi nilisema Bungeni kuwa tuna shida na Daktari wa Meno baada ya aliyekuwepo kufariki kwa ajali mwaka jana. Niombe sana suala hili lipewe kipaumbele maana sasa wananchi wanapata shida sana. Serikali ilichukulie kama jambo la dharura ili kuokoa afya ya kinywa na meno kwa wananchi wa Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Wizara hii iweze kujenga utamaduni wa kutembelea magereza ili kujua manyanyaso wanayoyapata wanawake hawa wawapo kwenye mikono ya Jeshi la Polisi (vituoni), wengi wanabakwa na kudhalilishwa kijinsia.

Pia waweze kuona ni jinsi gani wanawake maskini wanavyoonewa na kukosa misaada ya kisheria. Wengi wanakamatwa kwa makosa ya wanaume zao, wengine wana kesi za kudhaminika ila wapo, tena wengine wapo na watoto wadogo/wachanga, wengine ni mabinti wadogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Jeshi la Polisi kubaka/kuingilia kinyume wanawake tena mabinti ni kinyume kabisa na sheria na kanuni za kazi. Huu udhalilishaji ni lazima Wizara iufanyie kazi ili kulinda utu wa mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati sasa Serikali itenge fedha kwa ajili ya kitengo cha lishe. Serikali ya Awamu ya Tano haijawahi kutenga fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni mahitaji ya *ambulance* kwenye Kituo cha Afya cha Magena (Nkende) na kile cha Kenyamanyori. Upanuzi wa zahanati ile ya Nkongore Kenyamanyori na Ganasara (Nyandoto) kuwa Kituo cha Afya, ni muhimu sana na sisi tupate fedha za kukarabati na kupandisha hadhi ili ziweze kutoa huduma stahiki. Natambua huwa kuna fedha zinakuja tuweze kupatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha mwaka huu wa fedha, yaani 2019/2020 hakuna bajeti ya uzazi na mpango (*family planning*). Ningependa kujua ni kwa nini hamna au ni kufuatia kauli ya Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara lazima itoe elimu juu ya ugonjwa wa ini (*hepatitis*), magonjwa yasiyo ya kuambukizwa, kuwekeza kwenye kutoa elimu juu ya UKIMWI (*HIV*). Muhimu kuwekeza kwenye lishe, chanjo, vitamini kwa mama na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, afya ni nguvu kazi ya Taifa lolote. Kamwe Tanzania ya Viwanda haitawezekana kama wananchi wake hawana huduma bora za afya. Pamoja na unyeti na umuhimu wa afya bado Wizara hii imetengewa fedha kidogo sana. Pamoja na Bunge lako Tukufu kupitisha zaidi ya trilioni moja, lakini zilizoenda za maendeleo ni 16% tu. Hii haiendani kabisa na ubora wa afya kwani, miradi mingi imekwama, lakini pamoja na upungufu huo bado fedha zinapungua hadi bilioni 866.2. Hali hii haina ishara njema kwa afya zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na watumishi wachache na kufanya kazi kwenye mazingira magumu bado viongozi wa kisiasa na Kiserikali wasio na taaluma hii wamekuwa wakiwadhalilisha kwa ama kuwasimamisha kazi au kutaka kujieleza mbele ya wananchi. Hivyo, ni muhimu tabia hii mbaya ya kuwa-*demoralise* madaktari wetu wanaopatikana kwa gharama kubwa sana iachwe.



Mheshimiwa Naibu Spika, UKIMWI una uhusiano mkubwa sana na *TB*. Ni kama vile suala la *TB* halishughulikiwi sana. Hii ni hatari kubwa kwa kuwa, mgonjwa wa *TB* mmoja asiyetibiwa anaweza kuambukiza watu 10 – 20 kwa mwaka, lakini mbaya zaidi 40% ya wagonjwa wa UKIMWI pia, wana *TB*. Hivyo magonjwa haya yana mahusiano makubwa basi uzito unaopewa UKIMWI pia, uwekwe kwenye *TB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri nasaha ni muhimu sana hasa ikizingatiwa binadamu lazima akumbane na changamoto za maisha. Hivyo, ni muhimu kitengo hiki kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii kujipanga kimkakati kuona ni jinsi gani watakavyotoa huduma hii hata ikibidi kwa gharama kwa kuwa, kuna wanasihi binafsi (wachache) wanaotoa fedha. Pia, vijana (wanafunzi) wawe wanapewa mafunzo kwa vitendo ili wamalizapo waende kusaidia wananchi wenye sonona na misongo ya akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndoa za utotoni ni tatizo kubwa sana. Sheria hii ibadilishwe ili iendane na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, afya kwa wote haina mjadala ni muhimu sana, lakini Mtanzania awe na bima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuondolewa kwa tozo ya *VAT* katika *pads* bado ni kizungumkuti. Pamoja na Serikali kuondoa *VAT* bado fedha ni zilezile 2,000/= *per pct* na zaidi suala la je, kwa nini mpaka leo bado gharama ni ileile au zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Wazee toka 2001 hadi leo haina sheria. Ni lini Muswada wa Sheria utaletwa ili wazee hawa wapate ahueni?

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imesaini mkataba (*Abuja Declaration*) ambapo kila nchi husika zilikubali kutenga asilimia 15 ya bajeti kuu ya Serikali kugharamia sekta binafsi. Ni jambo la ajabu kwamba, sasa inaonekana Serikali haioni umuhimu huo kwa kuwa, hivi majuzi Waziri wa Fedha

alikiri haiwezekani kila mkataba tuutekeleze kama tulivyosaini kwa kuwa, sekta nyingine hazitapata kitu, nazo ni muhimu.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu ya Afya. Kama inavyojulikana ni ngumu sana nchi yoyote kupata maendeleo kama wananchi wake hawana afya bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watumishi wa Afya; pamoja na jitihada za kujenga mahospitali na vituo vya afya, lakini tumekuwa na upungufu mkubwa sana wa watumishi wa afya nchini. Mfano mpaka mwezi Machi, taarifa za Wizara zinaonesha zina upungufu wa watumishi kwa asilimia 48 na hii inaonesha kuwa kasi utoaji wa vibali vya kuajiri uko chini sana ukilinganisha na ongezeko la wagonjwa. Pia, ongezeko hili la ujenzi wa hospitali na vituo vya afya ni vema sana ungekwenda sambamba na ajira mpya za watumishi wa afya sambamba na kuwalipa watumishi wa afya waliopo wanaodai stahiki zao ili kuweza kuongeza tija ya utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la magari ya wagonjwa Jimboni Mikumi; Jimbo la Mikumi lina jiografia mbaya sana na katika kata 15 za Jimbo la Mikumi tuna vituo vya afya vinne tu navyo ni kuwa viwili, yaani Kituo cha Afya cha Kidodi na Kituo cha Afya cha Ulaya na vituo vipya vya afya vya Mikumi na Kituo cha Afya cha Malolo.

Kwa hali hiyo inasababisha wananchi wengi kufia njiani wakati wanasafirishwa umbali mrefu sana ambapo ni kutokana na ukosefu wa magari ya wagonjwa. Jimbo zima halina gari hata moja la wagonjwa kwenye zahanati zote pamoja na vituo vya afya vyote. Tunaiomba sana Serikali itusaidie magari ya wagonjwa mawili au zaidi ili tuweze kuwaokoa wananchi hawa wa Jimbo la Mikumi, hasa mama na watoto. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, Dada Umyy Mwalimu, atusaidie na kuokoa maisha ya wanawake na watoto wa Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NHIF*; uandikishaji wa Bima ya Afya ya *NHIF* umekuwa mdogo sana. Mfano, mwaka 2016/2017, walisajili 27% tu; mwaka 2017/2018, walisajili 32% tu; mwaka 2018/2019, walisajili 33%; na kusuasua huku kunatokana na ufinyu wa bajeti. Tunaomba sana Serikali izingatie sana bajeti ya afya kwa ujumla. Pia, Serikali iharakishe kuleta Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote yaani *Universal Health Coverage* ili tuweze kuupitisha na kuleta tija zaidi ya kuwasaidia na kuwaokoa Watanzania wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii; ni vema sasa tukajikita zaidi kwenye kinga kuliko tiba na watu wanaoweza kutusaidia zaidi kwenye jambo hili la kinga ni Maafisa Maendeleo ya Jamii ili waweze kusaidia jamii zetu huko chini ili wapate elimu zaidi ya afya kwani ni kweli tupu kwamba, kinga ni bora kuliko tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Ni ushauri wangu Serikali ione namna ya kuchukua ushauri wa hotuba hiyo ili kuboresha maendeleo ya Wizara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, afya ni kitu muhimu sana kwa binadamu yeyote. Bila kuwa na afya bora, hakuna kazi au maendeleo hapa duniani au Tanzania. Hivyo basi, pamoja na mambo mengi yanayofanyika, bila afya bora ni mzigu mkubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inashughulika na wazee, watoto na wanawake ambaPo wanawake hao ni kiwanda namba moja cha kuleta watoto duniani. Nianze na kuzungumzia afya ya mama na mtoto ndani ya Jimbo la Mlimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo na Kituo cha Afya Kata ya Mlimba ambacho kinahudumia takribani wakazi wa kata 10 na watu wasiopungua laki moja

na zaidi, inasababisha kituo hicho kuzidiwa na wagonjwa kwa upungufu wa madaktari ambapo wapo wanne tu na kufanya tatizo kubwa katika kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia dawa zinazopelekwa mara kadhaa hazikidhi haja kutokana na hadhi ya kituo kuhudumia watu wa kata 10. Hivyo tunaomba tufikiriwe kuongeza vituo vya afya ili kupunguza mzigo mkubwa katika Kituo cha Afya Mlimba. Naomba angalau tupate vituo vya afya vitatu ambapo kila kata tatu zitahudumiwa na kituo kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Jimbo la Mlimba liko kilometa 220 hadi kufika Hospitali ya Rufaa St. Francis na miundombinu ya barabara ni mbaya sana kwa barabara kutopitika kwa mwaka mzima, hivyo kuhatarisha maisha ya mama wajawazito na wagonjwa wanaopata rufaa, naomba tupate bajeti ya kutosha ili tujenge Hospitali ya Halmashauri ambapo kwa bajeti hii. Tumetengewa shilingi milioni 500 tu, ambayo itachukua muda mrefu ujenzi kwisha. Naomba tuongezewe hela ili tujenge haraka na kuokoa jamii ya Mlimba. Pia tunaomba gari la wagonjwa kwani gari lililopo ni chakavu na linaharibika mara kwa mara. Pia ahsante kwa kupeleka hela ya kuboresha Kituo cha Afya cha Mchombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee waishio vijijini wanashindwa kupata huduma kutokana na ukosefu wa vituo vya afya na kushindwa kupata huduma kwa sababu ya umbali wa kufikia kituo cha afya Mlimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alipotembelea Wilaya ya Kilombero, pamoja na mambo mengine, aliamuru watumishi/wauguzi na madaktari wote waliokuwa wanalipwa na Serikali katika Hospitali ya Rufaa ya St. Francis waondolewe na wapelekwe kwenye vituo au zahanati za Serikali. Uamuzi huo ingawa umefanywa kwa nia njema, lakini umesababisha upungufu mkubwa wa madaktari na wauguzi kwenye Hospitali hiyo ya Rufaa ambapo ni tegemeo kubwa kwa wakazi wa Wilaya ya Kilombero, Malinyi na Ulanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nashauri uangaliwe upya uamuzi huo kwani Mheshimiwa Waziri alipoagiza waangalie upya gharama ya matibabu, waliitekeleza kwa kuwashirikisha wadau na kupunguza gharama za matibabu. Hivyo, tatizo lililopo ni upungufu mkubwa wa madaktari na wauguzi. Ni matumaini yangu kuwa atalichukulia hilo kwa umuhimu.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Bima ya Afya iangalie utaratibu wa kupatia Bima Watanzania wote na bei ipungue.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Hospitali ya Mrara inahitaji ujenzi wa wodi ya wazazi na watoto. Tunashukuru kwa mkopo wa Bima ya Afya milioni 108 kwa hospitali hiyo. Tunaomba mtuongezee kwani bajeti yake ni zaidi ya shilingi milioni 800.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Afya na Zahanati katika Kata zote za Babati Mjini vimejengwa na nguvu za wananchi, lakini hakuna fedha zozote za Serikali zimepelekwa kukamilisha maboma hayo. Tunaomba fedha za ukamilishaji maboma hayo ambayo ni Zahanati ya Singe, Sigimo, Mutuka, Himiti na Chemchem.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunaomba *ambulance* katika Hospitali ya Mrara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawawatakia kila la heri katika majukumu yenu.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, *health tourism* ni eneo ambalo bado halijafanyiwa kazi vyema wala halijastawishwa sana. Naamini kama tukiweka hili kimkakati, mfano Mbeya kwa Zambia na Malawi; au Kagera kwa Burundi na DR Congo itakuwa vyema. Pia lazima kama nchi tuwe na *specialized areas* ambazo zitavuta majirani kufuata matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumearifiwa kuwa kuna fedha za mkopo wa riba ndugu juu ya *early childhood development* kiasi cha shilingi milioni 200 kwa miaka mitano na kuweza kusaidia eneo hili. Tunaambiwa the *money has been waiting for us - we drag our feet and the 0-5 child is not developed.*

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Wizara imetenga *partner fund* ili Serikali iweze ku- *access fund* kwenye taasisi, mashirika ya ufadhili ambayo yana masharti hayo? Je, ni kiasi gani hicho ambacho kimetengwa?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha kwenye kipindi hiki cha Ramadhani ya mwaka huu, kwani wapo tuliofunga nao mwaka jana, 2018 leo wako mbele ya haki na wengine wameshindwa kushiriki Ramadhani hii kwa hali na maradhi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo naomba nianze mchango wangu kwanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Manaibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote kwenye wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhudumia jamii yetu kwenye sekta hii muhimu ya kulinda afya zetu. Namwomba Mungu awape umri mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa bajeti ya mwaka 2018 kwa kunipa watumishi 80 wa Sekta ya Afya, lakini kutokana na uhaba mkubwa tulionao watumishi wale wamekuwa kama tone la damu baharini. Bado Hospitali ya Wilaya ya Liwale yenye wodi nne zinahudumiwa na mhudumu mmoja tu kwa *shift* ya usiku kutokana na uhaba wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitoe shukrani kwenye bajeti hii kwani wilaya yetu imetengewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, maana ile iliyopo ilikuwa ni kituo cha afya, hivyo kushindwa kukidhi hadhi ya

kuitwa Hospitali ya Wilaya. Ombi langu ni fedha kuja kwa wakati ili ujenzi huu uanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na vituo viwili vya afya vya Mpengerewa, Kibutuka, bado Halmashauri ya Liwale inakabiliwa na uhaba mkubwa sana wa gari la wagonjwa (*ambulance*). Jiografia ya Liwale yenye vijiji 76 ni ngumu sana. Hivyo, namna ya kuwafikisha wamama hasa wajawazito ni ngumu sana, ukizingatia kuwa zahanati zetu hazina wataalamu na vifaa vya kutosha. Kwa hiyo, uhitaji wa gari la wagonjwa ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza mlundikano wa wagonjwa kwenye hospitali na zahanati zetu, wakati sasa umefika wa kuimarisha kada ya Mabwana na Mabibi Afya kwenye Kata na Vijiji vyetu. Watumishi hawa ni muhimu sana kwenye jamii zetu. Waswahili husema, “kinga ni bora kuliko tiba.” Elimu ya afya ikiwafikia wanajamii juu ya kutunza afya zetu na mazingira yetu kwa ujumla tutaepuka magonjwa ya mlipuko. Kada hii ya Mabwana/Mabibi Afya ni kama imesahuliwa kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira kwa watoto ni jambo linalotishia maisha ya watoto wetu kwani kila kukicha bado ongezeo la ajira kwa watoto mitaani linaongezeka siku hadi siku hasa kwa mijini. Wako watoto wanaosukuma baiskeli kuwatembeza watu wenye ulemavu wa viungo na wasioona kwenye shughuli zao za kuombaomba. Vilevile wako watoto wanaotumwa na wazazi wao kwenda mitaani kupita kuombaomba. Hivyo, naiomba Wizara kuja na mkakati maalum wa kukomesha ajira hizi za watoto na kuwaondoa watoto wanaoombaomba mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania kukosa kuwaingiza kwenye mpango wa Bima za Afya (*NHIF*) ni kutokuwatendea haki, kwani familia za Maaskari wetu zimekuwa zikihangaika sana hasa zile familia zinazoishi uraiani. Pamoja na kazi ngumu wanazofanya za kulinda nchi

yetu, lakini bado hawana uhakika wa afya zao na familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Wazee nchini ni changamoto kubwa hapa nchini kwani hadi leo Serikali haitaki kuleta Sheria ya Wazee ili kuweza kutambua hao wazee. Pamoja na kuwa na matangazo sehemu mbalimbali kama vile "Pisha Mzee", "Wazee Kwanza", matangazo ambayo yanashindwa kuwatambua wazee hao, kwani hakuna sheria inayowatambua; kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi cha kuleta Sheria ya Wazee hapa Bungeni ili wazee hawa waweze kutambuliwa? Tukumbuke kuwa sisi sote ni wazee watarajiwa. Hivyo, hiki tunachokifanya ni kujikaanga kwa mafuta yetu.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia njia ya maandishi nichangie bajeti ya Wizara ya Afya. Awali ya yote nichukue fursa hi kuunga mkono hoja bajeti hii na niwapongeze viongozi na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuishauri Wizara iweze kupitia upya upangaji wa watendaji maalum katika wizara hii ili angalau kila mkoa upate hao wataalamu wa msingi. Mfano, mwezi wa tatu Mkoa wa Kagera kwa hospitali zote Umma na binafsi hakukuwepo Mganga kwa ajili ya magonjwa ya akina mama (*gynecologist*). Hoja hapa ni kuhakikisha kila mkoa unapata wataalamu hawa na hata wakati wa kutoa ajira muhimu, kutoa nafasi kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia bajeti hii, nishauri juu ya upangaji na ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali. Ushauri wangu ni kuwa suala hili lisimamiwe na Wizara ya Afya ambayo katika busara ya kawaida watatumia weledi kupanga maeneo ya taasisi hizo. Nikirejea ujenzi, uboreshaji wa zahanati na vituo vya afya katika Jimbo langu, inasikitisha kuona kuwa maeneo ambayo yalipashwa kupewa nguvu baada ya wananchi kuonyesha juhudi kwa kujenga maboma hayajafikiwa. Hii inaonyesha ukosefu wa



utaalamu katika kubaini wapi paendelezwe, kwani maeneo mengine yanaachwa bila huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ipitie ujenzi wa zahanati 12 zilizojengwa na wananchi kwa kipindi cha miaka mitatu ili tupate somo juu ya haja ya kuendeleza zahanati na vituo vya afya kwa ulinganifu na kwa kuzingatia zaidi mahitaji, lakini zaidi Serikali itusaidie kwa kuendeleza angalau Zahanati za Rutoro, Bumbire na Croglo kati ya zahanati hizo 12 kwa kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine la kuangalia ni upangaji wa wataalamu wa sekta ya afya. Ili kuepuka tatizo la sasa ambapo sasa kila wizara inataka watendaji wanaohusika na sekta zao walioko katika Halmashauri za Wilaya wawajibike Wizarani. Wizara ya Afya na TAMISEMI wapitie upya usimamiaji wa watendaji hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hii ni Serikali moja, unaweza kuwepo utaratibu ambapo wataalamu wa Wizara ya Afya wanaweza kupata miongozo tokea Wizara ya Afya ikiwa ni pamoja na kupata stahili zao wakiwa Halmashauri za Wilaya. Uwepo wa zahanati wa vituo vya afya ambavyo havina wataalamu ni kutokana na upungufu tu wa msimamizi (*DED*) kutokuwa na uelewa wa mguso wa sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umakini wa Serikali katika kutoa vibali vya kuajiri, naomba na kushauri vibali vya kuajiri watendaji wa sekta hii ni muhimu vitolewe. Hii italeti umaana wa kujenga miundombinu ya zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nichukue fursa hii kupongeza msimamo wa Serikali katika kuwasimamia watendaji wa Sekta ya Afya. Siyo busara kwa kila atakayesimama amwelekeze na kumkemea *Nurse*, *Daktari* au *Mtendaji* wa Afya. Kazi nyingine unaweza kuzifanya kwa sababu unajua kongea. Sekta ya Afya watendaji wake wanatumia muda mwingi shuleni, wanahitaji utulivu na wanashughulika na afya na uhai wa binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Tandahimba ina hospitali moja ya Wilaya na vitu viwili vya afya ambavyo ni vya zamani. Hata hivyo, tunaishukuru Serikali kwa kutupatia fedha shilingi milioni 400 za Tanzania kwa ajili ya ukarabati wa Kituo cha Afya Mahuta. Fedha hizi zimetumika vizuri. Kwa hiyo, ombi langu ni kupata fedha kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa kituo hiki ambacho kinahudumia zaidi ya kata kumi zilizopo jirani. Hata hivyo, Wilaya ya Tandahimba jiografia yake ni ngumu kidogo, kwa hiyo, naomba Wizara itusaidie fedha kwa ajili ya kujenga na kuendeleza vituo vya afya vipya vilivyojengwa na wananchi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Mnyawa wananchi kwa kupenda maendeleo wamejenga vituo vya afya ambavyo vinahitaji msaada wa Serikali ili tuweze kumaliza. Kata ya Mndumbwe nayo wananchi wamejitolea kujenga kituo cha afya. Tunaomba msaada kwa Serikali iweze kutusaidia tumalize ujenzi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wizara itujengee Kituo cha Afya katika Tarafa ya Litehu ambayo inahudumia wakazi zaidi ya 30,000. Tunaomba tupate kituo cha afya katika Kata ya Kitama I. Kituo ambacho kitasaidia kuboresha huduma za afya katika maeneo jirani kama Kata ya Miute, Michenjele, Mihambwe na Mkoreha. Wananchi wako tayari kujitolea, nami kama mwakilishi wa Jimbo la Tandahimba na mzaliwa wa Kitama, naahidi kuchangia mifuko 600 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho. Kwa unyenyekevu mkubwa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kuwasilisha.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika aya ya 185 ukurasa wa 136 Mheshimiwa Waziri ameeleza kuwa ili kuhakikisha haki za wazee zinalindwa, Wizara imeendelea kuratibu uanzishwaji wa Mabaraza ya

Wazee katika ngazi mbalimbali za Halmashauri ambapo hadi kufikia Machi, 2019, jumla ya Mabaraza ya Wazee 9,083 yameanzishwa katika Halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Mabaraza hayo yameanzishwa huku kukiwa hakuna Sheria ya Wazee nchini wala sheria ya kuwezesha kuanzishwa kwa Mabaraza hayo. Hivyo katika majumuisho Mheshimiwa Waziri aeleze ni lini Sheria ya Wazee italetwa Bungeni ambayo pamoja na mambo mengine itaeleza kuweka muundo na majukumu ya Mabaraza ya Wazee nchini. Aidha, sheria hiyo itawezesha kuundwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Wazee Nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, ipo hoja ya kutungwa kwa Sera ya Maendeleo ya Wanawake Nchini. Sera hiyo ifuatiwe na kutungwa Sheria ya Baraza la Wanawake la Taifa na kusimamiwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake nchini na wanawake wenyewe kupitia Baraza lao. Naomba kupata maelezo ya Serikali kuhusu hatua iliyofikia katika kuunda Mabaraza ya Watoto katika Jimbo la Kibamba. Haya yatawezesha watoto kujijenga ikiwemo Stadi za Uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imewezesha kuandaliwa kwa kanuni za mashirika yasiyo ya kiserikali za mwaka 2018 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 609 la tarehe 19 Oktoba, 2018. Baadhi ya vifungu na vipengele vya kanuni hizo umekamilika na wadau yakiwemo mashirika yasiyo ya kiserikali. Hivyo, Wizara ikae tena na mashirika yasiyo ya kiserikali kupitia vifungu na vipengele vilivyolalamikiwa na kufanya marekebisho. Aidha, Wizara iharakishe kuweka kanzidata ya mashirika yasiyo ya kiserikali kwa kuwa suala hili limechukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Maendeleo ya Jamii na Vituo vya Ustawi wa Jamii unaweza kuwa na malengo makubwa kwenye maendeleo na ustawi wa jamii. Vituo hivyo vilianzishwa wakati ambapo mazingira ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ni tofauti na sasa. Hivyo Wizara ifanye

tathmini ya Mitaa na mazingira ya vituo hivyo na kuja na mapendekezo ya maboresho kwa kuzingatia hali halisi iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitaala ya vituo hivyo ilenge kujibu changamoto zinazokabili jamii yetu kwa sasa na baadaye. Kadhalika Wizara itoe maelezo ya athari za fedha za maendeleo kutolewa kidogo katika Fungu la 53, Idara Kuu ya Maendeleo ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2019 kiasi cha shilingi bilioni 1.13 tu sawa na asilimia 23.0 tu ya fedha iliyotengwa kilikuwa kimepokelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ina wajibu wa kuzisimamia kwa karibu mashirika na taasisi yaliyoko chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) alikagua Bohari Kuu ya Dawa *MSD* na kubaini kuwa vifaa tiba ya shilingi bilioni 3.55 vilivyonunuliwa kwa mfumo wa manunuzi maalum vilivyorudishwa kutokana na kuzidi kiasi walichoagiza wateja. kutokuwa na sifa zilizotakiwa na wateja au kuzidi kiasi walichoagiza wateja. Baadhi ya vifaa tiba vilivyorudishwa vilikuwa vikikaribia kikomo cha muda. Hivyo, mfumo unapaswa kuboreshwa kuhakikisha kuwa hali kama hii hajirudii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia *CAG* alibaini katika mwaka 2017/2018 malipo ya shilingi bilioni 480 yalifanywa na Mfuko wa Bima ya Afya (*NHIF*) kwa vituo vya tiba ya afya kwa wateja ambao hawakuchangia mfuko. Hali hii kama ni kweli ni hatari kwa mustakabali wa mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, yapo madai kwamba malipo ya shilingi bilioni 13.99 yalifanyika kwa wanaodaiwa kuwa watoto wategemezi, lakini ukweli ni kuwa wamevuka miaka 18, hali ambayo inahitaji *NHIF* kuharakisha kuanzisha kanzidata ya umri wa wategemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara itumie majumuisho kueleza sababu ya madeni yasiyolipika (*bad*

*debts*) katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kutoka shilingi milioni 941.32 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 mpaka shilingi bilioni 1.44 kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2013 na 2016 palifanyika uthamini (*actual valuation*) mara mbili kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*). Uthamini wa mwaka 2013 ulionyesha kwamba uendelevu bora na mfuko kwa maana ya mfuko kuanza kupata hasara ulikuwa mwaka 2040. Hata hivyo, uthamini wa mwaka 2016 ambao ripoti yake ilitolewa mwaka 2018 unaonyesha kwamba kiwango kimeshuka mpaka mwaka 2025. Hii ni kutokana na uwiano wa malipo ya huduma za afya kukua kila mwaka ukilinganisha na malipo ya Bima za Afya. Wizara inapaswa ieleze nini chanzo cha hali hiyo na ni ufumbuzi upi wa kukabiliana na hali hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizo zihusishe pia kuboresha mfumo wa Bima ya Afya kwa wastaafu kwa kuwekeza kiwango cha michango ya wanachama ili makato hayo yaje kusaidia malipo ya wanachama katika kipindi cha kustaafu kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuanzishwa kwa Manispaa mpya katika Jiji la Dar es Salaam, Hospitali za Mikoa za Amana, Mwananyamala na Temeke zinapaswa kuhudumia Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke mtawalia. Hivyo, kuna haja ya kuanzishwa kwa hospitali za mikoa kwa Manispaa mpya za Ubungo na Kibamba. Kwa upande wa Wilaya ya Ubungo Makao Makuu mapya ya Wilaya yanajengwa katika Kanda ya Kwembe eneo la Luguruni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia patakuwa na ujenzi wa mji mpya wa pembeni (*satellite town*) eneo la Luguruni. Hivyo, mji unapanuka kuelekea eneo la Kibamba. Kwa mantiki hiyo, napendekeza badala ya kupandisha hadhi Hospitali ya Wilaya ya Sinza, Palestina, mchakato uanze wa kujenga Hospitali ya Mkoa Kibamba na Kwembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa upande wa Sekta ya Afya, ina jukumu la kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa kutekeleza afua mbalimbali. Kwa upande wa Hospitali ya Mloganzila, nimetembelea hospitali hiyo hivi karibuni na kubaini kwamba vipo vipimo ambavyo wagonjwa wanalazimika kwenda kuvipata kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majumuisho, Mheshimiwa Waziri wa Afya alieleze Bunge, ni vipimo na huduma zipi ambazo wagonjwa wanalazimika kutoka Mloganzila au vipimo vyao kuchukuliwa kupelekwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na ni mpango gani umewekwa wa kuhakikisha vipimo na huduma hizo zinapatikana katika Hospitali ya Mloganzila?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo niliyopita ni kwamba hata huduma ya *CT-Scan* wagonjwa kwa sasa wanalazimika kwenda kupata kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, utaratibu wa rufaa kutoka Hospitali za Mikoa ya Dar es Salaam zinapaswa kuboreshwa. Kwa sasa hauangalii umbali toka wagonjwa wanapoishi au wanaowahudumia wanapotoka katika kupanga kama mgonjwa husika apelekwe Muhimbili au Mloganzila. Hii inasababisha mathalan mgonjwa wa llala kupelekwa Mloganzila wakati ambapo ingekuwa ni rahisi zaidi kwa mgonjwa kama huyo kupelekwa Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majumuisho, Wizara ieleze ni utaratibu gani umewekwa wa rufaa kuhakikisha kwamba wagonjwa na wanaowahudumia hawaendi umbali mrefu? Aidha, utaratibu wa rufaa uzingatie uwiano ili kuwe na urari wa idadi ya wagonjwa kati ya Muhimbili na Mloganzila kwa kuzingatia miundombinu, watumishi na huduma zilizopo katika hospitali tajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alitoa maelekezo mbalimbali tarehe 3 Oktoba kuhusu uendeshaji wa Hospitali ya Mloganzila. Kati ya maelekezo aliyoyotoa ni pamoja na kuagiza wagonjwa kutoka Muhimbili kutohamishiwa katika Hospitali ya Mloganzila. Wakati Mheshimiwa Rais anatoa maagizo hayo, natambua kwamba wapo wagonjwa ambao tayari walikuwepo kwenye wodi za Mloganzila na pia Hospitali haikuwa na watumishi na huduma kwa kiwango kilichopo sasa. Matokeo ya maagizo hayo ni madai ya wagonjwa waliohamishiwa wengine kufariki kutokana na udhaifu wa huduma. Aidha, wapo wagonjwa ambao waliohamishwa wakiwa katika hali mbaya na kupoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majumuisho, Mheshimiwa Waziri aeleze ni wagonjwa wangapi walifariki katika kipindi hicho cha mpito na ni hatua gani zimeweza kuchukuliwa kupunguza idadi ya vifo vilivyotokea?

Mheshimiwa Naibu Spika, panakuwepo pia mgogoro wa mipaka baina ya Mkoa wa Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani kuhusu wapi hasa ipo Hospitali ya Mloganzila? Naomba katika majumuisho au katika mjadala, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na suala hili, atangaze kuwa Hospitali ya Mloganzila ipo katika Jili la Dar es Salaam Manispaa ya Ubungo.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kupitia taasisi mbalimbali zinazotoa matibabu ya kibingwa. Pia nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara ya Afya kwa ushirikiano wao kwa Waheshimiwa Wabunge katika kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu afya ya uzazi, mama na mtoto; Serikali imejitahidi sana kujenga zahanati na vituo vya afya na hivyo kupunguza mwendo mrefu wa wananchi pamoja na kinamama wajawazito ili kufikia huduma za afya, lakini bado vifo vya mama na mtoto idadi ipo juu hususan akina mama wajawazito ambapo takwimu zinaonesha kuwa

akina mama 24 wanafariki kila siku wanapokuwa wanajifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifo vingi hutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kutokwa na damu nyingi wakati wa kujifungua, kutokufanya maamuzi ya njia za kujifungua mapema kama vile upasuaji, ukosefu wa dawa aina ya *misoprostol and oxytocin* hususan vijijini na pia ukosefu wa vifaa tiba na wataalam wa kutosha katika vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho ni kwamba Serikali iweke mkakati wa kuajiri *Community Health Workers* na wasambazwe maeneo yote hususan katika zahanati na vituo vya afya vya vijijini ili waweze kutoa huduma za afya na elimu kwa akina mama wajawazito. Ni vyema Serikali itenge fedha kwa ajili ya kukabiliana na vifo vya mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba Serikali iharakishe mchakato wa kuleta sheria ya *Universal Health Coverage* ili kuwezesha wananchi wote wapate huduma bora za afya kwa usawa. Pia Serikali ijitahidi kutafuta wafadhili ili kusambaza vifaa kwa ajili ya kuanzia kusajili wananchi na huduma ya *NHIF* iliyoboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia mambo machache katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Kwanza nianze na suala la uzazi wa mpango. Kuna msemu unasema *if you fail to plan you have planned to fail*. Ongezeko la watu katika nchi yetu limekuwa likiongezeka kwa asilimia 27 katika nchi yetu. Tanzania inakadiriwa kuwa na watu milioni 150 ifikapo mwaka 2050.

Je, kama nchi tumejiandaa kuhudumia ongezeko hilo la watu ukizingatia ongezeko hilo la watu na *limited resources* tulizonazo?



Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu dhana ya Serikali ya kuongeza matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango kutoka 32% - 45% ifikapo mwaka 2020, pia kupunguza vifo vya akina mama wakati wa kujifungua kutoka vifo 556 - 292 kwa vizazi hadi vifo 100,000, ifikapo mwaka 2020; kupunguza mimba za utotoni toka 27% - 22% ifikapo 2020. Naomba majibu ya Serikali, sasa hivi tumefikia wapi katika malengo tajwa hapo juu ikiwa tumbakiza mwaka mmoja tu kufika mwaka 2020?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzungumzia suala la *Community Health Workers (CHWs)* au watoa huduma za afya ngazi ya jamii wamekuwa na mchango mkubwa sana katika kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano. *CHWs* wamekuwa wakitoa elimu kuhusu lishe ya watoto, akina mama wajawazito na kuhamasisha akina mama wajawazito kwenda kujifungulia katika vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano hai ni Kijiji cha Uturo Mbarali hakijaripoti kifo cha akina mama kwa zaidi ya miaka mitano kwa sababu wamekuwa wakiwatumia *CHWs* katika jamii. Nafahamu mpango mkakati wa IV wa Wizara ya Afya umetambua kada hii na umeonesha kwamba mpaka mwaka 2020 itakuwa imeajiri *CHWs* 5000, lakini mpaka sasa Serikali haijaajiri hata *CHW* mmoja licha ya *service scheme* kukamilika mwaka 2018, Desemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Global Funds* walitoa pesa kwa ajili ya motisha kwa *CHWs* na mradi huu unakamilika mwaka 2020, lakini Serikali imegoma kuwatumia *CHWs* kwa pesa za *Global Funds*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri akija kuhitimisha anijibu maswali yafuatayo:-

(a) Ni lini Serikali itaajiri *CHWs* kama ilivyoahidi kwenye mkakati wa IV wa Wizara ya Afya?

(b) Pesa zilizotolewa na *Global Funds* ziko wapi?

(c) Kwa nini Halmashauri zinazotaka kuajiri *CHWs* kwa makato yao ya ndani zinakatazwa kuajiri?

(d) Ni nini mkakati wa Serikali kupunguza vifo vya akina mama wajawazito hasa wanaojifungulia majumbani ikiwa Serikali haitaki kufanya kazi na kuwatambua *CHWs*?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na *team* yake kwa ujumla kwa kazi kubwa wanayoifanya. Mwenyezi Mungu awabariki sana *ADDS - Head Radiology*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lushoto ni Wilaya isiyopungua takribani watu 800,000 na wote hawa wanategemea Hospitali ya Wilaya. Cha kusikitisha, hospitali hii haina huduma muhimu kama *X-Ray mashine* na hii imesababisha wananchi wengi kukosa huduma hiyo na ukizingatia wananchi wengi hawana uwezo wa kwenda mbali kupata matibabu. Kwa hiyo, naomba Serikali yangu Tukufu ipeleke *X-Ray mashine* ili wananchi wa Lushoto waweze kupata huduma hiyo kuliko iliyo sasa, kwani wananyanyasika mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu maendeleo ya jamii. Suala la huduma kwa wazee imekuwa ni mtihani sana, kwani wazee hasa wa Lushoto wanapata adha kubwa kwa kukosa vitambulisho, hasa wale ambao wapo vijijini ambako hakuna hata zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hayo, kuna wananchi wengi wanaoishi vijijini, hata wale ambao wanauhitaji maalum pamoja na walemavu hawapati mahitaji yao kabisa. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu ipeleke dawa na vifaa tiba vyote vinavyohusika kwa watu hawa, ukizingatia vijijini hakuna zahanati wala kituo cha afya. Kwa mtaji huo, sasa Serikali itumie magari ya afya ili kufikisha huduma hii kwa walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lushoto ni Wilaya yenye milima, kwa hiyo, hata wananchi wakitaka kufuata huduma za afya, ni lazima wafunge safari ya siku mbili au tatu hasa ikitokea mgonjwa amezidiwa na anahitaji usafiri wa gari. Hii imepelekea wagonjwa wengi kupoteza maisha hasa kwa akina mama wajawazito. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu Tukufu tuangalie watu wa Jimbo la Lushoto hasa kwa Kituo cha Afya Mlola tuweze kupata gari la wagonjwa, kwani kwa sasa hali ni mbaya, wagonjwa wanapoteza maisha kila siku kwa ajili ya kukosa gari la wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naishukuru Serikali yangu Tukufu kwa kutupatia shilingi milioni 700 kwa ajili ya kujenga majengo matano na vifaa tiba. Kwa sasa majengo yemekamilika, kwa hiyo, tunahitaji sasa vifaa tiba ili kituo chetu kianze kufanya kazi; na kwa kuwa mmeshatutengea fedha, shilingi milioni 300, naomba Serikali yangu ipeleke vifaa hivyo ili kuwahisha huduma kwa wananchi na kupunguza msongamano katika Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna upungufu mkubwa wa Watumishi wa Afya katika Hospitali ya Wilaya ya Lushoto pamoja na kwenye Vituo vya Afya na Zahanati zetu. Mfano, sasa hivi Jimbo la Lushoto nina zahanati zaidi ya sita, zote zimekamilika, zinahitaji vifaa tiba pamoja na watumishi. Hivyo basi, naiomba Serikali yangu ipeleke vifaa tiba pamoja na watumishi katika zahanati zilizopo katika Jimbo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lushoto kulikuwa na hospitali kwa watu wanaopatwa na vichaa ambayo ilikuwa inamilikiwa na Kanisa, lakini huduma ile kwa sasa haipo. Kwa hiyo basi, naiomba Serikali yangu ione ni jinsi gani ya kufufua huduma ile muhimu, maana sasa hivi watu wenye ugonjwa huo wana pata taabu kusafiri umbali mrefu; na kama inavyofahamika watu wenye kupatwa na ugonjwa wa kichaa kumsafirisha inakuwa ni shida sana. Nisisitize tana Serikali yangu irudishe ile huduma ya kituo cha watu wenye ugonjwa wa kichaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuongeza watendaji katika Sekta ya Afya, kwani Madaktari ni wachache, hivyo wanazidiwa na kazi, wanachoka na hivyo kufanya kazi chini ya kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara hii kuhakikisha inatoa elimu juu ya afya za Watanzania badala ya kusubiri waugue ndipo wawaelimishe. Pia Wizara ya Afya itoe kinga nyingi ili kupunguza gharama za matibabu. Naishauri Serikali kutoa ufadhili kwenye magonjwa yasiyoambukiza, kwa mfano, kisukari kinawapata watu ambao uwezo wao wa kutafuta fedha za kujitibia hawana, hivyo, wazee hawa wanakufa kabla ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kuishauri serikali kuwa wagonjwa wa UKIMWI hawafi kwa kutotumia ARV bali wanakufa kwa magonjwa kama Kifua Kikuu, kuharisha na *typhoid*. Hivyo tunashauri kwenye ARV ziwepo *ceprine* ili pale mgonjwa anapopata magonjwa nyemelezi waweze kupewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nyongeza ya Madaktari wa upasuaji katika Hospitali ya Tumbi kwani hospitali hii inapokea wagonjwa wa ajali za barabara ya Morogoro. Wawili waliopo hawatoshi, tuongezewe, kwani hospitali hii imepandishwa hadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bima ya Afya imeonesha kasoro nyingi ikiwepo usumbufu wa kutopata huduma stahiki, mfano dawa mara nyingine uambiwe ukanunue au mara nyingine uambiwe ni kwa magonjwa baadhi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wahudumu wa afya msingi waajiriwe ili kusaidia huduma za vijijini. Wahudumu hawa walikuwa msaada sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, matibabu kwa wazee ni shida. Bima walizoahidiwa hawajapewa na waliopewa hawapati huduma hizo hospitalini.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nianze kwa kuungana na Taifa zima kuomboleza kifo cha Mheshimiwa Dkt. Reginald Mengi kilichotikisa Taifa zima. Dkt. Mengi amefanya mengi katika Taifa hili, hivyo tumuenzi kwa kuendeleza mema na wema wake. Aidha, kifo chake kimetokea kikifuatana na cha kijana mahiri Ruge Mutahaba na Ephraim Kibonde. Ni pigo kubwa pia jana tu tumempoteza Mtanzania mwingine Prof. Robert Mabele kilichotokea Hospitali ya Mloganzila. Profesa Mabele amewafundisha wengi na hata Waziri wetu wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mpango ni mwanafunzi wake. Tuwaombe wote pumziko la milele.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijikite katika hoja ya leo ya afya. Nami naungana na wengi kupongeza kazi nzuri anayofanya Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu na msaidizi wake Mheshimiwa Dkt. Ndugulile. Wote wametembelea Wilaya ya Muleba na kuona maendeleo na changamoto ambazo naomba niziorodheshe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anajua tuna Hospitali Teule ya Wilaya ya Rubya, aliitembelea. Tatizo ni kwamba utaratibu wa *PPP* katika kutoa huduma unaweza kuleta mkanganyiko ikiwa utaratibu wa kulinda uwezo uliojengwa hautawekwa bayana. Hospitali Teule ya Rubya imepoteza wafanyakazi muhimu na vifaa, wamehamishwa. Kwa hiyo, hakuna *degree holder* tena katika ukurasa wa tatu utaona hakuna maabara wala *generator*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mashine ya *viral load* imehamishwa na kwenda Bukoba. Hii inadhoofisha uwezo wa hospitali teule kuhudumia wananchi takriban 700,000

katika Wilaya. Upanuzi wa hospitali mpya usimaanishe kudhoofisha zile za zamani. Naomba kujua mkakati wa kuepusha jambo hili, tusipoteze uwezo uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Rubya pia kitengo chake cha meno hakitoshi kabisa, ni kama hakipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile uboreshaji wa vituo vya afya viwili; Kaigara na Kimeya tumeshuhudia na sasa upasuaji unaendelea. Hata hivyo, bado kuna upungufu wa maboma. Ninaomba jambo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ujenzi wa zahanati kadhaa kwa nguvu za wananchi unaendelea karibu katika kata zote. Tatizo ni fedha za kununua vifaa vya viwandani; saruji, nondo, vioo na kadhalika.

Naomba Wizara iangalie jinsi gani ya kupata fedha kukamilisha ujenzi wa zahanati hizo ikiwemo zifuatazo: Buhangaza, Buganguzi, Kishando – Muleba, Burunguna, Muzinga – Nshamba, Kashanda – Kubirizi, Kasindaga – Kata Kamombi – Kangazo – Nyakabango.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaona kwamba mahitaji ni makubwa sana. Bila Wizara ya Afya na TAMISEMI kutuwekea nguvu itakuwa vigumu kumaliza zahanati hizi. Eneo linalohudumiwa ni kubwa. Sina budi kuwashukuru TANAPA kutusaidia katika ujenzi wa zahanati kisiwa cha Ikuza. Ni Ukombozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Umy kutusaida kupata *ambulance* ya Hospitali ya Rubya. Pia, tunazo kwenye vituo vyetu vya afya, lakini wakati mwingine *ambulance* inasimama kwa sababu ya kukosa dereva. Ni suala la TAMISEMI, lakini ninaamini Wizara ya Afya ni mdau mkubwa katika jambo hili. Jamani hospitali kusimama kwa sababu tu hakuna dereva! Kama haupo utaratibu, tunaomba mwongozo utolewe wa kumwezesha Mkurugenzi kuhakikisha kamwe *ambulance* haisimami kwa kukosa dereva.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ajira kwa Madaktari na Wauguzi. Ni jambo la kushangaza kuwa baadhi ya Madaktari wanahitimu lakini wanahangaika kutafuta ajira na wengine kukata tamaa na kwenda nje ya nchi. Ninaomba kujua, hivi sasa tuna Madaktari wangapi ambao bado hawajaajiriwa, huku uhaba wa Madaktraiki na Wauguzi mbalimbali wakiwa hawatoshi katika hospitali zetu. Naomba mkakati wa *manpower planning* kwa Sekta hii uwekwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Mloganzila imekamilika na ninapongeza juhudi za Awamu ya Nne zilizojenga, lakini naamini ni muhimu sasa kuwa na mpango wa kujenga hospitali *town*. Hivi sasa madaktari hawana makazi na sijui kama dharura ikitokea itakuwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, *MSD* ya Kanda ya Ziwa Magharibi ipo Muleba. Mheshimiwa Waziri anajua kulikuwepo na tetesi kwamba itahamishwa kwenda Bukoba. Mheshimiwa Waziri Dkt. Ndugulile alitembelea *MSD* hiyo na kuona athari za kuihamisha. Aidha, mantiki ya kuiweka Muleba ni kwa kuwa ni katikati ya eneo la huduma; Kagera, Geita na Kigoma Kaskazini. Naomba hofu hii ya kuhamisha *MSD* ya Kanda iondolewe ili maendeleo yaliyopangwa yaendelee. Eneo la kutosha ekari tano zimetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bima ya Afya ni mkombozi na tunapongeza maendeleo yake. Changamoto zinazojitokeza ni ngazi ya *referral system*. Inaonekana hakuna *manual ya recommended drugs* kwa Hospitali za Rufaa. Hicho hicho cha hospitali za kawaida ndicho kinatumika Hospitali za Rufaa. Hii ina ukakasi, kwani Hospitali za Rufaa zina utaalumu zaidi na wanaweza kukubadilishia dawa. Sasa kuna Wakaguzi wa *NHIF* na uthibiti wa *abuse*, ni muhimu kwa sababu wakaguzi hao wanaweza wasikubaliane na daktari bingwa, inaleta ukakasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nilimwomba Mheshimiwa Waziri Ummy atambue Hospitali ya Mkoa ya Bukoba haikidhi viwango vya *referral* kutoka Hospitali Teule ya Rubya. Kwa hiyo, Bima ya Mkoa wa Kagera *referral* iwe

Bugando, hata kwa Bima ya jamii, yaani zahanati - wilaya - Bugando hadi Rubya Hospitali ya Mkoa itakapoboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri huduma za saratani ziendeleo kuboreshwa. Tunapongeza *Ocean Road* na Bugando kwa huduma zao lakini hazitoshi. Pia tuwekeze katika kuzuia kuenea kwa saratani, tupime afya, tusingojee mionzi. *Prevention is better than cure*. Inahitaji Wizara kupiga kampeni ya *rollback cancer*.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya katika Sekta hii muhimu sana kwa maisha ya mwanadamu. Nawapongeza pia Katibu Mkuu, viongozi na watumishi wote wa Wizara kwa bajeti nzuri na kwa kuchapa kazi. Mwenyezi Mungu aendeleo kuwawezesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa maboresho makubwa katika Sekta ya Afya nchi nzima. Hii ni kazi kubwa sana na ni ukombozi kwa wananchi wa Tanzania. Kufungamananisha uchumi na maendeleo ya wananchi kunaonekana katika sekta hii. Sasa naiomba Serikali yangu ilete Muswada Bungeni wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote ili wananchi wafaidike na huduma bora za afya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kulipatia Jimbo langu zaidi ya shilingi bilioni moja kujenga vituo vya afya viwili na kuvipatia vifaa tiba. Vituo hivyo ni Kerege na Matimbwa. Vituo hivi vitachangia sana kuboresha huduma ya afya Bagamoyo. Kituo cha Afya Kerege kimeanza kufanya kazi isipokuwa cha Matimbwa (Yombo) bado hakijaanza kazi. Namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kupata samani, vifaa tiba na watumishi wa ajili ya Kituo cha Afya cha Matimbwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji zaidi ya 20 (kata tano) katika barabara ya Bagamoyo Msata (kilometa 64) havina huduma ya kituo cha afya. Namwomba Mheshimiwa Waziri



atupangie kituo cha afya katika eneo hilo kubwa toka Bagamoyo mpaka Msata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu sana ukitoka Wizara ya Elimu. Hii ni Wizara yenye kushikilia maisha ya Watanzania. Bila kuimarisha Wizara hii, hakuna Serikali ya Viwanda wala Tanzania ya Viwanda kwani afya ni kila kitu. Watanzania wakiwa na afya bora ndiyo shughuli za kiuchumi zitakuwa na maendeleo, kwani mwenye kuleta maendeleo ni wananchi wenye afya bora na nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nitoe maoni yangu katika Wizara hii. Kwanza ni upungufu wa rasilimali watu katika Wizara hii ya Afya. Sekta hii ina upungufu mkubwa wa rasilimali watu. Sekta hii ina upungufu wa watumishi kwa asilimia 49 katika mwaka wa fedha 2016/2017. Tunaomba Serikali itoe hitaji la watumishi wa sekta hii ya afya ili wananchi wapate matibabu kwa wakati na kwa ubora wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri aone kilio cha Watanzania juu ya hitaji hili muhimu. Imekuwa na usumbufu kwa wananchi wanapohitaji matibabu wanachukua muda mrefu hospitalini, mtu anakwenda saa 12.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni ndiyo anapata matibabu kutokana na uhaba wa wahudumu. Mhudumu ana daktari mmoja, huyo anahitajika zaidi ya vitengo vitatu kwa wakati mmoja. Hii ni shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ituambie ni lini itatatua tatizo hili la upungufu wa watumishi katika sekta hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitazungumzia hali ya maambukizi ya VVU na UKIMWI nchini Tanzania. Hali hii inaendelea kukua kwa kasi zaidi kinyume na hali iliyotarajiwa. Dhana nzima ya 90 - 90 - 90 iliyoanzishwa na Umoja wa

Mataifa kuhusu HIV/AIDS mwaka 2013 kwamba ili kufikia mwaka 2020 kusiwepo na maambukizi ya UKIMWI Duniani. Kwa maana, kutambulika, waliotambulika wako kwenye matibabu ya ARV na wenye matumizi ya ARV, virusi vitakuwa vimefubaa na hakutakuwa na maambukizi mapya. Hii ndiyo azma ya 90 – 90 – 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Tanzania, hatujafikia hatua hii, ni hatari sana na ndiyo kwanza maambukizi yanazidi. Kwa mfano, vijana kati ya miaka 15 - 49 ndiyo rika hatari zaidi na wenye kuleta maambukizi zaidi. Hawa ni vijana ambao wako shuleni na vyuoni kwa asilimia 46. Je, Tanzania tumefikia wapi katika kufikia lengo la 90 – 90 – 90 na tukizingatia umebaki mwaka mmoja na nusu kufikia muda uliowekwa na Umoja wa Mataifa? Serikali itufahamishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali na Sekta hii itoe elimu kuhusu HIV/UKIMWI na isione haya kueleza vitu vinavyosababisha maambukizi, bila kificho. Kama Serikali haitaacha kupiga marufuku *condom* UKIMWI utaendelea kuwepo, kwani hivi ni vichochezi vya zinaa. Vitabu vya dini vinasema tusikaribie zinaa, zikishamiri maradhi yatazidi ama majanga na hili ni janga na siyo maradhi kwani kila maradhi huwa yana tiba ila UKIMWI hauna tiba. Ili UKIMWI uondoke, tuache zinaa tutake tusitake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inatisha sana hasa tukizingatia maambukizi kwa vijana hawa wadogo. Hii ina maana nguvukazi ya Taifa hii inapungua na kufa pia kwa kasi sana na tusipochukua tahadhari tatizo hili ni zito na kubwa sana, huenda miaka ya mbele tutakosa kabisa vijana wenye afya bora wa kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya kuweka mikakati madhubuti ya kuzuia maambukizi mapya na kuweka sheria, kama ni kosa la jinai kufanya zinaa au vitendo hivi bila ya kuwa na ndoa. Kinyume na hayo tutatenga pesa ama fedha nyingi za kutibu na maambukizi yataongezeka na mwisho tutakosa nguvukazi za Taifa na hivyo Tanzania ya Viwanda itabaki kuwa ndoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, nianze sasa kuchangia Wizara hii. Kwanza nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri kwa kunipatia *ambulance* mbili Kata ya Buhingu, kwenye kituo cha afya na ya pili Kituo cha Afya Kata ya Uvinza. Sambamba na shukrani hizi bado tuna changamoto kubwa kwenye Kituo cha Afya Kalya, kina umbali wa kilometa 250. Mheshimiwa Waziri alipofanya ziara alituahidi *ambulance* ya Kituo cha Kalya, tunaomba tuletewe hiyo *ambulance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyo vituo vya afya vinne vinavyojengwa ndani ya Jimbo langu. Vituo vitatu Ukanda wa Ziwa Tanganyika na kituo kimoja ukanda wa reli. Vituo hivyo ni hivi vifuatavyo: Kituo cha Afya Kabeba, Kituo cha Afya Kazuramimba na Kituo cha Afya Igalula (Rukoma). Tunazo pia zahanati mbalimbali zinazojengwa kwa jitihada za wananchi na kupitia Mfuko wa Jimbo. Mheshimiwa Waziri akiona inampendeza atusaidie fedha kwa ajili ya kumalizia maboma haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwa kutupatia shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Ujenzi umeshaanza, tunaendelea. Tunaomba kwenye bajeti hii tutengewe fedha nyingine kwa ajili ya kuendeleza hospitali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo hayawezi kwisha bila vifaa na watumishi. Hivyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri kwenye mgao wa watumishi, Uvinza iangaliwe kwa jicho la huruma, kwani jimbo ni kubwa na watumishi ni wachache sana. Sambamba na watumishi, tunaomba pia vitendeakazi, kwa mfano Ukanda wa Ziwa Tanganyika na Kituo cha

Nguruka wapate vifaatiba kama *X-Ray, Ultrasound* na vifaa vingine, kwani wagonjwa ni wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua fika Halmashauri ya Uvinza ilianzishwa tarehe 18 Mei, 2012 lakini hakuna idara hata moja iliyo na gari. Hii inasababisha Wakuu wa Idara kupata taabu sana kwenye kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa fedha zinazopelekwa huko chini kwenye kata, vijiji na vitongoji.

Namuomba Mheshimiwa Ummu atupatie gari moja, *Land Cruiser* ya watumishi kufuatilia miradi na utendaji kazi wa watumishi kwani malalamiko ya wananchi ni mengi, ni vyema gari ikapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimkumbushe Mheshimiwa Ummu Mwalimu ahadi yake ya kumpongeza Nesi Zainabu, anayefanya kazi kwenye Zahanati ya Mwakizega kwa kazi nzuri hadi wananchi wakaandamana kumlilia Nesi Zainabu. Maana tangu mwaka 2017 hakuna motisha yoyote aliyopewa kwenye Halmashauri ya Uvinza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, niendeleo kumpongeza mdogo wangu, Mheshimiwa Ummu Mwalimu, kwani ataacha kumbukumbu muhimu sana kwenye hii Wizara. Sote ni mashahidi, anafanya kazi yenye tija na kuridhisha sana. Baada ya pongezi naomba kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nitoe pongezi zangu kwa Serikali ya Awamu ya Tano, pia kwake Mheshimiwa Waziri Ummu na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. F. Ndugulile, kwa kufanya kazi kwa weledi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani hizi, naomba nikumbushe jambo moja kwamba Dongobesh, Kituo cha Afya na Jimbo la Mbulu Vijijini hatuna kabisa gari la wagonjwa (*ambulance*) la kuwahudumia wananchi. Pia

Mheshimiwa Mheshimiwa Ummu akumbuke ilikuwa ahadi yake pale Dongobesh baada ya ziara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli nakubali kazi wanayofanya Mheshimiwa Ummu na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Faustine, wamefanya ziara ya kuona changamoto za Mbulu Vijijini. Pia tumejengewa kituo kimoja cha afya cha Dongobesh, ahsanteni sana. Hospitali ya Halimashauri ya Wilaya inajengwa, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaombea Mungu warudi tena katika nafasi zao baada ya mwaka 2020 katika Uchaguzi Mkuu. Mungu atujalie, ahsanteni.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilombero haina Hospitali ya Wilaya, Hospitali inayotumika ni Mtakatifu Fransisko lakini gharama zake ni kubwa kidogo kwa watu wengi kuweza kumudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna Vituo vya Afya vya Kibaoni, Mang'ula na Kidatu. Vituo hivi havikidhi mahitaji ya kihuduma na tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Kilombero ni zaidi ya 500,000. Bila ya kupata Hospitali ya Wilaya, bado bituo hivi vitakuwa na kazi kubwa hivyo kupunguza ufanisi. Tunaomba kupatiwa Hospitali ya Wilaya ya Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Hivi karibuni Mheshimiwa Rais alifanya ziara Mkoani Mbeya, akiwa Wilayani Chunya, aliombwa na wananchi fedha za kukarabati Hospitali ya Wilaya. Mheshimiwa Rais aliahidi shilingi 200,000,000/= kwa ukarabati huo. Naiomba Wizara ifuatilie na kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile dakika ishirini.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuwepo katika Bunge lako Tukufu na kuweza kuchangia hoja iliyowasilishwa hapa Bungeni tarehe 07 Mei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia ya pekee kabisa naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kutumikia nafasi hii ya Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Aidha, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais pamoja na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa kwa maelekezo mbalimbali ambayo ameendelea kutupatia katika utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia ya kipee kabisa napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Umy Mwalimu, mimi namwita Daktari kwa ushirikiano wake wa hali ya juu sana na miongozo mbalimbali ambayo ameendelea kunipatia katika utekelezaji wa majukumu. Amekuwa ni nguzo moja muhimu sana na mafanikio haya tunayapata ni kwa sababu ya uongozi wake mahiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa michango yao, maoni yao na ushauri wao kwa kiasi kikubwa sana wamekuwa ni dira na miongozo wetu na tunaahidi kwamba tutazingatia maoni na ushauri wao katika kutekeleza majukumu yetu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru timu ya wataalam ambao na sisi tunawaongoza, Makatibu Wakuu wawili, Dkt. Zainabu Chaula, Katibu Mkuu wa Fungu 52 na

Dkt. John Jingu wa Fungu 53 kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameendelea kuifanya. Kazi nzuri inaonekana kwa sababu na kazi nzuri ambayo wao kama Makatibu Wakuu na Watendaji wote wameendelea kuifanya pamoja na Wakuu wa Taasisi, vyyo vya mafunzo na hospitali zetu zote ambazo na sisi kama Wizara tunazisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini haya yote yasingeweza kwenda vizuri kama nisingepata *support* ya wale wananchi ambao wamenileta hapa, wananchi wa Kigamboni na naomba nitambulishe pale juu *gallery*leo nina viongozi wa Chama cha Mapinduzi natumaini utapata fursa ya kuwatambua kutoka Wilaya ya Kigamboni na Waheshimiwa Madiwani wote kutoka Wilaya ya Kigamboni nao wapo hapa kuja kushuhudia wasilisho la hotuba hii. Niendeleo kusema kwamba Kigamboni tunawakilisha vizuri ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache sasa naomba nijielekeze katika baadhi ya hoja za msingi ambazo ziliweza kutolewa na Waheshimiwa Wabugne na nianze na hoja za Fungu 53, Fungu la Maendeleo ya Jamii. Niseme tu kwamba moja ya hoja ya msingi ambayo ilijadiliwa sana na Wabunge wengi ni suala la wazee, na suala la wazee sisi kama Serikali tunapaswa tujivunie sana. Katika moja ya mafanikio ambayo Serikali hii imeweza kufanya ni kuhakikisha kwamba umri wa Mtanzania kuishi umezidi kuongezeka, hivi tunavyoongea wastani wa Mtanzania kuishi ni miaka 64.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maana yake ni nini, ni kwamba ni mafanikio ya mikakati yetu ya lishe lakini mafanikio ya vilevile ya mkakati yetu ya kuhakikisha kwamba Watanzania hawa tunapata huduma nzuri za afya, na ndiyo maana tuna kundi kubwa la wazee ambalo lipo na tunatarajia kwamba kwa hali tuliyokuwa nayo watu wengi watafika zaidi ya miaka 60 ya umri wakiwa na afya njema na kuweza bado wakiwa na nguvu ya kuendelea kutumikia nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Sera ya Wazee ya Mwaka 2003, tunayo na tunaamini baada na sisi kuingalia tumeiona kwamba tunahitaji tuifanyie maboresho na kuja mkakati sasa ambao utakwenda kutibu baadhi ya changamoto hizi za wazee.

Lakini naomba niseme kitu kimoja, Serikali inatambua na kuthamini mchango wa wazee ndani ya Taifa letu, na ndiyo maana sisi kama Serikali tuna makazi 17 ya wazee ndani ya nchi lakini tunawahudumia takribani wazee 510 ndani ya makazi haya 17. Utaratibu uliokuwepo ni mmoja; sisi kama Serikali tunawachukua wale wazee ambao kwanza hawana watoto wa kuweza kuwahudumia, na kama wale wazee hawana watoto basi tunajaribu kuangalia, je, wazee hawa hawana ndugu wa kuwahudumia, na je, kama hawa wazee hawana ndugu wa kuhudumia, je, jamii haiwezi ikabeba jukumu hilo. Kama katika vigezo vyote hivi vitatu havipo basi sisi Serikali tunawachukua wale wazee na tunawagharamia kwa vitu vyote, malazi, makazi na mavazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema idadi ambayo ya wazee ambayo tunayo ni takribani 510 na wazee hawa tunawapa huduma hizo zote za msingi na katika jambo ambalo tunalihakikisha Wizara ni kuhakikisha kwamba, hawa wazee wanapata chakula, malazi na mavazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo tumeendelea kuhamasisha halmashauri kuzingatia agizo la Serikali la kuwapatia wazee vitambulisho kwa ajili ya matibabu ili wazee wapate matibabu kwa mujibu wa Sera ya Afya ya mwaka 2017 ambayo inasema wazee watapata matibabu bure. Lakini tulienda mbali zaidi na kuhakikisha kwamba hospitali zetu zote zinakuwa na dirisha la wazee, ili wazee wakifika pale waweze kupata matibabu bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sera mpya ya afya ambayo tunayo sasa hivi, tunataka sasa tuende mbali kuona kwamba kuna suala zima la matibabu ya magonjwa ya wazee, kwa sababu wazee hawa kadri kundi linavyozidi kubwa wanakuwa na magonjwa yao ambayo ni mahsusi,



*geriatric Medicine* kwa lugha ya kitaalam nayo tumeshaliona tunaliwekea mkakati ili kuhakikisha kwamba hawa wazee nao tunaweza kuwahudumia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja katika jambo ambalo Mheshimiwa Waziri allliongea katika hotuba yake, ni pamoja na haya magonjwa sugu ya *non communicable disease* ambayo tumeona kweli changamoto na mara nyingi wakienda katika hospitali, dawa nyingi wanazokosa ni zile dawa za *pressure*, za kisukari na nini, hilo tumeliona na ndiyo maana tumeazimia kama tulivyokuwa tuna mapambano na magonjwa mengine kama kifua kikuu, *TB* na malaria, tunataka tuanzishe Mpango wa Taifa wa Magonjwa Yasiyoambukiza na ambayo sasa yatakwenda kushuka mpaka katika ngazi ya chini ili huduma hizi za msingi za huduma za matibabu utambuzi, matibabu na tiba ya magonjwa yasiyoambukiza iweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala jingine ambalo nilikuwa nataka kuligusia ni suala la *NGO'S*, asas zisizokuwa za Kiserikali. Hivi karibuni tulibadilisha Kanuni, mara nyingi tunatambua mchango mkubwa sana wa Mashirika yasiyo ya kiraia katika kuleta maendeleo na kutusimamia kama sisi Serikali, na tunathamini, tunatambua mchango wao. lakini hivyo hivyo kama walivyotaka kutusimamia sisi na kutaka kupata uwazi na uwajibikaji na sisi tunataka tupate uwazi na uwajibikaji katika taasisi zisizo za kiserikali. Ndiyo maana tumebadilisha Kanuni ili sasa kuwepo na uwazi katika fedha ambazo wanazozipata, lakini uwazi katika uwajibikaji katika yale maeneo ambayo walisema wanaenda kuyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na changamoto kuna baadhi ya *NGO's* zimepata fedha nyingi sana, lakini haziendi katika malengo yale ambayo yalikuwa yanakusudiwa. Na baadhi ya *NGO's* zimetoka katika malengo na makusudio ambayo yalikuwa yanayafanya, wameenda kujiingiza katika mambo mengine. Wengine wanapata dola milioni 100 lakini zinazofika kwa walengwa ni chini ya dola milioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumeweka utaratibu kwamba fedha zote zinazolingia lazima tuzijue, zinaenda kufanya kazi wapi, lakini tunataka tulete uwiano kwamba kuna baadhi ya maeneo ndani ya nchi yetu huku, zimekuwa na *NGO's* nyingi sana lakini kuna maeneo ndani ya nchi yetu hazina *NGO's* shata moja na kote huko kuna Watanzania. Sasa tunataka tuweke utaratibu mzuri, tumeanzisha Kanzi *data*, tuna *NGO's* karibuni 9,000 ndani ya nchi yetu, mpaka sasa hivi tumeshaziingiza kwenye *Database NGO's* takribani 6,000, tunaendelea na usajili na lengo ni kusudio ni kwamba kila mmoja kule kule alipo hahitaji kuja Dodoma. Tunaweza tukapata taarifa zake tukajua yuko wapi, anafanya nini na fedha alizokuwa nazo kiasi gani, anawajibika kwa utaratibu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niendeleo kuwatoa shaka ndugu zangu lengo siyo baya, lengo ni kuweka uwajibikaji na uwazi ili kabisa kuhakikisha kwamba hizi *NGO's* ambazo na sisi kama Serikali tunatambua mchango wao ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo liligusiwa na Waheshimiwa Wabunge ni masuala ya Mitaala ya Vyu vyetu vya Maendeleo ya Jamii na Vyu vya Ustawi wa Jamii, haya Waheshimiwa Wabunge tumeyapokea, tutaenda fanyia kazi ili sasa Mitaala hii iendane na mazingira ya sasa na uhitaji wa sasa wa Tanzania ambayo tunaelekea katika Tanzania ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze katika maeneo mengine ya Sekta ya Afya hususan *Vote 52*. Namshukuru sana Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI amegusia suala la watumishi, rasilimali watu. Na mimi niendeleo kuongezea kidogo tu katika hili, pamoja na changamoto hii tuliyokuwanayo ya rasilimali watu, sisi kama Wizara ya Afya hatujakaa tukalala. Tumeangalia ubunifu ambao tunaweza tukatumia kuangalia jinsi gani tunaweza kutumia rasilimali chache, watu hawa tuliokuwa nao ili kuweza kuleta tija katika utoaji huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya jukumu ambayo tumeweza kulifanya katika lugha ya kitaalam wanaita *task shifting*...

**MBUNGE FULANI:** Yes.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** ...kwa sababu unaweza ukaenda katika kituo cha afya, daktari yule, kwa mafunzo ambayo tunayo, mimi ninaweza nikachoma sindano, nikafunga kidonda na ninaweza nikatoa dawa. Sasa inawezekana mtu akawa pale amemaliza majukumu yake, anaweza akaenda akafanya jukumu lingine ambapo ndani ya kituo. Tumeona tuweze ku-*reorient* haya majukumu ili basi huduma kwa mwananchi iweze kutolewa, kwa sababu wataalam wengi wa afya tumeweza kupata mafunzo katika nyanja mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tumeanza kutumia wataalam wengine ambao sio wataalam wa afya, wamepata *orientation*, kwa mfano kwa masuala ya upimaji na uchukuaji wa vipimo. Wameweza kupata *orientation* na wanaweza wakafanya hayo majukumu. Tunataka tufanye *orientation* ya Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii, basi nao waweze kutusaidia kutoa huduma katika baadhi ya maeneo ambayo tunaona yana tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeanza kutumia elimu mtandano (*telemedicine*). Kwa sasa hivi tunafunga mashine za digitali, dunia nzima ilishatoka huko. Sasa hivi Marekani *X-Ray* zinasomwa Australia ama inasomwa India. Nasi kwa nini wataalam wetu hawa wachache; na tumeshaanza, pale *MOI* na Muhimbili tunafunga mashine za kisasa, kutakuwa na *screen* ziko pale. Mashine zote hizi za *X-Ray* ambazo tunazifunga Tanzania nzima, itakuwa picha zake zote zinapelekwa Muhimbili na *MOI* zinasomwa na ndani ya dakika 15 au 20, mtu wa Tunduma, Ruvuma, Mbinga anaweza akapata majibu yake yamesomwa na wataalam. Hizi ni baadhi ya *innovation* ambazo tunaendelea kuzitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Madaktari wetu Bingwa hawa wachache tuliokuwa nao, tumesema pamoja na kwamba wako katika maeneo ya mjini na katika hospitali zetu kubwa, nami nashukuru sana Hospitali zetu za *JKCI*, Bugando, *MOI*, Mloganzila na *KCMC* wamekuwa wanatoa wataalam wao, wamekuwa wanaenda katika kambi mbalimbali mikoani, wanaendesha kambi za muda mrefu ili wale wananchi wa kule nao waweze kupata huduma hizi za kibingwa na zimekuwa na mchango mkubwa sana na tutaendelea na utaratibu huu kuhakikisha kwamba huduma za kibingwa nazo zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *innovation* tunazo nyingi na ndiyo maana unaona kwamba pamoja na changamoto tulizokuwanazo, hali ya utoaji huduma za afya bado zinaendelea kwa ubora ule ule ambao upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitukabidhi Hospitali za Rufaa za Mikoa, nasi tunaendelea kuzipanga. Mkakati wetu wa kwanza ni kuhakikisha kwamba hizi Hospitali za Rufaa katika mikoa ambayo hatuna, ni Hospitali za Rufaa za Mikoa ndiyo tunataka kuanza nazo; Mkoa wa Songwe, Njombe, Geita, Katavi na Simiyu. Ndiyo maana tumeweka nguvu kubwa sana katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili tunataka sasa katika maeneo ambayo tayari kulikuwa kuna majengo kwa maana ya Mikoa ya Singida, Tanga kule na Shinyanga, tunawekeza nguvu yale majengo yaanze kupata matumizi lakini awamu ya tatu sasa tutajielekeza katika hizi *RRH* nyingine kuhakikisha kwamba zile huduma za msingi nazo zinaweza kupatikana ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa vifaa na rasilimali watu. Tumewekeza sana sasa hivi katika mafunzo ya wataalam wa afya ili kuhakikisha sasa zile huduma za kibingwa na Madaktari Bingwa wanaweza kupatikana katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naamini katika mwaka wa fedha peke yake tumepata kama shilingi bilioni 1.5 kufundisha wataalam zaidi ya 300 na tunataka kwenda

mbali. Katika moja ya jambo ambalo tunalitafakari sasa hivi ni kubadilisha mfumo wetu wa mafunzo kwenda kwa utaratibu wa *fellowship*. Badala ya watu kukaa darasani, watu wanaweza wakaendelea kutoa huduma kule kule tukawapima zile *competence* zao ambazo tunazitaka na kuwatambua kwamba hawa ni Madaktari Bingwa. Wenzetu wameshapiga hatua kubwa sana katika utaratibu huu, nasi tunaamini ndani ya muda mfupi sisi kama Wizara tutakuwa tumepiga hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na mambo makubwa mawili au matatu kabla sijaandishia Wizara hii, kuna hoja ilikuja hapa kuhusiana na chanjo ya Malaria. Kwa nini wenzetu wa Malawi wamekuwa na chanjo ya Malaria na kwa nini sisi Tanzania tusianzishe chanjo ya Malaria?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maelezo ya kitaalam kidogo kwamba mpaka sasa hivi hakuna chanjo ya Malaria ambayo imethibitika asilimia 100 kutoa kinga dhidi ya Malaria. Chanjo nyingi tulizokuwa nazo hapa zinacheza kati ya asilimia 20 mpaka 40. Hamna chanjo ambayo imezidi zaidi ya hapo. Kwa hiyo, chanjo nyingi bado zipo katika ngazi ya hatua ya utafiti na naomba niseme kwamba Tanzania tuko vizuri sana katika masuala ya utafiti wa Malaria. Taasisi yetu ya *NIMR* inafanya kazi nzuri sana ya utafiti na Taasisi zetu za Ifakara *Institute* nayo inafanya kazi nzuri sana. Pale tutakapobaini kwamba kuna chanjo ambayo inaweza ikawa ina tija, basi na sisi kama Tanzania tutakuwa ni wa kwanza ku-*adopt* hizo chanjo kwa ajili ya kuwakinga wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kusema kwamba uwepo wa chanjo hauondi dhana ya sisi kuendelea na mikakati mingine yoyote ya kujikinga dhidi ya ugonjwa wa Malaria. Kwa hiyo, tuendeleo kwa sababu mazalia haya haya ya mbu ndiyo hayo hayo mazalia ya ugonjwa wa *Dengue*, Zika, Kichungunya na magonjwa mengi sana ambayo yapo. Kwa hiyo, nami nataka niwaombe Watanzania tuendeleo na mikakati yetu mingine, tunapiga hatua katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Malaria lakini tunahitaji tuongeze kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanjo ya gonjwa la ini, tuna tatizo la ugonjwa wa ini ndani ya nchi. Chanjo ya ugonjwa wa ini tunatoa kwa watoto wote chini ya miaka mitano, ni sehemu ya chanjo ambayo tunaitoa na kwa watu wazima tumekuwa tunatoa kwa wale ambao wako kwenye *risk* zaidi ikiwa ni pamoja na wataalam wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ambao tutakwenda nao na tulishakubaliana na Mheshimiwa Waziri ni kwamba kwa yule atakayekuwa anahitaji, tutaweka utaratibu wa chanjo hizi kupatikana kwa gharama nafuu ili mtu mwingine atakayekuwa anajisikia, basi aweze kuchanja kama nasi Waheshimiwa Wabunge tulipata fursa ya kuweza kuchanjwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa naomba niongelee suala la upimaji. Ni kweli tumekuwa na changamoto kubwa sana ya watu kubainishwa na ugonjwa wa *Typhoid* na *UTI*. Nimesema sana na ninaomba nitumie fursa hii kuongea na Bunge lako. Ukienda hospitali na ndani ya dakika tano Daktari akwambia *UTI* ama una *Typhoid*, naomba umwulize maswali ya msingi sana huyo daktari. Amejuaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utalam wetu sisi madaktari inahitaji kati ya masaa 48 mpaka 72 na achukue kipimo cha mkojo na achukue na kipimo cha damu kuja kukwambia wewe una ugonjwa wa *Typhoid* au una *UTI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba sana na Waheshimiwa Wabunge mtusaidie kutoa elimu kwa jamii kuwahoji wataalam wetu wa afya kwa sababu wengi sasa wameamua kwa kutumia homa ya *UTI* na *Typhoid* kama chanzo cha kupata fedha, lakini kimsingi hatuna tatizo kubwa sana la *UTI* na Malaria kama inavyosemwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kumaliza hizi hoja kama nyingi zilivyokuwa zimejitokea na nitoe fursa sasa kwa Mheshimiwa Waziri aweze kuendelea na hoja nyingine. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, namwita sasa Mheshimiwa Ummu Mwalimu, mwenye hoja ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile kwa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi wakati wa hoja ambayo iko mbele ya Bunge lako Tukufu. Kipekee napenda kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba ambaye aliwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuwashukuru Kambi ya Upinzani ingawa mambo mengi yameandikwa kwa kukosa taarifa na takwimu sahihi ya hali ya Sekta ya Afya inavyokwenda mbele toka Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ameingia madarakani. Kwa hiyo, nitawajibu hoja zao. Katika hatua hii tunawashukuru kwa kutoa hoja ambazo hazina mashiko ya takwimu sahihi na hali halisi ya utoaji wa huduma za afya nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hotuba yangu kwa kuzungumza na kwa maandishi ambao ni Wabunge 112; kati yao Wabunge 44 wamechangia kwa kuzungumza na Wabunge 59 wamechangia kwa maandishi. Aidha, Waheshimiwa Wabunge tisa walichangia wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge ni nyingi, kwa hiyo, nitashindwa. Haya makaratasi yote ni majibu ya hoja ambazo zimetolewa. Kwa hiyo, nitatoa tu ufafanuzi katika baadhi ya mambo makuu. Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba tumepokea maoni na ushauri wenu na tutaufanyia kazi katika kuhakikisha kwamba tunaboresha huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru katika hatua hii ya awali kwa pongezi kubwa nyingi ambazo wametupatia mimi, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wa Wizara na Katibu Mkuu. Naomba kupitia kwako niwaahidi Waheshimiwa Wabunge wote, pongezi hizi hazitatufanya sisi tukalewa sifa, bali ni chachu ya kufanya kazi vizuri zaidi ili tuweze kuhakikisha huduma bora za afya, maendeleo na ustawi wa jamii zinapatikana kwa Watanzania, lakini hasa wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia *Universal Health Coverage* hatuzungumzii tu Bima ya Afya, maana yake kila Mtanzania wa hali yoyote masikini, kipato cha kati, tajiri wa kijijini, wa mjini aweze kupata huduma za afya bila ya kikwazo chochote ikiwemo kikwazo cha fedha. Kwa hiyo, niseme tu kwamba tumepokea ushauri na pongezi lakini tutaendelea kufanya kazi kuhakikisha tunatatua changamoto za Sekta ya Afya katika nchi yetu, kwani tunatambua bila afya hakuna elimu, bila afya hakuna maendeleo, bila afya bora hakuna uchumi na bila afya bora hakuna ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa ufafanuzi, natambua kwamba Kanuni za Bunge zilishatoa pole, lakini kabla sijaendelea, naomba nami kuungana na Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu kutoa pole kwa familia ya Dkt. Reginald Mengi ambaye amekuwa mdau mkubwa wa Sekta ya Afya. Kwa hiyo, tunawapa pole familia na tunawaomba Mwenyezi Mungu awape subira na ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu.



Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shahidi, Dkt. Mengi amekuwa akitupa nafasi katika vyombo vyake *ITV, Radio One, East Africa Radio* kutoa Elimu ya Afya kwa Umma kuhusu masuala mbalimbali. Pia ameweza kusaidia watu wenye ulemavu. Kubwa, tutamkumbuka na kum-*miss* katika Sekta ya Afya kwa sababu alianza kuwekeza kujenga Kiwanda cha Dawa *M-Pharmaceuticals* Bagamoyo, lakini Mwenyezi Mungu hakupenda ndoto yake iweze kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa niruhusu nijibu baadhi ya hoja. Nikianza na hoja ambazo zimetolewa na Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii; tumepokea ushauri na maoni ya Kamati na kwa kweli yote tutayafanyia kazi. Jambo kubwa ambalo walilitolea maoni ni kwamba Serikali ihakikishe fedha zilizotengwa kwa Mwaka 2018/2019 zinatolewa zote na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubaliana na ushauri huu na niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba tutaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo zimetengwa katika bajeti ambayo inaisha Juni zinatolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazo habari njema. Mheshimiwa Dkt. Mpango na timu yako ninakushukuru sana. Katika mwezi wa Pili ambapo tulishatoka kwenye Kamati, tumepata shilingi bilioni 62 kutoka Hazina, shilingi bilioni 20 tumepata kwa ajili ya dawa; shilingi billioni 32 tumepewa baada ya kuwa tumeshawasilisha makadirio yetu kwenye Kamati ambazo zitatumika kwa ajili ya kuboresha huduma za matibabu ya kibingwa ikiwemo upandikizaji wa kutumia chembe chembe za mwili tunaita *bone marrow transplant*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumepata kutoka Hazina shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kuboresha huduma katika Hospitali za Rufaa za Mikoa. Nje ya bajeti ambayo ilipitishwa na Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Oscar Mukasa amesema hapa, sisi pia; mimi na Naibu Waziri na Katibu Mkuu, tunahangaika kutafuta vyanzo vingine vya fedha. Kwa hiyo,

nje ya bajeti ambayo imetolewa, ndani ya mwezi wa Nne tumepata shilingi bilioni 58 kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya ambao tumepeleka katika zahanati, katika hospitali za wilaya, katika vituo vya afya kwa ajili ya fedha za uendeshaji. Kwa hiyo, tunapokea maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ni Serikali ya kushughulikia na kutatua changamoto za watu hasa wanyonge na ndiyo maana fedha hizi zimeendelea kutoka kwa ajili ya kuboresha huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo limeelezwa na Kamati ni kwamba Serikali ikamilishe mchakato wa kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya. Tunakubaliana na ushauri huu na tunaamini, kama tulivyoahidi katika hotuba yangu, mwezi wa Tisa tutakuja Bungeni kwa ajili ya kuleta mapendekezo ya Sheria ya Bima ya Afya ambayo itamlazimu kila Mtanzania sasa kuwa na Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na hoja za Waheshimiwa Wabunge. Mtanzania masikini kama huna hela ni changamoto kupata matibabu. Tukiangalia takwimu ambazo nimezionesha katika kila Watanzania 100 ni Watanzania nane tu ndio wana Bima ya Afya ya *NHIF*. Sasa Mtanzania huyo awe na tatizo amezungumza kaka yangu Mheshimiwa Khatib kutoka Pemba, unatakiwa kufanya *dialysis session* moja ni shilingi 180,000/= mpaka shilingi 250,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Daktari anaweza akakwambia ufanye *dialysis*, yaani kuchuja damu sijui kusafisha damu au kutakasa damu (sijui *dialysis* kwa Kiswahili), Kutakasa damu nadhani kwa Kiswahili kizuri. Anaweza akakuandikia ufanye mara tatu; *minimum* anaweza kukwambia ufanye mara mbili kwa wiki. Mara mbili Mtanzania gani anaweza ku-*afford* shilingi 400,000/= kila wiki kwa ajili ya huduma za *dialysis*?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeoneshwa huduma za kupandikiza figo, kupandikiza vifaa vya kuweza kuwasaidia watoto kusikia, ni Bima ya Afya ndiyo zimefanya hii kazi ya kutoa huduma hizo ambazo zilikuwa zinapatikana kwa shilingi milioni 30 mpaka shilingi milioni 80. Kwa hiyo, tunakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba tutaleta Muswada wa Sheria, lakini pia kabla ya kuleta Muswada wa Sheria, tutaendelea pia kufanya uhamasishaji na kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kujiunga na Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kwamba Watanzania hawana pesa, kuna suala la *willingness to pay* na *affordability to pay*. Kwa hiyo, Watanzania wengi bado hawako tayari kulipa Bima ya Afya. Nitumie Bunge lako Tukufu kutoa rai kwa Watanzania. Ule utamadumi tuo jenga kuchangiana harus, kuchangiana *Kitchen Party*, tuujenge katika kuchangiana kununua Bima za Afya kwa ajili ya Watanzania masikini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limeongelewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge, jambo la tatu, ni suala la kufanya uboreshaji wa huduma za uzazi katika maeneo mbalimbali. Tunakubaliana na ushauri wa Kamati. Waheshimiwa Wabunge wenyewe ni mashahidi, hata vituo vya afya vinavyoboreshwa na vilivyoboreshwa 352, asili yake ya andiko la vituo hivi ni kuboresha huduma za uzazi, mama na mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tuliona, hivi sisi kama Mawaziri; nilikaa nikasema, hivi mimi Ummy Mwalimu, Waziri mwanamke, sina *background* ya Udaktari, lakini bado Mheshimiwa Rais ameniamini niongoze Wizara ya Afya, naacha *legacy* gani kwa Watanzania? Kwa hiyo, nawashukuru sana wataalam wa Wizara, tuliweza tukakaa tukaandika andiko na ndiyo maana sasa tunaboresha vituo vya afya takriban 350. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Jafo na timu yake kwa sababu walijiongeza na Dkt. Chaula. Sisi tungeweza tu tukatafuta fedha, lakini wao

wakaja na wazo la *Force Account* ambalo limeleta mafanikio makubwa katika uboreshaji wa miundombinu ya afya. Kwa hiyo, tunakubaliana na maoni ya Kamati. Tutaendelea kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nataka kusema mbele ya Bunge lako Tukufu, tunataka Watanzania hasa wanawake ambao ndio wapigakura wa chama changu Chama cha Mapinduzi kujionea kwamba huduma za afya ya mama na mtoto zimeboreka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na vituo vya afya, pia tumeanzisha kampeni mbalimbali za kuhamasisha uwajibikaji na matokeo chanya katika kupunguza vifo vya akina mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, ambaye amekuwa ndio mlezi wa kampeni hii. Tumeweza pia kuhakikisha tunaweka wataalam wakiwemo wataalam wa kutoa dawa ya ganzi na usingizi ambapo tumeweza kugharamia mafunzo takriban ya watu 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, wifi yangu, sijui kama naruhusiwa kusema hivyo, Mheshimiwa Esther Matiko nitamjibu baadaye, lakini anaweza akasema labda tunasema. Ukitaka kupima, je, tunakwenda mbele katika eneo hili la afya ya mama na mtoto au hatuendi mbele? Tunaangalia viashiria vikuu ambavyo vimewekwa na Shirika la Afya Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiashiria cha kwanza: Je, huduma za uzazi wa mpango zinaendelea? Kwa mujibu wa takwimu zetu, tumeongeza kiwango cha watumiaji wa huduma za uzazi wa mpango kutoka asilimia 32 hadi asilimia 38. Hizi ni takwimu za *NBS*. Tukiangalia *program data* tutakuwa tuko vizuri zaidi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Huo ndiyo ukweli.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati wenu wa kuchangia Mheshimiwa Waziri alikuwa kimya akiwasikiliza na ninyi msikilizeni anapowajibu. (Makofi)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Catherine Ruge mtulie, mpeni nafasi Mheshimiwa Waziri. Tukianza kujibizana hapa, tutaanza kuzitafuta Kanuni zetu zinasemaje. Tafadhali, naomba msijibizane. Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo ukweli. Hata tukiangalia akina mama wanaojifungulia katika vituo vya kutoa huduma za afya, kabla Mheshimiwa Dkt. Magufuli hajaingia madarakani ilikuwa ni asilimia 65 lakini kwa sababu huduma za uzazi za mama na mtoto zimeboreka, tumeongeza idadi ya akina mama wanaojifungua katika vituo vya kutoa huduma za afya kufikia asilimia 32. Huu ndiyo ukweli, hata katika ngazi ya mikoa, inaonekana kwamba hali ya huduma za mama na mtoto zinaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ambalo ndiyo viashiria vikuu vya afya ya uzazi ya mama na mtoto, je, kuna ongezeko la akina mama wajawazito ambao wanahudhuria kliniki angalau mara nne katika kipindi cha ujauzito wao. Tumeonyesha pia kwamba lipo ongezeko la zaidi ya asilimia 30 la wanawake ambao wanahudhuria kiliniki angalau mara nne. Kwa hiyo, hivi ndiyo viashiria vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunakuja kwenye takwimu, je, vifo vimepungua au havijapungua. Utafiti uliofanywa na Taasisi ya Takwimu ya Taifa *(NBS)*, ulikuwa ni utafiti wa mwaka 2015, kwa hiyo, sasa hivi hatuna takwimu zaidi ya hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu, *NBS* akifanya utafiti mwingine, sina shaka, vifo vya akina mama wajawazito vitakuwa vimepungua kwa zaidi ya asilimia 50. Tukikusanya takwimu ambazo tunazo katika mikoa, sipendi kuzitaja kwa sababu siyo takwimu rasmi, lakini hali inaonyesha kwamba tumepunguza kwa kiasi kikubwa vifo vya akina mama wajawazito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya nne ambayo imeelezwa na Kamati na ambayo tumeipokea ni suala la maambukizi ya UKIMWI na kwamba katika maambukizi mapya ya UKIMWI asilimia 44.6 ni vijana wakati sheria inakataza mtu mwenye umri wa miaka 18 kupima UKIMWI bila ya ridhaa ya wazazi lakini pia inakataza mtu kujipima UKIMWI mwenyewe isipokuwa apime katika vituo vya kutolea huduma za afya. Tumepokea ushauri na tayari tumeandaa marekebisho ya Sheria ya VVU na UKIMWI, Sura ya 431 ambayo tumependekeza turuhusu mtoto mwenye umri wa chini ya miaka 18 kupima UKIMWI bila kuhitaji ridhaa ya mzazi au mlezi.

Pia tunapendekeza kwamba tutafanya marekebisho ya sheria hiyo, kifungu 13(4) ili kuondoa ulazima wa watu kupima VVU katika vituo vya kutolea huduma za afya tu. Kwa hiyo, hayo tunategemea kuja katika Bunge lako Tukufu mwezi Septemba ili tuweze kufanya marekebisho haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Kamati kwamba hatuwezi kufikisha lengo la pili na la tatu la kuhakikisha tunatokomeza UKIMWI kama hatutatimiza lengo la kwanza ambalo sasa hivi takwimu rasmi za *NBS* zinaonyesha kwamba ni asilimia 51. Takwimu rasmi za programu data tunaonyesha kwamba watu ambao wanaishi na Virusi vya UKIMWI na wanajua hali yao ni asilimia 75. Kwa hiyo, sina shaka kwamba tukifanya haya marekebisho mawili ya kuruhusu watu kujipima UKIMWI na watoto kuruhusiwa kujipima bila ridhaa ya wazazi/walezi kwa sababu wanaolewa kwenye miaka 15 au 16 tutaweza kuongeza kasi ya kupambana na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tano ambalo limeongelewa na Kamati ni suala la afya ya usafi na mazingira kwamba tushirikiane na Wizara ya Maji, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Tumepokea yote haya na ni kweli nikiwa kama Waziri ambaye nasimamia sekta ya afya, tunaona mzigo mkubwa wa wagonjwa, takribani katika kila wagonjwa 100 wanaohudhuria *OPD* kwa maana ya wagonjwa wasio wa kulazwa asilimia 60 ni magonjwa haya yanayotokana na suala zima la usafi. Pia tuna taarifa ya Benki ya Dunia ambayo imeonesha kwamba Tanzania tunapoteza takriban shilingi bilioni 400 kila mwaka kutokana na hali duni ya usafi. Kwa hiyo, tumepokea ushauri kuhusiana na hali duni ya usafi na tutayafanyia kazi masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la sita ambalo limezungumzwa na Kamati kwa upande wa Fungu 52 ni huduma za lishe. Tunalipokea na sisi tutaendelea kuhamasisha wananchi kuhakikisha kwamba wanazingatia lishe bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende katika hoja zilizoletwa na Kamati kwa upande wa Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii na kubwa lilikuwa Serikali ihakikishe kwamba Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii inatengewa fedha kwa ajili ya kufanya kazi za maendeleo na ustawi wa jamii. Tumepokea ushauri huu na naamini Mheshimiwa Dkt. Mpango ananisikia kwamba Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii nao wana mchango mkubwa katika kuhakikisha tunajenga Tanzania ya Uchumi wa Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge, hata juzi nimeongea na Watendaji wa Wizara, Wizara hii ni moja, kwa hiyo, lazima sasa tuoneshe kwamba hakuna *Vote* ya Maendeleo ya Jamii ya Jamii au *Vote* ya Afya, bali ni Wizara moja. Kwa hiyo, tunaona Sekta ya Afya inapata rasilimali nyingi kutoka kwa wadau, kwa hiyo, tumeamua tutakuwa tunakata asimilia ya fedha za wadau ambazo tunazipata kwenye Sekta ya Afya, tutazipeleka kwenye Sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kubwa ambalo lilitolewa sasa na Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Kuna jambo moja naomba niliseme, hii hotuba ukisoma, kuna maneno mengine unasema, hivi huyu ni Mtanzania ambaye yuko Tanzania au yuko nje ya nchi, anazungumza mambo ambayo hajui nini kinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu anasema, anasema majigambo ya Serikali kwamba imeboresha sekta ya afya nchini ni kutafuta umaarufu wa kisiasa. Hivi unajuliza hivi huyu, anajua analolisema au basi tu anataka kusema ili aweze kusikika anaposema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, binadamu mwema ni yule mwenye kushukuru, lakini pia kazi kubwa imefanyika chini ya Utawala wa Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, shida iko wapi Mheshimiwa Esther Matiko tafadhali, hajakutaja wewe anaongea kwenye hotuba, kwa nini usimpe muda azungumze amalize, kwa nini usimpe nafasi azungumze? Tafadhali Mheshimiwa Esther Matiko, hii ni mara ya mwisho nakutaja jina humu ndani, tafadhali. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema huduma za afya zimeboreka hatutafuti umaarufu wa kisiasa, bali ndiyo ukweli.

Naomba nitoe mifano kama minne, wakati Mheshimiwa Dkt. Magufuli anaingia madarakani, watoto waliokuwa wanapata chanjo ni chini ya asilimia 85, leo asilimia 99 ya watoto wote wenye umri wa chini ya mwaka mmoja wanapata chanjo na nieleze ni halmashauri gani imekosa chanjo za watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati naingia, wazazi wamejifungua watoto hawana chanjo za kuwazuia na kifaduro, kifua kikuu, leo chanjo zinapatikana za watoto katika kila watoto 100, watoto 99 wanapata chanjo. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, katika huduma za matibabu ya kibingwa, Wabunge wameona, kabla Mheshimiwa Dkt. Magufuli hajaingia madarakani, niambieni kama kulikuwa na upandikizaji wa figo, niambieni kama kulikuwa na upandikizaji wa vifaa vya kuweza kusikia, lakini leo hadi ninaposema kuanzia mwaka 2017, Watanzania 38 wameweza kupandikiwa figo katika Hospitali yetu ya Taifa Muhimbili; Watanzania saba wameweza kupandikiwa figo katika Hospitali yetu ya Benjamin Mkapa. Hawa Watanzania, hawawezi kusema ni umaarufu wa kisiasa, ila wanamshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu amewezesha huduma hizi kupatikana na zingekuwa zinapatikana nje ya nchi, wasingeweza kutoa milioni 100, milioni 120 kupata huduma hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *cochlear implant*, upandikizaji watoto wa vifaa vya kuwasaidia kusikia, havijawahi kufanyika, vimefanyika wakati wa Mheshimiwa Dkt. Magufuli, watoto 21 wamefanyiwa. Sasa unajiliza, hivi huyu anaposema ni umaarufu wa kisiasa, nadhani tumsamehe bure. Hivi anaposema ni umaarufu wa kisiasa, anaandika kwenye *speech*, umaarufu wa kisiasa, watoto 21 wamepandikiwa vifaa vya kuwasaidia kusikia! *cochlear*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kutoa mifano, *health centers*, vituo vya afya 352 vinaboreshwa na vimekamilika, tuna Hospitali za Wilaya 67 zinaendelea kujengwa, lakini pamoja na msomaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, ana Kituo cha Afya kinaitwa Magena kimepata milioni 400. Halafu atasema ni umaarufu wa kisiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema, yapo mambo makubwa ambayo yamefanywa na Serikali ya Awamu ya Tano na kwa kiasi kikubwa huduma za afya zimeboreshwa. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kukiri kwamba, changamoto za afya bado ni nyingi na tutaendelea kuzifanyia kazi, lakini lazima tushukuru mambo makubwa na mazuri ambayo yamefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tena nimalize, suala la pili, ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani imehoji, kwamba bajeti ya afya imepungua kutoka shilingi trilioni moja hadi shilingi bilioni 866, lakini pia tunategemea fedha za wazungu. Kwa hiyo, hawa hawa Wabunge ndiyo wamekuwa wakituambia tupunguze utegemezi wa wahisani! Kwa hiyo, kilichopungua, Mheshimiwa Dkt. Mpango ni shahidi, tumepunguza fedha zilizotoka kwa wahisani, lakini fedha za ndani ya nchi, fedha za walipa kodi wa Tanzania, zimeendelea kuongezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia bajeti ya mwaka 2017/18 ilikuwa bilioni 628, lakini mwaka 2018/2019 bilioni 681; mwaka 2019/2020 bilioni 686.6, kwa hiyo, unazona fedha za ndani zinaendelea kukua, lakini ni kweli fedha za nje tumepunguza! Tulianza mwaka 2017/2018 ilikuwa ni bilioni 449, tumepunguza mpaka bilioni 184 na mwaka huu tunaomba fedha za nje bilioni 272. Kwa hiyo, inategemea unaliangalia kwa *perspective* gani, lakini kama ni kuongeza fedha za ndani, hakuna fedha ya afya ambayo imepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna swali pia limezungumzwa na Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu suala la PPP, hilo sisi niseme tulishaanza kulifanyia kazi na kwa mfano katika kufunga mashine za kupima maambukizi ya damu, tumeweza pia kuingia mikataba na mdau ambaye amefunga mashine hatutumii fedha za Serikali, lakini pia tumetangaza tenda ya kuweza kuhakikisha tunafunga vifaatiba bila kutumia fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limeelezwa na Kambi Rasmi ya Upinzani ni suala la huduma ya afya bila malipo kwa wanawake, lakini pia tumewasikia, suala la Wakunga wa Jadi kwamba wamezuiliwa. Tulichokitaka, siyo kuwazuia Wakunga wa Jadi, tunaendelea kutambua na kuthamini mchango wa Wakunga wa Jadi kama wadau wakubwa wa huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto. Sasa tunachokifanya, tunataka hawa watu wawe kama ni daraja letu kati ya vituo vya kutoa huduma za afya pamoja na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunasema kwamba Wizara itaendelea kuwaelimisha Wakunga wa Jadi kuhusu umuhimu wa kuwashauri wajawazito kwenda katika vituo vya kutolea huduma mapema ili kupata huduma bora na salama za kujifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hayo ndiyo makubwa ambayo ningetaka kuyajibu kutoka kwenye Kambi Rasmi ya Upinzani, lakini mengine yote tunakubaliana na wao, ikiwemo kuendelea, kuhakikisha tunatumia *Community Health Workers*, amezungumza Mheshimiwa Kandege kwamba changamoto ambayo tunaipata na kuna baadhi ya Wabunge wametoa mfano, kuna vituo vya afya vinaongozwa na *Medical Attendant* (Mhudumu wa Afya), lakini kuna vituo vya afya unakuta vinaongozwa na Wauguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo sasa ndiyo tunajaribu kuweka *balance*, uwiano. Je, tujaze watumishi wa kwenye *facilities* au twende kwenye *Community Health Worker*, lakini *as a matter of sera*, ikiwa ni suala la kimsingi, tunakubaliana nalo na *especially* mimi katika ajenda yetu ya kuhakikisha tunaongeza hali ya lishe kwa akinamama wajawazito na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano, lakini pia tunaongeza watu ambao wanajua maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na katika mapambano ya kifua kikuu tunaamini kwamba wahudumu wa afya ngazi ya jamii watato mchango mkubwa. Tunategemea kuajiri takriban 600 kupitia fedha ya Mfuko wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na *Malaria*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zilizoelezwa ni nyingi, ikiwemo uboreshaji wa huduma katika ngazi zote tumepokea na lengo letu kwa kweli tunataka kutoka kwenye bora huduma twende huduma bora na ndiyo maana Wizara ya Afya tunayo idara ya kusimamia uhakiki wa ubora wa huduma za afya. Kwa hiyo, tutahakikisha kinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunakusudia kutoa usajili wa vituo vya kutoa huduma za afya vya Serikali na binafsi. Lengo letu tukiona, hata cha Serikali tukikiona hakina ubora,

tunataka kukifungia kama vile tunavyofungia vituo vya afya vya binafsi. Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo tumekubaliana kwamba tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la vifaa na vifaatiba kwa ajili ya vituo vya afya vilivyoboresha, Mheshimiwa Naibu Waziri ameongea kwamba tumeanza kununua lakini tutahakikisha kwamba, kwa sababu hata zoezi hili la kukarabati vituo vya afya, lilienda kwa awamu, kwa hiyo niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tutahakikisha tunanunua vifaatiba na kuvifunga katika vituo vya afya vilivyoboreshwa ili viweze kutoa huduma bora zilizokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lilikuwa wazo, hoja ambazo pia zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge ni suala la *X-Ray machines*; wengi wameeleza kwamba hazifanyi kazi au ni za zamani. Naendelea kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba tumeshaagiza *x-rays* takriban 70 za kisasa, kwa hiyo, tutazisambaza katika Hosptali za Rufaa za Mikoa, lakini pia katika Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mzee wangu Deo Sanga, nimemsikia kuhusu Makambako, nakubaliana na yeye, hata kama ni kituo cha afya, kwa kweli tutahakikisha kwamba anapata *x-ray* ili kuweza kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kumezungumzwa suala la *ambulance*, Waheshimiwa Wabunge tumewasikia sana na tulikuwa tunaongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa, mahitaji ya *ambulance* ni mengi, lakini kama nilivyoeleza katika hotuba yangu, tayari tumeagiza *ambulances* 50, kwa hiyo tutazigawa katika maeneo yenye uhitaji, lakini tutaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kugawa *ambulance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza, nizungumzie suala ambalo pia limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge, kwamba maiti anachajiwa, anadaiwa sijui. Kwa kweli, tunapata changamoto, lakini naomba Waheshimiwa Wabunge watuelewe, angalau

katika Tanzania na hasa Hospitali yetu ya Taifa Muhimbili, kipaumbele wanakiweka kwa mgonjwa kupata huduma. Maana bora mtu angekufa kwamba kakosa huduma, lakini mtu kwanza anapata huduma, akishapata huduma ndiyo linakuja suala la deni. Nilikuwa naongea na Profesa Museru, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali yetu ya Taifa, Muhimbili, amenieleza, Mheshimiwa Waziri ambao wanakuja kwako pia, saa nyingine hawafuati taratibu. Kwa hiyo, nitoe rai kwa Watanzania, kwanza kuhakikisha tunawekeza kwenye afya zetu kwa kukata bima ya afya, lakini pale ambapo hatuna uwezo wa kulipia, basi tufuate utaratibu wa kupata matibabu bila malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazo takwimu hapa, tukiangalia Hospitali ya Taifa Muhimbili, kuanzia Julai mpaka Disemba, iliweza kutoa msamaha kwa wagonjwa wenye thamani ya shilingi bilioni 2.7, kwa hiyo, watu wanasamehewa. Vile vile tukiangalia Hospitali ya *MOI*, Julai hadi Desemba, ilitoa msamaha kwa wagonjwa wenye thamani ya shilingi milioni 347. Tukiangalia Mloganzila Julai hadi Desemba, 2018 walitoa msamaha kwa wagonjwa wenye thamani ya shilingi milioni 178.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazo takwimu mpaka za Hospitali zetu za Rufaa za Mikoa, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunaomba watuelewe, hapo hapo tunahitaji kuboresha huduma, sasa tukisema tu jamani kila kitu bure bure, jamani bure, bure ni gharama, bure ni gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena bure ni gharama, kwa hiyo muhimu tuendelee kuhakikisha kwamba, kwanza tunawekeza kwenye afya zetu, lakini pili pia tunafuata taratibu katika kupata huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze suala moja ambalo limeongelewa na Mheshimiwa dada yangu Taska Mbogo, kuhusu *Customary Declaration Order*, ni ya zamani na kandamizi na inabagua wanawake. Nakubaliana sana na Mheshimiwa Mbogo, kwamba sheria hii ni ya zamani, lakini kuna maamuzi ya Mahakama Kuu kwenye Kesi Na. 82

ya mwaka 2005 ambayo inatambulikana kama Elizabeth Stephen na mwenzake dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambayo ilitolewa maamuzi tarehe 8 Mwezi wa Tisa mwaka 2006, mbele ya Majaji watatu wa Mahakama Kuu kuwa, Serikali imeweka kifungu cha 12 cha Sheria ya *Judicature and Application of Laws Act*, ambacho kinamtaka mtu yeyote atakayeona kuna mila kandamizi inayomzuia kupata haki yake, kufuata utaratibu uliowekwa katika kifungu hicho kwa kuwasilisha maombi ya kubatilisha mila hiyo kupitia Waziri wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba kusema hii ni changamoto. Dada yangu Mheshimiwa Taska Mbogo, naomba nilichukue, tutakwenda kulifanyia kazi ili kuhakikisha ikiwezekana tunafuta sheria hii. Kwa sababu hoja ambayo ipo ni kwamba kuna baadhi ya mila zetu ambazo zimo ndani ya sheria hii siyo mbaya, za kutunza wazee na watoto wa ndugu. Kwa hiyo, tutaangalie yale ambayo yanamkandamiza mwanamke tutaweza kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mdogo wangu Mheshimiwa Amina Mollel amezungumzia suala la unyanyasaji wa wasichana hasa wanaosoma katika vyuo vya elimu ya juu. Sera ya Usawa wa Jinsia na Maendeleo ya Wanawake inahimiza kuanzishwa kwa Madawati ya Jinsia katika Taasisi, Wizara na Idara za Serikali. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuvitaka vyuo vya elimu ya juu nchini kuanzisha Madawati ya Jinsia ili kuweza kushughulikia changamoto mbalimbali za jinsia ikiwemo vitendo vya ukatili na unyanyasaji dhidi ya wanafunzi katika vyuo vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipongeze sana jitihada za Kamishna Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ambaye ameanzisha Dawati la Jinsia ndani ya *TAKUKURU* ili kuweza kupambana na rushwa ya ngono. Kwa hiyo, nitoe pia wito kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu juu ambao wananyanyaswa au wanakumbana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kuhakikisha kwamba wanatoa taarifa katika Dawati hili la Jinsia ambalo limeanzishwa mwaka huu chini ya *TAKUKURU*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, hoja ambazo zimeongelewa ni nyingi lakini kipekee niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge wa kutoka Mikoa mipya ya Katavi, Songwe, Njombe, Simiyu na Geita kwamba kipaumbele chetu kama Wizara tumekubaliana mwaka huu ni kukamilisha Hospitali za Rufaa za Mikoa ili ziweze kutoa huduma za rufaa katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika Mkoa wa Singida na Shinyanga, mdogo wangu Mheshimiwa Aisharose Matembe na ndugu yangu Mheshimiwa Azza Hillal, kama Wizara tumejipanga kuhakikisha tunakamilisha ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa. Lengo ni ili sasa tuweze kukabidhi Hospitali ya Shinyanga kwa Manispaa ya Shinyanga, pia tukabidhi Hospitali ya Singida kwa Manispaa ya Singida. Kwa hiyo, mdogo wangu Mheshimiwa Aisharose na ndugu yangu Mheshimiwa Azza Hillal tunataka kuwathibitishia kwamba jambo hili pia tutalikamilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hospitali nyingine za Rufaa za Mikoa kama tulivyosema tumezipokea kuanzia tarehe 1 Julai 2018. Tunachokifanya, tumeamua kuwekeza katika maeneo makubwa manne. Eneo la kwanza ni kuhakikisha tunakuwa na miundombinu ya kutoa huduma kwa wagonjwa wa dharura na ajali (*emergence medicine*) na tayari tumeanza kupata fedha kutoka *Global Fund* tutaanza kuweka vitengo vya dharura katika hospitali saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni kuweka huduma za *ICU*, huduma kwa wagonjwa wanaotaka uangalizi maalum. Huduma hii tutafanya pia katika hospitali zote za Rufaa za Mikoa. Eneo la tatu ni kuboresha huduma za uzazi. Eneo la nne tunataka kuhakikisha tunaweka Madaktari Bingwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa yote. Tumbainisha maeneo nane ya kipaumbele, tunataka kuhakikisha tuna Madaktari Bingwa wa magonjwa ya uzazi na wanawake angalau wawili, magonjwa ya watoto angalau wawili, upasuaji angalau wawili, upasuaji wa mifupa angalau wawili, usingizi na radiolojia na magonjwa ya ndani (*internal medicine*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hayo ni maeneo ambayo tumeyabainisha na tutahakikisha kwamba kila Hospitali za Rufaa za Mikoa zinakuwa na wataalam hawa. Kama alivyosema Naibu Waziri tayari tumeanza kusomesha madaktari na ili tuweze kukupa ufadhili wa kusoma *masters* ya udaktari tutawafungisha mkataba ili wakimaliza waweze kufanya kazi katika Hospitali zetu za Rufaa za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mambo ni mengi lakini kwa kweli kipee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, asiye na macho haambiwi tazama, kazi kubwa na nzuri imefanyika katika utoaji wahuduma za afya. Mimi niseme tutaendelea kuhakikisha tunatimiza ndoto yake ya kuifanya Tanzania ya viwanda kwa kuboresha huduma za afya kwa kuhakikisha kwamba Watanzania wanakuwa na afya bora badala ya kusubiri kwenye mambo ya tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge tumewasikia, Mzee wangu Mheshimiwa Lubeleje tumekusikia, tunataka na sisi tuondoke kwenye taifa la kulilia dawa, dawa, lakini liwe ni taifa la kulilia afya na lishe bora. Kwa hiyo, jambo hili pia tutalifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais, mama Samia Suluhu Hassan ambaye kwa kweli amekuwa akinipa msaada mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Namshukuru sana mama Samia katika kuimarisha afya ya uzazi ya mama na mtoto. Mheshimiwa dada yangu Mariam Kisangi ameonesha, watu wanaosema hakuna mabadiliko, Hospitali ya Mkoa wa Rufaa ya Temeke hakuna kifo kimetokea mwezi Machi, mama Kisangi ni shahidi na watu wanaona. Halafu watu wanasema hakuna kazi imefanyika, kazi imeonekana ndiyo maana hakuna vifo vya akina mama wajawazito.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa uongozi wake mahiri na nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote. Kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Naibu



Waziri kwa mchango mkubwa sana ambao ananipatia.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi niliambiwa unajua hawa madaktari wanaweza wakadharau lakini Naibu Waziri amekuwa akinipa mchango na heshima kubwa katika utendaji wa kazi zangu. Mheshimiwa Naibu Waziri nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimshukuru pia Katibu Mkuu (Afya), Dkt. Zainabu Chaula. Kwa kweli tunafurahi sana kama Wizara ya Afya tumepata mama ambaye anajua kusukuma mambo na anajua kusimamia utendaji katika Wizara ya Afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru sana Dkt. John Jingu ambaye naye ni Katibu Mkuu, Maendeleo ya Jamiii kwa kazi kubwa na nzuri ambayo amefanya katika kusimamia Sekta ya Maendeleo ya Jamii. Tunamshukuru sana pia Mganga Mkuu wa Serikali na madaktari wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili tunawashukuru madaktari, wauguzi na watoa huduma za afya nchini. Hapa naongea kama Waziri wa Afya, nitoe maelekezo na maagizo kwa viongozi wenzangu, tuache kuingilia fani za kitaaluma.  
(*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna daktari au muuguzi amekosea ashughulikiwe kwa mujibu wa taratibu za Utumishi wa Umma. Narudia tena, kama kuna daktari amekosea tulateeni kwenye Baraza la Madaktari, tutafuta usajili wake. Kama kuna muuguzi amekosa tulateeni kwenye Baraza la Wauuguzi na Wakunga tutafuta usajili wake. Kama kuna mfamasia amekosea tulateeni kwenye Baraza la Wafamasia ambalo ndiyo limeanzishwa kisheria kushughulikia changamoto kama hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka mitatu ambayo nimekaa katika sekta ya afya, Naibu Waziri ameongea, kazi ya wauguzi watano inafanywa na muuguzi mmoja halafu

bado huwezi ku-*appreciate* (kuthamini)? Madaktari hawa wanajituma sana, kwa kweli lazima tutambue mchango wao na tuheshimu kazi kazi yao nzuri. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi na Naibu Waziri tutaendelea kuwatetea madaktari na wauguzi wetu kwa sababu mwisho wa siku wanaopata matatizo ni Watanzania wanyonge. Mwenye hela zake haendi kwenye hospitali ya Serikali au kituo cha afya cha Serikali. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli inatia uchungu, sisi ambao tuko kwenye sekta hii tunaelewa changamoto ambazo watoa huduma za afya wanapata. Kwa hiyo, sisemi kwamba wote ni malaika au ni wazuri, hapana, wapo wabaya lakini tufuate taratibu za kuwawajibisha watumishi watoa huduma za afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mkubwa na mzuri ambao wamekuwa wakinipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Kipekee, nawashukuru wadau wetu wa maendeleo hususani wanaochangia Mfuko wa Afya wa Pamoja ambao ni Denmark, Canada, *KOICA*, *UNICEF* na *World Bank*, nadhani nimewamaliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru na wadau wengine ambao hawachangii kwenye Mfuko wa Afya lakini mchango wao ni mkubwa ikiwemo *Global Fund*, Mfuko wa Rais wa Marekani wa Kupambana na UKIMWI pamoja na watu wa GAVI, *Abbott Fund* wote hao wanatusaidia, pamoja mashirika yasiyo ya kiserikali na mashirika ya dini.

Nawashukuru sana Wakuu wa Taasisi na Idara za Serikali, Hospitali zetu za Taifa Muhimbili, Bugando, Jakaya Kikwete, *Ocean Road*, *MOI*, Benjamini Mkapa na hospitali nyingine zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niwaambie Waheshimiwa Wabunge tutajibu hoja zenu zote kwa maandishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana, Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 52 - Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

Kif.1001 - *Administration Human Resources Management*.....Sh. 8,450,857,436/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu hiki ndiyo kifungu chenye mshahara wa Waziri. Nimeletewa majina hapa kwa mujibu wa Kanuni zetu tena watu ambao wanataka ufafanuzi kwenye kifungu hiki. Tutaanza na Mheshimiwa Oscar Mukasa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi hoja yangu nataka *commitment* ya Serikali tena ya muda mfupi ya kufanya mapitio ya Sera ya Lishe kwa sababu imepitwa na wakati lakini pia haijumuishi sekta zote kwenye kupambana na utapiamlo na mambo mengine yanayoendana na lishe. Utakumbuka kwenye mchango wangu nilitoa takwimu hapa zinaonesha *risk factors* au visababishi vya vifo na ulemavu *malnutrition* ndiyo inaongoza pamoja na kwamba tunafanya vizuri sana kwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakusudia kushika shilingi ya Waziri endapo sitapata maelezo ya kuridhisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Oscar Mukasa. Kwa kweli nakubaliana na hoja yake lakini ningemwomba kwa kuwa sasa hivi Wizara inatengeneza Sera mpya ya Afya kwa sababu tumekuwa na Sera nyingi mwisho wa siku utekelezaji umekuwa siyo mzuri. Kwa hiyo, tumekubaliana na *single health care policy* ya Tanzania ambapo tutaweka *specific chapter* kwa ajili ya masuala la lishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tayari kuna *Multisectoral National Strategy* kuboresha hali ya lishe, kwa hiyo, mimi badala kutengeneza Sera tu ya Lishe, kwa sababu lishe ni jambo mtambuka, linahusisha sekta nyingi, kwa hiyo, kwenye Sekta ya Afya tutengeneze hiyo *policy statement* kuhusu lishe lakini tutakuja sasa na mkakati wa kitaifa ambao utakuwa ni *multisectoral* wa kuweza ku-*address* masuala ya lishe. Nakubaliana naye kwamba kwa kweli kiwango cha lishe nchini kwetu hasa kwa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano na akina mama wajawazito hakiko vizuri, kwa hiyo, tunahitaji kuongeza jitihada.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mukasa, naona umesimama.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi utayari wa Mheshimiwa Waziri lakini napata shida tunapishana tena pale anaposema tuwe na Sera moja ya Afya ambayo na lishe ni sehemu mojawapo hapo tunazua tatizo lingine...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mukasa, katika hatua hii kama umekubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri utakuwa umekubaliana nayo, kama hukubaliana nayo unatoa hoja ili uungwe mkono.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja ya kushika shilingi, sikubaliani naye.

**MWENYEKITI:** Hoja haijaungwa mkono. *(Kicheko)*

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imeungwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, waendeleo kusimama wale wanaotaka kuchangia kwenye hoja hii. Mheshimiwa Vulu, Mheshimiwa Kemilembe Lwota, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Kitandula na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Tuanze na Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu.

**MHE. ZAYNABU MATITU VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi sina haja ya kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri lakini hoja yangu ni kwamba hili suala la sera ni muhimu na umuhimu wake ni kwamba Wizara ya Afya peke yake hawawezi wakalitekeleza peke yao kwa sababu ni suala la mtambuka, kuna haja ya kuunganisha na Wizara nyingine, Wizara ya Maji, Wizara ya Afya yenyewe, TAMISEMI, Elimu, Kilimo, hata Wizara ya Kilimo na wenyewe wanapaswa wawepo. Kwa hiyo, ningepomba suala hili kama itawezekana ijumuishe Wizara hizo zote na litengenezwe, Wizara ya Afya inaweza ikachukua asilimia 20...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele imegonga Mheshimiwa, sasa hatujajua unaunga mkono hoja ama huungi mkono hoja ya Mheshimiwa Mukasa, neno moja tu.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja ya Mheshimiwa Mukasa lakini si kwa maana ya kutoa shilingi ya Waziri. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vulu, kote ni kuunga mkono tu, ukishasema unaunga mkono maana yake unaunga mkono. *(Kicheko)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Kemilembe Lwota.

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mukasa kwa sababu kiukweli kabisa suala lishe ni muhimu sana katika nchi yetu na ni bomu ambalo tunatengeneza litakuja kuwa tatizo kubwa sana siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha Nyanda za Juu Kusini ambako ndiyo kuna chakula kingi lakini bado tuna tatizo kubwa sana kwenye utapiamlo. Hili suala linaanzia kuanzia kwa akina mama wajawazito mpaka umri wa miaka mitano ambao Mheshimiwa Waziri amezungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi namwomba Mheshimiwa Waziri isiwe *chapter* moja kwa sababu ni suala kubwa na mtambuka. Nashauri itengenezwe sera ambayo itasimamia lishe kwa ujumla nchini kwetu. Nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tukiendelea na michango, tujikumbushe tu sisi wenyewe michango yetu tunazungumza kana kwamba hii sera haiwezi kutengezwa na Wizara ya Afya peke yake, wakati tukijadili hapa navyosikiliza. Kwa hiyo, hata tunaposema tunaunga mkono ile hoja ya kwamba kuwe na sera moja kwa ajili tu ya lishe halafu Waziri wa Afya ndiyo aseme maana yake Mawaziri wote tunaowataja wote wakakae pamoja.

Tunaendelea na Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mukasa na naomba Serikali iiangalie kwa upana wake. Yeye alichoomba ni *commitment* kwamba badala ya kufuata utaratibu wa kawaida ambao utachukua muda mrefu atupe muda maalum kwamba ndani ya muda fulani Serikali itaweza kukaa na kuhakikisha Wizara zote ambazo zinahusika katika suala hili zima la lishe liweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama Wizara ya Afya itakuwa inasimamia jambo hilo lakini Wizara zote ambazo ni mtambuka ambazo zinashughulikia suala hilo wote wahusike pamoja kwa sababu ni tatizo kubwa kuliko mambo mengine yote. Kinga ni bora kuliko tiba. Ni vizuri tuwekeze kwenye kinga na Wizara zote zihusike, gharama itakuwa ni ndogo kuliko huko tunakoelekea kwenye tiba. Kwa hiyo, naunga mkono hoja yake ifanyiwe kazi haraka. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, hili suala la lishe ni mtambuka, liko Kilimo, liko Elimu, liko TAMISEMI, liko kote na Taifa lijalo litakuwa na viwatu vimedumaa. Sisi hapa wote tulikuwa na lishe bora ndiyo maana tuko namna hii na mbaya zaidi sasa hiyo asilimia ya watoto wa umri wa miaka mitano inafika asilimia 34 ya Tanzania katika *data* zile za mwaka 2015/2016 sijaona hizi za karibuni za 2017/2018. Sasa kama halitafanyiwakazi mapema tukisema tu ni sera ni sera na elimu kule hawana, watu hao hao lishe ni duni hata walio darasani wanapelekewa Uji tu na Maharage bila chochote, hivi kweli tutakuwa na Taifa lenye nguvu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni la haraka na dharura, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naungana na Mheshimiwa Mukasa kwamba iko haja ya kuwa na *a standalone policy* ya lishe na sababu ni nini? Sababu ni kwamba jambo hili ni *cross cutting* lakini tuna wasiwasi kwamba likiachwa hivi lilivyo kwamba lika-*appear* kama *chapter* moja tu kwenye Sera jumuiishi linaweza kusababisha matatizo makubwa na maeneo mengine yakasahaulika hasa tukizingatia kwamba *intervention* zinazotokana na sekta ya afya peke yake zina-*solve* tatizo hili kwa asilimia 20 tu, asilimia 80 inatokana na maeneo

mengine kwa hiyo ipo haja ya kulifikiria vizuri eneo hilo.  
(Makofi)

**MWENYEKITI:** Nadhani tunarudi pale pale asilimia 20 ndiyo tunashikia mshahara leo siyo? Asilimia 80? Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Afya kwa kulisemea hili vizuri lakini niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa kulizungumza jambo la lishe kama ni jambo la kipaumbele katika Taifa letu. Lakini niwapongeze pia Waheshimiwa Wabunge wameona kwamba jambo hili la lishe ni jambo mtambuka, siyo jambo ambalo linaweza likachukuliwa na sekta moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu nikuhakikishie kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu kama Ofisi ambayo imepewa jukumu la kuratibu sera zote kaatika Taifa letu tayari imeshaliona jambo hili kama ni jambo la msingi kabisa. Ndiyo maana kwa kuanzia ili kuzikutanisha sekta zote kwa pamoja tayari Ofisi ya Waziri Mkuu imeshatengeneza mkakati wa Kitaifa wa kupambana na tatizo la lishe nchini ambapo mkakati huo unaunganisha sekta zote ikiwemo sekta ya afya, sekta ya kilimo na sekta nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuelewa Mheshimiwa Oscar anaona katika Wizara hii ya Afya labda Waziri ndiyo angefanya *commitment* lakini akifanya *commitment* Waziri wa Afya peke yake kuwa na sera kwenye sekta ya afya haitatutoa kwenye tatizo ambalo tukonalo. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu, waratibu wa sekta na waratibu wa mambo yote ambayo yanatakiwa kuratibiwa na sekta zote tunalibeba jambo hili kama ni jambo la msingi ili tulifanyiekazi na kupata majibu ya pamoja kwa Taifa zima. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo nimuombe sana Mheshimiwa Oscar Mukasa kwa sababu Serikali inaona



umhimu wa lishe bora nchini na inatambua kufanya *coordination* ya sekta zote ili kutatua tatizo la lishe amuachie Mheshimiwa Waziri shilingi yake na siis kama Ofisi ya Waziri Mkuu tuendeleo kuliratibu jambo hili na mwisho wa siku tuwe na Sera ambayo itasaidia ku-*coordinate* sekta zote kupambana na tatiz la lishe nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oscar Mukasa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nawashukuru pia Mheshimiwa Ummy, Mheshimiwa Jenista na wachangiaji wengine wote, Mheshimiwa Kitandula na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema vizuri sana mwishoni hapa Mheshimiwa Jenista ingawa hata Mheshimiwa Ummy amasema vizuri yeye alikuwa anasema kwa upande wake wa sekta ya afya lakini nianze na mfano; UKIMWI ni jambo mtambuka, Sheria iko Wizara ya Afya, Sera iko Ofisi ya Waziri Mkuu na ndiyo maana tunafanya vizuri. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Jenista kwamba tupokee hiyo *commitment* tukazungumze tuone ili kuiweka kwenye Sheria moja ya afya ukilinganisha na kuiweka kama jambo mtambuka kwa pamoja tukubaliane tunatoka vipi. Kwa hiyo, naiachia shilingi, naomba tuendeleo lakini Serikali tuzungumze basi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nadhani Mheshimiwa Waziri wa Afya hiyo haiondoi umuhimu wa kuweka vifungu mahususi vinavyohusu Wizara yako. Mheshimiwa Mwitwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kupata ufafanuzi. Naomba kupata ufafanuzi; *center* ya kugawa madawa katika nchi yetu iko kwenye Shirika letu la *MSD* lakini Shirika hili sasa linadai kulipwa hela nyingi sana kutoka Serikalini karibu bilioni 222. Hivi karibuni, Shirika hili la *MSD* limepata heshima ya kutoa

huduma ya vifaa tiba katika Nchi 16 za *SADC*, ni heshima kubwa ambayo nchi yetu imepata kupitia Shirika hili lakini tusisahau Shirika hili limesifiwa na *CAG* na pia Mheshimiwa Rais amelisifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika hili hivi karibuni limepewa jukumu la kununua, kugawa na kutoa vifaatiba katika vituo vyote vya afya vinavyojengwa nchi nzima. Shirika hili pia ndilo linalo-*determine* madawa yetu katika Nchi nzima kwamba yanakwenda vizuri katika maeneo haya. Sasa naomba *commitment* ya Serikali, ni lini sasa litalipwa hizo hela zinazodai karibu bilioni 22? Nisipopata maelezo ya kutosha nitaingia kwenye kutoa mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere hili jambo kwa mujibu wa Kanuni zetu kwa sababu umetoa maelezo marefu nitampa Mheshimiwa Waziri fursa ya kuzungumza lakini siyo jambo linaloweza kuzungumzwa kwenye kifungu hiki kwa sababu wewe umeuliza swali na umeuliza swali kuhusu malipo kwa *MSD* ambayo umeyataja kabisa ni kiasi gani kwa hiyo siyo jambo ambalo Kikanuni unaweza kuuliza kwa namna hiyo. Pengine Mheshimiwa Naibu Waziri unataka kutoa ufafanuzi? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii imeendelea kuwekeza katika Bohari hii ya dawa na bajeti ya dawa imeongezeka kutoka bilioni 31 Mwaka 2015/2016 hadi kufikia bilioni 270 katika Mwaka huu wa fedha.

Tunatambua kweli kulikuwa na deni hili la *MSD*, na sisi kama Serikali kupitia hazina wamefanya uhakiki wa hili deni na Serikali kupitia hazina wameendelea kulilipa hili deni kadri uwezo wa Serikali uliopo na labda nimtoe shaka tu kwamba uwepo wa hili hauathiri utendaji wa *MSD* kwa maana ya upatikanaji wa dawa hapa nchini lakini hautaathiri hali ya upatikanaji wa dawa katika Bara zima na nchi za *SADC*. Kwa sababu utaratibu wa fedha na ununuzi wa dawa *SADC* hauna muingiliano kabisa na utaratibu wa dawa katika mifumo yetu hapa ndani.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kabla sijakwenda kwenye shilingi yangu ningependa tu kuweka sawa; kwanza nashukuru hotuba yetu umeisifia kwa asilimia 80 ukaponda tu vitu viwili lakini kwenye *maternal mortality* niweke tu data sawa; wewe mwenyewe umekiri kwamba kuanzia 2015 bado hakuna *statistics* tulizonazo lakini 2017/2018 ulituletea hapa taarifa kwamba vizazi vifo vya 2016/2017 ilikuwa ni vifo 444 kwa vizazi hai laki moja, Mwaka jana ukatuambia 556 kwa vizazi hai laki moja ina maana inapanda. Mwaka huu umekula chaka baada ya kuona inapanda *so we judge with that trend*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine bajeti; utekelezaji wa maendeleo asilimia 16 halafu tusiseme kweli? *We are not prayers and worship teams here* tunaisimamia Serikali ifanyekazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya msingi sasa; wazee wa Taifa hili wamelitumia sana Taifa na kwa kweli wanatakiwa kuenziwa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko hilo ni jambo tofauti na hapa inabidi jambo liwe moja sasa umezungumzia habari za uzazi sasa hivi unakwenda Wazee. Ni jambo la uzazi, maliza hoja yako huwezi kurukia wazee ndiyo Kanuni zetu zinavyosema, jambo mahususi moja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema naanza kile alichokuwa amesema sija...

**MWENYEKITI:** Hapana, hapana utakuwa unakosea Kanuni na unafahamu utaratibu Mheshimiwa, hapana. Kama hoja yako ni ya wazee ulitakiwa uende kwenye wazee ndiyo utaratibu. Huwezi kuwa umeanza wewe kuchangia na Kanuni unazijua kwa hiyo nikikupa fursa zungumza habari ya uzazi siyo tena wazee kwa sababu Wazee ni hoja nyingine tofauti na wewe Kanuni unazifahamu.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona mnakimbia majukumu, *anyway I will go with that* uzazi, nitazungumzia vizazi *there is no problem*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vifo vya wakina mama wajawazito na watoto; nikianza tu kwa kuangalia *trend* hata kwenye hiki kitabu cha maendeleo ambacho kimekuja, bajeti iliyotengwa kwa Mwaka 2018/2019 ilikuwa bilioni 12, Mwaka 2019/2020 bilioni tano kwa hiyo hapa nitashika shilingi nisiporidhika. Kwa takwimu ambazo nimezitoa awali na sasa hivi nataka kupata mkakati thabiti wa kupunguza vifo vya mama na watoto kujenga vituo vya afya tu tena vichache kati ya vituo 4000 tulizonazo, mmejenga...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther ngoja tuongozane vizuri kwa sababu kengele imeshagonga, hoja yako ni nini? dakika moja, hoja yako ni nini?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipate mkakati thabiti ambao utakwenda kupunguza vifo vya Mama na mtoto Tanzania na siyo *story*.

**MWENYEKITI:** Hawa Wabunge wa siku nyingi inavyoonekana hizi Kanuni tunahitaji semina. Mheshimiwa Waziri ufafanuzi. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme Mheshimiwa Esther Matiko takwimu za 556 katika kila vizazi hai laki moja ni takwimu rasmi ambazo zimefanywa na Taasisi ya takwimu ya Taifa. Kwa mwaka tuna *deliveries*, tuna wazazi takribani milioni mbili kwa hiyo ukifanya *calculation* ni takribani ni hao hao watu 11,000 kwa Mwaka Wanawake wanafariki kutokana na uzazi na sawa sawa na Wanawake 30 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo bado hakuna mgongano wowote kwenye takwimu lakini nikasema hivi; kwa sababu ya uwekezaji mkubwa ambao Serikali ya Awamu

ya Tano ya Dkt. John Pombe Magufuli imefanya katika kuboresha huduma za uzazi, Mama na mtoto tunategemea ukifanyika utafiti rasmi, Mwaka 2019/2020 tutakuwa na takwimu ambazo ni chache sasa anasema kuna mkakati gani wa Serikali wa kupunguza vifo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema hakukuwepo na vituo, kwanza niseme; asilimia 80 ya wakina Mama wajawazito wanajifungua bila *complication* ni *normal delivery*, asilimia 20 ndiyo wanakuwa na *complication* ndiyo maana tukaboresha vituo vya afya kujenga kitu kinaitwa *SIMOC* ili kuviwezesha kutoa huduma za uzazi wa dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni maana yake mwanamke mjamzito akiwa na tatizo la uzazi pingamizi sasa hivi atapata huduma pale pale katika eneo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika bajeti hii zamani wanawake kwanini wanafariki? Kumwaga damu nyingi. Dawa ya kuzuia mwanamke mjamzito kumwaga damu baada ya kujifungua (*oxytocin*) inapatikana mpaka zahanati Tarime Mjini, zinapatikana bure. Dawa kwa ajili ya wakinamama mjamzito kuzuia kifafa cha mimba (*magnesium sulfate*) zinapatikana bure sasa anataka mikakati gani zaidi ya kuboresha miundombinu, zaidi ya kuhakikisha upatikanaji wa dawa, zaidi ya kuhakikisha tuna wataalam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepeleka wataalam wa kusomea usingizi 200 hospitali zetu za Taifa za Muhimbili, Bugando na MOI kwa ajili ya kujifundisha. Kwa hiyo, mikakati ipo lakini tumeenda mbali tukasema mambo mazuri bado Wanawake wajawazito wanafariki ndiyo maana tukaja na kampeni "jiongeze tuwavushe salama". Kwanza Mama mjamzito mwenyewe ajiongeze, anatakiwa kwenda *clinic* mara tu akijiona mjamzito, aende ngalau mara nne lakini tunataka watoa huduma za afya wajiongeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali changamoto ya vifo vya wakina Mama wajawazito na watoto bado ipo lakini nakuhakikishia kwenye Bunge hili tukifanya utafiti vitapungua zaidi ya asilimia 50. Tunazo takwimu vifo havizidi 3000 sasa

hivi kwa hiyo mikakati ipo tuendeleo kutekeleza. Namuomba Mheshimiwa Esther wifu yangu niachie shilingi yangu tukatekeleze kazi ya kuboresha huduma za uzazi, Mama na mtoto.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika kabisa na majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo amesema ni wifu yangu kwa sababu ni Mwanamke na umetaja vizuri kabisa kwamba *complication* ambazo zinatokana ni *20 percent* sasa *out of 20 percent* wanafariki watu 30 kwa siku...

**MWENYEKITI:** Toa hoja Mheshimiwa ijadiliwe kwa kuwa hujaridhika

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Natoa hoja tu-*discuss* hii kitu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono wabaki wamesimama wanaotaka kuchangia kwenye hoja hii. Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Frank Mwakajoka. Huwezi kupewa hujawahi, kupewa na mimi? Mbona mnakuwa namna hiyo!! Mheshimiwa Mch. Msigwa yaani tuwe tunaheshimiana wewe ushapewa nafasi mara nyingi mbona unakuwa hivyo? Mbona unakuwa na mambo! Wewe! Ulivyozungumza ulitaka usisikiwe? Nimekusikia na umeshapewa mara nyingi na ni kweli leo hupewi, ni kweli leo hutapewa Mheshimiwa kwa hiyo, vumilia tu. Mheshimiwa Bashe

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji Msigwa tumeshalimaliza hilo naomba unyamaze, naomba unyamaze tafadhali, naomba unyamaze. Mheshimiwa Ally Keissy, Mheshimiwa Kigwangala, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya. Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Esther Matiko kuhusu vifo vya Mama na mtoto. Ninachokiona hapa Serikali kwanza inakiri kwamba *NBS* haijafanya utafiti kuanzia Mwaka 2015 leo tunazo *statistical data* kutoka *AMREF* na *SIKKA* zinazoonyesha na sasa hizo ndizo *recent* ya *statistical data* tulizonazo kwamba vifo vya Mama na mtoto vimeongezeka na Waziri anakubali wala hajapinga. Ukiacha hilo nadhani hili ndiyo chanzo cha Serikali kuja na ile idea ya kwamba bila takwimu inayokuwa *approved* na Serikali hatupokei takwimu yoyote kwa sababu na ndiyo anatumia hapa tsubiri 2019/2020 tupate *data* za Serikali. Haya ni Mashirika ya Kimataifa na yameshasema kwamba kifo cha Mama na mtoto kimeongezeka Tanzania. Serikali mpaka...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele imegonga, unaunga mkono hoja ama hapana? Kengele imeshagonga.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimsema tangia mwanzo naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Esther Matiko.

**MWENYEKITI:** Basi ahsante sana. Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kwanza nimeshangaa sana Mheshimiwa Waziri alichokuwa anazungumza hapa maana yake amegoma kwamba hawana takwimu hapa katikati wanatumia takwimu za mwaka 2015.

Lakini ukweli kwenye bajeti ya Mwaka 2016/2017 vifo vya Mama na mtoto viliripotiwa kutokana na taarifa ya Mheshimiwa Waziri, hotuba yake, kati ya vizazi laki moja, vizazi 444 walikuwa wanapoteza maisha. Mwaka jana 2017/2018, kati ya vizazi lakini moja, 556 walikuwa wanapoteza maisha lakini leo wanasema kwamba wana *data* za...kwa hiyo hizi *data* za katikati hapa zilikuwa zinatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunaona bajeti inaendelea kushuka. Mwaka 2017/2018 bajeti ilikuwa juu leo iko bilioni tano peke yake kati ya bilioni kumi na kitu sasa tunasema hivi vifo vya wakinamama na mtoto nani atavipunguza kama Serikali haijaweka mkono kati ya kuhakikisha kwamba jambo hilo linafanyika? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Hussein Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimwombe dada yangu Mheshimiwa Esther amwachie Mheshimiwa Ummy shilingi yake na kwa sababu, tukiwa *fair* kabisa swali la Mheshimiwa Esther ni *very clear*; nini mkakati? Mheshimiwa Ummy amejibu mkakati wa kwanza *as a country* tumefanya *expansion* ya uwepo wa vituo vya afya zaidi ya 300 ambapo mwanzo havikuwepo. Kwa hiyo, ni *service delivery*, imekwenda. Tukitazama bajeti kutokana na Wizara ya Afya peke yake tutakuwa hatuko *fair*. Suala la *health* linahusu TAMISEMI vilevile *how much i-spend* kwenye *health component* kwenye suala la TAMISEMI. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nchi, kuna *plan* ya kuwepo kwa *universal health system*. Kwa hiyo, ina maana huu ni mkakati kwamba tunataka mkakati *globally*, Wizara ya Afya ime-*play a great role*, lakini tunapo-*compare* takwimu mbona tunasahau *component* ya *growth* ya *population* ambayo ina-*grow*? Kwa hiyo, akina mama na wenyewe wataongezeka, hakuna anayeunga mkono mama kupoteza uhai, lakini kama Bunge tunaona *clear plan* inayofanywa na Wizara ya Afya katika eneo hili. *Let us support* Wizara ya Afya na nadhani kama tutakuwa *fair*, Wizara hii imefanya jitihada kubwa sana kuleta *awareness* ya haki ya... (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)



**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Muda umekwisha. Mheshimiwa kengele imegonga. Mheshimiwa Ally Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi simuungi hoja Mheshimiwa Esther Matiko kwa sababu na sisi wenyewe tunachangia vifo wa akina mama na watoto. Haiwezekani mwaka mmoja mimba mbili na ushahidi kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge humu wamo.

Sasa na sisi tuwahamashe nyota ya kijani kwanza. Serikali imejitolea kujenga vituo vya afya na hospitali nchi nzima na Waganga wameajiriwa lakini nasi Wabunge tuhamasishe nyota ya kijani. Haiwezekani! Kuna ushahidi kwa baadhi ya Wabunge humu, mwaka mmoja mimba. Hivyo, tutaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. (*Makofi/kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hatuwezi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigwangalla unasikika wewe, endelea.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hatuwezi kuzungumzia kupungua ama kuongezeka kwa takwimu za vifo vya akinamama wajawazito na watoto katika kipindi hiki kwa sababu *the Tanzania demographic and health survey* huwa inatoka kila baada ya miaka mitano na huu ndiyo utafiti pekee ambao utatupa hali ya sasa ikoje katika Sekta ya Afya nchini. Kwa maana hiyo, utafiti wa mwisho ulifanyika mwaka 2014 na matokeo yakatoka 2015 na yatatoka tena mwaka 2020. Nina uhakika yatakapotoka matokeo ya *Demographic and Health Survey* ya mwaka 2020 lazima tutaona kuna upungufu wa changamoto ambazo zimeonekana kwa sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu mikakati mingi ya kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua imefanyika sana na kasi kubwa zaidi kuanzia mwaka 2016 mpaka leo na mikakati yenyewe ni pamoja na aliyoitaja Mheshimiwa Waziri. Mmojawapo ni huo wa kutoa *oxytocin* wakati akinamama wanaenda kujifungua kuhakikisha kuna damu na akina mama wanaongezewa damu katika vituo vya afya na vile vile ujenzi wa vituo vya afya zaidi ya 350 ambavyo hata kule Tarime tumepeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mikakati hiyo pamoja na kutoa *antibiotics* pamoja na kuhakikisha kuna dawa za kutosha kwenye ngazi ya vituo vya afya, itatusaidia sana ifikapo mwaka 2020 kushusha idadi ya vifo ambavyo vinatokana na uzazi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tuvute subira mpaka mwaka 2021 kama tutajaliwa tunaweza tukajadili mambo haya. Kwa sasa tunatumia takwimu ambazo ni za nyuma sana, kabla ya *Demographic and Health Survey*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Esther Matiko ameuliza swali zuri kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri amempa majibu mazuri sana kwa sababu alitaka kujua mkakati ni upi? Mheshimiwa Waziri amesema mkakati wa mwaka huu kwenye bajeti hii ni kumalizia na kuimarisha hospitali za rufaa za mikoa yote, ambao ni mkakati mkubwa sana kila mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili labda niseme ni kwamba, kule Tarime Mheshimiwa Esther Matiko amesema Hospitali ya Wilaya ina shida ina msongamano mkubwa sana, lakini tumeelekeza TAMISEMI kwamba fedha zipelekwe pale ili wakaimarishe hospitali ile. Kwa hiyo, ina maana akinamama watapata huduma muhimu. Pale Nkende wamepata shilingi milioni 400, Sirari wamepata shilingi milioni 500, Nanyakwa tumepata shilingi milioni 800, Kerende pale Nyamongo

tunajenga kituo cha afya na gari ya wagonjwa linapelekwa. Sasa hiyo ni mikakati ya akina mama kwamba wakipata *complication* kwenye uzazi wapate huduma haraka ya uzazi salama na Mheshimiwa Waziri amejii-commit. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukaona michango yetu, Mheshimiwa Ummu Mwalimu ni mwanamke mwenzao hawa akina Mheshimiwa Esther Matiko; amesifiwa hotuba yake ilikuwa *hot* kweli huku ndani, kila mtu alikuwa anashangilia. Nilitarajia Mheshimiwa Esther Matiko asimame hapa ampongeze mwanamke mwenzake amtie moyo bajeti ipite na tukafanye kazi kubwa sana. Akina mama lazima waungane mkono. Sasa katika mazingira haya kukwamishana inakuwaje? (Makofi/kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi/kicheko)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Esther Matiko ondoa shilingi kwa sababu zifuatazo: Waheshimiwa Wabunge tukubaliane, Wizara ya Afya kwa miaka hii mitatu wamefanya makubwa sana kuokoa maisha ya akina mama na watoto. Kama mtakumbuka Wizara ya Afya iligawa *ambulance* 100; ni mkakati. Tumejenga vituo vya afya; ni mkakati. Tunajenga hospitali za Wilaya nchi nzima; ni mkakati; Tunajenga Hospitali za Rufaa za Mikoa; ni mkakati. Yote haya ni kutaka kuhakikisha akina mama wa nchi hii wanajifungua salama. *Effort* ni kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hayo, tuangalie *trend* ya bajeti ya Wizara ya Afya hasa katika eneo hilo la kuokoa maisha ya akina mama na watoto. *Trend* ni kubwa, fedha zinaongezeka kila mwaka, yote hii ni mikakati. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo Mheshimiwa Waziri amelisema kwamba baada ya kuangalia hali nzima, wanakuja na sera pana ya afya nchini ili kuangalia tunavyotatua changamoto za afya Tanzania. Nadhani tunalo

jukumu kama Waheshimiwa Wabunge, kuwaunga mkono ili waendelee kutatua hizi changamoto zilizopo nchini. *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Muda umekwisha Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru wachangiaji wote. Kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwamba hizi takwimu zinatoka baada ya miaka mitano, lakini sisi kama Wizara tunakusanya kitu kinaitwa *routine data*, ndiyo maana tunaweza kusimama kifua mbele kusema baada ya miaka mitano tutakapokuwa tunatakiwa tukadirie kiasi kingine, vifo vya akina mama Tanzania vitakuwa vimepungua sana. Hii inatokana na mikakati yote hii ambayo inakwenda na siyo tu ndani ya Sekta ya Afya, lazima tuangalie hata hili suala la elimu bure nalo linachangia sana mabinti kuchelewa kupata ujauzito na kupunguza idadi ya akina mama wanaojifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la barabara ambazo zinajengwa na Serikali, masuala ya umeme ambayo wanafanya, yote haya yana mchango mkubwa sana. Niendelee kumwomba tu Mheshimiwa Esther Matiko, mtuamini tunachokisema hapa. Bahati nzuri katika Sekta ya Afya hatupigi porojo, takwimu tulizonazo zinaonesha kwamba hatuna vifo vya akina mama 30 kwa siku wala hatuna vifo wa akina mama 11,000 ndani ya mwaka mmoja. Hivyo havitakuwepo kutokana na mikakati hii ambayo ipo. Kwa hiyo, tunaomba mturudishie shilingi ili tuweze kwenda kutekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba tu kusema kwamba kwanza kabisa alichokisema Mheshimiwa Keissy na Wabunge wa CCM

mkaki-*support* kwa asilimia kubwa inaonesha ni jinsi gani tuna Wabunge ambao hampo kwa maslahi ya Watanzania. Ni juzi tu tumetoka kutaka kuongeza shilingi kwenye maji mkakataa. Hivi nyie mnafurahia akina mama 30 kufariki kwa siku! *No wonder*, mnafurahi hata watu wakitekwa mnaona siyo! Yaani ni Tanzania tu mnaweza kuangalia Mtanzania hata mmoja akifariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema tumejenga vituo va afya sijui Nkende, Sirari, hamna watalaam wamama wakienda pale. Pia tuzingatie katika vituo vya afya wanavyojenga 300 tuna Kata 4000, kuna vijiji 19,800, miundombinu ya barabara dhoofu ilhali wamama wajawazito wa Tanzania watafika kwenye *health center* ambako kuna Kata moja iko imekuwa *scattered* sana. Watu 11,000 ni sawa sawa na Jimbo moja la Zanzibar au mawili, wanakufa *and then* mna-*clap* makofi. Nataka mkakati Serikali ya Chama cha Mapinduzi, mtatimiza vipi sera yenu ya kuwa na kituo cha afya kila Kata, zahanati katika kila kijiji tuwe na watumishi wa kutosha na vifaa tiba kupunguza vifo vya mama na mtoto? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyotoa *priority* kwenye Wizara ya Ujenzi, narudia; kama nilivyosema juzi tutoe fedha hapa tujenge miaka 58 ya uhuru, tunazungumzia vituo 300 *and we clap*. Nakubali Nkende nimepata, *but is not enough*. Kituo kimoja cha afya *out of nane!* Siwezi... (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha Mheshimiwa. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Umesema...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umesema tupige kura maana yake sjaridhika ili sasa ijulikane.

**MWENYEKITI:** Umemaliza. Waheshimiwa Wabunge, kwanza tuelewane vizuri kunakuwa na upotoshaji huko nje mtu akiwasha *mic* saa ya kuitika kura. Sisi wote humu ndani

ni watu wazima na kuna watu hawajisikii vibaya kufanya upotoshaji. Sasa humu mnafahamu kwa idadi wapi wako wengi. Kwa hiyo, tuangalie vizuri na kama kuna sababu, kanuni zetu zinaruhusu ili kura zihesabiwe. Tuwe wavumilivu. Kama kuna mtu ana taabu, kanuni zetu zinaruhusu utaratibu, lakini tusifanye upotoshaji ambao hauna sababu yoyote.

Waheshimiwa Wabunge nitawahoji.

*(Hoja iliitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tutaendelea na Mheshimiwa Abdallah Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ukiangalia Sera ya Afya inasema kwamba huduma za matibabu katika nchi hii ni za uchangiaji. Imetumia neno “uchangiaji”, haijatumia neno “malipo”, maana yake ni kwa sababu kiasi ambacho mwananchi analipa kwa huduma ya afya ni kidogo sana kulingana na thamani halisi ya huduma anayopewa na Serikali inachangia kwa kiasi kikubwa. Tunaipongeza Serikali kwa kutembea katika sera hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha hospitali kuzuia maiti zisitoke hospitalini mpaka deni la matibabu lilipwe, hii haijaka vizuri. Nimemsikia Mheshimiwa Waziri wakati anajibu amesema kwa jitihada kubwa ambazo Serikali inazifanya siyo rahisi isamehe kila deni la matibabu ya kila mgonjwa anayefariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa siyo kusamehe madeni, lakini tunataka Serikali iweke utaratibu ambao mtu akifariki ndugu, jamaa, marafiki na majirani waweze kuchukua maiti wakazike na bado wawe na fursa ya kuja kulilipa lile deni baadaye, kwa sababu kitendo cha kuendelea kubaki na maiti hakileti picha nzuri. Maana yake maiti inakuwa *bond* ya gharama za matibabu, jambo

ambalo siyo la kiungwana na siyo la kiutamaduni kwa mila zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba *commitment* ya Serikali katika hili na kama nisiporidhika, basi nakusudia kutoa shilingi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Mtolea. Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni zetu, muda uliobaki unanitaka nihoji mafungu kwa pamoja. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fung 52 – Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,  
Wazee na Watoto**

Kif. 1001 – <i>Administration and Human Resources Management</i> .....	Sh. 8,450,857,436/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh. 1,486,211,596/=
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i> .....	Sh. 1,261,499,537/=
Kif. 1004 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 391,551,336/=
Kif. 1005 – <i>Government Communication Unit</i> .....	Sh. 386,423,562/=
Kif. 1006 – <i>Procurement Management Unit</i> ...	Sh. 302,732,000/=
Kif. 1007 – <i>Legal Service Unit</i> .....	Sh.162, 660,063/=
Kif. 1008 – <i>Information and Communication Technology Unit</i> .....	Sh. 280,096,480/=
Kif. 2001 – <i>Curative Service</i> .....	Sh. 219,991,668,419/=
Kif. 2003 – <i>Chief Medical Officer</i> .....	Sh. 37,502,929,116/=
Kif. 2004 – <i>Nursing and Midwifery Services Division</i> .....	Sh. 552,896,936/=
Kif. 2005 – <i>Pharmaceutical Services Unit</i> .....	Sh. 385,051,336/=
Kif. 3001 – <i>Preventive Services</i> .....	Sh.19,266,898,424/=
Kif. 3002 – <i>Health Quality Assurance Division</i> .....	Sh. 516,151,382/=
Kif. 4002 – <i>Social Welfare</i> .....	Sh. 399,555,336/=

Kif. 5001 – <i>Human Resource Development</i> .....	Sh.12,590,595,556/=
Kif. 6001 – <i>Amana Regional Referral Hospital- Dar es Salaam</i> .....	Sh. 5,806,680,932/=
Kif. 6002 – <i>Bombo Regional Referral Hospital- Tanga</i> .....	Sh. 5,098,106,324/=
Kif. 6003 – <i>Dodoma Regional Referral Hospital</i> .....	Sh. 6,847,156,802/=
Kif. 6004 – <i>Geita Regional Referral Hospital</i> .....	Sh. 1,601,737,746/=
Kif. 6005 – <i>Iringa Regional Referral Hospital</i> .....	Sh. 5,394,379,596/=
Kif. 6006 – <i>Kagera Regional Referral Hospital</i> .....	Sh. 3,915,547,873/=
Kif. 6007 – <i>Katavi Regional Referral Hospital</i> .....	Sh. 2,368,264,624/=
Kif. 6008 – <i>Ligula Regional Referral Hospital – Mtwara</i> .....	Sh. 3,285,599,596/=
Kif. 6009 – <i>Manyara Regional Referral Hospital</i> .....	Sh. 2,814,757,772/=
Kif. 6010 – <i>Mara Regional Referral Hospital</i> .....	Sh. 3,701,590,622/=
Kif. 6011 – <i>Maweni Regional Referral Hospital - Kigoma</i> .....	Sh. 3,056,223,596/=
Kif. 6012 – <i>Mawenzi Regional Referral Hospital – Kilimanjaro</i> ...	Sh. 5,843,907,828/=
Kif. 6013 – <i>Mbeya Regional Referral Hospital</i> .....	Sh. 4,208,295,596/=
Kif. 6014 – <i>Morogoro Regional Referral Hospital</i> .....	Sh. 6,840,236,932/=
Kif. 6015 – <i>Mount Meru Regional Referral Hospital - Arusha</i> .....	Sh. 5,660,399,596/=
Kif. 6016 – <i>Mwananyamala Regional Referral Hospital- DSM</i> .....	Sh. 4,974,388,436/=
Kif. 6017 – <i>Njombe Regional Referral Hospital</i> .....	Sh. 1,537,033,448/=
Kif. 6018 – <i>Sekou Toure Regional Referral Hospital – Mwanza</i> ....	Sh. 4,970,951,386/=
Kif. 6019 – <i>Shinyanga Regional Referral Hospital</i> .....	Sh. 3,637,721,596/=



Kif. 6020 – Simiyu Regional Referral Hospital.....	Sh. 1,857,080,648/=
Kif. 6021 – Singida Regional Referral Hospital.....	Sh. 3,762,526,632/=
Kif. 6022 – Sokoine Regional Referral Hospital – Lindi.....	Sh. 3,347,827,596/=
Kif. 6023 – Songea Regional Referral Hospital – Ruvuma.....	Sh. 5,733,932,596/=
Kif. 6024 – Songwe Regional Referral Hospital.....	Sh. 821,246,811/=
Kif. 6025 – Sumbawanga Regional Referral Hospital – Rukwa.....	Sh. 2,804,199,596/=
Kif. 6026 – Tabora Regional Referral Hospital.....	Sh. 3,402,726,055/=
Kif. 6027 – Temeke Regional Referral Hospital- Dar es Salaam.....	Sh. 6,158,812,756/=
Kif. 6028 – Tumbi Kibaha Regional Referral Hospital – Pwani.....	Sh. 1,635,150,495/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### **Fungu 53 – Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

Kif 1001 – Administration and Human Resources Management.....	Sh. 2,323,579,813/=
Kif. 1002 – Finance and Accounts Unit.....	Sh. 415,150,000/=
Kif. 1003 – Policy and Planning Unit.....	Sh. 877,588,800/=
Kif. 1004 – Internal Audit Unit.....	Sh. 323,676,301/=
Kif. 1005 – Government Communication Unit.....	Sh. 2,575,929,598/=
Kif. 1006 – Procurement Management Unit...Sh.	478,857,000/=
Kif. 1007 – Information and Communication Technology.....	Sh. 479,459,943/=
Kif. 1008 – Legal Service Unit.....	Sh. 236,464,500/=
Kif. 2001 – Training and Folk Development...Sh.	211,044,000/=
Kif. 2002 – Community Development.....Sh.	11,650,733,357/=
Kif. 3001 – Gender Development.....	Sh. 944,777,000/=
Kif. 3002 – Children Development.....	Sh. 867,140,000/=

Kif. 4001 – *Non-Government Organizations*.....Sh. 784,298,120/=  
Kif. 5001 – *Social Welfare Division*.....Sh. 6,426,671,568/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## KITABU CHA NNE

### MIPANGO YA MAENDELEO

#### **Fungu 52 – Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

Kif. 3001 – *Policy and Planning Unit*.....Sh. 45,188,873,128/=  
Kif. 2001 – *Curative Services*.....Sh. 42,891,039,000/=  
Kif. 2005 – *Pharmaceutical Services Unit*.....Sh. 200,000,000,000/=  
Kif. 3001 – *Preventive Services*.....Sh. 256,057,990,469/=  
Kif. 3002 – *Health Quality Assurance Division*..... Sh. 0  
Kif. 5001 – *Human Resource Development*..... Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 53 – Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

Kif. 2002 – *Community Development*.....Sh. 1,000,000,000/=  
Kif. 3001 – *Gender Development*.....Sh. 1,124,040,000/=  
Kif. 3002 – *Children Development*.....Sh. 191,350,000/=  
Kif. 5001 – *Social Welfare Division*.....Sh. 444,671,013/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae, Mtoa Hoja.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari 2016 kanuni ya 104(3) (a) na (b) kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono ahsanteni sana sasa kwa utaratibu wetu niwatahoji.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 – Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto yalipitishwa na Bunge*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nianze kwanza kwa kutoa pongezi nyingi kwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wanaofanya kazi katika Wizara hii. Pongezi hizi nadhani nyingi mmezipokea kutoka kwa Waheshimiwa wabunge. Sasa kwa sababu Bunge limeshafanya uamuzi kuhusu yale mliyokuwa mmeyaleta kwetu pamoja na yale ambayo Kamati imewashauri na ninyi mmeyachukua, kwa hiyo, niwapongeze kwa niaba yetu sisi sote kwamba mnafanya kazi nzuri pamoja na changamoto za hapa na pale, lakini kwa ujumla wake mnafanya kazi nzuri ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge wanatambua uwepo wenu kwenye majimbo yao na uwepo wa kazi zenu kwenye Majimbo yao. (*Makofi*)

Kwa hiyo, yale ambayo wamechangia humu ndani tunaamini kwamba yataboresha utendaji kazi wenu, lakini

pengine hapa na pale panapohitaji marekebisho, basi mtafanya hayo marekebisho kwa kadri mlivyoshauriwa na Kamati na Waheshimiwa Wabunge wale ambao hawakupata fursa ya kushiriki kwenye Kamati. Nasi tuchukue fursa hii kuwatakiya kila la kheri kwenye utekelezaji wa yale yote ambayo umeyaahidi kwamba mnaenda kuyafanya na pia yale ambayo mmesema mnaenda kuboresha kwa mujibu wa Waheshimiwa Wabunge walivyotoa mapendekezo yao. Tunawatakiya kila la kheri. *(Makofi)*

Pia kwa yale ambayo yamezungumzwa hapa ya jumla moja ni kuhusu Bima ya Afya kama Bunge na sisi tungependa kutoa huo msisitizo na Waheshimiwa Wabunge; sisi kama Wawakilishi wa Wananchi ni vizuri kuendelea kuzungumza na wananchi wetu tunapopata fursa ya kuonana nao kuona umuhimu wa kuwa na bima. Kwa hiyo, tuendeleo kuwashauri, siyo jambo litakalobadilika kwa siku moja lakini naamini kwa sababu wananchi waliokuamini kuja humu ndani wanawaamini pia mkiwapa ushauri. Tusichoke kuendelea kuwashauri wananchi tunaowawakilisha humu ndani ili waone umuhimu wa kuwa na Bima ya Afya.

Jambo lingine Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza hapa baada ya michango ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu vipimo vya homa ya matumbo na pia vipimo vya maambukizi kwenye mrija au mirija ya haja ndogo, nadhani tukisema tu sisi tukienda hospitali ndio tuwaulize sio wote wenye ujasiri wa kumwuliza daktari anaposema amepima kitu fulani na majibu yametoka.

Nadhani ni muhimu kwa upande wa Wizara ya Afya kutoa mwongozo mahususi ili wale watu wanapotupima watupime kitaalam kwenye hayo huenda ndiyo tunayoumwa, lakini watupime kitaalam, wasitupime wakatupa dakika mbili kwa majibu yanayochukua siku mbili. Nadhani hiyo sasa ni ya upande wenu kuliko sisi tukiwa wagonjwa maana wakati mwingine mgonjwa anaweza kuwa anaogopa, daktari akamwandikia sindano hata kama kuna vidonge kwa sababu anajua amemwuliza maswali magumu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tafadhali kwenye hili Wizara ya Afya mtusaidie kwa sababu maana yake watu wanaweza kuwa wanakunywa dawa ambazo hawaumwi magonjwa hayo na baadaye wanaweza kuja kupata changamoto za magonjwa makubwa kama aliyokuwa anataja Mheshimiwa Khatib hapa. Kwa hiyo, hilo nadhani ninyi mnaweza kulifanyia kazi kwa haraka, siyo jambo gumu ili wenzetu wa vipimo wawe wanatupima sawasawa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuzungumza hayo yaliyo ya jumla, wapo wageni ambao tuko nao Bungeni jioni hii. Tunao wageni 18 wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ambaye ni Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi, Madiwani na watumishi kutoka Wilaya ya Kigamboni Jijini Dar es Salaam. Hawa wameongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ambaye ni ndugu Henry Chaula. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 80 wa Mheshimiwa Godfrey Mgimwa ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, wanaotokea Jimbo la Kalenga karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12.01 jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi, Tarehe 9 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*